




# MUUNGANO WA TANGANYIKA NA ZANZIBAR

CHIMBUKO, MISINGI NA  
MAENDELEO







# MUUNGANO WA TANGANYIKA NA ZANZIBAR

CHIMBUKO, MISINGI NA  
MAENDELEO

KIMECHAPISHWA NA  
Mkuki na Nyota Publishers Ltd  
S. L. P. 4246  
Dar es Salaam, Tanzania  
[www.mkukinyota.com](http://www.mkukinyota.com)

Kwa ajili ya  
Ofisi ya Makamu wa Rais,  
Mji wa Serikali, Eneo la Mtumba  
S.L.P. 2502  
Dodoma, Tanzania  
[www.vpo.go.tz](http://www.vpo.go.tz)

© Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, 2022

ISBN 978 9987 753 66 6 (Jalada Gumu)  
ISBN 978 9987 753 67 3 (Jalada Laini)

Haki zote zimehifadhiwa. Hairuhusiwi kunakili, kuhifadhi, kuchapisha kwa njia ya kielektroniki au mekaniki, kutoa vivuli, kurekodi au kubadili sehemu yoyote ya kitabu hiki kwa njia, namna au mfumo wowote bila idhini ya maandishi kutoka kwa Katibu Mkuu, Ofisi ya Makamu wa Rais.

# YALIYOMO

VIFUPISHO VYA MANENO .....	ix
TAMKO LA MHESHIMIWA RAIS WA JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA NA MHESHIMIWA RAIS WA ZANZIBAR NA MWENYEKITI WA BARAZA LA MAPINDUZI .....	xiii
SHUKRANI .....	xvii
UTANGULIZI .....	xix

## SURA YA KWANZA

### DHANA YA MUUNGANO, HISTORIA YA TANZANIA BARA NA TANZANIA ZANZIBAR

Maana na Dhamira ya Muungano .....	1
Aina za Muungano .....	1
Changamoto Kufikia Muungano .....	4
Vita vya Marekani (1861–1865) .....	4
Vita vya Ireland ya Kaskazini (1968–1998) .....	4
Harakati za Catalonia Kujitenga na Hispania .....	5
Jitihada za Kuungana Barani Afrika .....	6
Misingi ya Muungano Imara .....	9
Historia ya Tanzania Bara na Tanzania Zanzibar .....	11
Tanzania Bara .....	11
Tanzania Zanzibar .....	26

## SURA YA PILI

### MISINGI YA MUUNGANO WA TANGANYIKA NA ZANZIBAR

Misingi ya Muungano .....	43
Mazingira Rafiki na Wezeshi .....	43
Uzoefu wa Pamoja katika Utumwa, Ukoloni na Harakati za Uhuru .....	47
“Ushindi wa Mezani” wa ZNP na ZPPP .....	49
Kauli na Matendo ya Viongozi Shuruti Yaakisi Muungano .....	51
Uwiano katika Mgawanyo wa Madaraka na Ustawi .....	52
Mapokezi ya Muungano Kimataifa .....	53

## **SURA YA TATU**

### **MUUNGANO WA TANGANYIKA NA ZANZIBAR**

Matukio Muhimu Kuelekea Muungano . . . . .	55
Hatua Muhimu Kukamilisha Muungano . . . . .	56
Wazungu, Wasomi na Hoja ya Muungano . . . . .	62
Muundo wa Muungano . . . . .	66
Hati ya Makubaliano ya Muungano, Katiba na Sheria . . . . .	66
Maelekezo Mahususi ya Hati ya Muungano . . . . .	67
Uchaguzi wa Mfumo wa Serikali (Moja, Mbili au Tatu) . . . . .	68
Ukusanyaji wa Maoni ya Wananchi . . . . .	69
Muungano Shirikisho au Jumuishi? . . . . .	70
Mambo ya Muungano . . . . .	71
Kuongezeka kwa Mambo ya Muungano . . . . .	72
Sababu za Kuongezeka kwa Mambo ya Muungano . . . . .	72
Uhai wa Muungano . . . . .	75

## **SURA YA NNE**

### **UTEKELEZAJI WA MAMBO YA MUUNGANO**

Katiba ya Tanzania na Serikali ya Jamhuri ya Muungano . . . . .	77
Katiba ya Jamhuri ya Muungano . . . . .	77
Bunge . . . . .	77
Utawala Bora . . . . .	78
Mambo ya Nje . . . . .	80
Mchango wa Tanzania katika Ukombozi . . . . .	82
Tanzania na Upatanishi wa Nchi . . . . .	84
Ulinzi na Usalama . . . . .	85
Jeshi la Ulinzi la Wananchi wa Tanzania (JWTZ) . . . . .	86
Mchango wa JWTZ kwa Dunia . . . . .	87
Polisi . . . . .	88
Uraia . . . . .	90
Uhamiaji . . . . .	90
Mikopo na Biashara ya Nje . . . . .	92
Mikopo . . . . .	92
Biashara ya Nje . . . . .	93
Utumishi wa Umma . . . . .	94
Utumishi wa Umma katika Jamhuri ya Muungano . . . . .	95
Kodi ya Mapato, Ushuru wa Forodha na Bidhaa . . . . .	95
Bandari . . . . .	96
Posta na Simu . . . . .	96
Ubinafishaji wa TTCL . . . . .	98
Usafiri na Usafirishaji wa Anga . . . . .	98

Mambo yote Yanayohusika na Sarafu, Fedha, Mabenki na Fedha za Kigeni . . . . .	100
Enzi za Utawala wa Ujerumani (1880 hadi 1919) . . . . .	101
Enzi za Utawala wa Waingereza, 1919 - 1961 . . . . .	101
Kuanzishwa kwa Bodi ya Sarafu ya Afrika Mashariki . . . . .	102
Benki Kuu ya Tanzania (BoT) . . . . .	102
Baada ya Azimio la Arusha, 1967-1991 . . . . .	103
Baada ya 1991 . . . . .	103
Leseni za Viwanda na Takwimu . . . . .	104
Elimu . . . . .	104
Elimu Kipindi cha Ukoloni . . . . .	105
Tanzania Bara . . . . .	106
Zanzibar . . . . .	107
Elimu ya Juu . . . . .	109
Maboresho ya Elimu ya Juu . . . . .	110
Baraza la Taifa la Mitihani . . . . .	112
Utafiti . . . . .	112
Utabiri wa Hali ya Hewa . . . . .	114
Takwimu . . . . .	114
Mahakama ya Rufani . . . . .	116
Uandikishaji wa Vyama vya Siasa . . . . .	116

## **SURA YA TANO**

### **HOJA ZA MUUNGANO NA UTATUZI WAKE**

Hoja za Muungano . . . . .	117
Kamati na Tume Zilizoundwa . . . . .	117
Tume ya Jaji Kisanga 1999 . . . . .	118
Kamati ya Shellukindo 1992 . . . . .	118
Kamati ya Pamoja ya SMT na SMZ ya Kushughulikia Masuala ya Muungano . . . . .	119

## **VIAMBATISHO**

1. Hati ya Muungano wa Tanganyika na Zanzibar . . . . .	129
2. Mtazamo wa Makundi Mbalimbali Kuhusu Muungano . . . . .	134
Wasomi na Wanazuoni . . . . .	134
Viongozi wa Dini . . . . .	135
Wanasiasa . . . . .	136
Vijana . . . . .	137
Nukuu za Waasisi wa Muungano wa Tanganyika na Zanzibar	140
Mwalimu Julius Kambarage Nyerere . . . . .	140
Sheikh Abeid Amani Karume . . . . .	143

3. Awamu za Uongozi Katika Jamhuri ya Muungano wa Tanzania . .	147
Awamu ya Kwanza ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mwaka 1964 Hadi 1985 . . . . .	147
Awamu ya Pili ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Kuanzia Mwaka 1985 Hadi 1995. . . . .	150
Awamu ya Tatu ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Kuanzia Mwaka 1995 Hadi 2005. . . . .	153
Awamu ya Nne ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Kuanzia Mwaka 2005 Hadi 2015. . . . .	155
Awamu ya Tano ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mwaka 2015-2021 . . . . .	158
Awamu ya Sita ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Kuanzia Mwaka 2021 . . . . .	161
4. Kamati iliyoandaa Kitabu cha <i>Muungano wa Tanganyika na Zanzibar: Chimbuko, Misingi na Maendeleo</i> . . . . .	162



## VIFUPISHO VYA MANENO

AA	African Association
ANC	African National Congress
ASP	Afro-Shiraz Party
ATC	Air Tanzania Corporation
AUPEC	Aberdeen University Petroleum and Economic Consultants
BET	Board of External Trade
BIT	Board of Internal Trade
BIZANJE	Shirika la Biashara za Nje
BoT	Bank of Tanzania
BRELA	Business Registration and Licensing Authority
CCM	Chama Cha Mapinduzi
CHADEMA	Chama cha Demokrasia na Maendeleo
CIA	Central Intelligence Agency
COSTECH	Commission for Science and Technology
CUF	Civic United Front
DIB	Deposit Insurance Board
DITF	Dar es Salaam International Trade Fair
DRC	Democratic Republic of Congo
EACSO	East African Common Services Organisation
EAMD	East African Meteorological Department
e-RCS	Electronic Revenue Collection System

GAPEX	General Agricultural Products Export Company
GBS	General Budget Support
IMF	International Monetary Fund
IMO	International Maritime Organization
JWTZ	Jeshi la Ulinzi la Wananchi wa Tanzania
KAR	King's African Rifles
KIST	Karume Institute of Science and Technology
MDRI	Multilateral Debt Relief Initiative
MoU	Memorandum of Understanding
NBS	Natioanal Bureau of Statistics
NCCR-Mageuzi	National Convention for Construction and Reform – Mageuzi
NIDA	National Identification Authority
NPSS	Nationalist Party of the Subjects of the Sultan
OAU	Organization of African Unity
PAFMECA	Pan-African Freedom Movement for Eastern and Central Africa
RORO	Roll on Roll off
SA	Shirazi Association
SADC	Southern African Development Community
SMT	Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania
SMZ	Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar
SUMATRA	Surface and Marine Transport Regulatory Authority
SUZA	State University of Zanzibar
TAA	Tanganyika African Association
TANTRADE	Tanzania Trade Development Authority
TANU	Tanganyika African National Union
TBC	Tanzania Broadcasting Corporation
TMA	Tanzania Meteorological Authority
TMF	Tanganyika Military Force
TPA	Tanzania Ports Authority
TR	Tanganyika Rifles
TRA	Tanzania Revenue Authority

TRAT	Tanzania Revenue Appeals Tribunal
TTCL	Tanzania Telecommunications Company Limited
UDP	United Democratic Party
ZMA	Zanzibar Maritime Authority
ZNP	Zanzibar Nationalist Party
ZPFL	Zanzibar and Pemba Federation of Labour
ZPPP	Zanzibar and Pemba People's Party
ZU	Zanzibar University
ZYL	Zanzibar Youth League



**TAMKO LA  
MHESHIMIWA RAIS WA JAMHURI  
YA MUUNGANO WA TANZANIA  
NA MHESHIMIWA RAIS WA  
ZANZIBAR NA MWENYEKITI WA  
BARAZA LA MAPINDUZI**



**MHE. SAMIA SULUHU  
HASSAN**



**MHE. DKT. HUSSEIN ALI  
MWINYI**

Muungano wa Tanganyika na Zanzibar umejengeka kutokana na historia ya uhusiano wa udugu wa damu, harakati za pamoja na ushirikiano wa vyama vya ukombozi vya Tanganyika na Zanzibar katika kupigania uhuru. Mahusiano hayo yaliyowezeshwa na kudumishwa na waasisi wa Jamhuri ya Tanganyika na Jamhuri ya Watu wa Zanzibar, Mwalimu Julius Kambarage Nyerere na Sheikh Abeid Amani Karume ndiyo yaliyorasimisha Muungano wa Tanganyika na Zanzibar. Hivyo, tunawashukuru Waasisi hao kwa kutujengea na kuturithisha misingi ya udugu, uzalendo, amani, mshikamano na utulivu ambavyo ni nguzo kuu ya Muungano wetu.

Tunapoadhimisha miaka 58 ya Muungano wetu, Watanzania wote tuna kila sababu ya kutafakari na kutathmini masuala muhimu yaliyokusudiwa na Waasisi wa Taifa letu ambao walitia saine Hati ya Makubaliano ya Muungano kwa niaba ya wananchi wa nchi hizo mbili. Pamoja na Waasisi wetu kutangulia mbele ya haki, misingi waliyotuachia imeendelea kuimarisha umoja, amani, na utulivu wa Taifa letu. Tumuombe Mwenyezi Mungu awapumzishe mahali pema peponi, Amina.

Muungano wetu umedumu kutokana na mizizi yake kujikita kwa wadau wakuu wa Muungano (wananchi) na umakini na usikivu wa Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kuwa na sera endelevu ya Muungano na kufuatilia kwa karibu changamoto zinazojitokeza na kuzipatia ufumbuzi. Hakika utamaduni tuliojiingia wa kuwa na vikao vya pamoja vya kujadili na kuzipatia ufumbuzi changamoto zinazojitokeza kwa kuzingatia misingi ya umoja na mshikamano, umeimarisha na kudumisha Muungano kwa kiasi kikubwa.

Katika kipindi cha zaidi ya nusu karne ya Muungano wetu, tumeshuhudia mafanikio makubwa ya kujivunia kwani ni Muungano wa kipekee uliodumu kati ya majaribio kadhaa ya aina hiyo barani Afrika. Tumeshuhudia kuimarika kwa amani, utulivu pamoja na ulinzi na usalama ndani ya nchi na kwenye mipaka yetu. Aidha, pande zote mbili za Muungano zimejenga mifumo ya kuendesha Serikali zake kwa uwazi chini ya misingi ya sheria, demokrasia na utawala bora. Misingi hiyo imeimarika kutokana na uelewa mzuri wa dhana ya uwajibikaji na utashi wa kisiasa kwa viongozi wa ngazi zote.

Uchumi umeimarika kutokana na mazingira na mahusiano mazuri ya kibiashara kati ya Tanzania Bara na Tanzania Zanzibar. Aidha, tumeshuhudia kuimarika kwa miundombinu, hususan ya barabara na huduma za jamii ikiwamo afya, maji na elimu.

Hata hivyo, pamoja na mafanikio yaliyopatikana, tumekumbana na changamoto ambazo kwa ujasiri mkubwa tumekabiliana nazo kwa kushirikiana. Ni matarajio yetu kuwa, tutaendelea kuenzi, kuulinda, kuuimarisha na kuudumisha Muungano wetu na kukuza ushirikiano uliopo kwa manufaa ya wananchi wa pande zote mbili za Muungano.


Tunatumia nafasi hii adhimu kuwashukuru kwa dhati Viongozi wa Awamu zote za Uongozi za Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar. Hekima na busara zao zimewezesha Taifa kuwa imara na kudumisha udugu wa wananchi wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Pia, tunawashukuru Wananchi wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa moyo wao wa kujitolea katika kulijenga Taifa letu. Vilevile, tunawashukuru Washirika wa Maendeleo kwa mchango wao mkubwa katika kuunga mkono jitihada za kulitea maendeleo Taifa letu.

Ni matumaini yetu kuwa misingi imara ya amani na utulivu uliopo, rasilimali watu, maliasili na vivutio vya utalii ni fursa zinazoweza kuleta maisha bora zaidi kwa kila Mtanzania ikiwa kila mmoja wetu atatimiza wajibu wake ipasavyo.

Kwa kuthamini juhudi za Waasisi wa Muungano wetu na mafanikio yaliyopatikana kutokana na Muungano, kwa pamoja tunaahidi kuendelea kuenzi, kuulinda na kuudumisha Muungano wetu Adhimu.


Ni imani yetu kuwa Kitabu hiki kinachoelezea Historia ya Muungano wa Tanganyika na Zanzibar, Chimbuko, Misingi na Maendeleo, kitakuwa rejea muhimu kwa vizazi vya sasa na vijavyo.

**MUNGU IBARIKI AFRIKA, MUNGU IBARIKI TANZANIA,  
MUNGU UBARIKI MUUNGANO WETU**



Samia Suluhu Hassan

**RAIS WA JAMHURI YA  
MUUNGANO  
WA TANZANIA**



Dkt. Hussein Ali Mwinyi

**RAIS WA ZANZIBAR NA  
MWENYEKITI  
WA BARAZA LA MAPINDUZI**

Aprili, 2022





## SHUKRANI



MHE. DKT. PHILIP ISDOR  
MPANGO

Nimepitia kitabu hiki na kufarijika sana na uandishi wake ambao umetufunza mengi kuhusu Muungano. Kitabu hiki kimeainisha kwa kina historia ya Muungano wetu, misingi ya Muungano, muundo na matukio muhimu ya Muungano, mafanikio pamoja na kutoa ufafanuzi wa hoja mbalimbali za Muungano na namna zilivyoshughulikiwa.

Kazi ya kuandaa kitabu hiki ilihusisha wataalamu kutoka pande zote mbili za Muungano. Tunatambua michango ya hali na mali

iliyotolewa katika kufanikisha jukumu hili la kihistoria. Hivyo, ninapenda kuwashukuru na kuwapongeza wataalamu hao pamoja na wote walioshiriki kwa namna moja au nyingine kutoa maoni na ushauri uliowezesha kufanikisha maandalizi ya Kitabu hiki.

Ninatoa shukrani za pekee kwa Menejimenti ya Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano na Mazingira) na Menejimenti ya Afisi ya Makamu wa Pili wa Rais (Sera, Uratibu na Baraza la Wawakilishi) kwa kusimamia uandishi wa Kitabu hiki. Aidha, ninazishukuru Wizara zote za SMT na SMZ kwa ushirikiano wao katika upatikanaji wa taarifa mbalimbali.

Natoa rai kwa Watanzania wote kusoma kitabu hiki ili kupata uelewa wa historia ya Muungano wetu pamoja na mafanikio yaliyopatikana kutokana na ushirikiano mzuri baina ya pande mbili za Muungano. Aidha, natoa wito kwa wananchi na viongozi wote wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kutimiza wajibu wa kuenzi, kuudumisha, kuimarisha na kuuendeleza Muungano kwa faida yetu na vizazi vijavyo.

**MUNGU IBARIKI AFRIKA, MUNGU IBARIKI TANZANIA,  
MUNGU UBARIKI MUUNGANO WETU**



Dkt. Philip Isdor Mpango

**MAKAMU WA RAIS WA JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

Aprili, 2022

# UTANGULIZI

Jamhuri ya Muungano wa Tanzania inatokana na muungano wa nchi mbili huru zilizokuwa zikiitwa Jamhuri ya Tanganyika na Jamhuri ya Watu wa Zanzibar<sup>1</sup> ambao umefafanuliwa katika Hati ya Makubaliano ya Muungano iliyosainiwa na Mwalimu Julius K. Nyerere, Rais wa Jamhuri ya Tanganyika na Sheikh Abeid A. Karume, Rais wa Jamhuri ya Watu wa Zanzibar, tarehe 22 Aprili, 1964 na kufuatiwa na matukio mbalimbali ya Muungano yaliyohitimishwa rasmi tarehe 26 Aprili, 1964.

Pamoja na Hati ya Makubaliano ya Muungano kusainiwa tarehe 22 Aprili, 1964 zipo sababu za kihistoria na kimahusiano zilizochoecha nchi hizi kuungana na Muungano huo kushamiri na kudumu. Sababu hizo ni pamoja na ujirani wa karibu; urafiki na udugu wa damu wa miaka mingi; lugha ya pamoja ya mawasiliano – Kiswahili; shughuli za pamoja za kiuchumi – uvuvi, kilimo na biashara; uzoefu wa pamoja vipindi vya utumwa na ukoloni; na mahusiano ya karibu ya kisiasa katika kupigania uhuru wa Tanzania Bara na Tanzania Zanzibar.

Sababu hizi ndizo zinazoufanya Muungano wa nchi hizi mbili kuwa wa kipekee, na ni sababu ambazo hazina budi kuzingatiwa na wadau, watafiti na waandishi wa historia wanapolitalii suala hili adhimu la Muungano huo. Bila kufanya hivyo, chimbuko la Muungano wa Tanzania halionekani bayana na upekee wa Muungano huo haujitokezi waziwazi.

---

<sup>1</sup> Ibara ya 151(1) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977 inafafanua kuwa Jamhuri ya Tanganyika na Jamhuri ya Zanzibar ndiyo Tanzania Bara na Tanzania Zanzibar mtawalia, baada ya Muungano.

Juhudi za kutosha zimefanywa na Serikali zote mbili – Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kuhakikisha kuwa wanafunzi wengi wa ngazi mbalimbali pamoja na wananchi kwa ujumla wanapata taarifa sahihi kuhusu historia, changamoto na mafanikio makubwa ya Muungano wa Tanzania ambao umebaki kuwa Muungano pekee barani Afrika uliodumu na kushamiri kwa zaidi ya nusu karne na kuendelea kuyaishi malengo ya Umajumui wa Afrika.

Hata hivyo, bado kuna upotoshaji na uelewa mdogo miongoni mwa Watanzania kuhusu Muungano, udhaifu ambao utaondoka kwa uchapishaji zaidi wa taarifa sahihi kuhusu Muungano na usambazaji wake shuleni, vyuoni, kazini na sehemu nyingine zinazokusanya watu wengi na kuibua mijadala chanya ya kujenga uelewa mpana wa wadau. Uandaaji wa kitabu hiki chini ya usimamizi wa Ofisi ya Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, una mwelekeo huo.

Kitabu hiki kimegawanyika katika Sura Tano na kina viambatisho vinne.

Sura ya Kwanza inaelezea dhana ya Muungano, Historia ya Tanzania Bara na Tanzania Zanzibar. Hivyo, inafafanua maana na dhamira ya Muungano na aina za Muungano. Aidha, changamoto kufikia Muungano zinajadiliwa kwa kirefu kwa kuangalia uzoefu wa Marekani na vita vya wenyewe kwa wenyewe (1861-1865), uzoefu wa Uingereza na vita vya Ireland ya Kaskazini (1968-1998) na harakati za Catalonia kujitenga na Hispania.

Sura hii pia inajadili jitihada mbalimbali za kuungana barani Afrika zilizyoshindikana na sababu zake na inaainisha misingi mikuu ya Muungano kuendana na uzoefu wa Muungano wa Tanzania.

Pamoja na mambo mengine, Historia ya Tanzania Bara inaonesha mchango wa viongozi mbalimbali wa kimila katika mapambano dhidi ya ukoloni na hivyo kusahihisha dhana potofu kuwa Tanzania Bara ilipata uhuru bila kutumia nguvu. Aidha, pamoja na mambo mengine, historia ya Zanzibar inaungana na historia ya Tanzania Bara katika Sura hii ya Kwanza ili kufuatilia mizizi mirefu ya Chama Cha Mapinduzi (CCM) kuanzia miaka ya 1920 na 1930 ambapo Jumuiya tatu za Kiafrika na Kishirazi zilianzishwa kutetea maslahi ya Waafrika na Washirazi.

Jumuiya hizo tatu ndizo katika miaka ya 1950 zilijigeuza kuwa vyama vya siasa – *Tanganyika African National Union* (TANU) na *Afro-Shirazi Party* (ASP) na baadaye mwaka 1977 vyama hivyo viwili vikaungana na kuunda Chama Cha Mapinduzi chenye Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar.

Sura ya Pili inafafanua zaidi Misingi ya Muungano wa Tanganyika na Zanzibar: mazingira rafiki na wezeshi ambayo yapo pande zote mbili za Muungano, ukaribu kijiografia wa Tanzania Bara na Tanzania Zanzibar ambao ni muhimu kwa upande wa wananchi katika kuimarisha Muungano siku hadi siku, na mwingiliano wa miaka mingi kibiashara, kijamii na kiutamaduni katika nchi hizi mbili.

Pia Sura hii inaongelea uzoefu wa pamoja wa pande hizi mbili za Muungano katika vipindi vigumu vya utumwa na ukoloni na katika harakati za kuwania uhuru, matendo na kauli za viongozi wake wa kwanza wa uhuru, Mwalimu Julius Nyerere na Sheikh Abeid Karume, zilivyoakisi na kujinasibisha na Muungano.

Sura ya Tatu inajihusisha na Matukio Muhimu kuelekea Muungano, hatua muhimu kukamilisha Muungano na hoja mbalimbali za wasomi wa nje na ndani kuhusu Muungano huu adimu na adhimu katika Bara la Afrika. Aidha, Sura hii inaongelea Muundo wa Muungano wa Tanzania kwa kuzingatia Hati ya Makubaliano ya Muungano ya mwaka 1964, uchaguzi wa Mfumo wa Serikali Mbili, maoni na matakwa ya wananchi, Mambo ya Muungano na sababu za kuongezeka kwake na kinachoupa Muungano wa Tanzania uhai.

Sura ya Nne inaelezea Utekelezaji wa Mambo ya Muungano kama yalivyoainishwa katika Nyongeza ya Kwanza ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977.

Sura ya Tano inaongelea Hoja za Muungano na utatuzi wake pamoja na Tume na Kamati mbalimbali zilizoundwa kushughulikia hoja mahususi za Muungano.

Kitabu hiki kina viambatisho vinne: Hati ya Makubaliano ya Muungano ya mwaka 1964; Mtazamo wa Makundi Mbalimbali kuhusu Muungano; Awamu za Uongozi katika Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Kuanzia Mwaka 1964-2022; na Kamati Iliyoandaa Kitabu cha Muungano wa Tanganyika na Zanzibar, Chimbuko, Misingi na Maendeleo

Aidha, kitabu hiki kinazijadili hoja zenye mwelekeo wa kupotosha historia ya Tanzania kwa nia njema ya kuziweka sawa zikiwamo harakati za kutafuta uhuru na hatima yake, Mapinduzi Matukufu ya Zanzibar na Muungano wa Tanganyika na Zanzibar na faida zake kwa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Afrika kwa ujumla.

1. Ipo dhana ya muda mrefu kwamba Tanzania Bara ilipata uhuru kwa mazungumzo. Sura ya Kwanza inaelezea vita vilivyoongozwa na viongozi mbalimbali wa kimila Tanganyika kukataa kutawaliwa

na wageni. Iliwachukua wakoloni wa Kijerumani takriban miaka 10 kumaliza vita hivyo kijeshi na sehemu nyingine kwa makubaliano.

2. Picha maarufu ya Mwalimu Nyerere akichanganya udongo wa Tanzania Bara na Tanzania Zanzibar ambayo katika vitabu na nyaraka mbalimbali inaelezwa kuwa ilichukuliwa Jumapili tarehe 26 Aprili, 1964 katika sherehe za Muungano na baadhi ya watu kuhoji kwa nini Sheikh Karume hakushirikishwa katika zoezi hilo.

Ukweli ni kwamba picha hiyo ilichukuliwa Jumatatu tarehe 26 Aprili, 1965 kwenye maadhimisho ya mwaka wa kwanza wa Muungano wa Tanzania kama inavyoelezwa katika Sura ya Tatu. Hivyo, Mwalimu Nyerere alichanganya udongo akiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania aliyebeba dhamana ya pande zote mbili za Muungano akishuhudiwa na Sheikh Karume, Makamu wa Kwanza wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi na Mhe. Rashid Mfaume Kawawa, Makamu wa Pili wa Rais wa Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Waziri Mkuu. Aidha, walioshika chungu katika picha hiyo ni Bw. Hassan Omar Mzee kutoka Tanzania Zanzibar na Bw. Hasanaeli Mrema kutoka Tanzania Bara.

3. Kuna madai kwamba Muungano wa Tanganyika na Zanzibar haukutokana na matakwa ya ndani ya nchi hizo mbili bali ulitokana na shinikizo la Shirika la Ujasusi la Marekani (CIA) ili kuzuia siasa za mrengo wa kushoto za baadhi ya viongozi wa Zanzibar baada ya Mapinduzi.

Pamoja na kuwasilisha hoja zenye ushahidi kuwa Muungano wa Tanzania uliasisiwa na Watanzania wenyewe, Sura ya Tatu imenukuu taarifa ya Shirika la Ujasusi la Marekani (CIA) ya tarehe 02 Desemba, 1968 ikionesha wazi kuwa shirika hilo halikuwa na taarifa zozote mapema kuhusu Muungano bali tetesi za kibalazi kuhusu hali tete ya kisiasa Zanzibar baada ya Sultani kupewa “uhuru” na Waingereza.

4. Madai kwamba Muungano wa Tanzania uliamuliwa na Nyerere na Karume peke yao ili kulinda maslahi tofauti waliyokuwa nayo viongozi hao: Nyerere na ulinzi/usalama wa Tanganyika dhidi ya uongozi wa mrengo wa kushoto Zanzibar na Karume na ulinzi wa Mapinduzi ya Zanzibar dhidi ya Waarabu, hayana mashiko.

Sura za Kwanza, Pili na Tatu, zinaelezea kwa kirefu kuwa msingi wa Muungano wa Tanganyika na Zanzibar ni historia ya karne nyingi ya ushirikiano wa watu wa nchi hizi mbili, ushirikiano ambao ulirasimishwa tarehe 26 Aprili, 1964. Wageni na wasomi

wengi wanashindwa kuliona hilo, wanaishia kumwona Mwalimu Nyerere na Sheikh Karume na siyo nguvu ya umma nyuma yao iliyowapa dhamira ya kusonga mbele na kurasimisha ushirikiano wa nchi hizi mbili.

5. Yapo madai kuwa Muungano haukuungwa mkono na Wazanzibari na Watanganyika mwaka 1964 na hata baadaye. Ni madai ambayo hayana msingi kwani hayatokani na utafiti wowote ule uliofanyika Tanganyika na Zanzibar mwaka 1964. Katika Sura ya Tatu, Jaji Joseph Sinde Warioba, Waziri Mkuu na Makamu wa Pili wa Rais mstaafu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ambaye alikuwa Rais wa Umoja wa Wanafunzi wa Tanganyika waliokuwa wakisoma Chuo Kikuu cha Dar es Salaam mwaka 1964 wakati Muungano unafanyika, anakumbuka jinsi umoja wao ulivyopokea Muungano kwa nderemo na vifijo (kama ilivyokuwa kwa wananchi) na kutoa taarifa rasmi ya maandishi kupongeza hatua hiyo.

Ushuhuda wa Jaji Warioba unaungwa mkono na taarifa ya ukurasa wa mbele wa gazeti la kihafidhina la Marekani la *The New York Times*, lililochapishwa tarehe 24 Aprili, 1964 likielezea furaha ilivyokuwa imetamalaki bara na visiwani wakati taarifa za Muungano zilipotangazwa.<sup>2</sup>

6. Kwamba hakuna ushahidi kama Hati ya Makubaliano ya Muungano iliridhiwa na Baraza la Mapinduzi la Zanzibar, hivyo ni batili; uchambuzi wa kina umefanyika Sura ya Tatu kuhusu madai haya na kubainisha udhaifu mkubwa wa hoja hiyo kisheria na kimantiki.
7. Kwamba uhuru wa Zanzibar ulipatikana tarehe 10 Desemba, 1963 kutoka kwa Mwingereza; Sura ya Kwanza hadi ya Tatu zinabainisha kuwa tarehe 10 Desemba, 1963 Zanzibar haikupata uhuru kwa maana ya wazawa, wenye nchi kurejeshewa nchi yao iliyokuwa inatawaliwa na taifa la nje, kama ilivyokuwa sehemu nyingine barani Afrika (Tanganyika, Kenya, Uganda, Rwanda, Burundi, Malawi, Zambia n.k.) ambako wenye nchi walirejeshewa nchi zao kuziendesha. Kilichotokea Zanzibar ni taifa la nje, lililokuwa linaitawala Zanzibar, kuhalalishwa kuendelea kuitawala Zanzibar na Zanzibar kubadilishwa na kuwa Usultani wa Kiarabu Afrika ya Mashariki, Kusini mwa Jangwa la Sahara. Uhuru wa kweli wa Zanzibar ulipatikana kupitia Mapinduzi Matukufu ya Zanzibar ya tarehe 12 Januari, 1964 na ndoto ya Waingerereza na Waarabu

---

<sup>2</sup> Mazungumzo na Jaji Warioba, nyumbani kwake Oysterbay, Dar es Salaam saa 5, Jumatano, tar. 16/02/2020.

ya kubadilisha demografia ya Kusini mwa Jangwa la Sahara ikasambaratika.

8. Kwamba Muungano wa Tanzania siyo wa shirikisho ila wa serikali moja kama Kenya, Uganda, Zambia, Malawi n.k., na kwamba Muungano wa Tanzania kuwa shirikisho unahitaji serikali 3 na siyo 2; kitabu hiki katika Sura ya Tatu kinathibitisha kwa hoja za kisheria kuwa Muungano wa Tanzania ni wa shirikisho kama ilivyo kwa mashirikisho mengine duniani ya India, Nigeria, Ujerumani, Marekani, n.k.

Hati ya Makubaliano ya Muungano wa Tanganyika na Zanzibar ya 1964, iliendeleza na kudumisha ubunifu ulioanzishwa na Baba wa Taifa katika kujenga misingi imara ya kikatiba kwa nchi changa, ubunifu wa kuhakikisha mifumo ya kisheria ya nchi inayorithi au kupokea kutoka kwa watawala wa jana, inarekebishwa kuendana na hali halisi ya nchi husika.

9. Kwamba Waarabu wa Oman waliishi Zanzibar wakitawala kwa muda mrefu sana, wakajitenga na Oman, wakachanganyika na wenyeji na kuachana na mila, desturi na utamaduni wa Oman (ikiwamo lugha) na hivyo kuwa sehemu ya wenyeji wa Zanzibar; Sura ya Pili ya Kitabu hiki inalijadili suala hili kwa kina.

Kwa ujumla, Kitabu hiki hakikatai watu kuchanganyika na kuwa wamoja, lakini si kwa hali ya Zanzibar ambapo watawala, badala ya kujenga madaraja kuondoa matabaka na migawanyiko au badala ya kuvunja kuta kutengeneza maridhiano kijamii na kisiasa ili kujenga taifa jipya, waliendeleza njia ileile ya kikoloni ya “wagawe ili uwatawale”.

10. Kwamba msingi wa Muungano wa Tanzania ungekuwa imara zaidi kama ungetanguliwa na kura ya maoni na elimu kwa raia kabla ya Muungano. Kitabu hiki katika Sura ya Tatu kinahoji busara kwa nchi iliyonyang’anywa utu, haki na uhuru wake kupitia utumwa na ukoloni kwa karne kadhaa, inapopata uhuru baada ya mapambano ya muda mrefu, inaitisha kura ya maoni kujua kama wananchi wanataka uhuru, umoja au ushirikiano waliokuwa nao kabla ya ukoloni kuwanyang’anya uhuru wao na kuwatengenezea mipaka ya kuwatenganisha? Je, hatua ya kwanza ni “kuwaelimisha” wananchi kuhusu faida za umoja au ushirikiano waliokuwa nao wananchi kabla ya ukoloni? Kwa muktadha huo, hata kampeni ya kutokomezwa biashara ya utumwa basi ilitakiwa isifanyike bila kupata msimamo wa watumwa wenyewe kupitia kura ya maoni.



Kitabu hiki katika Sura zake kadhaa kinasisitiza kuwa msingi wa Muungano wa Tanganyika na Zanzibar ni historia ya karne nyingi ya ushirikiano wa watu wa nchi hizi mbili, ushirikiano ambao ulirasimishwa tarehe 26 Aprili, 1964.

11. Muungano ulianza na Mambo 11 tu ya Muungano lakini yakaongezwa mengine 11 kinyemela, kwa hila.

Sura ya Tatu inaongelea suala hili kwa kina na kutoa ufafanuzi mrefu kwamba nyongeza yoyote ile katika Mambo ya Muungano inatawaliwa na Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977 ambayo imeweka masharti magumu ya kuhakikisha kuwa pande zote mbili za Muungano zinarithia mabadiliko yoyote yale.

12. Mapinduzi ya Zanzibar yalisababisha mauaji ya kimbari; suala hili nalo linajadiliwa kwa kirefu katika Sura ya Kwanza ya kitabu hiki kwamba lilipotoshwa kwa lengo la kutengeneza hisia hasi kimataifa dhidi ya Mapinduzi ya Zanzibar ya 1964. Kitabu hiki kinathibitisha kuwa siyo Waarabu tu waliouawa kipindi cha Mapinduzi, na Waafrika vilevile walipoteza maisha hasa vijijini ambako matajiri walijihami kwa bunduki za kuwindia na silaha nyingine walizopewa na serikali ya Sultani.



## SURA YA KWANZA

# DHANA YA MUUNGANO, HISTORIA YA TANZANIA BARA NA TANZANIA ZANZIBAR

### MAANA NA DHAMIRA YA MUUNGANO

Muungano ni tendo la nchi kadhaa kuachia na kukabidhi mamlaka yao yote au baadhi ya mamlaka yao kwa serikali moja kuu itakayotekeleza mamlaka hayo kwa masharti mahususi ya kikatiba. Mamlaka hayo hutekelezwa na Serikali Kuu kwa niaba ya nchi husika. Aidha, nchi zilizo katika Muungano huo hazibaki na mamlaka yoyote ya mwisho au zinabaki na mamlaka ya ndani tu au ya nje kwa masharti mahususi yaliyoainishwa kikatiba.

Lengo kuu ni kuunganisha nguvu katika maeneo yote au maeneo lengwa ili kuchochea tija kiuchumi, kijamii, kisiasa, kiulinzi, kiusalama na katika ushirikiano na nchi nyingine mbalimbali duniani. Hivyo basi, msingi mkuu wa Muungano ni nchi husika kuongeza tija katika nyanja zote za maisha na maendeleo.

### AINA ZA MUUNGANO

Muungano huchukua sura na muundo wa aina mbalimbali kufuatana na malengo au matakwa ya wahusika. Uzoefu unaonesha kuwa nchi zinapodhamiria kuungana, hupendelea muundo kati ya hii mitatu: **muungano wa serikali moja au jumuishi, muungano wa shirikisho na muungano maalum.** Hata hivyo, muundo wowote ule wa muungano unaweza ukachukua baadhi ya sifa za miundo mingine ili kuendana na mazingira na mahitaji ya wadau wa muungano husika kama ilivyo kwa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

**Muungano Jumuishi**, maarufu kama muungano wa serikali moja, ni matokeo ya nchi zaidi ya moja zinapoamua kuunda mamlaka moja ya muungano yenye Serikali Kuu ambayo nchi hizo zinaikabidhi mamlaka yao yote ya mwisho ya maamuzi na utendaji kwa mujibu wa Katiba na Sheria walizozitunga. Hata hivyo, kwa kuzingatia Katiba ya nchi husika, Serikali Kuu ya **Muungano Jumuishi** inaweza ikaanzisha mamlaka za mikoza au majimbo na kukasimu sehemu ya mamlaka yake ili kusogeza uongozi na utawala karibu na wananchi, na hivyo, kurahisisha utekelezaji wa shughuli mbalimbali za maendeleo.

Nchi nyingi duniani zina mfumo wa **Muungano Jumuishi** kwani kati ya nchi 193 wanachama wa Umoja wa Mataifa, nchi 166 zina mfumo huo. Ni dhahiri kuwa huu ni mfumo unaopendwa kutokana na urahisi katika kuuendesha kwa kuwa huwa na mamlaka moja kuu yenye mtandao mmoja wa uongozi mpaka chini kupitia mfumo wa ugatuzi wa madaraka. Kwa kulinganisha na mifumo mingine, **Muungano Jumuishi** una gharama nafuu ya uendeshaji kutokana na udogo wa serikali, uchache wa viongozi na watendaji na vyombo vya serikali.

Hata hivyo, yapo malalamiko kuwa uongozi wa juu wa Serikali Kuu ambao unahodhi mamlaka yote ya mwisho, unakuwa mbali mno na wananchi. Kwa mantiki hiyo, malalamiko toka chini yanakuwa si rahisi kuufikia uongozi wa juu mapema kutokana na ukiritimba wa kiserikali. Hivyo, ni rahisi zaidi katika mfumo wa **Muungano Jumuishi** kwa nchi zisizo na uzoefu mkubwa katika uongozi wa kidemokrasia kuwa na uongozi wa kiimla usiotambua hisia za wananchi wa kawaida.

Muungano wa pili ni wa **Shirikisho** ambao sifa yake kuu ni mgawanyo mahususi wa madaraka na mamlaka kati ya Serikali Kuu ya **Shirikisho** na serikali za nchi zinazounda shirikisho. Picha kamili ya mgawanyo huo wa madaraka na mamlaka, inaainishwa bayana na Katiba ya **Shirikisho** na ni mwiko kwa mamlaka moja kuingilia utekelezaji wa mamlaka nyingine kinyume na maelekezo ya Katiba. Hivyo basi, Serikali Kuu ya **Shirikisho** na serikali za washirika, zote zina mamlaka ya mwisho kwenye maeneo yaliyoainishwa na Katiba.

Nchi kubwa nyingi duniani, kwa mfano, Urusi, Kanada, Marekani, Brazil, India, Argentina, Nigeria, Ujerumani na Mexico zina mfumo wa **Shirikisho** wenye sifa kuu ya kuondoa mkusanyiko wa madaraka mikononi mwa wachache na kuyagawa madaraka kwa urari maeneo mbalimbali ya uongozi na mamlaka, hivyo, kuwasogeza karibu wananchi katika uongozi wa shirikisho na kupanua ushiriki wao. Kwa maneno mengine, mfumo wa shirikisho hautoi fursa kiurahisi kwa uongozi wa kiimla kujijenga.

Muungano mwingine ni wa **Shirikisho Maalum** ambapo nchi washirika zikiwa na mamlaka yao kamili, zinaungana kwa masuala kadhaa mahususi yanayohusiana na vyombo na nchi nyingine, huku chombo kikuu cha **Shirikisho Maalum** kikitegemea zaidi (katika maamuzi yake ya mwisho) maridhiano au muafaka wa washirika. Umoja wa Ulaya unakaribia kukidhi sifa zote za **Shirikisho Maalum**. Jumuiya ya Afrika ya Mashariki itakapofikia ngazi ya kuwa na maamuzi ya pamoja na utaratibu wa pamoja katika kujadiliana na kufikia maamuzi na vyombo vya nje, nayo itaingia hatua ya **Shirikisho Maalum**.

Muungano wa **Shirikisho Maalum** ni ushirikiano ulio dhaifu baina ya mataifa huru ambayo huwa yameunganishwa na mikataba baina yao. Msingi mkubwa wa uendeshaji wa muungano wa aina hii huwa ni mikataba ya kimataifa ambapo nchi washirika zinabaki na hadhi ya kuwa dola huru<sup>1</sup>. Udhaifu wa aina hii ya muungano unatokana na ukweli kwamba mkataba baina ya nchi husika hauzifungi pande zilizo katika mkataba huo kutekeleza makubaliano yaliyofikiwa, hivyo, kupingana na kanuni ya msingi ya mikataba ya kimataifa kuzifunga pande zilizo katika mkataba husika.

Katika muungano huu, washirika huweza kujitoa wakati wowote wanapoamua na bila ya kuwepo kwa vikwazo vya kikatiba. Kujitoa kwa washirika huathiri hata mwingiliano wa kiuchumi, kijamii na kisiasa uliopo baina ya nchi husika. Kimsingi, ni muungano dhaifu.

Kabla ya karne ya 19 muungano wa aina hii ulimaanisha uwepo wa mamlaka dhaifu ya kisiasa juu ya mataifa yaliyokubali kushirikiana. Mifano ya muungano wa aina hii ni pamoja na uliokuwa muungano wa Uswisi kabla ya mwaka 1848; muungano wa Marekani kabla ya mwaka 1787, muungano wa majimbo ya Uholanzi kabla ya mwaka 1579 na himaya ya Kijerumani kati ya mwaka 1871 – 1918. Muungano huo katika nchi hizo haukuwa na nguvu ya kisheria kwa washirika wake bali kazi yake ilikuwa kupambana na changamoto zilizowakabili.

**Shirikisho Maalum** au muungano wa mkataba kama wengine wanavyopenda kuita, ni rahisi kwa muundo wake ulivyo, kusababisha migogoro na uhasama baina ya nchi washirika kiasi cha kuathiri usalama, uchumi na mustakabali wa nchi wanachama na muungano wenyewe.<sup>2</sup>

<sup>1</sup> Ramesh, D., *Geography and Federalism*, in Annals Association of American Geographers, vol. 61, No. 1 (Mar., 1971), pp. 97-115.

<sup>2</sup> Angalia: Hamilton, A., *The Federalist*, No.22, 135-41, 143-46, 14<sup>th</sup> December, 1787

## CHANGAMOTO KUFIKIA MUUNGANO

Historia ya dunia imesheheni mifano kadhaa ya nchi mbalimbali zikisukumwa na sababu za kihistoria, kijiografia, kiulinzi, kiusalama, kijamii, kiuchumi na kisiasa, zikiwa na dhamira ya kuungana hasa kwa mifumo ya Muungano Jumuishi na Shirikisho ili kuunda himaya kubwa zaidi. Pamoja na faida bayana za kuungana kwa nchi husika, yaani kuunganisha nguvu kwa lengo la kuchochea tija katika nyanja zote za maendeleo, jitihada mbalimbali za kuunganisha nchi zimekuwa zikikwama katika hatua za awali au baada ya kipindi kirefu cha kusuasua.

### Vita vya Marekani (1861–1865)

Mataifa kongwe duniani yenye mifumo ya muungano, yalifikia hatua hiyo kwa mapanga na mitutu ya bunduki hadi mifumo hiyo ikatengamaa. Mfano ni **Shirikisho** la Marekani lenye nchi 50<sup>3</sup>, lilitengamaa baada ya vita vya miaka minne vya wenyewe kwa wenyewe kati ya mwaka 1861 na mwaka 1865 vilivyopoteza maisha ya Wamarekani zaidi ya 800,000. Vita vilianza baada ya majimbo 13, mengi ya kusini, kujitoa kwenye **Shirikisho** la Marekani na kuanzisha **Shirikisho Maalum** lililojiita *Confederate States of America* kutokana na kutoelewana kuhusu suala la watumwa na hatima yao, kodi na uhuru zaidi wa maamuzi kwa washirika katika **Shirikisho**. Waasi walizidiwa nguvu, wakasalimu amri na kurejeshwa kwenye **Shirikisho**.

### Vita vya Ireland ya Kaskazini (1968–1998)

**Muungano Jumuishi** wa Ufalme wa Uingereza na Scotland, Wales na Ireland ya Kaskazini au *United Kingdom*, ambao chini ya ugatuzi wa madaraka, nchi washirika zina kiasi fulani cha madaraka ya ndani, uliingia matatizo makubwa mwaka 1968 wakati Wakatoliki wa Ireland ya Kaskazini walipoanzisha mapambano ya silaha ili kujitoa kwenye muungano huo na kutaka kuwa sehemu ya Jamhuri ya Ireland.

Ili kuyaelewa vizuri mazingira ya vita hivi vya wenyewe kwa wenyewe kwenye taifa kubwa na kongwe kama Uingereza, hatuna budi kurejea kwenye historia kwamba kisiwa cha Ireland kilikuwa koloni la Waingereza kuanzia karne ya 13. Ifahamike kwamba sehemu kubwa ya Waingereza ni Waprotestanti wa Kianglikana lakini wakaitawala Ireland yenye idadi kubwa ya Wakatoliki na hivyo kutengeneza mpasuko mkubwa wa kidini.

<sup>3</sup> Kipindi hicho Marekani ilikuwa shirikisho lenye jumla ya nchi 34.

Baada ya miaka mingi ya kudai uhuru, Uingereza ikakigawa kisiwa hicho kwa msingi wa kulinda maslahi ya Waprotestanti waliokusanyika zaidi Kaskazini Mashariki mwa kisiwa hicho. Hivyo, harakati za kudai uhuru zilipopamba moto miaka ya 1920, Ireland ya Kaskazini ikatangaza kuendelea kuwa sehemu ya ufalme wa Uingereza, hivyo, kuzua mgogoro mpya kati ya Waprotestanti na Wakatoliki katika jimbo hilo, Waprotestanti wakitaka nchi hiyo ibakie kuwa sehemu ya muungano na Wakatoliki wakiukataa muungano huo na kutaka jimbo hilo lirejee kuwa sehemu ya Jamhuri ya Ireland.

Mwaka 1949, kisiwa hicho bila sehemu yake ya kaskazini mashariki (yaani Ireland ya Kaskazini) kikajitangaza kuwa Jamhuri ya Ireland na kujitoa kwenye Jumuiya ya Madola. Uhasama mkubwa ukapamba moto kati ya makundi hayo mawili ndani ya Ireland ya Kaskazini na kusababisha kuanza kwa mapambano ya silaha mwaka 1969.

Vita hivyo vilidumu kwa miaka 30 (1968 – 1998) na kugharimu maisha ya watu 3,600 na wengine 30,000 kujeruhiwa kabla ya kupata muafaka ambao umeipa Ireland ya Kaskazini madaraka ya kujiongoza katika maeneo kadhaa na mfumo wa uongozi shirikishi. Jimbo hilo lina bunge lake lenye mamlaka kwenye maeneo yaliyoainishwa na ambayo Bunge la Uingereza haliyagusi. Vilevile, yapo mamlaka ya utendaji ya pamoja ambapo kuna Waziri Kiongozi na Naibu wake wenye mamlaka sawa na wanatoka makundi makubwa mawili yaliyohasimiana kwa miaka mingi jimboni humo.

## Harakati za Catalonia Kujitenga na Hispania

Muungano wa Hispania ulifanyika mwaka 1474 lakini kuanzia mwaka 2012 ulipata msukosuko mkubwa wa kisiasa baada ya jimbo la Catalonia kutaka kujitenga kutoka kwenye muungano huo wa karne nyingi. Ili kuelewa vizuri kiini cha msukosuko huo wa kisiasa unaotokea katika jimbo la Catalonia, ni vyema kuelezea kwa kifupi historia ya muungano huo.

Miaka ya nyuma takriban karne 5 zilizopita, Catalonia ilikuwa sehemu ya shirikisho maalum la falme kadhaa zilizotawala Hispania ya Mashariki, eneo la *Mediterranean* na kusini mwa Italia. Moja ya falme hizo ilikuwa Falme ya Aragon iliyokuwa na majimbo kadhaa ikiwamo Catalonia, jimbo kubwa lililokuwa na mafanikio makubwa katika biashara, utamaduni, sanaa na ushawishi mkubwa katika siasa, na jiji lake lililokuwa limejengeka vizuri la Barcelona. Pamoja na mafanikio hayo, ufalme ulikuwa upande wa jimbo jirani la Aragon lililobeba jina la falme hiyo.

Mwaka 1469 Mfalme wa Aragon, Ferdinand II akamuoa Malkia Isabella I wa jimbo kubwa zaidi la Castile, ndoa ambayo ilileta muungano wa Castile na Aragon, na Catalonia ikamezwa humohumo mwaka 1474. Kutokana na ukubwa wa Castile kieneo na wingi wa watu wake (karibu mara 5 ya watu wa Aragon nzima), muungano huo wa kifalme uliendeshwa zaidi na maamuzi kutoka Castile na mwaka 1561 makao makuu ya ufalme yakahamishiwa Madrid.

Haukupita muda mrefu, mwaka 1640 Catalonia iliasi dhidi ya maamuzi kutoka Castile. Uasi huo ukazimwa na hatua mbalimbali zikachukuliwa kuibana Catalonia ikiwa ni pamoja na kuzuia kuenea kwa lugha ya Catalan na maamuzi yote muhimu kuhusu Catalonia kufanyikia Madrid. Hivyo basi, chanzo cha misukosuko ya kisiasa tunayoiona ikizidi kuanzia mwaka 2012 nchini Hispania, ni pamoja na msingi wa muungano wa nchi hiyo kongwe kuwa ndoa ya watu wawili.

Mifano hii mitatu ya muungano wa Marekani, Ireland ya Kaskazini na Catalonia ni kielelezo tosha kuwa kuunganisha nchi ni kazi ngumu na yenye mitihani mingi. Kwa maneno mengine, muungano wa aina yoyote haujengeki bila utashi na ridhaa ya wenye nchi, bila kuzingatia maslahi ya muda mfupi na mrefu ya pande zote husika, bila mgawanyo wa madaraka kwa uwiano na bila mfumo wa kupokea, kujadili na kutatua changamoto zinapotokea. Mazingira wezeshi ya aina hii yakikosekana, muungano husambaratika na uokozi wake una gharama kubwa kwa mali na watu.

## Jitihada za Kuungana Barani Afrika

Tunayo mifano mingi barani Afrika ya majaribio kadhaa ya muungano kushindikana kutokana na sababu hizohizo zilizoainishwa hapo juu ikiwamo kukosekana kwa mazingira wezeshi. Mifano michache ifuatayo inajieleza yenyewe:

1. **Shirikisho la Ethiopia na Eritrea:** Lilifanikishwa mwaka 1952 kwa msaada wa Umoja wa Mataifa baada ya Italia kusitisha rasmi utawala wake wa kikoloni nchini Eritrea. Shirikisho hilo lilivunjika mwaka 1962 kufuatia matukio kadhaa ya ukiukwaji wa masharti ya shirikisho na hivyo kuzua harakati za kudai uhuru Eritrea.
2. **Shirikisho la Mali:** Lilihusisha nchi za Senegal na Mali kipindi cha ukoloni wa Ufaransa. Shirikisho hilo lilisambaratika mwaka 1960, miezi miwili tu baada ya nchi hizo kupata uhuru. Mivutano ya kisiasa kuhusu itikadi, misingi ya shirikisho, mwelekeo wa taifa hilo huru na jipya na changamoto iliyojitokeza ya Ufaransa kuendelea





*Viongozi wawili wa Afrika baada ya Uhuru (kushoto Mwalimu Julius Nyerere wa Tanzania na kulia Kwame Nkrumah wa Ghana) waliobeba ndoto ya Muungano wa nchi za Afrika*

kuwa na kituo cha kijeshi nchini humo, vilichangia kuua muungano wa nchi hizo mbili.

3. **Shirikisho la Rhodesia (Zimbabwe na Zambia) na Nyasaland (Malawi):** Lilisambaratika miezi michache tu kabla ya uhuru wa Malawi na Zambia (mwaka 1964) kutokana na shirikisho hilo kukosa baraka za wananchi na hivyo kuasisiwa na kulelewa na serikali ya kikoloni ya Uingereza kwa maslahi finyu ya walowezi wachache.

4. **Shirikisho la Senegambia:** Lilianza rasmi tarehe 1 Februari, 1982 likizihusisha nchi za Senegal na Gambia. Shirikisho hilo lililenga kuunganisha vyombo vya ulinzi na usalama, kuwa na uchumi na sarafu ya pamoja na sera ya pamoja ya mambo ya nje, na kuunda mihimili ya shirikisho kwa maana ya Bunge, Ofisi ya Rais na Mahakama.

Pamoja na utekelezaji wa masuala hayo kuanza Julai, 1982 Gambia yenye eneo dogo la kilomita za mraba 10,689 na watu takriban milioni 1.5 ukilinganisha na kilomita za mraba 196,722 za Senegal na watu takriban milioni 16.6 iliingiwa na wasiwasi kuhusu hatima ya mamlaka na uhuru wake ndani ya shirikisho mpaka likavunjika mwaka 1989.

5. **Muungano Maalum wa Ghana, Guinea na Mali:** Ulianzishwa mwaka 1958 ukihusisha nchi tatu kwanza (Ghana, Guinea na Mali) na kuacha milango wazi kwa nchi zote huru za Afrika kujiunga bila kujali mgawanyiko wa lugha uliotengenezwa na wakoloni wa Kiingereza, Kifaransa au Kireno. Muungano huo uliitwa Muungano wa Nchi Huru za Afrika na ulidhamiria kuwa na sarafu moja na sera moja ya mambo ya nje kwa kuanzia.

Ni bahati mbaya kwamba kampeni hii ya muungano ilikuja kipindi ambacho kilikuwa na mgawanyiko wa mawazo miongoni mwa wakuu wa nchi kuhusu umoja wa Afrika, baadhi wakitaka nchi huru zote za Afrika ziungane na kuunda Shirikisho la Afrika. Kundi hili la viongozi wa Afrika lililojulikana kama Kundi la Casablanca kutokana na kikao chake kufanyikia Casablanca, Morocco mwezi Januari 1961, liliongozwa na nchi za Algeria, Misri, Ghana, Guinea, Libya, Mali na Morocco.

Viongozi wengine walitaka shirikisho au muungano wa nchi huru za Afrika ujengeke hatua kwa hatua kuanzia ushirikiano/mtangamano wa kikanda, ndipo hatua ya kuunda Shirikisho la Afrika ifikiwe. Kundi hili la viongozi lilijulikana kama Kundi la Monrovia kutokana na kikao chake kufanyika Monrovia, Liberia mwezi Mei, 1961 likiwa na nchi nyingi zaidi: Ethiopia, Liberia, Nigeria, Sierra Leone, Somalia, Togo, Tunisia, Congo (Kinshasa), Tanganyika na nchi 12 zilizojulikana kama Kundi la Brazzaville<sup>4</sup>.

<sup>4</sup> Kundi hili lilikuwa na nchi zilizokuwa chini ya utawala wa kikoloni wa Ufaransa: Cameroon, Congo Brazzaville, Ivory Coast, Dahomey (Benin), Gabon, Upper Volta (Burkina Faso), Madagascar, Mauritania, Niger, Central African Republic, Senegal na Chad. Kundi hili lilishaweka msimamo wake wa kihafidhina mapema mwezi Desemba, 1960 kuendeleza uhusiano wa karibu na Ufaransa kwenye mkutano wa viongozi wake mjini Brazzaville, Congo.

Kutokana na mgawanyiko huo mkubwa ambao ulileta mvutano kati ya vinara wa makundi haya, hatua ya kuunganisha nchi huru za Afrika kwenye **Muungano Maalum wa Ghana, Guinea na Mali** uligonga mwamba. Muungano huo maalum ukasambaratika mwaka 1963. Hata hivyo, makundi haya mawili yakaungana kuunda chombo kingine kikubwa chenye sura ya muungano maalum tarehe 25 Mei, 1963 na kuitwa **Umoja wa Nchi Huru za Afrika**.

6. **Muungano wa Misri na Syria:** Ulianza rasmi mwaka 1958 na kuvunjika mwaka 1971 ukijulikana kama “Jamhuri ya Muungano wa Waarabu”. Muungano huo ambao ulihusisha nchi mbili tu: Jamhuri ya Kiarabu ya Misri na Jamhuri ya Syria, ulizua manung’uniko mengi miongoni mwa Wasyria wakidai kupoteza uhuru wao na Misri haikuonekana kujali. Matokeo yake, miaka mitatu ndani ya muungano huo, Serikali ya Misri ikapinduliwa na jeshi. Muungano ulipoteza nguvu, ukadhoofika polepole na hatimaye mwaka 1971 ukavunjika kutokana na manung’uniko ya mshirika mmoja kutoridhika na mgawanyo wa madaraka, manung’uniko ambayo yalikosa sikio katika muungano huo.

## MISINGI YA MUUNGANO IMARA

Mifano yote tisa iliyojadiliwa hapo juu inatosha kusesitiza kuwa jukumu la kuunganisha nchi si jepesi na halina njia ya mkato hasa kwa jamii zilizokuwa hazina misingi ya pamoja ya kihistoria, kiutamaduni, kijiografia na kimatarajio. Hata pale ambapo misingi ya kijiografia na kihistoria ipo, kama ilivyokuwa kwa baadhi ya mashirikisho yaliyoelezwa, utangamano hushindikana kutokana na michakato husika kushindwa kujinasibisha na maslahi na hamasa ya wananchi wa pande zote katika kipindi husika.

Mathalani, miaka ya 1950 na 1960 ilikuwa ya vuguvugu la ukombozi barani Afrika, ukombozi dhidi ya utumwa na ukoloni na madhila yake yote. Hiyo ndiyo iliyokuwa ajenda kuu ya kisiasa barani Afrika kipindi hicho. Hivyo basi, harakati zote za kuunganisha nchi zetu kipindi hicho na baadaye, zilizimwa na wadau wakuu wa mtangamano, wananchi, katika muktadha huo wa uhuru, uhuru dhidi ya utumwa na ukoloni na madhila yake yote.

Mashirikisho ya Ethiopia na Eritrea, Mali, Senegambia, Rhodesia na Nyasaland hayakudumu kutokana na maudhui yake kushindwa kuakisi matarajio ya uhuru wa wananchi. Wananchi wa Eritrea walitarajia makubwa zaidi baada ya utawala wa kikoloni wa Mwitulia kumalizika, walitarajia uhuru zaidi, fursa zaidi, ustawi zaidi chini ya Shirikisho,

mambo ambayo hawakuyapata wala kuyaona hivyo, wakalikataa shirikisho hilo.

Wananchi ndani ya Shirikisho la Mali waliuona muungano wao kuwa mwendelezo wa ukoloni wa Mfaransa kinyume na azma yao kuu ya uhuru, hasa baada ya majeshi ya Ufaransa kukubaliwa kubaki kwenye ardhi ya taifa hilo jipya na huru. Hivyo, shirikisho la aina hiyo kwao halikuwa na faida, wakalikataa. Vivyo hivyo, wananchi ndani ya Shirikisho la Rhodesia na Nyasaland waliuona muungano wa nchi zao tatu kuwa mwendelezo tu wa kulinda maslahi ya kikoloni ya Wazungu walowezi wachache kuendelea kutawala njia kuu za kiuchumi, hivyo, haukuwa na tija kwao, wakaukataa.

Shirikisho la Senegambia na Muungano wa Misri na Syria, ni mifano ya muungano uliokosa urari wa madaraka upande wa wahusika, hivyo, Syria na Gambia waliojisiikia kumezwa huku wakijiona, wakavuruga muungano. Muungano wa Hispania na Muungano Maalum wa Ghana, Guinea na Mali, ni mifano ya muungano ulioshushwa kutoka juu kuja chini na kutarajia ufanye kazi. Pamoja na nguvu nyingi kutumika katika historia kuzima “uasi” wa Catalonia, msingi wa jimbo hilo kuingizwa kwenye muungano ulikuwa dhaifu sana - ndoa ya mfalme wao!

Vivyo hivyo, Muungano Maalum wa Ghana, Guinea na Mali uliotegemewa kuungwa mkono na nchi nyingine za Afrika, ulikuwa na msingi dhaifu kwani uliamuliwa na Kwame Nkrumah (Ghana), Ahmed Sekou Toure (Guinea) na Modibo Keita (Mali) peke yao bila maridhiano na viongozi wenzao wa Afrika na bila uhamasishaji wowote wa watu wao wenyewe.

Hivyo, misingi mikuu ya muungano imara (kuendana na uzoefu wa Muungano wa Tanzania) ni kama ifuatavyo:

- Kuwapo kwa mazingira wezeshi au rafiki, hii ni kwa maana ya ujirani na ukaribu wa wanamuungano au wanashirikisho kijiografia; utambulisho wao kufanana au kushabihiana; kuwa na mapito ya kihistoria ya pamoja; na kuwa na utashi na matarajio yanayofanana ya wadau wakuu wa muungano au shirikisho, yaani wananchi;
- Misimamo, kauli na matendo ya viongozi kushabihiana na utashi na matarajio ya wananchi juu ya muungano au shirikisho na kuyaishi matarajio hayo kisheria na kikatiba;
- Uwiano katika mgawanyo wa madaraka na katika faida za muungano au shirikisho kwa wanamuungano au wanashirikisho wote; na
- Utaratibu mahususi wa kupokea changamoto au hoja (za muungano au shirikisho) na njia rasmi za utatuzi wake.

# HISTORIA YA TANZANIA BARA NA TANZANIA ZANZIBAR

## Tanzania Bara

Tanzania Bara ambayo hadi muungano wake na Tanzania Zanzibar mwaka 1964 ilijulikana kama Tanganyika<sup>5</sup> ni sehemu ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ambayo kwa upande wa kaskazini inapakana na nchi za Kenya na Uganda na upande wa kusini na Msumbiji, Malawi na Zambia. Magharibi inapakana na Rwanda, Burundi na Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo (DRC) na mashariki ipo Bahari ya Hindi na ukanda wa pwani wenye urefu wa kilomita 1,424. Ina maziwa makuu matatu ambayo yanatumika kwa uvuvi, uchukuzi, mahitaji ya kila siku ya binadamu na kilimo kwa ushirikiano na majirani zake ambayo ni ziwa Victoria (Kenya na Uganda), ziwa Tanganyika (Burundi, DRC na Zambia) na ziwa Nyasa (Malawi).

Tanzania Bara ina ukubwa wa kilomita za mraba 945,000 na kwa mujibu wa taarifa ya Ofisi ya Taifa ya Takwimu (NBS) kwa mwaka 2020, Tanzania Bara ilikadiriwa kuwa na idadi ya watu 55,966,030. Inajivunia kuwa na mlima Kilimanjaro, mlima mrefu kupita yote duniani uliosimama peke yake wenye urefu wa mita 5,895 na hifadhi maarufu za wanyama duniani kama vile Serengeti, Ngorongoro, Tarangire, Ruaha na Gombe ambayo ni maarufu kwa sokwe mtu. Aidha, ina madini mbalimbali hususan Tanzanite inayopatikana Tanzania pekee.

Pia ki-akiolojia, Tanzania Bara inatambulika duniani kote kuwa ni chimbuko la binadamu kufuatia ugunduzi wa mabaki ya binadamu wa kale uliofanyika mwaka 1959. Binadamu huyo wa kale alikuwa na umri wa miaka milioni 1.75 ugunduzi ulipofanyika<sup>6</sup>. Pia, Tanzania Bara inajulikana duniani kutokana na kugunduliwa kwa masalia ya mnyama wa kale mkubwa aitwaye dinosoria. Wanasayansi wamekadiria kwamba dinosoria huyo aliyetoweka duniani miaka milioni 65 iliyopita na ambaye masalia yake yaligunduliwa mwaka 1909 katika eneo la Tendaguru, mkoani Lindi; alikuwa na urefu wa mita 23, kimo cha mita 13 na uzito usiopungua tani 30.

---

<sup>5</sup> Ibara ya 151(1) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977 inatamka kuwa “Tanzania Bara maana yake ni eneo lote la Jamhuri ya Muungano ambalo zamani lilikuwa eneo la Jamhuri ya Tanganyika”.

<sup>6</sup> Ni eneo la Olduvai Gorge lililoko kwenye kreta ya Ngorongoro, Mkoa wa Manyara.

Pamoja na Tanzania Bara kuwa na makabila zaidi ya 120 yenye lugha na lahaja tofauti, kila Mtanzania Bara anatumia lugha ya Kiswahili kwa mawasiliano.

## Historia Fupi ya Tanzania Bara

### *Maisha na Uchumi kabla ya Wageni*

Kabla ya ujio wa wakoloni, jamii nyingi za Tanganyika zilitegemea zaidi kilimo cha mazao katika kujikimu. Shughuli nyingine za kiuchumi zilikuwa uvuvi, ufugaji, urinaji wa asali maporini, uwindaji na uvunaji madini kama makaa ya mawe, chokaa na chumvi. Biashara ya kubadilishana bidhaa ilishamiri. Watu wa jamii mbalimbali walibadilishana mazao ya kilimo, uvuvi, ufugaji na uwindaji na zana tofauti kutokana na miti, chuma, udongo, nyasi na majani.

Kuanzia karne ya 17, baadhi ya watu katika jamii kadhaa, kwa mfano, jamii ya Wayao na Wanyamwezi, walianza kushiriki katika biashara ya masafa marefu. Hatimaye, biashara hiyo ilipanuka na kufika mwambao wa Bahari ya Hindi, na hivyo, kuunganisha jamii za pwani na bara. Bidhaa muhimu zilizokuwa zikiuzwa na kununuliwa ni pamoja na chumvi, dhahabu, pembe za ndovu, vipusa na vyakula mbalimbali vikiwamo vya kukaushwa kama vile samaki wa maji baridi, nyama ya porini, mboga za majani na makopa.

### *Ujio wa Wapelelezi na Wamisionari kutoka Ulaya*

Mwishoni mwa karne ya kumi na tisa, watu kutoka bara la Ulaya walikuja Tanganyika katika makundi makubwa mawili. Kundi la kwanza lilikuwa la wapelelezi ambao walikuja kudadisi na kupeleleza mazingira ya Bara la Afrika na maliasili zilizomo. Taarifa zilizokusanywa na kupelekwa Ulaya na wapelelezi hao ndizo zilizoshawishi mataifa ya Ulaya kuanzisha makoloni barani Afrika. Kundi la pili lilikuwa la Wamisionari wa Kikristo, ambao walikuja kwa lengo kuu la kueneza dini na kuweka misingi ya uchumi wa kutumia fedha. Wamisionari wa kwanza kufika Tanganyika walikuwa Wakatoliki kutoka Ufaransa ambao walifikia Zanzibar kabla ya kuhamia bara mwaka 1864. Kundi hilo lilifuatiwa na makundi mengine kutoka mataifa ya Ulaya.

Pamoja na kueneza dini ya Kikristo, Wamisionari pia walitoa huduma mbalimbali za kijamii, zikiwamo elimu na afya, na kushiriki katika kupiga vita biashara ya utumwa. Kwanza walihubiri dini na kuanzisha vituo ambako waliwafundisha watumwa waliokombolewa stadi za kazi, na baadaye walijiingiza ndani ya jamii mbalimbali za pwani na bara na kuendelea kufanya kazi hizo. Wamisionari wa kwanza walitoa huduma

za elimu na ufundi hata kwa Waafrika waliokataa kupokea imani ya Kikristo, ingawa huduma hizo zilikuwa za msingi tu na hazikuwafikia watu wengi.

### *Kutawaliwa kwa Tanzania Bara na Mwitikio wa Wenye-Nchi*

Wapelelezi wakiwamo David Livingstone wa Uingereza na Karl Peters wa Ujerumani waliwarubuni viongozi wa Kiafrika na kutwaa maeneo makubwa ya ardhi kwa kutumia mikataba ya ulaghai iliyolenga kuvuna rasilimali za Bara la Afrika bure. Vitendo hivyo vya kupora ardhi na rasilimali nyingine za Afrika, vikafungua milango ya Afrika kwa mataifa ya Ulaya na hatimaye Afrika ikagawanywa vipandevipande na kutawaliwa.

Katika mgawanyo huo, mipaka ya Tanzania Bara ya sasa inatokana na maamuzi ya kiimla ya nchi za kibeberu zilizokutana Berlin mwaka 1884/85 kugawana na kujimilikisha maeneo ya Bara la Afrika kwa lengo la kuimarisha uchumi wao wa viwanda kwa kutumia rasilimali lukuki za Afrika.

Katika zoezi hilo, Wajerumani walijimilikisha *Deutsch Ost-Afrika* ikiwa na nchi tatu zilizotambulika baadaye kama Tanganyika, Rwanda, Burundi na sehemu ndogo ya Msumbiji iitwayo Kionga-Dreieck au Kionga-Triangle. Eneo hili la Afrika ikiwamo Tanganyika, lilitawaliwa na Wajerumani kuanzia mwaka 1884 mpaka mwishoni mwa Vita Kuu ya Kwanza ya Dunia iliyoanza mwaka 1914 na kumalizika mwaka 1918.

Wajerumani hawakupata mteremko katika kutawala nchi, bali upinzani mkali kutoka kwa wakazi mbalimbali wa Tanganyika wakiwamo Waarabu wahamiaji waliouona utawala wa Kijerumani kuwa tishio kwa maendeleo ya biashara zao.

### *Vita vya Abushiri (Pangani) na wana Heri (Saadani) 1888*

Al Bashir ibn Salim al-Harhi, maarufu kama Abushiri, akisaidiwa na wafanyabiashara wenzake wa Kiarabu na watumwa aliokuwa nao Pangani, aliongoza mashambulizi kwenye vituo mbalimbali vya Wajerumani, pwani ya Afrika Mashariki mwaka 1888 na kuviteka. Pia, katika vita hivyo, Abushiri aliungwa mkono na Sultani wa Saadani, Bwana Heri bin Juma aliyekuwa na nguvu kubwa ya kabila lake la Wazigua nyuma yake.

Ilimlazimu kiongozi wa Ujerumani Otto von Bismarck amtume *Deutsch Ost-Afrika* afisa wake mwandamizi wa kijeshi, Hermann Wissmann, kwenda kuunda kikosi cha kwanza cha jeshi la Kijerumani,

Schutztruppe, kilichosaidiwa na jeshi la majini la nchi hiyo kurejesha maeneo yote mwishoni mwa mwaka 1889 yaliyotekwa na Abushiri na wenzake.

Wissmann vilevile akaishambulia Saadani na kumlazimu Bwana Heri akimbilie msituni na kuendesha vita dhidi ya Wajerumani kutokea huko. Hatimaye, Abushiri alikamatwa na kunyongwa. Aidha, Bwana Heri baada ya mashambulizi mfululizo ya Wajerumani mapema mwaka 1890, alijisalimisha wakamdhibiti.

### *Wayao Wakataa Kutawaliwa na Mjerumani 1890*

Ngome ya Wajerumani Kilwa ilishambuliwa mwaka 1890 na kundi kubwa la wenyeji wakiongozwa na Hassan bin Omar. Kiongozi huyo wa Wayao aliyejulikana zaidi kwa jina la Makunganya, alikamatwa mwezi Mei, 1890 na kunyongwa hadharani. Kiongozi mwingine wa Wayao, Chifu Machemba wa Tunduru naye mwaka 1890 aliugomea utawala wa kigeni na ikawachukua Wajerumani miaka tisa kujadiliana naye kuleta amani eneo hilo la kusini mwa Tanganyika.

### *Vita vya Isike dhidi ya Wajerumani 1889-1893*

Unyanyembe vilevile ilikuwa siyo salama kwa Wajerumani. Mtemi Isike Mwana Kiyungi alilikataa katakata wazo la kuiweka himaya yake ya Unyanyembe chini ya utawala wa Wazungu. Akaimarisha ngome yake na kuamua kupigana ili kuilinda himaya yake.

Kwa miaka minne kuanzia mwaka 1889, Isike alipambana kwa ujasiri na vikosi mbalimbali vya Wajerumani na kuvirudisha nyuma. Ikabidi Wajerumani waagize vifaa bora zaidi vya kivita kupambana na shujaa huyo. Ndipo mwaka 1893 Wajerumani wakiwa na vifaa bora vya kivita wakaishambulia ngome ya Isike na kufanikiwa kuiteka na kumkamata Mtemi Isike. Isike alipoona tayari amezingirwa, akawaponyoka askari na kujinyonga kuchelea fedheha ya kudhalilishwa kama mfungwa mbele ya watu wake.

### *Vita vya Mkwawa na Wajerumani 1891-1898*

Kiongozi wa Wahehe, Chifu Mkwavinyika Munyigumba Mwamuyinga aliyejulikana kwa kifupi kama Chifu Mkwawa, naye hakujisalimisha kwa Wajerumani walipoingia nchini. Wajerumani walitaka machifu au watemi wote katika *Deutsch Ost-Afrika* wajisalimishwa kwao bila masharti.

Kikosi chao cha jeshi la Kijerumani kikiongozwa na kamanda Emil von Zelewsky kilitumwa Kalenga kumdhibiti Mkwawa na watu wake



ili watambue kwamba *Deutsch Ost-Afrika* yote ikiwamo Kalenga na maeneo yote ya Wahehe, ilikuwa chini ya utawala na mamlaka ya Wajerumani. Kikosi hicho, bila kutarajia kikakutana na nguvu kubwa ya jeshi la Mkwawa la askari zaidi ya 3,000 katika eneo la Lugalo tarehe 16 Agosti, 1891 na kupata kipigo kikali.

Maafisa kumi wa Kijerumani akiwamo Zelewsky na askari 300 wa jeshi hilo la kigeni, waliuawa Lugalo, bunduki 300 na bunduki kubwa tatu za kufyatulia mizinga zikatekwa. Maafisa na askari wachache wa kikosi hicho cha jeshi la Kijerumani, walifanikiwa kurudi nyuma na kuweza kujitetea kwa kurusha risasi nyingi zilizoua watu takriban 200 upande wa Mkwawa<sup>7</sup>.

Baada ya mapambano hayo Mkwawa aliweka wazi msimamo wake kuwa yeye na watu wake walikuwa wanataka amani na kilichotokea Agosti 16, 1891 kilikuwa kitendo cha kujitetea kwa lengo la kujilinda.

Kipigo hicho cha Agosti, 1891 kiliwafanya Wajerumani watafakari kwa kina hatua za kuchukua dhidi ya Mkwawa. Wajerumani wakamtumia Mkwawa ujumbe uliomtaka: atambue utawala wa Wajerumani *Deutsch Ost-Afrika*; alipe fidia kwa hasara yote waliyoipata Wajerumani kwenye mapigano yaliyotokea Lugalo Agosti, 1891; arejeshe kwa Wajerumani bunduki zote 300 na nyingine tatu za kufyatulia mizinga alizoteka; na afungulie njia zote za mawasiliano na biashara zilizokuwa zinapita kwenye himaya yake.

Mkwawa akayakataa masharti yote manne hivyo, mwezi Agosti, 1894 kikosi kikubwa cha jeshi la Kijerumani kikiongozwa na Gavana mpya wa Ujerumani, Friedrich von Schele, kilielekea Uheheni kupambana na shujaa Mkwawa. Tarehe 30 Oktoba, 1894 kikosi hicho kikaishambulia ngome ya Mkwawa ya Kalenga kwa mizinga iliyoangukia ndani ya ngome na kuuu watu. Mashambulizi hayo yaliruhusu askari wa Kijerumani kupanda ukuta na kuingia Kalenga kuwashambulia askari wa Mkwawa na kumsaka Mkwawa mwenyewe, lakini Mkwawa alishatorokea msituni na askari wake zaidi ya 2,000.

Kutoka hapo maisha ya Mkwawa yalikuwa ya kutafutana na kushambuliana na Wajerumani misituni na hatimaye tarehe 19 Julai, 1898 maadui walimsogelea sana, akaamua kujiua kwa kujipiga risasi kuepuka fedheha ya kukamatwa na kuwekwa chini ya ulinzi na wakoloni. Kwa jinsi Mkwawa alivyowapa taabu, Wajerumani wakaamua

<sup>7</sup> Kumbukumbu za afisa wa jeshi la Kijerumani, *Captain Tom von Prince, Gegen Araber und Wahehe: Erinnerungen aus meiner ostafrikanischen Leutnantszeit 1890-1895*, Berlin, 1914, uk. 72.

kukata kichwa chake na kukipeleka Ujerumani kwa uchunguzi na kumbukumbu ya historia.

Wajerumani waliposhindwa kwenye Vita Kuu ya Kwanza ya Dunia mwaka 1918, walilazimika chini ya Ibara ya 246 ya Mkataba wa Versailles wa 1919 wa kumaliza Vita ya Kwanza ya Dunia, kurejesha kwa Serikali ya Uingereza fuvu la kichwa la Mkwawa ambalo lilifikishwa Tanganyika tarehe 9 Julai, 1954.



*Chifu Mkwawa (kushoto) aliyepigana vita na Wajerumani kwa miaka saba 1891 – 1898 ambaye Wajerumani walikata kichwa chake na kukipeleka Ujerumani, fuvu la Chifu Mkwawa lilirejeshwa Tanganyika tarehe 9 Julai, 1954. Kinjengitile Ngwale (kulia) kiongozi wa Vita vya Maji Maji 1905 – 1907.*

### *Vita vya Mangi Meli na Wajerumani 1892-1893*

Uchagani nako kulikuwa uwanja wa mapambano ambapo kwa nyakati tofauti viongozi wa kimila wa Kichaga walipigana na Wajerumani kukataa kutawaliwa ingawa walisalitiana sana, na hivyo, kuwapa nguvu Wajerumani. Februari, 1891 Wajerumani waliishambulia ngome ya Mangi Sina wa Kibosho ambaye pamoja na kujitetea kishujaa, alilazimika kujisalimisha ili kuokoa maisha ya watu wake.

Pia, Mangi Meli Kiusa bin Rindi Makindara wa Moshi, alipambana na Wajerumani kwa siku mbili mfululizo mwezi Juni, 1892. Mbali na kuwashinda Wajerumani, alimuua kiongozi wao wa kijeshi von Bulow na kuwafukuza kabisa eneo hilo. Mwaka mmoja na miezi miwili baadaye, Wajerumani walirejea Moshi (mwezi Agosti, 1893) wakiwa na askari mamluki wengi na vifaa vya kisasa zaidi vya kivita kumshambulia

Mangi Meli. Katika vita hivyo, walipambana kwa siku mbili na hatimaye kumshinda shujaa huyo wa Kichaga.

Wajerumani walimpa adhabu Mangi Meli na watu wake ya kutoa vifaa na nguvu kazi kwa ujenzi wa kituo kipya cha jeshi la Wajerumani Old Moshi, akatekeleza. Pamoja na hilo, Wajerumani bado walikuwa na wasiwasi na kiongozi huyo na kuamua kumnyonga pamoja na viongozi wenzake 19 wa eneo hilo kwa tetesi tu kwamba walipanga njama ya kuwashambulia na kuwaondoa Wazungu katika eneo lote la Kilimanjaro.

Wajerumani kama ilivyokuwa kawaida yao ya kupenda kukata vichwa vya watu, walifanya hivyo kwa Mangi Meli pia na fuvu lake likapelekwa Ujerumani<sup>8</sup>.



*Mangi Meli wa Moshi (kushoto) aliyepigana vita na Wajerumani 1892 – 1893 na Liti Kidanka (kulia) Mwanamke shujaa wa Singida aliyepambana na Wajerumani kwa miaka mitatu kwa kutumia nyuki 1908 – 1910. Vichwa vya mashujaa hawa wawili vilikatwa na kupelekwa Ujerumani na havijarejeshwa mpaka sasa*

### *Vita ya Liti Kidanka na Mjerumani 1908-1910*

Mjerumani alifika Singida ambapo alipambana na mwanamama wa Kinyaturu na mpigania uhuru shupavu, Liti Kidanka, ambaye hakutaka kabisa Wajerumani waingie eneo ambalo sasa ni mji wa Singida.

Liti na askari wake walipambana na Wajerumani mara mbili na kuwakimbiza nje ya Singida kwa kutumia silaha yake ya mwisho, nyuki wakali, ambao vita ikipamba moto walikuwa wakifunguliwa na

<sup>8</sup> Wajerumani walikusanya maelfu ya mafuvu kutoka barani Afrika kwa utafiti wa kibaguzi. Utafiti ulioendelea hadi 2022, uligundua katika lundo hilo la mafuvu kuwa kulikuwa na mafuvu 200 kutoka Tanzania. (Vyanzo: [bbc.com](http://bbc.com), *The Search for the lost skull of Tanzania's Mangi Meli*, Novemba 13, 2018; [theguardian.com](http://theguardian.com), "Germany to investigate 1,000 skulls taken from African colonies for 'racial research'", Ijumaa, Oktoba 6, 2017). Mbali na Mkwawa na Meli, walikata na kuondoka na vichwa vya Mwami Gwasa wa Waha, Chabruma Nkosi wa Wangoni, Liti Kidanka wa Unyaturu, Mtemi Chenge wa Wasukuma na Nduna Songea Lwafu Mbano wa Wangoni.

kuwashambulia Wazungu tu na askari wao. Mapambano kati ya Liti na Wajerumani yalidumu miaka mitatu kuanzia mwaka 1908-1910.

Mara ya tatu na ya mwisho, Liti kutokana na kusalitiwa na mmoja wa washirika wake, hakufua dafu tena kwa Wajerumani ambao walimkamata yeye na mume wake, Nyalandu Mtinangi, wakauawa. Kichwa cha Liti kikakatwa na kupelekwa Ujerumani.

### *Vita vya Maji Maji 1905–1907*

Kati ya mwaka 1905 na 1907 ukanda wa mikoa ya Ruvuma, Mtwara na Lindi uligeuka kuwa eneo la Vita vya Maji Maji kupinga utawala wa kikoloni wa Wajerumani. Vita hivi vilisababisha vifo vya mashujaa wa Tanganyika zaidi ya 120,000, baadhi wakiwa watoto, wazee na wanawake waliouawa kiholela na askari wa Kijerumani walioingiwa na woga kutokana na ari kubwa ya kupambana waliyokuwa nayo mashujaa hao.

Kiongozi wa vita hivyo Kinjeketile Ngwale aliwahasisha na kuwashawishi wananchi kuwa risasi za Mjerumani zingegeuka kuwa maji tu zikiwafikia mwilini. Katika vita hivyo, Kinjeketile na Mashujaa wenzake akina Selemani Mamba na Digalu Kibasila walinyongwa wakitetea uhuru wa Waafrika.

Mkoani Ruvuma, jumla ya mashujaa wapatao 68 wakiwamo machifu (nkosi) na wasaidizi wa machifu (nduna), walinyongwa na kuzikwa katika kaburi la pamoja, mmoja wao alikuwa mwanamke shupavu Nduna Nnkomanile wa Lugongolo (Kitanda, Songea). Kabla ya kunyongwa kwa mashujaa hao wa Maji Maji, kiongozi wa manduna, Mpambalyoto Soko, aliwaambia Wajerumani maneno haya:

*“Mnatuonea sisi, mtakuja kupambana na watoto wetu nao watawafukuza katika nchi hii. ... Ninyongeni mimi lakini Chabruma atakuja kulipiza kisasi!”*

Ni dhahiri shahiri, maneno ya mwisho ya shujaa Mpambalyoto kabla ya kunyongwa, yalikuja kutimia miaka 55 baadaye ambapo Chabruma aliyemtambiria kuja kuwangoa wakoloni nchini, alikuja lakini kwa taswira ya Baba wa Taifa Mwalimu Julius Nyerere, Mwasisi wa Mapinduzi Matukufu ya Zanzibar, Sheikh Abeid Amani Karume na majemadari wao akina Rashid Mfaume Kawawa, Sheikh Thabit Kombo, Bibi Titi Mohamed na wengine wengi.

Kitabu hiki kinasisitiza kwamba madai katika nyaraka na matamshi mbalimbali kuwa Tanzania Bara haikutumia nguvu katika kusaka uhuru wake, bali iliupata kwa majadiliano si sahihi. Ni madai yasiyotokana na ukweli wa kihistoria, kwani mapambano ya kudai uhuru siyo tukio bali

mnyororo wa matukio yanayoimarishana na kuzalisha nguvu kubwa yenye matokeo chanya mwishoni.

### *Vita Kuu ya Kwanza ya Dunia na Kushindwa kwa Ujerumani*

Miaka saba tu baada ya Vita vya Maji Maji kumalizika, Vita Kuu ya Kwanza ya Dunia vikaanza mwaka 1914 vikimhusisha Mjerumani na washiriki wenzake wa Mkutano wa kuligawa Bara la Afrika mwaka 1884/85 mjini Berlin. Mjerumani alishindwa vibaya katika vita hivyo vilivyopiganwa zaidi Ulaya na kunyang'anywa makoloni yote aliyokuwa akiyashikilia, ikiwamo *Deutsch Ost-Afrika*.

### *Tanganyika Chini ya Utawala wa Waingereza*

Kwa usimamizi na uangalizi wa Umoja wa Mataifa, *Deutsch Ost-Africa au German East Africa* ikagawanywa katika maeneo mawili ya utawala: Tanganyika na Ruanda-Urundi. Tanganyika ilikabidhiwa kwa Uingereza, Ruanda-Urundi kwa Ubelgiji na Kionga Triangle ikawa sehemu ya Msumbiji chini ya Wareno. Wajibu wa nchi hizi mbili za Ulaya ulikuwa kuyasimamia maeneo hayo mawili mpaka pale wananchi wake watakapokuwa tayari kujiongoza wenyewe.

Tatizo lililojitokeza hapa ni Umoja wa Mataifa wenyewe kukabidhi hizo nchi kwa malezi bila vigezo mahususi vya kuzingatiwa na nchi walezi. Matokeo yake ni nchi hizo changa kutawaliwa kama makoloni badala ya kuongozwa ili kukidhi vigezo vya msingi kwa nchi kuweza kujiendesha kwa maana ya kuwa na rasilimali watu ya kuridhisha katika uongozi, utawala, afya/ tiba, haki jinai na suala zima la utawala wa sheria na utawala bora.

### **Kuelekea Uhuru wa Tanzania Bara**

Kabla na baada ya Vita Kuu ya Pili ya Dunia, kilikuwa kipindi cha mwamko mkubwa wa Umajumui wa Kiafrika kilichoshuhudia kufanyika kwa mkutano mkubwa wa tano wa wana-Umajumui wa Kiafrika, jijini Manchester, Uingereza, mwaka 1945 wakipaza sauti zao dhidi ya ukoloni barani Afrika na mshikamano wa Waafrika wote duniani kupinga ukoloni na ubaguzi wa rangi. Hakika kipindi hicho hakikuwa cha kawaida barani Afrika kutokana na kutamalaki kwa vuguvugu la ukombozi Afrika nzima.

*Pan African Movement of Eastern and Central Africa (PAFMECA)*, vuguvugu la kupigania uhuru wa nchi za Afrika Mashariki na Kati lililozinduliwa Mwanza, mwezi Septemba, 1958, ni moja ya matokeo ya harakati za Umajumui wa Kiafrika zilizowahusisha viongozi wa Afrika

Mashariki kwa karibu sana, wakiwamo Mwalimu Julius Nyerere na Sheikh Abeid Amani Karume.

Malengo makuu ya PAFMECA yalikuwa kujenga umoja, mshikamano na ushirikiano miongoni mwa watu wa Afrika waliokuwa wanatawaliwa katika nchi zao na kudai uhuru na ukombozi. Pili, kuunganisha nchi zao baada ya uhuru. Takriban viongozi wote wa vyama vya ukombozi vya nchi zote za Afrika Mashariki na Kati walijiunga na PAFMECA.

Kunako Aprili, 1959 Sheikh Abeid Amani Karume, Rais wa Chama cha ASP, alikuwa mwenyeji wa mkutano wa PAFMECA uliofanyika katika Viwanja vya Mnazi Mmoja, Zanzibar kwa mafanikio makubwa. Baada ya mkutano wa Zanzibar, viongozi wa PAFMECA walikutana Nairobi, Kenya mwezi Septemba 1959 na baadaye Addis Ababa, Ethiopia mwaka 1960.

Katika mkutano wa Addis Ababa, viongozi wa PAFMECA walijumuika na viongozi wenzao wa harakati za ukombozi wa kanda nyingine na wa nchi za Afrika zilizokuwa huru. Katika mkutano huo, masuala ya kuongeza nguvu katika harakati za ukombozi na Umoja wa Afrika yalizungumzwa na hivyo kupanda mbegu iliyozaa Umoja wa Nchi Huru za Afrika mwaka 1963.

## Mchango wa Jumuiya mbalimbali kwenye Harakati za Ukombozi

Mwaka 1927 Waafrika wa Tanganyika walianzisha jumuiya ya kimaslahi iliyoitwa *African Association (AA)*, chombo cha kutetea maslahi ya Waafrika na kusaidiana kwenye masuala ya kijamii. Miaka sita baadaye (1933), ndugu zao wa Zanzibar nao wakaunda *African Association (AA)*, lengo likiwa lilelile la kutetea maslahi ya Waafrika. Mwaka 1938 nayo *Shirazi Association (SA)* ikaundwa. Vikundi hivi vitatu ndivyo katika miaka ya 1950 viliunda vyama vya ukombozi wa Tanganyika na Zanzibar.

Wanahistoria, B. F. Mrina na W. T. Mattoke, wanakumbusha kuwa, AA ya Tanganyika na AA ya Zanzibar bila kujua kuwa jumuiya hizo zilikuwa zinajenga msingi wa miaka zaidi ya 38 baadaye, zilikuwa na ushirikiano wa karibu sana kiasi kwamba kati ya mwaka 1939 na 1941 zilikuwa zina vikao vya mwaka vya pamoja na kwa mzunguko katika miji ya Zanzibar, Dar es Salaam na Dodoma. Vikao hivyo vilisitishwa mwaka 1942 kuheshimu masharti ya kusafiri kipindi cha Vita Kuu ya Pili ya Dunia.

Mwaka 1948 *African Association* ya Tanganyika ikawa *Tanganyika African Association (TAA)* na mwaka 1954 ikawa chama cha siasa

kikuu cha Tanganyika kilichoitwa *Tanganyika African National Union (TANU)*. Waasisi wa TANU waliohudhuria na kushiriki katika Mkutano wa kuzaliwa kwa TANU tarehe 7 Julai, 1954, walikuwa 17 wafuatao:

1. Mwalimu Julius Kambarage Nyerere
2. Germano Pacha – Jimbo la Magharibi
3. Joseph Kimalando – Jimbo la Kaskazini
4. Japhet Kirilo – Jimbo la Kaskazini
5. C.O. Milinga – Jimbo la Mashariki
6. Abubakari Ilanga – Jimbo la Ziwa
7. L.B. Makaranga – Jimbo la Ziwa
8. Saadani A. Kandoro – Jimbo la Ziwa
9. Suleman M. Kitwana – Jimbo la Ziwa
10. Kisung'uta Gabara – Jimbo la Ziwa
11. Tewa Said Tewa – Jimbo la Mashariki
12. Dossa A. Aziz – Jimbo la Mashariki
13. Abdulwahid Sykes – Jimbo la Mashariki
14. Patrick Kunambi – Jimbo la Mashariki
15. Joseph K. Bantu – Jimbo la Mashariki
16. Ally Sykes – Jimbo la Mashariki
17. John Rupia – Jimbo la Mashariki



*Baadhi ya waasisi wa TANU waliohudhuria na kushiriki mkutano wa kuzaliwa kwa TANU tarehe 7 Julai, 1954*

## Uchaguzi wa Kwanza Tanganyika

Katika uchaguzi wa kwanza wa nchi uliopangwa kufanyika mwaka 1958 ukivihusisha vyama vingi vya siasa, serikali ya kikoloni ikaona njia pekee ya kuizuia TANU isipate ushindi wa kimbunga Tanzania Bara ilikuwa kuweka baadhi ya masharti kuwa magumu kwa Waafrika ili wasijitokeze kwa wingi kwenye uchaguzi huo.

Mbali na masharti ya kawaida ya mpiga kura kuwa na umri kuanzia miaka 21 na makazi katika jimbo husika, kila mpiga kura alitakiwa apige kura tatu katika jimbo lake (kumchagua Mwafrika, Mzungu na Mhindi); na awe na kipato cha paundi 150 za Kiingereza kwa mwaka; au awe na angalau miaka miwili ya elimu ya sekondari; au awe na ajira mahususi.

Masharti yote hayo manne ya mwisho ya serikali ya kikoloni chini ya Gavana Edward Twining, yalilenga waziwazi kuwakomoa Waafrika ambao dhamira yao pekee ilikuwa uhuru dhidi ya utumwa na ukoloni. Mashujaa wao walikuwa Nyerere na wenzake ndani ya TANU. Aidha, Waafrika wengi kipindi hicho hawakupata fursa ya kwenda shule, hivyo, walikosa sifa ya kuajiriwa na uwezo wa kipato kikubwa kutokana na ajira zao.

Ikumbukwe vilevile kuwa kipindi hicho cha uchaguzi, pato la wastani la Mtanganyika kwa mwaka (kwa mujibu wa Benki ya Dunia) lilikuwa takriban paundi 114 tu, ukilinganisha na pato la paundi 150 kwa mwaka alilotakiwa mpiga kura awe nalo! Masharti hayo yalisababisha mvutano mkali miongoni mwa wana-TANU, baadhi wakitaka uchaguzi huo ususiwe na wengine wakitaka uchaguzi uendelee kwani dhamira ya uhuru ya walio wengi ingeshinda tu pamoja na masharti hasi ya kushiriki katika uchaguzi huo waliyowekewa na serikali ya kikoloni.

Sauti ya wengi ikataka TANU ishiriki kwenye uchaguzi huo na kusababisha baadhi ya wana-TANU waliokuwa na msimamo mkali, wakiongozwa na aliyekuwa Katibu Mwenezi wa TANU, Zuberi Mtemvu, kujitoa TANU na kuunda chama kipya cha siasa, *African National Congress (ANC)*. Pamoja na mtihani huo, TANU iliibuka kidedea katika awamu zote mbili za uchaguzi huo. Uchaguzi wa awamu ya kwanza uliofanyika Septemba 8 na 12, 1958 ukihusisha majimbo matano ya Tanganyika (Kaskazini, Mashariki, Magharibi, Tanga na Nyanda za Juu Kusini) ulishuhudia TANU ikishinda viti vyote vitano vya Waafrika na viti nane kati ya kumi vya Wazungu na Wahindi. Hivyo TANU ikapata viti 13 kati ya 15.




## Awamu ya Pili ya Uchaguzi

Awamu ya pili ya uchaguzi ilifanyika chini ya Gavana mpya, Richard Turnbull, Februari 9 na 15, 1959. Pamoja na masharti hasi iliyowekewa, TANU ikaibuka tena na ushindi wa kishindo kwa kupata viti vyote 15. Hivyo, kwa ujumla TANU ilipata viti 28 kati ya 30 vilivyogombewa katika majimbo yote yaliyobaki. Viti vingine 34 katika Baraza la Kutunga Sheria vilikuwa vya kuteuliwa. Ikumbukwe kuwa kati ya viti 30 vya Baraza vilivyokuwa vinagombewa, viti 15 (yaani nusu) vilienda kwa wagombea wa TANU ambao walipita bila kupingwa. Huo ni ushahidi wa kukubalika kwa TANU miongoni mwa wananchi wa Tanganyika kipindi cha kuelekea uhuru.

## Uchaguzi wa 1960

Pamoja na vyama vya upinzani kubebwa na serikali ya kikoloni kwa kuikandamiza TANU kwa kesi mbalimbali na kuzuia mikutano yake mbalimbali nchini, TANU (chama kilichoakisi na kubeba dhamira ya Waafrika ya uhuru dhidi ya utumwa na ukoloni) kilithibitisha tena umaarufu wake kwa wananchi kupitia uchaguzi wa tarehe 30 Agosti, 1960. TANU ikapata ushindi mkubwa wa kihistoria wa viti 70 kati ya 71 vilivyogombewa. Hata hicho kiti kimoja kilikwenda kwa mwana-TANU aliyeingia kwenye uchaguzi huo kama mgombea binafsi.

Uchaguzi huo ulikuwa na wapiga kura 885,000 waliojiandikisha ukilinganisha na wapiga kura 40,606 tu waliojiandikisha uchaguzi wa 1958/59. Hali hiyo ilitokana na masharti ya upigaji kura kulegezwa na hamasa na shauku kubwa ya uhuru waliyokuwa nayo wananchi na iliyokuwa ikiongezeka kila kukicha na kufanya Umoja wa Mataifa uridhie tarehe ya mapema kwa Tanganyika kujitawala.



*Rais wa TANU Mwalimu Nyerere akiwa na Kiongozi wa Wanawake Bibi Titi Mohamed katika moja ya Mikutano ya Kampeni za TANU*

### **Nyerere Waziri Mkuu**

Kufuatia ushindi huo wa TANU, tarehe 2 Septemba, 1960 Mwalimu Nyerere akawa Waziri Kiongozi na tarehe 3 Septemba, 1960 aliunda Serikali ya Madaraka. Katika hatua nyingine ya kuelekea uhuru, tarehe 1 Mei, 1961 Tanganyika ilipewa Mamlaka ya Ndani na Mwalimu Nyerere akawa Waziri Mkuu. Tarehe 9 Desemba, 1961 Tanganyika ikapata uhuru na kutangazwa kuwa mwanachama wa 104 wa Umoja wa Mataifa.

## TANU na Mchakato wa Jamhuri

Pamoja na kwamba Mwalimu Nyerere alikuwa Waziri Mkuu wa kwanza wa Tanganyika na kiongozi wa Serikali ya Uhuru, chini ya Katiba ya Uhuru ya mwaka 1961, Mkuu wa Nchi alikuwa Malkia wa Uingereza.

Suala la Malkia wa Uingereza kuwa Mkuu wa Nchi halikuifurahisha TANU, hivyo, mwezi mmoja tu baadaye chama hicho cha ukombozi wa Tanganyika kikatangaza kuwa kilishaishauri Serikali kuanzisha mara moja mchakato wa kikatiba kuipa Tanganyika hadhi ya kuwa Jamhuri ndani ya Jumuiya ya Madola<sup>9</sup>. Tarehe 22 Januari, 1962 Mwalimu Nyerere alijiuzulu nafasi ya Uwaziri Mkuu na nafasi hiyo ilichukuliwa na Mzee Rashidi Mfaume Kawawa aliyekuwa Waziri asiye na Wizara Maalumu. Lengo la Mwalimu Nyerere kujiuzulu nafasi hiyo lilikuwa ni pamoja na kukiimarisha chama cha TANU kuweza kuyakabili vizuri majukumu ya uhuru.

## Uchaguzi wa Rais wa Jamhuri

Uchaguzi wa Rais wa Jamhuri ya Tanganyika ulifanyika tarehe 1 Novemba, 1962 ambapo mgombea wa TANU, Mwalimu Julius Nyerere alipata kura 1,127,978 na mshindani wake mkubwa Zuberi Mtemvu, Rais wa ANC, alipata kura 21,276.

Tarehe 23 Novemba, 1962 Katiba ya Jamhuri ya Tanganyika ikatungwa,<sup>10</sup> ikaunganisha ukuu wa serikali na ukuu wa nchi. Tarehe 9 Desemba, 1962 Tanganyika ikawa rasmi Jamhuri na Mwalimu Julius Kambarage Nyerere akaapishwa kuwa Rais Mtendaji, Mkuu wa Nchi, Kiongozi wa Serikali na Amiri Jeshi Mkuu.

## Baraza la Kwanza la Mawaziri la Tanganyika

Mwalimu Julius Kambarage Nyerere alishirikiana na viongozi wenzake kujenga misingi mikuu muhimu katika ujenzi wa taifa jipya, hususan mifumo ya siasa, uongozi, utawala, uchumi, jamii na utamaduni. Misingi hiyo, ambayo ndiyo utambulisho wake kati ya mataifa, ni pamoja na utu, uhuru, maendeleo, usawa, haki, kujitegemea, umoja, utaifa na uzalendo, amani na maadili.

Baada ya kupata uhuru mwaka 1961, Tanganyika ilikuwa na Baraza la Mawaziri lenye mawaziri 12 tu, idadi ndogo kuliko serikali zote zilizofuata. Mawaziri hao ni hawa wafuatao:

<sup>9</sup> Tangazo la TANU kwenye Mkutano wa Halmashauri Kuu ya Taifa, tarehe 16 Januari, 1962.

<sup>10</sup> C.A. Act No. 1 ya 1962, (Sura ya 499).

1. Waziri Mkuu - Mwalimu Julius Kambarage Nyerere;
2. Waziri Asiyeye na Wizara Maalumu - Rashidi Mfaume Kawawa;
3. Waziri wa Elimu - Oscar Kambona;
4. Waziri wa Serikali za Mitaa - Job Lusinde;
5. Waziri wa Mawasiliano, Nguvu za Umeme na Ujenzi - Amir Jamal;
6. Waziri wa Biashara na Viwanda - Nsilo Swai;
7. Waziri wa Ardhi na Upimaji - Tewa Saidi Tewa;
8. Waziri wa Sheria - Chief Abdalah Said Fundikira;
9. Waziri wa Afya na Kazi - Dereck N. M. Bryceson;
10. Waziri wa Kilimo - Paul Bomani;
11. Waziri wa Fedha - Ernest Vassey; na
12. Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi - Clement G. Kahama.



*Baraza la Kwanza la Mawaziri mwaka 1961, kutoka kushoto waliosimama ni Ndugu Job Lusinde, Ndugu Rashidi Mfaume Kawawa, Ndugu Nsilo Swai, Ndugu Oscar Kambona, Ndugu Tewa Said Tewa na Ndugu Dereck Bryceson na kutoka kushoto walioketi ni Ndugu Paul Bomani, Abdallah Fundikira, Mwalimu Julius Kambarage Nyerere, Sir Ernest Vassey na Amir Jamal*

## Tanzania Zanzibar

Tanzania Zanzibar<sup>11</sup> ambayo ni sehemu ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, inajumuisha visiwa vikubwa viwili vya Unguja na Pemba

<sup>11</sup> Ibara ya 151(1) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977 inatamka kuwa Tanzania Zanzibar ni eneo lote la Jamhuri ya Muungano ambalo zamani lilikuwa eneo la Jamhuri ya Watu wa Zanzibar na lilikuwa likiitwa Tanzania Visiwani.

pamoja na visiwa vingine vidogovidogo ambavyo vipo katika Bahari ya Hindi kati ya nyuzi za Latitudo 5 na 6 Kusini mwa Ikweta na Longitudo ya nyuzi 39 na 41 Mashariki mwa mstari wa Griniwichi.

Kisiwa cha Unguja kina eneo lenye ukubwa wa kilomita za mraba 1,666 na wakazi wapatao 1,104,983 kwa mujibu wa makadirio ya Ofisi ya Taifa ya Takwimu (NBS) ya mwaka 2020. Aidha, kisiwa cha Pemba kina ukubwa wa kilomita za mraba 988 na kilikadiriwa na NBS mwaka 2020 kuwa na idadi ya watu 566,615. Hivyo, Tanzania Zanzibar inakadiriwa kuwa na ukubwa wa kilomita za mraba 2,654<sup>12</sup> na idadi ya watu inayokadiriwa kuwa 1,671,598.

Unguja na Pemba ni visiwa vilivyojijengea umaarufu mkubwa duniani katika biashara ya viungo vya chakula na biashara ya utalii kwa kuwa na fukwe za bahari nzuri zenye mchanga mweupe, samaki wa aina mbalimbali na *kima punju* wanaopatikana Zanzibar pekee duniani. Umbali kati ya visiwa hivi vikubwa viwili ni kilomita 50.

Tanzania Zanzibar pamoja na ukanda wa pwani wa Tanzania Bara ni chimbuko la lugha ya Kiswahili na Wazanzibari wote kama ilivyo kwa ndugu zao wa Tanzania Bara, wanazungumza Kiswahili. Umbali kati ya kisiwa cha Pemba na mwambao wa Tanga, Tanzania Bara ni kilomita 32 na kati ya Unguja na ukanda wa pwani Tanzania Bara ni kati ya kilomita 25 (kwa sehemu zilizokaribiana) hadi kilomita 50 (kwa sehemu zilizoachana sana).

## Historia Fupi ya Zanzibar

### *Wakazi wa Asili na Ujio wa Wageni Zanzibar*

Wakazi wa asili wa Zanzibar ni Waafrika wenye asili ya Wabantu ambao wengi walitoka eneo la Tanganyika. Aidha, baadhi ya Wabantu walifika Tanganyika na Zanzibar kutoka sehemu nyingine za Afrika, yakiwamo maeneo ya kati, kaskazini na kusini. Uchumi wa wakazi wa asili wa Zanzibar ulitegemea kwa sehemu kubwa uvuvi katika Bahari ya Hindi, kilimo cha mazao ya chakula na viungo, ufugaji na ufundi wa zana za kufanyia kazi.

Wageni walianza kuja Zanzibar karne nyingi zilizopita. Baadhi ya wageni hao ni Washirazi kutoka Iran ambao katika miaka ya 1200 walifika Kilwa, Mafia na maeneo mengine ya pwani ya Afrika Mashariki kwa lengo kuu la biashara. Katika miaka ya 1500, Kisiwa cha Zanzibar kilikuwa kimegawanywa katika wilaya mbalimbali za kifalme, kila wilaya ikiwa na mfalme wake kikiwamo kisiwa cha Tumbatu. Baadaye watawala wa kienyeji Mwinyi Mkuu upande wa Unguja na Mkamandume upande

<sup>12</sup> Chanzo: Office of the Chief Government Statistician, Revolutionary Government of Zanzibar, *Zanzibar in figures 2020*, June 2021, uk.2

wa Pemba waliunganisha mamlaka ndogondogo na kuunda himaya kubwa zaidi.

### *Wareno na Utawala wa Kwanza wa Kikoloni*

Umuhimu wa Zanzibar na pwani ya Afrika Mashariki kibiashara, ulivutia mataifa ya nje mengi zaidi katika eneo hili la Afrika yakiwa na malengo mapya ya kikoloni. Polepole utawala wa wenyeji wakiwamo Mwinyi Mkuu (Unguja) na Mkamandume (Pemba) ukaanza kudhoofu. Katika karne ya 16, Wareno walitwaa miji kadhaa pwani ya Afrika Mashariki hadi pwani ya Msumbiji (kuanzia Lamu, kuja Malindi, Mombasa, Pemba, Unguja, Kilwa hadi Sofala) na kuanzisha utawala wao na kuifanya Mombasa kuwa makao makuu. Huo ukawa mwanzo wa kuwaengua watawala wa kimila na kuanzishwa kwa tawala za kikoloni.

Uroho wa kutwaa maeneo mengi harakaharaka uliwapunguzia Wareno uwezo wa kijeshi na kiutawala kuyalinda na kuyashikilia maeneo yote waliyoyatwaa siyo tu ukanda wa pwani wa Afrika Mashariki hadi Msumbiji, bali vilevile Ghuba ya Uajemi kwa maana ya Muscat na kisiwa cha Hormuz. Hivyo, hatua ya Waajemi mapema karne ya 17 ya kuwang'oa Wareno kisiwa cha Hormuz na miaka 28 baadaye Waarabu wa Oman kuikomboa Muscat kutoka mikononi mwa Wareno, iliwadhoofisha sana Wareno na kuanza kupoteza maeneo zaidi.

### *Waomani, Ukoloni na Biashara ya Utumwa*

Ushindi wa Muscat ulimpa nguvu Sultani wa Oman ambaye alituma jeshi lake la majini Afrika Mashariki kupambana na Mreno ambaye kufikia mwishoni mwa karne ya 17 alipoteza maeneo yote ukanda wa Pwani. Kama alivyofanya Mreno, Sultani wa Oman naye kwa mabavu akajimilikisha Unguja, Pemba, Mafia na ukanda wa pwani wa Afrika Mashariki na kwa busara ya nyoka kuvamia kichuguu na kukigeuza kuwa mali yake, akahamisha makao makuu yake kutoka Muscat kuja Zanzibar.

Kilimo cha karafuu kilipamba moto Zanzibar mwanzoni mwa karne ya 19 huku mapinduzi ya viwanda yakishamiri Ulaya na Marekani, vyote kwa pamoja vilichochea uhitaji wa nguvu kazi. Jibu likawa “watumwa” wa kumenyeka kwenye mashamba ya karafuu na minazi Zanzibar pamoja na mashamba ya malighafi ughaibuni (pamba, pareto, ngozi, miwati, chai, kahawa, katani n.k). Hivyo, biashara ya utumwa ikashamiri, Waarabu wa Oman wakiwa miongoni mwa wadau wakubwa duniani wa biashara hiyo.

Zanzibar na Bagamoyo vikawa vituo vikubwa upande wa Bahari ya Hindi kwa usafirishaji wa watumwa ambao waliuzwa ughaibuni, walitumika mashambani na majumbani Unguja na Pemba. Idadi ya watumwa waliotumika mashambani Zanzibar ikaongezeka kwa kasi na kuzidi idadi ya Waarabu wa Oman waliomiliki mashamba makubwa ya karafuu na minazi Unguja na Pemba kwa uwiano wa moja kwa tisa.

Pamoja na Sultani kuhamishia makao makuu yake Zanzibar ili kulilinda kwa karibu “koloni lake” hilo jipya, mkakati huo uliharibika mwishoni mwa karne ya 19 kufuatia Mkutano wa Berlin wa 1884/85 ulioitishwa na mabeberu kugawana Bara la Afrika.

### *Mkutano wa Berlin na Ujio wa Wajerumani*

Mkutano huo wa Berlin ukafuatiwa (kimkakati) mwaka 1886 na mkutano wa maelewano kati ya Uingereza na Ujerumani kuhusu mipaka ya maeneo kadhaa waliyoyatwaa Afrika Mashariki na madai ya Sultani wa Zanzibar kuwa himaya yake ilihusisha maeneo kadhaa ya ukanda wa pwani. Matokeo ya mkutano huo ni Mkataba wa Uingereza na Ujerumani wa mwaka 1886 ambao ulitambua rasmi mamlaka ya Sultani katika maeneo yafuatayo: Zanzibar, Pemba, Lamu, Mogadishu, Merca, Brava na kwenye ukanda wote wa pwani wenye upana wa kilomita 16 kati ya mto Tana (Kenya) na mto Ruvuma (Tanganyika)<sup>13</sup>.

Aidha, eneo lote la bara kuanzia ukanda wa pwani wa Sultani, likawekewa mpaka (ambao upo hadi leo) kutenganisha eneo la kaskazini (Kenya) chini ya mamlaka ya Uingereza na eneo la kusini (Tanganyika) chini ya mamlaka ya Ujerumani. Ni katika muktadha huo, Waingereza na Wajerumani wakakodishwa na Sultani wa Zanzibar eneo la pwani ili waendeleo kulitumia kwa malipo.<sup>14</sup>

### *Maelewano Mapya baina ya Wakoloni*

Mwaka 1890 ukafuatia mkutano mwingine kati ya mataifa hayo mawili makubwa ya kikoloni kumalizia changamoto nyingine kadhaa zilizogubika mahusiano yao katika kufaidika na rasilimali tele za Bara la Afrika. Kila upande ulifaidika kwa mambo kadhaa: Ujerumani iliachiwa

<sup>13</sup> Wakati huo Kenya ilikuwa ikiitwa British East Africa na Tanganyika iliitwa German East Africa au Deutsch-Ostafrika kwa Kijerumani. Rwanda na Burundi (wakati huo zikiwa eneo moja la Rwanda-Urundi) na Kionga au Kionga Triangle au Kionga Dreieck kwa Kijerumani, eneo dogo kwenye mdomo wa Mto Ruvuma, upande wa Kusini yalikuwa maeneo chini ya Deutsch-Ostafrika.

<sup>14</sup> Waingereza walimlipa Sultani wa Zanzibar pauni za Kiingereza 17,000 kwa mwaka na Wajerumani wakaamua kulikodisha eneo lao kutoka kwa Sultani kwa ada ya pauni za Kiingereza 200,000.

na Uingereza ukanda wa Caprivi, kaskazini mashariki mwa Namibia (wakati huo ikiitwa *German South West Africa*) na kisiwa kilichoko *North Sea* kiitwacho Heligoland ambacho Ujerumani ilikiona kuwa cha kimkakati, kiusalama na kiulinzi.

Aidha, Uingereza ikajipa wajibu wa kutumia “ushawishi wake wote” kumtaka Sultani wa Zanzibar aachie kisiwa cha Mafia na maeneo yake yote Tanganyika ambayo Wajerumani walikuwa na madai kwa kuelewa kuwa Sultani angelipwa fidia stahiki kwa mapato ambayo angepoteza kwa hatua hizo.<sup>15</sup>

Ujerumani nayo ikaikabidhi Uingereza mamlaka yake kuulinda Usultani wa Witu, eneo la pwani ya Kenya lililogomea kwa miaka mingi shinikizo la kuwa chini ya himaya ya Usultani wa Zanzibar. Aidha, Uingereza ikaachiwa maeneo mengine yaliyoonekana kufaa kwa ujenzi wa reli hadi Ziwa Victoria.

Ujerumani pia iliahidi kuheshimu mamlaka ya Sultani wa Zanzibar na ulinzi wa Uingereza wa himaya hiyo ya Kiarabu. Ahadi hiyo ya Ujerumani ilileta ahueni kwa Sultani wa Zanzibar ambaye hakuwa na imani na Wajerumani. Aliwaona kuwa tishio la usalama wa utawala wake kufuatia matukio kadhaa ya kutofautiana (kuhusu umiliki wa maeneo mbalimbali ya Tanganyika na ukanda wa Pwani wa Afrika Mashariki) yaliyosababisha mwezi Agosti, 1885 manowari za kivita za Ujerumani kutia nanga Unguja na kutishia kuisambaratisha ngome ya Sultani. Ushawishi wa Uingereza ulizuia hilo lisitokee.

### *Mwingereza na Ulinzi wa Zanzibar*

Usultani wa Zanzibar kuwekwa chini ya ulinzi/usimamizi wa Uingereza kwa mujibu wa Mkataba huo wa 1890, ilikuwa taarifa njema kwa wapinga biashara ya utumwa duniani ambao waliiona nafasi hiyo ya Uingereza kuwa fursa adhimu ya kuidhibiti Zanzibar iliyokuwa miongoni mwa vituo vikubwa vya biashara hiyo haramu duniani. Lakini kwa watumwa wenyewe haikuwapo sababu ya kusherehekea kwani Waingereza walikuwapo toka zamani kulinda maslahi yao wenyewe.<sup>16</sup>

<sup>15</sup> Ibara ya XI ya Mkataba huo wa 1890 ilitamka: “*Great Britain engages to use all her influence to facilitate a friendly arrangement, by which the Sultan of Zanzibar shall cede absolutely to Germany his possessions on the mainland comprised in existing concessions to the German East Africa Company, and their dependencies, as well as the island of Mafia. It is understood that His Highness will, at the same time, receive an equitable indemnity for their loss of revenue resulting from such cessions*”.

<sup>16</sup> Uingereza ilianzisha uhusiano wa kibalazi na Zanzibar mwaka 1841 na kufungua ofisi ya ubalazi mdogo mjini Zanzibar.



Kama Waswahili wanavyonena, “hakuna mumiani bora, wote huishia kunyonya damu”.

Sultani kwa kutambua kuwa Uingereza ilipiga marufuku biashara ya utumwa kitambo (mwaka 1807), akahisi kuwa nchi hiyo kwa nafasi yake mpya ya ushawishi iliyopata, ingechukua hatua za haraka kuzuia biashara hiyo Zanzibar. Hivyo, ujumbe ukasambazwa na wafanyabiashara wa karafuu kuwaambia Waingereza kuwa kusitishwa kwa biashara ya utumwa kwa haraka kutaua kabisa uchumi wa Zanzibar ambao unategemea zao moja kuu la karafuu.


Uingereza, kwa kauli na matendo, ikaonesha kubadilisha msimamo wake bayana wa kukomesha haraka biashara haramu ya utumwa Zanzibar. Sera ya “polepole”, yaani kuondosha utumwa “polepole” au hatua kwa hatua, ikatawala ndimi za watawala-wenza wa Zanzibar, Waingereza. Ndiyo maana ikawachukua Waingereza miaka saba toka 1890 kufikia uamuzi wa kumshawishi Sultani wa Zanzibar kupitisha sheria ya uhuru wa watumwa iliyosainiwa tarehe 5 Aprili, 1897 ambayo iliwapa haki watumwa kudai uhuru wao wakati wowote na vilevile haki ya mabwana zao kulipwa fidia kwa kuwaachia huru.

### *Mduara Hasi wa Uhuru wa Watumwa*

Sheria hiyo na nyingine zilizopitishwa baadaye kufanikisha azma ya kuondokana na biashara ya utumwa, zilizingatia sana fidia kwa wamiliki wa watumwa kwa hasara ambayo wangepata lakini hazikuzingatia hali ya maisha au hatima ya watumwa baada ya kupata uhuru wao. Hivyo, matokeo yake yalitengeneza mduara hasi na ovu wa unyanyasaji na unyonyaji ambapo watumwa “huru” wakiwa hawana mahali pa kuishi wala njia za kuanza maisha huru, wengi walilazimika kurejea kwa mabwana zao wa zamani kuuza nguvu zao kwa ujira mdogo wa kujikimu (wa malazi na chakula), baadhi wakapata ajira mpya mijini na vijijini na wengine wakafuatilia mizizi yao bara na kuanza maisha mapya.

Dhana ya “utumwa wa hiari” na “utumwa wa shuruti” ilijitokeza Zanzibar. Ikawa wazi kuwa kwa Mwingereza utumwa wa hiari ulikuwa ruksa, lakini si utumwa wa shuruti! Lakini kwa vyovyote vile, “uhuru” huo wa watumwa ukatengeneza jeshi kubwa Zanzibar la walalahoi lililokuja baadaye kubeba umuhimu mkubwa katika siasa za Zanzibar. Kulikuwa na kada kadhaa za watumwa Zanzibar: watumwa katika mashamba ya mikarafuu na minazi; watumwa wa kazi za ndani; masuria

ambao walikuwa vijakazi wenye kazi moja tu ya kumstarehesha bwana<sup>17</sup>; watumwa wenye stadi za kazi (kama useremala, uashi na ujenzi); na watumwa wa mjini waliowatumikia Wazungu, Wahindi na mataifa mengine.



*Watumwa katika Soko la Watumwa Zanzibar mnamo karne ya 19*

<sup>17</sup> Kada hii ya watumwa haikuhusika moja kwa moja na sheria hiyo ya uhuru wa watumwa kwani masuria walichukuliwa kuwa nyumba ndogo ya bwana au *harem* kwa Kiingereza.

### *Makovu ya Utumwa na Mwamko wa Kisiasa Zanzibar*

Pamoja na mfumo wa utumwa kupigwa marufuku Unguja na Pemba mwaka 1897, mfumo huo dhalimu ulibakia mioyoni, majumbani, mashambani na katika mahusiano binafsi ya watu na kuendelea kuigawa jamii ya Wazanzibari kati ya mabwana na watwana. Mabwana waliwakilishwa na Waarabu na watwana waliwakilishwa na Waafrika, ngozi nyeusi. Waingereza waliliona hilo, lakini wakalifumbia macho kuchelea kuua uchumi wa Waarabu na nafasi yao kisiasa na kijamii<sup>18</sup>.

Hivyo, mwamko mpya wa harakati za uhuru ulipopamba moto barani Afrika hasa baada ya Vita Kuu ya Pili ya Dunia ambayo iliwafungua macho askari wengi wa Kiafrika waliokwenda nje ya bara hili kushiriki kwenye vita hivyo. Mwamko huo ulisambaa kwa kasi na kwa urahisi kutokana na mazingira mazuri ya kudai uhuru. Vyama vya kiraia au kijamii vilivyoanzishwa mapema miaka ya 1920 na 1930 kama vile Jumuiya ya Waarabu, Jumuiya ya Wahindi, Jumuiya ya Waafrika, na Jumuiya ya Washirazi, vilibadilika na kuwa vyama madhubuti vya kisiasa. Jumuiya ya Washirazi na Jumuiya ya Waafrika zilikataa mchezo wa kufitinishwa na wakoloni na kutambua faida za umoja.

### *Kuelekea Uchaguzi Mkuu*

Chama cha ASP kilikuwa na mtaji mkubwa wa watu waliokata tamaa ya maisha chini ya utawala wa mabavu, ubaguzi, unyonyaji, ukandamizaji na udhalilishaji wa utawala wa Waarabu wa Oman uliodumu Zanzibar kwa zaidi ya karne mbili. Hivyo, ASP kwa njia yoyote ile kingeshinda uchaguzi wowote ule Zanzibar kwa sababu ya idadi ya Waafrika miaka ya 1930/40 (ikilinganishwa na idadi ya Wazungu, Waarabu, Wahindi na wengineo kwa pamoja) bado ilikuwa ni zaidi ya theluthi mbili ya wakazi wote wa Zanzibar.

Lakini Sultani na wakoloni wake wenza (Waingereza), aliamini atafanikiwa kupunguza kura za Waafrika kwa kutumia mbinu mbili: ya kwanza ni kuwachonganisha Waafrika na ndugu zao Washirazi kwa kuwambia wimbo kuwa Washirazi walikuwa bora zaidi ya Waafrika na ndiyo maana walikuwa hawachukuliwi utumwa na pili kuwapa Washirazi upendeleo katika utoaji wa huduma mbalimbali mpaka Waafrika wajikane wenyewe.

Njaa kali ilipoikumba Zanzibar mwaka 1942, kipindi cha Vita Kuu ya Pili ya Dunia, serikali ya kikoloni ikaanzisha mgao wa chakula ambao

<sup>18</sup> Mwakyembe, H.G., *Tanzania's Eighth Constitutional Amendment & Its Implications on Constitutionalism, Democracy and the Union Question*, Lit Verlag, Hamburg, 1995, p.38.

kwa makusudi ulifanyika kwa kuzingatia rangi za watu ili kuwakomoa Waafrika: Wazungu walipatiwa mahitaji yote waliyotaka ya chakula; Waarabu, Wahindi na Wangazija walitengewa paundi sita za mchele na paundi tatu za sukari kwa kichwa kwa wiki; Waafrika wakanyimwa mgao wa mchele badala yake wakapatiwa unga wa mahindi paundi sita na paundi mbili za sukari kwa kichwa kwa wiki.

Mgao huo ukazua malalamiko ya kubaguliwa miongoni mwa Waafrika, madai ambayo serikali ya kikoloni iliyapuuza. Washirazi “wakashauriwa” walalamike kama Washirazi, tofauti na Waafrika, wakiiomba serikali ya kikoloni kuzingatia historia yao, hivyo, wachukuliwe kama watu wa Asia. Ombi lao likakubaliwa na zaidi ya hapo Waafrika wote waliokuwa na vitambulisho vya chama cha Washirazi wakaongezewa mgao wa chakula kama “wenzao wengine” wa Asia na hatua hiyo ikawashawishi Waafrika wengi kujiunga na Chama cha Washirazi<sup>19</sup> kama Waingereza na Waarabu walivyotarajia.

Hata baada ya kipindi cha njaa kupita, vivutio vya kuwashawishi Waafrika waukane Uafrika wao na kupata hadhi ya Mwarabu au Mshirazi vikaongezeka kwa maana ya fursa zaidi za ajira, biashara na elimu. Matokeo ya kampeni hiyo yakaanza kuonekana kwenye Sensa ya Mwaka 1931 ambapo idadi ya Waafrika, wengi wao tititi, waliodai kuwa na damu ya Kiarabu ilipanda toka 18,884 (mwaka 1924) hadi 33,401 (mwaka 1931), ongezeko la asilimia 77 ndani ya miaka saba tu.<sup>20</sup> Dhamira ya Waarabu kwa kushirikiana na Waingereza kuhlalisha uwepo wa himaya ya Kiarabu Afrika ya Mashariki, Kusini mwa Jangwa la Sahara, ilishika kasi.

### *Uchaguzi Mkuu wa Zanzibar wa Mwaka 1957*

Uchaguzi huo ulifuatiliwa kwa umakini na Sultani na watawala wenza wa Kiingereza ili kujua ni kwa kiasi gani kampeni ya kuwavuruga Waafrika kisaikolojia ilikuwa imefanikiwa.

Tukio la tarehe 5 Februari, 1957 la kuunganisha *Shirazi Association* na *African Association* kuunda chama cha ASP, halikupewa umuhimu sana kwani waliamini sehemu kubwa ya Washirazi wasingeunga mkono umoja huo kutokana na upendeleo waliokuwa wanapewa na serikali ya kikoloni.

<sup>19</sup> Mapuri, O.R., *The 1964 Revolution: Achievements & Prospects*, TEMA Publishers Co. Ltd, Dar es Salaam, 1996 kur. 13 na 14.

<sup>20</sup> Hettiger. M., *kama hapo juu*, uk. 9



*Baadhi ya waasisi wa Afro Shirazi Party waliohudhuria uzinduzi wa kuzaliwa kwa ASP tarehe 5 Februari, 1957*

Pamoja na wafuasi wa chama cha *Zanzibar Nationalist Party (ZNP)* kumfungulia mashtaka ya uongo kiongozi wa ASP, Sheikh Abeid Karume, tarehe 11 Juni, 1957 kwamba hakuwa raia wa kuzaliwa wa Zanzibar, na kesi hiyo ikatupiliwa mbali; pamoja na masharti magumu kwa Waafrika ya kushiriki kwenye uchaguzi huo (kujua kusoma na kuandika kwa Kiingereza na Kiarabu au Kiswahili; kumiliki mali isiyopungua thamani ya Paundi za Kiingereza 150, kipato kwa mwaka kisichopungua Paundi za Kiingereza 120; au ajira katika Serikali); na pamoja na Chama cha Washirazi cha Pemba kukataa kujiunga kwenye umoja mpya, matokeo ya uchaguzi huo yalidhihirisha wazi kuwa nguvu ya pamoja ina tija, kwani umoja huo ASP ulishinda viti 5 kati ya 6 vilivyokuwa vinashindaniwa.

Matokeo hayo yaliwashawishi Washirazi wa Pemba kujiunga na ASP. Mshindani mkubwa wa ASP, ZNP chama cha Waarabu, kilichojivalisha sura ya udanganyifu ya uzalendo kikidai kupigania maslahi ya Waafrika kwa kauli mbiu yake “Afrika kwa ajili ya Waafrika”, huku kikimpigia kampeni Sultani kuwa lazima abaki kuwa mtawala, kilishindwa vibaya kwenye uchaguzi huo kutokana na undumilakuwili ambao wananchi waliuona waziwazi.

Ushindi wa kishindo wa ASP ulimfurahisha Mwalimu Julius Nyerere na viongozi wenzake wa TANU ambao kwa nyakati tofauti walilihangaikia suala la umoja wa *African Association* na *Shirazi Association*. Ushindi huo pia uliwapa wasiwasi mkubwa kuhusu hatua ambazo Sultani, kwa

kuchochewa na ZNP, angeweza kuchukua kuivuruga ASP bila aibu wala huruma. TANU ambayo ilikuwa ngome muhimu na kubwa ya ASP, ilikuwa haina budi kuongeza msaada.

Historia ya ZNP ilikuwa inajulikana. Ilikuwa inaanzia kwenye chama kikongwe cha kijamii cha Waarabu cha *Arab Association* chenye historia ndefu ya kupigania maslahi ya Waarabu. Chama hicho kilikuwa mstari wa mbele kudai fidia ya kutosha kwa Waarabu waliokatishwa kufanya biashara ya utumwa visiwani. Aidha, kiliendesha kampeni ya nguvu ndani na nje ya Zanzibar kuisitiza kuwa Zanzibar ilikuwa taifa la Kiarabu.<sup>21</sup>

Mwaka 1955 chama hiki kikongwe kikajiunga na chama kidogo kipya cha kisiasa kilichoitwa Chama cha Umoja wa Kitaifa cha Raia wa Sultani (NPSS) kilichoanzishwa na kundi dogo la wakulima wa Kiembesamaki. Chama hiki kilijulikana kwa Kiarabu kama *Hizbu l'Watan l'Riaia Sultan Zanzibar*, kwa kifupi HIZBU.

Kujiunga kwa *Arab Association* kwenye chama hicho kipya cha NPSS kukasababisha matokeo mawili: kwanza NPSS ikabadilisha jina mwezi Desemba, 1955 kuwa *Zanzibar Nationalist Party* (ZNP) ili kuondoa hisia (kutokana na jina lake la mwanzo) kuwa chama kilichokuwa karibu sana na Sultani na wafuasi wake, na hivyo, kuweza kuwazuia baadhi ya Wazanzibari, hasa Waafrika, kujiunga na chama hicho; pili, ZNP ikabebeshwa malengo yote ya *Arab Association* ya kutetea maslahi ya Waarabu<sup>22</sup>; na tatu, ZNP ikavishwa sura ya udanganyifu ya uzalendo wa kupigania umoja wa Wazanzibari na maslahi ya Waafrika kwa kaulimbiu yake ya ghiliba ya “*Africa for Africans*”; na nne, ZNP ikawateua Waafrika, Miraj Shaalab na Maalim Maksud, kuwa Rais na Makamu wa Rais wa chama hicho ili kuwaondolea shaka Waafrika kuwa ZNP kilikuwa chama cha Waarabu.<sup>23</sup>

Hivyo kushindwa kwa ZNP kupata kura za kutosha kwenye uchaguzi huo wa Julai 1957, pamoja na mbinu zote hizo za kukisaidia chama hicho, kuliwaamsha Waarabu na Waingereza kutumia kila mbinu kuidhoofisha ASP. Kampeni hiyo ikafanikiwa mwaka 1959 kwa wanachama wengi wa ASP Pemba kushawishiwa kukihama chama hicho na kuunda chama

<sup>21</sup> Mapuri, O.R., *kama hapo juu*, uk.10

<sup>22</sup> Hata serikali ya kikoloni iliiona ZNP kuwa mwendelezo wa *Arab Association* katika medani ya siasa. *Angalia* Zanzibar Government, Report, 1958, imenukuliwa katika Mapuri, O.R., *kama hapo juu*, uk.19.

<sup>23</sup> Kumbukumbu zinaonesha kuwa wenye nguvu kwenye chama hicho hawakuwa hao Waafrika wawili na nafasi zao hizo kubwa, bali Ali Muhsin Barwan na Amour Zahor, wote Waarabu. Soma Mapuri, O.R., *kama hapo juu*, uk. 17

kipya cha Washirazi kwa jina la *Zanzibar and Pemba People's Party (ZPPP)*.

### *Uchaguzi wa Mwaka 1961*

TANU ikaongeza juhudi kuisaidia ASP. Viongozi wake, akiwamo Bi. Lucy Lameck na Bibi Titi Mohammed wakajichimbia Zanzibar kuhamasisha wafuasi wa ASP. TANU vilevile ikatuma shilingi 11,000/= na doti 11,000 za kanga kwa ASP ili ziuzwe kupata fedha za uchaguzi wa 1961. ASP nayo ikafungua ofisi ndogo kwenye jengo la makao makuu ya TANU, Dar es Salaam, kuimarisha uratibu. Mikutano ya mara kwa mara ya viongozi waandamizi wa TANU na ASP ikaongezeka.

Katika uchaguzi wa 1961, ASP ilipata viti 10, ZNP viti 9 na ZPPP viti 3, lakini Waingereza wakadai hakuna chama kilichoshinda, hivyo, ukaitishwa uchaguzi mpya mwezi Juni mwaka huohuo kumpata mshindi waliyemtaka. ZNP na ZPPP wakaungana na kupata viti 13, ASP viti 10 pamoja na kwamba ASP iliushinda umoja huo wa ZNP na ZPPP kwa zaidi ya kura 1,092. Machafuko yakatokea, watu 68 wakauawa.

Hatimaye, ZNP na ZPPP wakaunda Serikali ya pamoja mwishoni mwa Juni, 1961. TANU ambayo kuanzia tarehe 9 Desemba, 1961 ilikuwa tayari inaongoza Serikali ya Madaraka Tanganyika, ikaongeza nguvu kuisaidia ASP.

### *Uchaguzi wa 1963*

Katika uchaguzi wa mwisho wa Julai, 1963 ambao wanawake kwa mara ya kwanza waliruhusiwa kupiga kura, ZNP ilipata kura 47,943 na kushinda viti 12, ASP ilipata kura 87,402 na kushinda viti 12 na ZPPP ilipata kura 25,610 na kushinda viti sita. ASP ilipata asilimia 54.2 ya kura zote au kura 13,849 zaidi ya kura za ZNP na ZPPP kwa pamoja,<sup>24</sup> lakini ikashindwa.

### *Uhuru Pasipo Uhuru*

Uhuru wa bandia ulipatikana tarehe 10 Desemba, 1963 na tarehe 16 Desemba, 1963 Zanzibar ilipata uanachama wa Umoja wa Mataifa na kuwa mwanachama wa 112 wa chombo hicho kikuu cha kimataifa. Katiba ya Zanzibar ya mwaka 1963 ilianzisha bila majadiliano wala makubaliano **mfumo wa usultani wa kikatiba** Zanzibar ambao ulimpa Sultani ukuu wa nchi, vilevile ulimpa Sultani na “warithi wake” uongozi wa Zanzibar usio na ukomo wa muda.<sup>25</sup>

<sup>24</sup> Chanzo, Mapuri, O.R., *kama hapo juu*, uk. 36.

<sup>25</sup> Ibara ya 32,33,34,35 na viapo First Schedule, Part II.

Kwa kutumia tafsiri oanishi ya katiba, Katiba ya Zanzibar ya mwaka 1963 ilifanikisha ndoto ya Waingereza ya kuunda taifa jipya la Kiarabu Kusini mwa Jangwa la Sahara. Kimsingi, utawala wa kisultani ndio uliotawala Zanzibar kabla ya kuja kwa utawala wa ubia na Waingereza.

Uingereza ilikuwa ngome kuu ya ulinzi wa himaya hiyo Uarabuni na Afrika Mashariki kwa muda mrefu na iliweza hata kuingilia na kuamua mizozo ya kifamilia ya urithi kama ilivyotokea mwezi Agosti, 1896 Zanzibar alipofariki Sultani Hamad bin Thuwaini. Binamu yake Khalid bin Barghash akachukua uongozi lakini Waingereza walimtaka Hamoud bin Mohammed na ikawa hivyo.

Pamoja na kwamba Zanzibar ilikuwa koloni la Kiarabu, Uingereza ilifanya kila lililowezezana kuonesha kuwa Zanzibar ilikuwa koloni la Waingereza na siyo la Waarabu. Huenda Uingereza ilikuwa inafanya hivyo kumlinda Sultani dhidi ya mataifa mengine yenye nguvu ambayo yangeweza kumng'oa visiwani kwa urahisi. Mataifa makubwa hayakumchukulia Sultani kama tishio au mshindani na ndiyo maana hayakumpa mwaliko wala taarifa kuhudhuria mkutano wa Berlin hata kama msikilizaji tu. Hivyo, Waingereza walimbeba, naye alilitambua hilo.

Pili, Uingereza ilikuwa inamlinda Sultani dhidi ya wimbi kubwa la Waafrika walioamka na kudai uhuru barani Afrika miaka ya 1950 na 1960, wimbi ambalo Sultani peke yake asingelimudu. Hivyo, Uingereza isingeweza kwa vyovyote vile kukabidhi visiwa hivyo kwa ASP hata pale ushindi wa ASP kwenye kura zote zilizofanyika Zanzibar ulipokuwa bayana.

Uingereza ilitaka dunia itambue kuwa Zanzibar ilikuwa koloni lake na kwamba Sultani na Waarabu wenzake wa Oman walikuwa Wazanzibari waliotawaliwa na Uingereza na waliokuwa na uhalali kama Waafrika, kudai uhuru wa Zanzibar kutoka Uingereza pamoja na tahadhari aliyotoa Karume mara kadhaa.

Sheikh Karume alitamka kwenye mkutano wa hadhara Raha Leo mwezi Desemba, 1959 kwamba ASP ilitaka Zanzibar iwe Jamhuri, kauli ambayo serikali ya kikoloni haikukubaliana nayo<sup>26</sup>. Kwa kuwa milango yote ya kidemokrasia kwa upande wa Waafrika ilikuwa imefungwa na Waingereza na Waarabu, ASP iliiona njia moja tu ya kuleta uhuru wa kweli Zanzibar ni Mapinduzi ya Umma.

### *ASP na Mapinduzi*

Kamati ya vijana jasiri na shupavu iliundwa mapema hata kabla ya igizo la uhuru wa tarehe 10 Desemba, 1963 kwa lengo la kuratibu kwa

<sup>26</sup> ASP, *Afro-Shirazi – A Liberatin Movement*, ZPPC, 1973, uk. 56



siri ya hali ya juu suala zima la Mapinduzi. Wakalifanya zoezi zima la maandalizi kwa usiri mkubwa na katika tarehe aliyoridhia Sheikh Karume, yaani tarehe 12 Januari, 1964 Mapinduzi Matukufu ya Zanzibar yakafanyika kwa kuzingatia maelekezo kwa asilimia 100. Hatua yao ya kwanza ilikuwa ni kuteka vituo muhimu vitatu vya polisi: Mtoni, Ziwani na Malindi ili kupata silaha za kufanikisha mapinduzi. Mtoni na Ziwani vikawa vituo vya kwanza vya polisi kuchukuliwa na wanamapinduzi.

Kituo cha Polisi cha Malindi, wakati huo kikiongozwa na Afisa wa Polisi wa Kiingereza, J.M. Sullivan, hakikuwa rahisi kukiteka kwani kila wanamapinduzi walipojaribu kukivamia, walirudishwa nyuma kwa risasi. Sullivan na askari wake wakajisalimisha saa za alasiri walipoishiwa risasi. Mapambano hayo hayakusababisha vifo upande wa polisi bali upande wa wanamapinduzi na Waafrika wengi waliokuwa eneo hilo kwa udadisi na wengine kuwaunga mkono wanamapinduzi.<sup>27</sup>

Mbali na vituo vya polisi, wanamapinduzi walifanikiwa kukamata kituo cha redio cha Zanzibar, kituo cha mawasiliano, majengo makubwa yote mjini Zanzibar na kuelekea kasri ya Sultani ambaye alikwishatoroka na kupanda boti ya “Seyyid Khalifa” kuelekea Dar es Salaam kuomba msaada na hifadhi.

Kamati ya Waasisi wa Mapinduzi ya Zanzibar<sup>28</sup> ilikuwa na wajumbe wafuatao: -

1. Seif Bakari Omar – Mwenyekiti
2. Ramadhan Haji Faki
3. Mohamed Abdalla Kaujore
4. Said Iddi Bavuai
5. Hamid Ameir Ali
6. Pili Khamis Mpera
7. Said Washoto Mnyuke
8. Khamis Darwesh Mdingo
9. Hafidh Suleiman Almasi
10. Eddington Herbert Kisasi
11. Abdalla Said Natepe
12. Yusuf Himid Maftah
13. Abdulla Mfaranyaki

Sultani Jamshid bin Abdullah akang'olewa pamoja na serikali yake na hatimaye tarehe 12 Januari, 1964 Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar chini ya ASP ikatangazwa.

<sup>27</sup> Mapuri, O.R., *kama hapo juu*, uk.2; Babu, A. M., *kama hapo juu*, uk. 241

<sup>28</sup> Sheria ya Kuwaenzi Viongozi wa Kitaifa Na. 5 ya mwaka 2019.

### *Taarifa kwa Wazanzibari*

Tarehe 13 Januari, 1964 tukio nadra kufanyika duniani lilifanyika mjini Zanzibar ambapo Sheikh Karume akiwa amefuatana na aliyekuwa Waziri Mkuu wa Serikali ya Sultani na kiongozi wa ZPPP, Mohammed Shamte Hamad na kiongozi wa ZNP, Ali Muhsin Barwan, akaenda Redio Zanzibar kutangaza rasmi kwamba Mapinduzi yamefanikiwa na kwamba Zanzibar ni Jamhuri yenye Serikali mpya. Akahimiza utulivu na amani na kuahidi kwamba serikali mpya “itaendeshwa na watu, kwa ajili ya watu na kwa kuzingatia matakwa ya watu”.

Sheikh Karume akatumia muda huo kuuelezea umma wa Wazanzibari kuwa mbali na Mohammed Shamte na Ali Muhsin Barwan aliokuwa amefuatana nao, viongozi wengine katika serikali iliyopinduliwa kama vile Sheikh Idarusi, Sheikh Ibuni Salehe, Sheikh Juma Alley na mawaziri, walikuwa mikononi mwa serikali mpya na akaahidi kuwalinda mpaka hali itakapotulia.

Mohammed Shamte Hamad kwa upande wake, akawasihi wanachama na wapenzi wa ZPPP kuacha malumbano na mapambano na kusalimisha silaha zao kwa utaratibu uliowekwa na kuwataka wanachama wa ZPPP kuitii Serikali mpya. Mohammed Shamte alisema, “Serikali iliyoundwa jana, ndiyo Serikali ya Nchi na wanachama wetu wote hawana budi kuitii Serikali mpya”.

Naye Sheikh Ali Muhsin akatoa wito kwa wananchi kuacha mapambano na kusalimisha silaha zao na kuitii Serikali akisema, “Tukio limetokea, utake usitake. Kinachohitajika sasa ni kuijenga Zanzibar mpya na sote hatuna budi kushiriki”.<sup>29</sup>

Tukio hili la kihistoria linakwenda tofauti na taarifa nyingi kwenye magazeti, vitabu, mitandao, majarida na kauli za baadhi ya watu kuwa Sultani Jamshid aliikimbia nchi akiwa na Waziri Mkuu Shamte na Mawaziri wake.<sup>30</sup>

Tarehe 21 Januari, 1964 Mhe. Abeid Amani Karume, Rais wa Jamhuri ya Watu wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi alitangaza wajumbe wa Baraza la Mapinduzi la Serikali ya Jamhuri ya Watu wa Zanzibar wafuatao:

<sup>29</sup> ASP, THE AFRO-SHIRAZI REVOLUTION 1964 - 1974, Printpak Tanzania Ltd, Dar es Salaam, 1974, kur. 7-10.

<sup>30</sup> Wikipedia, *Zanzibar Revolution*, en.m.wikipedia.org; Conley R., “*African Revolt Overturns Arab Regime in Zanzibar*”, New York Times, January 13, 1964, p.1; Spellar, I., “*An African Cuba? Britain and the Zanzibar Revolution, 1964*”, in *Journal of Imperial & Commonwealth History*, 2007, p. 7.

1. Abdulla Kassim Hanga - Makamu wa Rais;
2. Abdurahman M. Babu - Waziri wa Mambo ya Nje na Biashara;
3. Hasnu Makame Mwita - Waziri wa Fedha;
4. Salehe Saadalla Akida - Waziri wa Kilimo;
5. Aboud Jumbe Mwinyi - Waziri wa Siha na Majumba;
6. Othman Shariff Mussa - Waziri wa Elimu;
7. Idriss Abdulwakil - Waziri wa Kazi na Nguvu za Umeme;
8. Abdulaziz Ali Twala – Msaidizi Waziri wa Ofisi ya Rais;
9. Hassan Nassor Moyo – Msaidizi Waziri wa Kazi na Nguvu za Umeme;
10. Seif Bakari Omar – Mjumbe;
11. Ramadhan Haji Faki – Mjumbe;
12. Abdalla Said Natepe – Mjumbe;
13. Said Iddi Bavuai – Mjumbe;
14. Said Washoto – Mjumbe;
15. Yusuf Himid – Mjumbe;
16. Mohamed Ameir (Kaujore) – Mjumbe;
17. Pili Khamis – Mjumbe;
18. Mohamed Mfaume Omar – Mjumbe;
19. Hafidh Suleiman Almas – Mjumbe;
20. Khamis Hemed Nyuni – Mjumbe;
21. Mohamed Mfaranyaki – Mjumbe;
22. Hamid Ameir – Mjumbe;
23. Khamis Daruwesh – Mjumbe;
24. Mohamed Juma Pindua – Mjumbe;
25. Khamis Abdulla Ameir – Mjumbe;
26. Edington Kisasi – Mjumbe;
27. Daudi Mahmoud Jecha – Mjumbe;
28. John Okello – Mjumbe; na
29. Muhsin bin Ali – Mjumbe.

### Baraza la Kwanza la Mapinduzi Zanzibar Mwaka 1964



*Chanzo: Zanzibar Government, 1990, kur. 28 na 29.*

# SURA YA PILI

## MISINGI YA MUUNGANO WA TANGANYIKA NA ZANZIBAR

### MISINGI YA MUUNGANO

#### Mazingira Rafiki na Wezeshi

Muungano wa Tanganyika na Zanzibar wa tarehe 26 Aprili, 1964 umekuwa na matokeo tofauti kabisa na mifano yote iliyojadiliwa katika Sura ya Kwanza. Mifano hiyo imedhihirisha wazi kuwa zoezi la kuunganisha nchi kwa nia njema ya kupata nguvu ya pamoja ili kuimarisha ulinzi na usalama na kuchochea tija kwenye nyanja zote za maendeleo, siyo jambo rahisi. Ni Muungano wa Tanganyika na Zanzibar pekee duniani uliofikiwa kwa makubaliano ya hiari baina ya wananchi wa nchi mbili huru na ambao hadi mwaka 2022 umedumu kwa zaidi ya nusu karne.

Sababu kuu ya kwanza iliyofanikisha Muungano huu udumu na kushamiri ni mazingira rafiki na wezeshi yaliyopo pande zote mbili za Muungano. Mazingira hayo wezeshi ambayo yanajieleza yenyewe kwenye Sura ya Kwanza ya kitabu hiki yalikosekana katika nchi nyingine zilizoungana au kujaribu kuungana.

#### Kihistoria

Watu wa Tanganyika na Zanzibar wana historia ya pamoja ya karne nyingi za ustawi bila kuingiliwa na wageni, na historia ya pamoja ya miongo mingi ya ukoloni, utumwa na mapambano ya ukombozi kama inavyobainishwa kwenye Sura ya Kwanza na sehemu mbalimbali za kitabu hiki. Ushahidi tele wa kihistoria unaonesha kuwa visiwa vya Zanzibar na ukanda wa pwani wa Tanzania Bara ambao ni sehemu

ya ukanda mrefu wa pwani wa Afrika Mashariki, ni eneo elekezi kwa vyombo vya majini vya safari ndefu za Mashariki ya Kati, India na Afrika na lenye fukwe rafiki na salama kwa vyombo vya majini kutia nanga kwa urahisi na wasafiri/mabaharia kujipatia mahitaji mbalimbali ya maji ya kunywa na vyakula nchi kavu bila matatizo.

Hakuna kumbukumbu za wafanyabiashara wa kale zinazosimulia hatari kwa maisha na mali kwenye fukwe za Afrika Mashariki. Kumbukumbu pekee za wafanyabiashara wa kale wa Kiajemi ni kukutana na wenyeji wenye ngozi nyeusi waliofanya nao biashara ya vyakula, bidhaa na mahitaji mengine na kuviita visiwa hivyo “Zanzibar” kutokana na neno la Kiajemi “Zinjibar” likimaanisha ukanda wa pwani wa watu weusi, yaani watu waliowakuta wakiishi kwenye visiwa hivyo.

Mwanzoni mwa karne ya tatu Waarabu walianzisha rasmi biashara na wenyeji wao, wengi wakiwa jamii ya Wabantu waliowakuta Zanzibar na pwani ya Afrika Mashariki ambao waliwasiliana kwa ishara na mchanganyiko wa Kiarabu na Kibantu. Katika mwingiliano huo ambao uliwahusisha wafanyabiashara wengine wa kigeni toka Uajemi, Bara Hindi, Ulaya na maeneo mengine, jamii ya rangi mchanganyiko haikuepukika visiwani na ukanda wa pwani wa bara.

Lugha mpya ya mawasiliano (Kiswahili), ikashika kasi na kuwa lugha kuu ya kiserikali, kibiashara na katika sanaa na mawasiliano ya mtu na mtu Tanzania Bara na Tanzania Zanzibar. Kiswahili kimewaunganisha wananchi wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kuwa jamii moja.

## Kijiografia

Tanganyika na Zanzibar kijiografia ni karibu kama inavyofafanuliwa kwa kina katika Sehemu ya Pili ya Sura ya Kwanza, Ujirani huo ndio ulioruhusu mwingiliano rahisi na mkubwa kati ya watu wa bara na visiwani kwa karne nyingi katika kutafuta fursa za kibiashara na maeneo mapya na mazuri ya kuishi na kuendesha kilimo cha mazao mbalimbali vikiwamo viungo na matunda. Umbali kijiografia kati ya nchi husika ni moja ya sababu zinazozuia mawasiliano ya haraka na ya moja kwa moja baina ya wadau wakuu wa Muungano au Shirikisho, yaani wananchi na hivyo kulifanya zoezi zima la Muungano au Shirikisho kuhodhiwa kwa kiasi kikubwa na viongozi.

Sura ya Kwanza inaujadili Muungano wa Misri na Syria uliounda Jamhuri ya Muungano wa Waarabu mwaka 1958 na kuvunjika rasmi mwaka 1971. Umbali wa kijiografia kati ya Misri na Syria ulichangia sana Muungano huo kudhoofika na hatimaye kuvunjika. Kwani kuifikia Misri au Syria ni kwa kuvuka nchi kadhaa, hivyo, ni lazima mtu awe na hati ya kusafiria na kibali maalum cha kuingia nchi nyingine.



*Ramani ikionesha eneo la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania mwaka 1964*

Ili Mmisri afike Syria, ilibidi apitie Jordan, Israel au Lebanon. Ikishindikana ilibidi avuke Mfereji wa Suez, aingie Saudi Arabia na kuivuka, halafu aingie Iraq nayo aivuke, ndipo aingie Syria.

Kwa watu wa Tanganyika na Zanzibar, hali ilikuwa tofauti. Hakuna nchi katikati ya kuivuka na ambayo ingemtaka Mtanganyika au Mzanzibari awe na hati ya kusafiria na viza. Walichohitaji ndugu hawa wawili kwa karne nyingi ni kuwa na chombo imara cha kusafiria kama jahazi, ngalawa, boti au mashua. Ikumbukwe kuwa, hitaji la hati ya kusafiria na viza lilikuja kuwekwa na wakoloni baadaye na hitaji hilo lilikuja kuondolewa baada ya Muungano.

### **Kibiashara, Kijamii na Kiutamaduni**

Mwingiliano ulioelezwa hapo juu kati ya wenyeji na wageni lukuki kutoka Mashariki ya Kati, Asia na Ulaya waliokuwa wakisaka fursa za kibiashara ukanda wa pwani ya Afrika Mashariki haukuathiri udugu wa damu wa bara na visiwani, ila ulizaa utamaduni maalum wa mwambao pamoja na kurutubisha lugha kuu ya mawasiliano, Kiswahili.

Kiswahili ni lugha ya Kibantu iliyokopa kama lugha nyingine zote duniani zinavyofanya katika ukuaji wake na katika mwingiliano wake na tamaduni nyingine. Hivyo, Kiswahili kina asilimia 60 ya lugha za Kibantu na kimekopa baadhi ya maneno kutoka lugha mbalimbali zikiongozwa na Kiarabu asilimia 30 na lugha nyingine: Kiingereza, Kireno, Kijerumani, Kiajemi na Kihindi asilimia 10<sup>1</sup>. Hivyo, asili ya Kiswahili, lugha ya kwanza ya Mtanzania ni Zanzibar na ukanda wa pwani wa Afrika Mashariki ambao sehemu kubwa upo Tanzania Bara<sup>2</sup>.

Mwingiliano wa watu kutoka mataifa mbalimbali katika ukanda wa pwani uliongezeka kuanzia karne ya saba ambapo mbali na kufanya biashara, wakaanza kueneza dini, hasa za Kiislamu (Waarabu) na Kikristo (Wareno). Kuanzia takriban karne ya 17 hadi mwishoni mwa karne ya 19, Tanganyika na Zanzibar zilikuwa sehemu ya mfumo mkubwa wa kibiashara uliunganisha mabara ya Afrika, Asia na Ulaya, na kufaidisha sana wageni waliokuwa wamekubuhu kibiashara.

Bidhaa muhimu kama vile: chumvi, viungo, vyakula, dhahabu, pembe za ndovu na vipusa, zilisafirishwa kutoka Tanganyika na maeneo mengine ya Afrika Mashariki, kati na kusini hadi pwani ya Afrika Mashariki na hatimaye kusafirishwa kwenda Uarabuni, India na Ulaya kupitia Zanzibar. Vivyo hivyo, bidhaa kutoka Uchina, Uarabuni, India na Ulaya ziliingia Afrika Mashariki na Kati kupitia Zanzibar.

Sehemu kubwa ya Watanzania ni Waislamu na Wakristo kutokana na historia ya mwingiliano mkubwa na wageni walioacha nchini sehemu ya utamaduni wao ambao umekuwa sehemu ya utamaduni wa nchi bila kutishia amani. Kwa Watanzania kuhama dini na kuoleana katika makundi haya makubwa ya dini si mambo ya kusimamisha mapigo ya moyo, bali ni sehemu ya maisha chini ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977 inayolinda haki ya uhuru wa mtu binafsi na uhuru wa mtu kuamini dini atakayo.<sup>3</sup> Katiba ya Zanzibar ya mwaka 1984 nayo inalinda uhuru huo.<sup>4</sup>

Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, ina kamati na asasi kadhaa za pamoja za viongozi wa kiroho zinazopewa ushirikiano na vyombo vya dola kupokea, kujadili na kufikisha Serikalini changamoto zinazojitokeza

<sup>1</sup> Ababaker, E. A., Maendeleo ya Lugha ya Kiswahili na Athari zake kwa Jamii ya Kiarabu: Mtazamo wa Kilughamiya, Tasnifu ya PhD Kiswahili, OUT 2013, Uk. 6

<sup>2</sup> Urefu wa pwani ya Tanzania Bara kutoka mpaka wake wa kusini na Msumbiji mpaka mpaka wake wa kaskazini na Kenya ni km 1,084.

<sup>3</sup> Haki ya uhuru wa mtu binafsi (Ibara ya 15) na uhuru wa mtu kuamini dini atakayo (Ibara ya 19).

<sup>4</sup> Haki na uhuru wa mtu binafsi (Ibara ya 14) na uhuru wa mtu kuamini dini atakayo (Ibara ya 19).



katika eneo la imani. Majukwaa haya ya majadiliano yamesaidia sana kuleta umoja na kuimarisha mshikamano wa kitaifa katika Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

## **Uzoefu wa Pamoja katika Utumwa, Ukoloni na Harakati za Uhuru**

Sura ya Kwanza ya kitabu hiki imeongelea historia ya Tanzania Bara na Tanzania Zanzibar ambayo imegusia masuala ya utumwa, ukoloni, harakati za ukombozi na mbio za uhuru na vikwazo vyake. Tanzania Bara na Tanzania Zanzibar zilipitia uzoefu uleule.

Mfano dhahiri ni biashara haramu ya watumwa Zanzibar. Pamoja na kwamba Zanzibar ilikuwa soko kubwa la watumwa katika ukanda wa Afrika Mashariki, watumwa wengi walikuwa wanatokea Bara na nchi za jirani kupitia bandari ya Bara ya Bagamoyo. Kama ni somo, pande zote mbili za Muungano zimelipata.

Ni kweli Sultani alitawala Zanzibar kwa zaidi ya karne mbili. Lakini wenye hoja dhidi ya Sultani wako pande zote mbili za Muungano kwani Sultani wa Zanzibar alikuwa vilevile mtawala wa eneo kubwa pwani ya Tanganyika lenye urefu wa kilometa 1,084 na upana wa zaidi ya kilometa 19. Hivyo, Watanganyika ukanda wa pwani walikuwa chini ya utawala wa Sultani wa Zanzibar kwa takriban miaka 190 kabla ya eneo hilo kuachiwa Wajerumani kwa makubaliano maalum kati ya Uingereza na Ujerumani.

Ni ukweli usiofichika kwamba, miaka 190 ni kipindi kirefu sana kuwasahaulisha watu madhila waliyopitia chini ya utawala wa Sultani. Ni Sultani aliyepua uhuru wa watu wa pwani kwenda na kutoka Zanzibar kila walipotaka. Ni Muungano wa Tanganyika na Zanzibar uliorejesha uhuru huo wa kwenda Zanzibar au kwenda Bara bila pasi ya kusafiria au viza.

Sura ya Kwanza pia imegusia uanzilishi na uanachama wa Mwalimu Nyerere na Sheikh Karume wa PAFMECA, vuguvugu la kupigania uhuru wa nchi za Afrika Mashariki na Kati lililozinduliwa Mwanza mwezi Septemba, 1958. Waliokuwa hawamjui Sheikh Karume vizuri walidhani alishawishiwa na Mwalimu Nyerere kushiriki bila kujua kuwa uzoefu wa miaka mingi wa Sheikh Karume katika nchi mbalimbali duniani, ulimkutanisha na miamba kadhaa ya Umajumui wa Kiafrika, akashawishika na hotuba zake zinathibitisha hilo.

Mwezi Aprili, 1959 Sheikh Karume, Rais wa ASP, alikuwa mwenyeji wa mkutano wa PAFMECA uliofanyika Zanzibar kwa mafanikio

makubwa. Ujumbe ulikuwa: ‘uhuru kwa nchi ambazo zilikuwa bado zinatawaliwa, na muungano wa nchi huru za Kiafrika kama msingi wa kuunganisha bara zima la Afrika’. Kuelekea azma hiyo, hatua ya kwanza waliipiga Karume na Nyerere, waumini wawili wakubwa wa *pan-Africanism*. Uwepo wa viongozi wa aina hiyo, ni mazingira wezeshi tosha kuupa muungano wowote ule msukumo stahiki.

TANU upande wa Bara na ASP upande wa Zanzibar vilimwelewa vizuri adui yao waliyekuwa wanakabiliana naye: Mwingereza, akimkingia kifua Mwarabu upande wa Zanzibar. Hivyo basi, vyama hivyo vikuu vya ukombozi vikajitengenezea mkakati wa kushirikiana kwa karibu na kusaidiana kwa hali na mali.

Mvuto mkubwa ambao vyama hivyo vilikuwa nao, ulichochea nguvu kubwa itumike upande wa serikali za kikoloni na vyama pinzani ili kuvipunguza nguvu na kasi. Ndiyo sababu ya shughuli nyingi za kisiasa za TANU na ASP kipindi hicho kuendeshwa kwa njia za kificho Bara na Zanzibar - kukwepa rungu la mkoloni na hujuma nyingine. Kesi dhidi ya Sheikh Abeid Karume iliyofunguliwa Mahakama Kuu tarehe 11 Juni, 1957 ili kumzuia asijiandikishe kama mpiga kura kwenye uchaguzi mkuu uliokuwa unafanyika wiki chache baadaye, ni mfano mzuri wa hila za kisiasa kipindi hicho. Mlalamikaji, Ali Ahmed Riyami (Mwarabu), alikula kiapo kusema kweli, kweli tupu kwamba alimwona Karume akiwa mdogo mgongoni kwa mama yake, wakishuka kutoka kwenye ngalawa akitokea Bara. Kesi hiyo ilitupiliwa mbali na Mahakama baada ya kubaini kuwa Riyami alikuwa mdogo kiumri kwa Karume kwa miaka 12.<sup>5</sup>

Mwalimu Julius Nyerere, Sheikh Abeid Karume na viongozi wenzao wa TANU na ASP walizitumia sana shughuli za kijamii (posa, harusi, ibada n.k.), burudani (ngoma, muziki wa dansi n.k.) na shughuli za michezo hasa mpira wa miguu uliokuwa kivutio kikubwa cha watu wengi kipindi hicho, kuhamasisha wananchi kudai haki yao ya kujitawala.

Mapema miaka ya 1950, Mwalimu Nyerere akiwa bado anafundisha shule ya sekondari ya *St. Francis* (baadaye Pugu) alifanyia mikutano yake ya siri ya kisiasa kwenye makao makuu ya klabu ya mpira wa miguu ya Yanga, jijini Dar es Salaam. Mikutano hiyo iliandamana na burudani nzito ya taarabu kutoka kikundi cha *Egyptian Musical Club* ili kuwapoteza njia Wazungu. Hata Mwalimu Nyerere alipoacha kazi ya kufundisha Pugu, mwezi Machi 1955, dereva aliyeaminiwa

<sup>5</sup> Mapuri, O.R., *The 1964 Revolution: Achievements & Prospects*, TEMA Publishers Company Ltd, 1996, Dar es Salaam, kur. 28 & 29; Mrina, B.F. na Mattoke, W.T., *Harakati za Ukombozi Zanzibar*, TPH, 1980, Dar es Salaam, uk. 62.

kumzungusha Mwalimu Nyerere nchini kunadi malengo ya TANU kwa wananchi, alikuwa Said Tanu, mwanachama maarufu wa Yanga. Sheikh Karume alitumia michezo hususan mpira wa miguu kuwahamasisha Waafrika kuunga mkono kampeni za kupata uhuru, siyo tu Zanzibar bali vilevile Bara. Sheikh Karume alianzisha klabu ya soka ya *African Sports* ya Zanzibar na aliichangia fedha Klabu ya Yanga ya Dar es Salaam ambayo iliwezesha kujenga Makao yake Makuu Mtaa wa Jangwani. Aidha, Sheikh Karume aliichangia fedha Klabu ya *African Sports* ya Tanga. Klabu hizo zilishiriki kwa njia mbalimbali kwenye kampeni za uhuru, Bara na Zanzibar.

Kumbukumbu zinaonesha viongozi wa Yanga na *African Sports* ya Tanga walikutana Zanzibar na baadaye Dar es Salaam kabla ya uhuru wa Tanganyika kuongelea “ushirikiano katika michezo” huku wakijiweka malengo na mikakati ya kuvisaidia vyama vya ukombozi wa Tanganyika na Zanzibar, TANU na ASP.

Moja ya matokeo ya mikutano hiyo ni mapambano mawili ya soka Gymkhana (Karume), Dar es Salaam na Kajengwa Makunduchi, Zanzibar, yaliyofana sana. Fedha iliyopatikana kutokana na viingilio, ilipelekwa moja kwa moja TANU na ASP kuendeleza mapambano dhidi ya ukoloni. Hivyo, harakati za ukombozi wa Tanganyika na Zanzibar zilikwenda sambamba ndani ya jamii na kuratibiwa kwa pamoja ili kuzishinda mbinu za Waingereza na Waarabu, watawala wenza wa Zanzibar.

Mambo mengi aliyoyafanya Sheikh Karume Tanganyika na Zanzibar kabla ya uhuru wa Tanganyika na kabla ya Muungano, ni ushahidi tosha kuwa kiongozi huyu alikuwa mwana-Umajumui wa Kiafrika wa kweli na muumini wa mstari wa mbele wa Muungano wa Tanganyika na Zanzibar na umoja wa Afrika.

### “Ushindi wa Mezani” wa ZNP na ZPPP

Taarifa za uchaguzi ulivyoendeshwa Bara na Zanzibar zimejadiliwa kwa kirefu katika Sura ya Kwanza na Sura hii ya Pili na mbinu za kuongeza majimbo zilivyofanyika Zanzibar na kusababisha matokeo ya kichekesho: mwenye kura nyingi zaidi ya nusu ya kura zote anapata viti vichache. Ushindi wa aina hii huitwa “ushindi wa mezani”. Madhumuni ya uchaguzi Zanzibar hayakuwa ya kumtafuta mshindi wa kuunda Serikali, yalikuwa ya kumsindikiza Sultani kuendelea na utawala wa kikoloni Zanzibar. Matokeo hayo hayakuinyong’onyesha ASP peke yake na wanachama wake bali vilevile TANU, wanachama wake, Watanzania Bara wote na wana-Umajumui wa Kiafrika wote.

ASP muda wote ilikuwa inapigania uhuru wa Zanzibar kutoka kwa Waingereza na Waarabu wa Oman. Ilikuwa inapigania upatikanaji wa Jamhuri ya Watu wa Zanzibar. Walicholetewa Wazanzibari ni Usultani wa Kiarabu na uzinduzi rasmi wa taifa la Kiarabu Kusini mwa Jangwa la Sahara ambalo kwa vyovyote vile lingeendelea kuwa sehemu ya himaya ya Oman.<sup>6</sup>

Pamoja na Sheikh Karume na viongozi wenzake wa ASP kusikika mara kadhaa wakisisitiza kuwa Zanzibar ni nchi ya Kiafrika ambayo haiwezi kugeuzwa kuwa ya Kiarabu,<sup>7</sup> azma ya watawala iliendelea kuwa tofauti. Waingereza walishayafanya haya Australia, walitwaa ardhi yote ya wenyeji bila ya makubaliano wala fidia kwa kutumia kanuni ya kisheria ya *terra nullius*, yaani ardhi isiyo na mtu, hivyo, ruksa kwa aliyewahi kuihodhi na kuitumia. Hoja hiyo iliandaliwa kutumika Zanzibar.

Kanuni hiyo ya kihafidhina ilisababisha kutungwa nchini Australia sheria za ardhi zilizowanyang'anya wazawa haki yote kuhusu ardhi yao, na hivyo, maeneo mbalimbali yakachukuliwa na raia na makampuni ya Uingereza bila makubaliano wala fidia yoyote. Kesi za kudai haki kwa wazawa zikashindwa mwaka 1971, 1977, na 1979 kwa mahakama za Australia kuisitiza kuwa kabla ya kuingia kwa Wazungu, ardhi yote ilikuwa haina mwenyewe.

Bila kukata tamaa, wazawa wengine watano (Eddie Koiko Mabo na wengine wanne) wakalifikisha tena suala hilo mahakamani (Mabo dhidi ya Queensland) mwaka 1982. Kesi hiyo ilinguruma kwa miaka 10 na hatimaye, tarehe 03 Juni, 1992, Mahakama Kuu ikatupilia mbali hoja hiyo ya *terra nullius* na kuwarejeshea wazawa haki yao ya ardhi.<sup>8</sup> Hakuna aliyetarajia kipindi hicho cha miaka ya 1950 na 1960 kuwa kanuni hiyo ingekuja kutupiliwa mbali na mahakama ya juu katika mfumo wa sheria wa *common law* ambao unatumia pia na Tanzania.

Kwa maelezo yote yaliyotangulia, vuguvugu la uhuru miaka ya 1950 na 1960 lilishuhudia nguvu kubwa ikitumiwa na wakoloni kuhakikisha kuwa maslahi yao yanaendelea kulindwa baada ya uhuru. Lakini kutokana na mshikamano wa nguvu wa wananchi wa Tanganyika na

<sup>6</sup> Waandishi wengi wa historia walikuwa wakiita Zanzibar ya kabla ya Mapinduzi, "Oman's overseas territory" au eneo la ng'ambo la Oman.

<sup>7</sup> Hotuba ya Karume kwenye mkutano wa hadhara Raha Leo mwezi Desemba, 1959 inakumbukwa na wazee wengi hadi leo kubeba ujumbe huo. Angalia *Parliamentary Debates (Commons)*, 5<sup>th</sup> Series, DLXXVIII (London: H.M.S.O., Dec.3, 1957), Cols. 190-191.

<sup>8</sup> Soma uamuzi wa Mahakama Kuu katika kesi ya *Mabo v. Queensland (2)*, Mahakama Kuu ya Australia, 1992. Walikaa kusikiliza na kufanya maamuzi majaji 7: sita walikubali kuitupilia mbali hoja ya *terra nullius*, lakini jaji mmoja akakataa.

Zanzibar, ushirikiano wa karibu wa vyama vyao vya awali vya kiraia vya *African Association* vilivyoanzishwa mwaka 1927 (Tanganyika) na 1933 (Zanzibar) na mikakati ya pamoja ya vyama vyao vya kupigania uhuru vya TANU na ASP, wakoloni hawakufua dafu.

Ushahidi wa kihistoria upo wa *African Association* ya Tanganyika na ya Zanzibar kufanya mikutano ya pamoja ya mwaka kuanzia mwaka 1939 hadi mwaka 1941 ambapo mikutano hiyo ilisitishwa kutokana na sababu mbalimbali ikiwamo kuzuka kwa Vita kuu ya Pili ya Dunia ambayo iliigusa Afrika Mashariki vilevile.<sup>9</sup> Mikutano hiyo ilifanyika Zanzibar, Dar es Salaam na Dodoma kwa mzunguko.

Yote haya ni sehemu ya misingi imara iliyojengeka kwa miaka mingi ya Muungano, ambayo mtu hawezi kupata mfano wake duniani. Ni katika misingi hiyohiyo, vyama vya ukombozi na uhuru vya TANU na ASP, viliweza kwa shangwe na hamasa kuungana na kuunda chama kipya cha pamoja, Chama Cha Mapinduzi (CCM) miaka 13 baada ya kuzaliwa kwa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Hatua hiyo vilevile haina mfano wake duniani.

## Kauli na Matendo ya Viongozi Shuruti Yaakisi Muungano

Viongozi wa kitaifa wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania wanapokabidhiwa madaraka kuiongoza nchi wanakula kiapo “kuihifadhi, kuilinda na kuitetea Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania” na “kutetea na kudumisha Umoja kwa mujibu wa Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania”. Kwa Watanzania Muungano ni sehemu ya tunu ya Taifa ya Umoja ambayo viongozi hawana budi kuiishi au kufanana nayo kwa kauli na vitendo.

Tanzania ilibahatika kupata viongozi wake wa kwanza, Mwalimu Julius Nyerere na Sheikh Abeid Karume, waumini wa Umajumui wa Kiafrika walioamua kuanza na nchi zao kutimiza ndoto ya kuunganisha nchi huru za Afrika kikanda na hatimaye kuunda Muungano wa nchi za Afrika. Wakaunda vuguvugu la ukombozi wa nchi za Afrika Mashariki, Kati na Kusini - PAFMECA<sup>10</sup> na kujihusisha na shughuli zake kimamilifu.

<sup>9</sup> Mrina, B na Mattoke, W., Harakati za Ukombozi Zanzibar, TPH, Dar es Salaam, 1980, kur. 45-49.

<sup>10</sup> Baadaye PAFMECA ilipopanuka na kujihusisha pia na ukombozi wa nchi za kusini mwa Afrika ikaitwa PAFMECSA.

Hawakuishia hapo, kwa juhudi zao wakashuhudia Tanzania ikiaminiwa kuwa Makao Makuu ya Kamati ya Ukombozi ya Umoja wa Afrika na Mwenyekiti wa Nchi zilizokuwa Mstari wa Mbele wa Ukombozi Kusini mwa Afrika. Kuhusu Muungano, Mwalimu Nyerere na Sheikh Karume waliongoza kwa mifano, kauli zao na matendo yao yaliakisi Muungano.

Viongozi hao wawili waliichia Jamhuri ya Muungano msingi imara wa umoja na muungano kwani hata baadaye maswali yalipojitokeza kuhusu muundo wa Muungano, Serikali haikusita kuchukua hatua na kuunda Tume ya Jaji Kisanga mwaka 1999 ambayo ilihoji wananchi wapatao 600,000.

Matokeo yalikuwa kama ifuatavyo: Tuwe na Serikali Moja tu ya Tanzania (waliounga mkono asilimia 6.54); Tubaki na Serikali Mbili (waliounga mkono asilimia 88.87) na Tuwe na Serikali Tatu (waliounga mkono asilimia 4.32).

## Uwiano katika Mgawanyo wa Madaraka na Ustawi

Moja ya masuala makubwa ya Muungano ambayo Mwalimu Julius Nyerere aliyahubiri kwa muda mrefu na kuacha nasaha nzito miongoni mwa wananchi ni hadhi ya Zanzibar kama nchi iliyoungana na Tanganyika kuunda Tanzania na uhuru wake kwenye mambo yasiyokuwa ya Muungano. Kwa mujibu wa Baba wa Taifa, suala lolote la Muungano lazima liwe na ushiriki wa pande zote mbili kwa uzito unaolingana hata kama idadi ya washiriki itatofautiana kwa hesabu za uwakilishi.

Mfano ni upitishaji wa mabadiliko ya mambo ya Muungano kuhusu kuwapo kwa Jamhuri ya Muungano, kuwapo kwa Ofisi ya Rais wa Jamhuri ya Muungano, madaraka ya Serikali ya Muungano, kuwapo kwa Bunge la Jamhuri ya Muungano, madaraka ya Serikali ya Zanzibar, Mahakama Kuu ya Zanzibar, Orodha ya Mambo ya Muungano na Idadi ya Wabunge kutoka Zanzibar, unahitaji kuungwa mkono na theluthi mbili ya wabunge wote kutoka Tanzania Bara na theluthi mbili ya wabunge wote kutoka Tanzania Zanzibar. Hapa wabunge wanaweza kupishana kwa idadi lakini si kwa uzito wa maamuzi yao.

Elimu kwa umma imesaidia sana kupunguza maswali kuhusu Muungano. MATHALANI, Mambo ya Muungano kuhisiwa tu kuwa yanaongezwa kinyemela wakati yanapitishwa na pande zote mbili za Muungano kwa mujibu wa Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya 1977 na hakuna suala la Muungano lisilojadilika. Haki ya Mzanzibari kumiliki ardhi Zanzibar na sehemu nyingine yoyote ya Jamhuri ya

Muungano kuonekana kuwa upendeleo uliopitiliza kwa Wazanzibari na uonevu kwa ndugu zao wa Bara. Elimu kwa umma imesaidia kuondoa hisia kama hizo kwa maelezo kuwa mbali na uhaba wa ardhi Zanzibar, Tanzania Bara ina ardhi ya kutosha kwa kila Mtanzania mhitaji na hata wageni wenye nia ya kuwekeza.

Sura ya Tano ya kitabu hiki inaelezea kwa kirefu hoja za Muungano na utatuzi wake, hivyo mambo yote ya msingi kuhusu utatuzi wa changamoto mbalimbali za Muungano yamejadiliwa.

## Mapokezi ya Muungano Kimataifa

Wananchi kuunga mkono maamuzi makubwa kama ya kuunganisha nchi, ni suala muhimu la kutia nguvu linaloupa Muungano msukumo mkubwa. Jumuiya ya kimataifa kuunga mkono maamuzi kama hayo, ni suala la kutia moyo na kuufanya Muungano ushamiri. Muungano wa Tanganyika na Zanzibar ulipata yote haya mawili, haukupokelewa kwa hisia za kipekee ndani ya nchi tu bali hata jamii ya kimataifa nayo iliutazama Muungano wa nchi hizi mbili kwa jicho la matumaini.

Hali hiyo ilidhihirika wazi pale ambapo nchi mbalimbali duniani zilipotuma salamu za pongezi kwa Rais wa Jamhuri, Mwalimu Julius Kambarage Nyerere, mara baada ya kutangazwa kuanzishwa kwa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania (wakati huo ikiitwa Jamhuri ya Muungano wa Tanganyika na Zanzibar).

Miongoni mwa nchi zilizotuma salamu za pongezi mapema ni nchi ya Marekani kupitia Rais wake wakati huo Lyndon B. Johnson ambaye katika salamu zake alieleza:

Kwa niaba ya Serikali na watu wa Marekani nakupelekea salaam nyingi za pongezi kwa ajili ya kuzaliwa kwa Jamhuri ya Muungano wa Tanganyika na Zanzibar. Jambo hili lililoanzishwa na Waafrika la kuunganisha nchi mbili zilizo huru, litatazamwa kote duniani kuwa ni mwenge wa Afrika kumulika njia iendayo kwenye haki ya watu kujichagulia wenyewe wapendalo kufanya na umoja, na njia hiyo hatimaye itaishia katika kupatikana utashi wa watu wote wa Afrika...

Kwa upande wake Waziri Mkuu wa Uingereza, Sir Alec Douglas-Home, alisema:

Nakupa pongezi nyingi wewe mwenyewe (Rais Nyerere) na Makamu wa Kwanza wa Rais, Karume kwa hatua ya busara mliyochukua hata mkaanzisha Muungano wa Tanganyika na Zanzibar. Nawaombea heri, furaha na ustawi watu wa Tanganyika na Zanzibar katika ushirikiano wao mpya.

Baadhi ya viongozi wakuu wengine waliotuma salamu zao walikuwa Rais Sekou Toure wa Guinea, Rais Aden Abdullah Osman wa Jamhuri ya Somalia, Rais Ahmed Ben Bella wa Algeria na Mfalme Haile Selassie I wa Ethiopia. Sambamba na hao, marais Radhakrishnan wa India, Philbert Tsiranana wa Madagascar, Ahmadou Ahidjo wa Shirikisho la Jamhuri ya Cameroun, William V. S Tubman wa Liberia na Gamal Abdel Nasser wa Muungano wa Jamhuri ya Kiarabu walituma salamu za pongezi.

Pamoja nao, wengine waliotuma salamu za pongezi ni: Waziri Mkuu Jomo Kenyatta wa Kenya, Waziri Mkuu wa Canada Lester B. Pearson, Waziri Mkuu wa Rhodesia ya Kaskazini Kenneth Kaunda na Mwenyekiti Liu Shao-chih wa Jamhuri ya Watu wa China.

Salamu hizo za viongozi mbalimbali duniani wakiwamo hao wa Uingereza na Marekani zinaonesha wazi namna Muungano wa Tanganyika na Zanzibar ulivyoleta shauku kubwa duniani, shauku ambayo ilikuwa deni kwa Mwalimu Nyerere na Sheikh Karume kuhakikisha kuwa Muungano unafanikiwa.

Katika muktadha wa kimataifa, salamu zinazotolewa na viongozi wakuu wa nchi kuelekea nchi zilizoungana ni kitendo kinachoashiria kulikubali jambo lililofanywa na nchi hizo na kutoa mwelekeo wa ushirikiano baina ya serikali zao na serikali za nchi zilizoungana kama ilivyokuwa kwa Jamhuri ya Tanganyika na Jamhuri ya Watu wa Zanzibar. Kinyume chake serikali au nchi zilizoungana huweza kukosa ushirikiano kutoka kwa nchi nyingine na hata kutokukubaliwa kuwa sehemu ya jumuiya ya kimataifa.<sup>11</sup>

Hivyo basi, salamu kutoka kwa viongozi hao kwa Muungano wa Tanganyika na Zanzibar ziliashiria mwitikio chanya wa nchi hizo kuanzia Uhuru wa Tanganyika tarehe 9 Desemba, 1961, kuwa Jamhuri tarehe 9 Desemba, 1962, Mapinduzi ya Zanzibar tarehe 12 Januari, 1964 na hatimaye Muungano tarehe 26 Aprili, 1964.

---

<sup>11</sup> Lauterpacht, H., *Recognition in International Law*, 1<sup>st</sup> Edition, Cambridge University Press, Cambridge, 2013.



# SURA YA TATU

## MUUNGANO WA TANGANYIKA NA ZANZIBAR

### MATUKIO MUHIMU KUELEKEA MUUNGANO

Muungano wa Tanganyika na Zanzibar ulitanguliwa na matukio kadhaa muhimu ya kisiasa ambayo yaliwezesha nchi mbili hizo kuungana. Matukio muhimu yaliyotokea kuelekea Muungano huo yameainishwa katika Sura hii.

Kupatikana kwa uhuru wa Tanganyika tarehe 9 Desemba, 1961 ambao uliwapa Watanganyika madaraka ya ndani tu ambapo Mwalimu Nyerere alikuwa Waziri Mkuu, hivyo Mkuu wa Serikali na Malkia wa Uingereza alikuwa Mkuu wa Nchi. Hali hii iliwanyima usingizi viongozi wa TANU ambao walitaka Tanganyika iwe Jamhuri bila ya uhusiano wa moja kwa moja na Ufalme wa Uingereza mapema iwezekanavyo.

Hivyo, mwezi mmoja tu baada ya uhuru wa Tanganyika, TANU ikapendekeza Serikalini kuanzishwa mara moja kwa mchakato wa kuiondoa Tanganyika kutoka kwenye himaya ya Uingereza na kuwa Jamhuri. Tarehe 5 Februari, 1962 Bunge la Tanganyika likaipitisha hoja ya kuelekeza Serikali kuandaa muswada wa mabadiliko ya Katiba kuiwezesha Tanganyika kuwa Jamhuri ndani ya Jumuiya ya Madola. Mwezi Novemba, 1962 ukashuhudiwa uchaguzi wa Rais wa Kwanza wa Jamhuri ya Tanganyika<sup>1</sup> na utungaji wa Katiba ya Jamhuri ya Tanganyika<sup>2</sup>. Tanganyika ikawa Jamhuri chini ya Rais Julius Kambarage Nyerere.

<sup>1</sup> President Designate (Election) Act, No. 40, 1962

<sup>2</sup> Republican Constitution, C.A. Act No.1, 1962 (Cap.499)

Uhuru bandia wa Zanzibar tarehe 10 Desemba, 1963 ulianzisha Usultani wa Kikatiba na himaya ya Kiarabu Afrika Mashariki. Wazalendo wa Zanzibar wakaamua kuusahihisha “uhuru” huo kupitia Mapinduzi Matukufu ya tarehe 12 Januari, 1964 na kuzaliwa Jamhuri ya Watu wa Zanzibar chini ya Rais Abeid Amani Karume. Kimsingi Mapinduzi Matukufu ya Zanzibar yalikitika kiu ya Wazanzibari kujikomboa kutoka katika makucha ya wakoloni na utawala wa Sultani na kutimiza malengo ya Umajumui wa Kiafrika.

Akithibitisha dhamira ya Umajumui wa Kiafrika aliyokuwa nayo Mwalimu Nyerere, Sheikh Karume na viongozi wengine wa Kiafrika kipindi cha vuguvugu la ukombozi wa Afrika; Mwalimu alitamka bayana tarehe 2 Januari, 1965 kwamba hata kama ASP ingeingia madarakani kwa njia ya kikatiba na wala si kwa mapinduzi, bado Muungano wa Tanganyika na Zanzibar ungefanyika<sup>3</sup>. Dhamira ya dhata ya viongozi hao ilikuwa ni chachu ya kurasimisha Muungano uliokuwapo miaka mingi kati ya watu wa nchi hizi mbili.

## HATUA MUHIMU KUKAMILISHA MUUNGANO

Hatua saba muhimu ziliifikisha Jamhuri ya Muungano wa Tanzania hapa ilipo:

**Hatua ya Kwanza:** Waasisi wa Muungano, Mwalimu Julius Kambarage Nyerere na Sheikh Abeid Amani Karume, kuwa na mazungumzo ya siri wao na viongozi wengine kwa niaba ya wananchi. Mazungumzo hayo yalikuwa yakifanyika pande zote mbili za Muungano, yakiratibiwa na kusimamiwa na wao wenyewe ili kuepusha kuvuja kwa siri kutokana na mazingira ya kisiasa yaliyokuwepo wakati ule, ambapo Zanzibar ilitoka katika kupata uhuru wake wa kweli kupitia Mapinduzi. Kwa vyovyote vile tahadhari ilihitajika ili kuepusha kutoa nafasi kwa maadui wa Muungano kuingilia na kuathiri uwepo wa Muungano huo. Ikumbukwe kuwa, Muungano wetu umefanyika miezi mitatu tu baada ya kufanyika Mapinduzi ya Zanzibar ambayo yalifanyika tarehe 12 Januari, 1964 na Muungano ukafanyika tarehe 26 Aprili, 1964.

**Hatua ya Pili: Tarehe 22 Aprili, 1964** Rais Nyerere na Rais Karume, kwa niaba ya wananchi wote wa Tanganyika na Zanzibar (walionesha njia ya ushirikiano kwa miaka mingi) kwa kusaini Hati ya Makubaliano ya Muungano Ikulu, Mjini Zanzibar. Wakati mkataba wa Muungano unasainiwa, Rais Nyerere aliambatana na Roland Brown (Mwanasheria Mkuu wa Serikali), P.R.N Fifoot (Mwandishi Mkuu wa Sheria), Oscar

<sup>3</sup> Salaam za mwaka mpya za Rais Nyerere kwa wananchi.

Kambona (Waziri wa Mambo ya Nje), Job Lusinde (Waziri wa Mambo ya Ndani), na Bhoke Munanka (Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais).

Kwa upande wake, Rais Karume wa Zanzibar aliambatana na Abdulla Kassim Hanga (Makamu wa Rais wa Zanzibar), Abdulazizi Twala (Naibu Waziri Afisi ya Rais) na Ali Mwinyigogo (Msaidizi wa Rais Ikulu).



*Mwalimu Julius Kambarage Nyerere na Sheikh Abeid Amani Karume wakisaini Hati za Makubaliano ya Muungano, Tarehe 22 Aprili, 1964 Zanzibar. Wanaoshuhudia kwa karibu tukio hilo kushoto kwa Mwalimu ni Kasim Hanga na kulia ni Oscar Kambona*

**Hatua ya Tatu: Tarehe 25 Aprili, 1964** Hati ya Makubaliano ya Muungano iliridhiwa na Mamlaka za Kutunga Sheria. Kwa wakati ule, kwa upande wa Tanganyika chombo kilichokuwa na Mamlaka ya Kutunga Sheria kilikuwa ni Bunge na kwa upande wa Zanzibar chombo cha kutunga sheria kilikuwa ni Baraza la Mapinduzi ambalo lilifanya kikao chake asubuhi ya siku hiyo ya tarehe 25 Aprili, 1964 Ikulu, Zanzibar na Bunge la Tanganyika lilifanya kikao chake siku hiyohiyoni katika Ukumbi wa Bunge wa Karimjee, Dar es Salaam.

Wakati Zanzibar ikiridhia Hati ya Makubaliano ya Muungano, Mwalimu Nyerere alimtuma Oscar Kambona (Waziri wa Mambo ya Nje) kama mjumbe wake kwenda kushuhudia tukio hilo baada ya kupewa mwaliko kutoka kwa Rais Karume. Vilevile, Rais Karume kupitia mwaliko aliopata kutoka kwa Mwalimu Nyerere alimtuma Salim Rashid (Katibu Mkuu wa Baraza la Mapinduzi), kwenda kushuhudia tukio la kuridhia Hati ya Makubaliano ya Muungano ambapo kwa mujibu wa aliyekuwa Katibu wa Spika wa Bunge la Tanganyika, Bwana Pius Msekwa, alimpokea mjumbe huyo kama mgeni maalum kutoka kwa Rais Abeid A. Karume.

Kwa mujibu wa Bwana Pius Msekwa, akizungumza na waandishi wa kitabu hiki, alieleza kuwa, baada ya Bunge la Tanganyika kuridhia Hati ya Makubaliano ya Muungano tarehe 25 Aprili, 1964, alipeleka Muswada wa Sheria ya Muungano wa Tanganyika na Zanzibar kwa Rais Nyerere saa mbili na nusu usiku wa siku hiyohiyo Ikulu ya Magogoni - Dar es Salaam na Mheshimiwa Rais Mwalimu Julius Kambarage Nyerere alisaini Muswada huo.

Tukio la Rais Nyerere kusaini Muswada wa Sheria ya Muungano wa Tanganyika na Zanzibar lilishuhudiwa na baadhi ya Viongozi akiwamo Mzee Rashid Mfaume Kawawa (Makamu wa Rais wa Serikali ya Jamhuri ya Watu wa Tanganyika), Pius Msekwa (Katibu wa Bunge), Bw. Amir Jamal (Ofisi ya Rais), Bw. Bhoke Munanka (Waziri katika Ofisi ya Makamu wa Rais) na Bw. Roland Brown (Mwanasheria Mkuu wa Serikali).

Kwa mujibu wa Sheria ya Muungano wa Tanganyika na Zanzibar, Sheria namba 22 ya mwaka 1964, Sheria ya Muungano wa Zanzibar na Tanganyika pamoja na Hati ya Makubaliano ya Muungano ziliweka bayana kuwa, baada ya kuridhiwa kwa Hati ya Makubaliano ya Muungano, siku inayofuata ndiyo itatambulika rasmi kuwa ni siku ya Muungano. Kwa muktadha huo, tarehe 26 Aprili, 1964 ikawa ndio siku rasmi ya Muungano wa Tanganyika na Zanzibar.



*Picha ya pamoja ya viongozi wa Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania*

**Hatua ya Nne: Tarehe 27 Aprili, 1964** ndiyo siku ambapo Bunge jipya la Jamhuri ya Muungano lilianza kazi, moja ya tukio kubwa katika tarehe hiyo ilikuwa ni kubadilishana Hati ya Makubaliano ya Muungano, tukio ambalo lilifanyika katika Ukumbi wa Karimjee, mjini Dar es Salaam wakati wa kikao cha Bunge cha jioni. Mheshimiwa Spika wa Bunge hilo, Mhe. Chief Adam Sapi Mkwawa, aliwatangazia Wabunge kuwa, Rais Nyerere atahudhuria katika Bunge hilo pamoja na Rais Karume ili waweze kubadilishana Hati za Makubaliano ya Muungano, hivyo, kutokana na taratibu za Bunge aliliahirisha Bunge kwa muda na baadaye zoezi la kubadilishana hati likafanyika, likiambatana na vigelegele na shangwe kubwa pamoja na vilio vya 'Uhuru na Umoja', 'Uhuru na Muungano' kutoka kwa Waheshimiwa wajumbe wa Bunge la Tanganyika na wa Baraza la Mapinduzi la Zanzibar<sup>4</sup>. Pamoja na matukio mengine, katika kikao hicho waliapishwa kiapo cha uaminifu ndani ya Bunge Wajumbe kutoka Zanzibar wakiongozwa na Sheikh Abeid Amani Karume, Bw. Abdalla Kassim Hanga, Bw. Abdulrahman Mohamed Babu, Bw. Hassan Nassor Moyo na Sheikh Idriss Abdulwakil Nombe.



*Sheikh Abeid Amani Karume akiapishwa katika Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania tarehe 27 Aprili, 1964*


<sup>4</sup> Taarifa rasmi ya majadiliano ya Bunge katika kikao cha pili cha tarehe 27 Aprili, 1964.

Kuapishwa kwa viongozi hao siku hiyo ni kutokana na kutimiza matakwa ya kisheria kupitia Sheria ya Kuridhia Makubaliano ya Muungano, ambayo imeweka vifungu mahususi kwa ajili ya Utekelezaji wa Makubaliano hayo. Kwa mfano, Kifungu cha 5 (c) kinaeleza kwamba, wateuliwe Makamu wawili wa Rais wa Jamhuri ya Muungano. Uteuzi huo ulifanyika siku hiyo ya tarehe 27 Aprili, 1964 ambapo Sheikh Abeid Amani Karume, Rais wa Zanzibar, aliteuliwa kuwa Makamu wa Kwanza wa Rais wa Jamhuri ya Muungano, na Bw. Rashid Mfaume Kawawa aliteuliwa kuwa Makamu wa Pili wa Rais wa Jamhuri ya Muungano. Aidha, Kifungu cha 5 (d) kinaeleza kwamba, wawepo wawakilishi wa Zanzibar katika Bunge la Jamhuri ya Muungano.

**Hatua ya Tano: Tarehe 28 Aprili, 1964** ambapo Baraza Jipya la Jamhuri ya Muungano wa Tanganyika na Zanzibar lenye Mawaziri 23 liliapishwa katika ukumbi wa Karimjee huku watano kati yao wakiwa ni kutoka Zanzibar. Kuapishwa kwa Baraza hilo ilikuwa ni kielelezo cha kwamba, Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanganyika na Zanzibar imeanza rasmi kwa mara ya kwanza tokea kusainiwa kwa Makubaliano ya Muungano ya tarehe 22 Aprili, 1964.

**Hatua ya Sita: Tarehe 30 Aprili, 1964** Wizara ya Mambo ya Nchi za Nje ilimjulisha Katibu wa Umoja wa Mataifa, Bw. U Thant kuwa, Nchi za Jamhuri ya Tanganyika na Jamhuri ya Watu wa Zanzibar zimeungana na kuunda nchi moja inayoitwa “Jamhuri ya Muungano wa Tanganyika na Zanzibar”. Wakati huo Waziri wa Mambo ya Nchi za Nje alikuwa Bw. Oscar Kambona, na hapo ndipo nafasi ya Jamhuri ya Muungano wa Tanganyika na Zanzibar katika ukumbi wa vikao vya Umoja wa Mataifa ikawa ni kati ya Uingereza (*United Kingdom*) na Marekani (*United States of America*). Mwezi Oktoba, 1964 Bunge la Jamhuri ya Muungano lilibadili jina la Jamhuri ya Muungano wa Tanganyika na Zanzibar na kuwa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kupitia Sheria ya Kubadili Jina la Jamhuri ya Muungano wa Tanganyika na Zanzibar ya mwaka 1964. Kufuatia mabadiliko hayo, tarehe 2 Novemba, 1964 Katibu Mkuu wa Umoja wa Mataifa alifahamishwa kuhusu mabadiliko ya jina la nchi naye alikiri kujulishwa tarehe 18 Desemba, 1964.

**Hatua ya Saba: Tarehe 26 Aprili, 1965** tukio la kuchanganya udongo wa Tanganyika na Zanzibar lilifanyika katika Uwanja wa Uhuru, Dar es Salaam kama alama ya kudhihirisha Muungano wa udugu wa kudumu. Sehemu ya udongo huo ilitumika kupanda mti wa mwembe katika Viwanja vya Ikulu ya Dar es Salaam ambao upo hadi sasa. Baada ya tukio hilo, kulifanyika sherehe za kuadhimisha mwaka mmoja wa Muungano.



*Mwalimu Julius K. Nyerere akichanganya udongo wa Tanganyika na Zanzibar huku akishuhudiwa na Rais Abeid Amani Karume na Mhe. Rashidi Mfaume Kawawa Makamu wa Pili wa Rais na Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania wakati wa sherehe za Muungano tarehe 26 Aprili, 1965. Walioshika chungu ni Bw. Hassan Omari Mzee (kulia) na Bw. Hasanaeli Mrema (kushoto)*



*Mwembe uliopandwa katika Viwanja vya Ikulu, Dar es Salaam kwa kutumia sehemu ya udongo wa Tanganyika na Zanzibar uliochanganywa tarehe 26 Aprili, 1965*

## WAZUNGU, WASOMI NA HOJA YA MUUNGANO

Kutokana na kasumba ya muda mrefu kwamba hakuna jema linaloweza kufanyika Afrika bila mkono wa Mzungu, wasomi lukuki wamekuwa wakihaha kuutafuta mkono huo wa Mzungu.

Amrit Wilson, mwandishi wa vitabu na mwandishi wa habari mwenye asili ya India anayeishi Uingereza, alitunga kitabu mwaka 1989 akiueleza ulimwengu kuwa Muungano wa Tanganyika na Zanzibar haukutokana na juhudi za Nyerere na Karume wala sababu zozote za ndani, bali mikakati ya kijasusi ya Marekani na Uingereza kuzuia kusambaa kwa ukomunisti Afrika ya Mashariki.<sup>5</sup>

Madai hayo yaliwafurahisha sana wapinga Mapinduzi ya Zanzibar na Muungano wa Tanganyika na Zanzibar, wakiambiwa kuwa yangeleta shinikizo la kimataifa kuirejesha Zanzibar chini ya utawala wa kikoloni wa Waarabu wa Oman. Utangulizi wa kitabu hicho uliandikwa na Abdurahman Babu akikubali madai ya uwepo wa mashinikizo ya kijasusi kuunda Muungano wa Tanzania.

Madai ya Wilson hayakutokana na uchambuzi wa kisomi wa hali halisi na ushahidi wowote ule wa kihistoria, bali vivuli vya mawasiliano ya maandishi kati ya maafisa wa Serikali ya Marekani na Uingereza na wa balozi zao Afrika Mashariki wakiulizana kuhusu hali ya Zanzibar bila uthibitisho kama mawasiliano hayo yalifanyiwa kazi.

Akijibu madai ya Amrit Wilson, Prof. Ethan Sanders wa Chuo Kikuu cha Bridgewater, Massachusetts, Marekani amesema:

Ufuatiliaji wa karibu wa nyaraka za siri za kiusalama za Marekani ambazo hivi karibuni ziliondolewa usiri ... zinathibitisha kuwa Muungano huu haukuwa mpango wa Marekani wala Uingereza. ... **Ushahidi unaonesha kuwa Wamarekani hawakujua kilichokuwa kinaendelea. Wazo la kuunganisha Tanganyika na Zanzibar lilikuwa bila shaka yoyote la Waafrika wenyewe, wazo lenye historia yake ndefu kuanzia miaka ya 40 kabla ya wasiwasi wa Wamarekani na Waingereza kuhusu Mapinduzi ya Zanzibar**<sup>6</sup> (Msisitizo umeongezwa).

Hata Rais George H. W. Bush wa Marekani wakati huo akiwa Mwakilishi wa Kudumu wa Marekani katika Umoja wa Mataifa, akichangia mjadala kwenye Kikao cha 26 cha Baraza la Umoja wa Mataifa, tarehe 25 Oktoba, 1971 saa 9 mchana alitoa mfano wa Tanganyika na Zanzibar kuwa nchi mbili huru barani Afrika zilizoungana kwa hiari na kuwa nchi moja.

<sup>5</sup> Wilson, A, *US Foreign Policy and Revolution; the Creation of Tanzania*, London, Pluto Press, 1989, kur. 1, 8-9

<sup>6</sup> Sanders, E.R., *Conceiving the Tanganyika-Zanzibar Union in the Midst of the Cold War: Internal and International Factors*, *African Review*, Vol. 41, Nov. 1, 2016, pp.35-70.



Wakati wasomi wa nje wanakiri kuwa Muungano wa Tanganyika na Zanzibar ni matokeo ya fikra na juhudi za Waafrika wenyewe, baadhi ya wasomi na wanahabari wa Kiafrika bado wanang'ang'ania nadharia ya mkono wa Mzungu! Mathalani, kila mwaka kipindi cha Muungano baadhi ya magazeti ya Tanzania yanazitumia porojo hizo za Magharibi kuuzia magazeti yao na vichwa vya habari visemavyo: "MUUNGANO WA TANGANYIKA-ZANZIBAR 1964: CIA ILIVYOANZA KUINGILIA SIASA ZA ZANZIBAR"; "SHIRIKA LA UJASUSI LA MAREKANI (CIA) LILIHUSIKA KUUNDWA MUUNGANO WA TANGANYIKA NA ZANZIBAR KUKABILIANA NA UKOMUNISTI"<sup>7</sup> n.k. bila kujali athari zake kwa vijana wa Taifa la Tanzania.

Pamoja na makala hizo kukosa hoja za utafiti wa kitaalamu, bado ni fedheha kwa Waafrika kushindwa kuona kuwa Muungano wa Tanganyika na Zanzibar ni mfano pekee wa malengo ya Umajumui wa Kiafrika uliobaki na kudumu kwa zaidi ya nusu karne baada ya majaribio mengine mengi kushindwa. CIA wenyewe wamekiri kutohusika, lakini Waafrika wenyewe pengine kutokana na miaka mingi ya kutawaliwa, bado wanaamini kuwa kila zuri linalotokea Afrika lazima liwe na mkono wa Mzungu.

Baba wa Taifa alitufundisha kuwa: *Ili tuendelee, tunahitaji vitu vinne tu: watu, ardhi, siasa safi na uongozi bora. Mzungu anaingizwaje hapa?*

Katika kudhihirisha kukosekana kwa hoja kwa wakosoaji wa Muungano, Mapuri anasisitiza kuwa:

Muungano ulikuwa matokeo yaliyotarajiwa ya mahusiano ya karibu baina ya vyama vya Waafrika vya Tanganyika na Zanzibar ambayo yaliendelezwa kipindi chote cha kudai uhuru kupitia vyama vya TANU na ASP. ... (Muungano) uliasisiwa na Watanzania kwa maslahi yao wenyewe na siyo kwa maslahi ya Wamarekani.<sup>8</sup>

Maelezo ya kina katika sura hii ya uhusiano wa miaka mingi (hata kabla ya ujio wa wakoloni) kati ya Watanganyika na Wazanzibari kijamii, kibiashara na kisiasa ndiyo msingi wa Muungano wa nchi hizi mbili. Hivyo, hata madai ya baadhi ya wasomi kwamba Muungano haukujengwa kwenye misingi imara<sup>9</sup> (maana walitegemea kura ya maoni ifanyike) na kwamba wananchi hawakushirikishwa ipasavyo<sup>10</sup>

<sup>7</sup> Mwananchi, Ijuma, Aprili 12, 2019, kuhusu Muungano wa Tanganyika na Zanzibar 1964, sehemu ya 3.

<sup>8</sup> Mapuri, O.R., *kama hapo juu*, uk. 6

<sup>9</sup> Shivji, I., Pan-Africanism or Pragmatism? Lessons of Tanganyika-Zanzibar Union, pp.97-99; Mwakikagile, G., *the Union of Tanganyika and Zanzibar: Product of Cold War?*

<sup>10</sup> Shivji, I., *kama hapo juu*, uk. 98.

(maana walitegemea mchakato huo utanguliwe na uelimishaji wa wananchi) yamepata sehemu ya majibu katika Sura hii.

Wanachosahau wasomi wengi ni kuchambua kila suala katika muktadha wake na uhalisia wake. Tanganyika na Zanzibar zilikuwa nchi huru mpya ambazo huko nyuma zilitengenezewa mipaka na kutawaliwa bila ridhaa ya wananchi. Ni nchi zilizopitia kipindi kirefu cha fedheha na mateso ya zaidi ya karne moja ya watu wake kukamatwa kwa ajili ya biashara ya utumwa na kuuzwa nje kama mifugo.

Katika hali ambayo uhuru unapatikana baada ya mapambano ya zaidi ya miaka 200 dhidi ya ukoloni, je, hatua ya kwanza kwa nchi mpya ni kuitisha kura ya maoni kujua kama wananchi wanataka umoja au ushirikiano waliokuwa nao kabla ya ukoloni kuwatengenezea mipaka ya kuwatenganisha? Je, hatua ya kwanza ni “kuwaelimisha” wananchi kuhusu faida za umoja au ushirikiano waliokuwa nao kabla ya ukoloni?

Ndiyo maana imesisitizwa mara kadhaa katika kitabu hiki kuwa msingi wa Muungano wa Tanganyika na Zanzibar ni historia ya karne nyingi ya ushirikiano wa watu wa nchi hizi mbili, ushirikiano ambao ulirasimishwa tarehe 26 Aprili, 1964. Wasomi wengi wanashindwa kuliona hilo, wanaishia kumwona Mwalimu Nyerere na Sheikh Karume na siyo nguvu ya umma nyuma yao iliyowapa dhamira ya kusonga mbele na kurasimisha ushirikiano wa nchi hizi mbili.

Matukio yote ya kurasimisha Muungano kama utiaji saine wa Hati ya Makubaliano ya Muungano uliofanywa na Rais Nyerere wa Tanganyika na Rais Karume wa Zanzibar tarehe 22 Aprili, 1964 mjini Zanzibar na tukio la kubadishana Hati ya Makubaliano ya Muungano tarehe 27 Aprili, 1964 katika Ukumbi wa Karimjee, jijini Dar es Salaam, yalifuatiliwa na wananchi pande zote mbili kwa hamasa na shauku kubwa. Gazeti la kihafidhina la *The New York Times* likiripoti kutoka Dar es Salaam tarehe 23 Aprili, 1964 lilithibitisha kuwa taarifa za Muungano wa nchi hizi mbili zilipokewa vizuri na wananchi na kuleta ahueni nchini.<sup>11</sup>

Kumekuwapo pia na madai ya muda mrefu kwamba Zanzibar haikuridhia Hati ya Makubaliano ya Muungano, hivyo, msingi wa kisheria wa Muungano ulikuwa na utata. Aliyeanzisha mjadala huo alikuwa Wolfgang Dourado, Mwanasheria Mkuu wa Zanzibar, katika kipindi cha Muungano aliyedai katika mada yake mwaka 1983 kuwa Mkataba huo wa Muungano uliridhiwa na Bunge la Tanganyika lakini

---

<sup>11</sup> Ukurasa wa mbele wa gazeti la Marekani la *The New York Times*, lililochapishwa tarehe 24 Aprili, 1964.

siyo Baraza la Mapinduzi, kinyume na matakwa ya Hati ya Makubaliano ya Muungano.<sup>12</sup>

Baadhi ya watafiti walihoji dhamira ya Dourado, Mwanasheria Mkuu wa Zanzibar aliyekuwa na dhamana ya kuhakikisha kuwa mikataba inaridhiwa na kutangazwa kwenye Gazeti la Serikali. Mwanasheria Mkuu huyohuyo kuibuka miaka 19 baada ya Hati ya Makubaliano ya Muungano kuridhiwa na kuanza kulalamikia uhalali wa nyaraka alizokuwa anazisimamia yeye mwenyewe, kulizua mashaka mengi ikiwamo hujuma upande wa maafisa wa sultani walioendelea kuitumikia Serikali ya Mapinduzi kama Dourado. Hii ni kwa sababu haukuwa wajibu wa Karume wala wa wajumbe wenzake wa Baraza la Mapinduzi kuhakikisha kuwa maamuzi yote ya kisheria ya Baraza yanachapishwa kwenye Gazeti la Serikali, bali wajibu wa Mwanasheria Mkuu.<sup>13</sup>

Ni Zanzibar hiyohiyo ambayo baada ya Mapinduzi ilichapisha maelfu ya vitabu vya historia mwaka 1973 vilivyoandaliwa na ASP, ambavyo vilielezea historia ya Zanzibar katika juzuu tatu kwa uwazi kuhusu madhila ya Waafrika kabla ya Mapinduzi na wakati wa mapambano ya kudai uhuru. Vitabu hivyo vilivyotarajiwa kusambazwa katika shule zote ili kujenga uelewa wa kutosha wa historia kwa watoto, vilitoweka bila nakala kubaki. Mapuri anaamini kuwa hiyo ilikuwa kazi ya wapinga Mapinduzi.<sup>14</sup>

Watafiti wengi akiwamo Prof. Shivji walichunguza kwa kina madai ya Dourado na kubaini kuwa kweli hakukuwa na nakala yoyote ya Gazeti la Serikali ya Zanzibar mwaka 1964 na 1965 iliyoweka kumbukumbu ya kuridhiwa kwa Hati ya Muungano kwa mujibu wa sheria.<sup>15</sup> Hata hivyo, mwanazuoni huyo anasema kuwa kukosekana kwa ushahidi wa uridhaji wa Mkataba wa Muungano kwenye Gazeti la Serikali hakuwezi peke yake kisheria kuwa ushahidi kwamba Mkataba huo haukuridhiwa.

Prof. Shivji anakumbushia ushahidi uliomo kwenye kumbukumbu za majadiliano ya Bunge kuanzia Aprili 25 hadi Mei 12, 1964; ubadilishanaji wa nyaraka za maridhiano Bungeni (ukumbi wa Karimjee) tarehe 27 Aprili, 1964; uapishwaji siku hiyo wa wajumbe watano wa Baraza la Mapinduzi kuwa Wabunge wa Jamhuri ya Muungano wa Tanganyika na Zanzibar (Karume, Hanga, Moyo, Babu na Wakil), na kwamba hakuna

<sup>12</sup> Dourado, W., *Consolidation of the Union*, mada aliyowasilisha katika semina ya Chama cha Wanasheria cha Tanganyika, Dar es Salaam, tar. 28 Julai, 1983.

<sup>13</sup> Angalia Mlimuka A., *Constitutional Development and the Democratisation Process in Zanzibar (1964-1985)*, LL.M Dissertation, UDSM, uk. 246, Mwakyembe, H.G., *kama hapo juu*, uk. 181

<sup>14</sup> Mapuri, O.R., *kama hapo huu*, uk. 6.

<sup>15</sup> Shivji I.G., *Tanzania: The Legal Foundations of the Union*, Dar es Salaam University Press, 1990, uk. 4.

kipindi chochote ambapo uhalali wa Hati ya Makubaliano ya Muungano ulihojiwa na Baraza la Mapinduzi.<sup>16</sup>

“Hivyo basi”, Shivji anahitimisha kwa kusema, “Uongozi Zanzibar pamoja na vyombo vya Serikali vinaweza kuchukuliwa kuwa viliridhia Hati ya Makubaliano na Muungano kwa kuafiki kwa vitendo”.<sup>17</sup>

Pamoja na ufafanuzi wa Prof. Shivji kuendana na Sheria za Kimataifa na maamuzi ya Mahakama ya Kimataifa katika kesi mbalimbali za aina hiyo, kwamba kimya au kutochukua hatua katika kukamilisha makubaliano kwa muda mrefu, ni kuafiki kwa vitendo, suala hili lilipata jibu la uhakika mwaka 1992 kupitia Tume ya Nyalali iliyoundwa kupendekeza mfumo wa chama kimoja au vyama vingi. Dourado aliteuliwa miongoni mwa wajumbe 23 wa Tume hiyo.

Tume ya Nyalali (akiwamo na Dourado) iliridhika kuwa Baraza la Mapinduzi lilikutana na kuridhia Hati ya Makubaliano ya Muungano tarehe 25 Aprili, 1964 kuendana na maelezo kwa Tume ya wajumbe wawili wa Baraza la Mapinduzi, Abdurahman Babu na Khamis Ameer.<sup>18</sup>

## MUUNDO WA MUUNGANO

### Hati ya Makubaliano ya Muungano, Katiba na Sheria

Muundo wa Muungano wa Tanganyika na Zanzibar umefafanuliwa katika Hati ya Makubaliano ya Muungano iliyosainiwa na Mwalimu Julius K. Nyerere, Rais wa Jamhuri ya Tanganyika na Sheikh Abeid A. Karume, Rais wa Jamhuri ya Watu wa Zanzibar tarehe 22 Aprili, 1964 mjini Zanzibar.

Hati hiyo ya Makubaliano ya Muungano ndiyo msingi mkuu kikatiba na kisheria wa kuasisiwa kwa Muungano wa Tanganyika na Zanzibar. Hati hii ina hadhi ya mkataba wa kimataifa. Aidha, kwa mfumo wa kikatiba uliopo unaotaka Mikataba ya Kimataifa ipate ridhaa ya Bunge kwa kutungiwa sheria mahususi ili kuifanya Mikataba hiyo kuwa na nguvu ya kisheria na kuanza kutumika<sup>19</sup>, Ibara ya (viii) ya Hati ya Makubaliano ya Muungano ilieleza kuwa, Bunge la Tanganyika na Baraza la Mapinduzi yatatakiwa kutunga sheria za kuuridhia Mkataba wa Muungano.

<sup>16</sup> Shivji, *kama hapo juu*, uk. 4 na 5.

<sup>17</sup> *Kama hapo juu*.

<sup>18</sup> Othman, H., *Tanzania: The Withering Away of the Union*, Chr Michelsen Institute, 1993, Bergen, uk. 20.

<sup>19</sup> Mfumo huo unaitwa *dualism*. Nchi nyingine hufuata mfumo wa *monism* ambapo mikataba ya kimataifa inapewa uzito uleule wa sheria za ndani na kuanza kutumika bila ya kuridhiwa na Bunge.

Ni kwa muktadha huo, Bunge la Tanganyika lilitunga Sheria ya Muungano wa Tanganyika na Zanzibar, Sheria Na. 22 ya mwaka 1964 ambayo ilichapishwa katika Gazeti la Serikali ya Muungano Na. 243 la tarehe 1 Mei, 1964 ili kukamilisha mchakato wa kuridhia Mkataba huo. Vilevile, kwa upande wa Zanzibar, Baraza la Mapinduzi lilitunga Sheria ya Muungano wa Zanzibar na Tanganyika ya mwaka 1964. Hivyo, Sheria za Muungano pamoja na Hati ya Makubaliano ya Muungano zimekuwa sehemu ya Sheria za Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kuanzia tarehe 26 Aprili, 1964.

## **Maelekezo Mahususi ya Hati ya Muungano**

Sheria ya Muungano pia ilitambua kuwapo kwa Baraza la Wawakilishi na Serikali ya Zanzibar kwa mujibu wa Sheria za Zanzibar na kwa mambo ambayo siyo ya Muungano. Vilevile, Sheria za Muungano zilimtaka Rais wa Jamhuri ya Muungano kutoa Amri ili kuirekebisha Katiba ya Tanganyika iweze kukidhi matakwa ya Hati za Muungano na kuweza kuiongoza Jamhuri ya Muungano. Aidha, kwa mujibu wa kifungu cha 10 cha Sheria ya Muungano, Rais alipaswa kuziwasilisha Amri hizo Bungeni kwa taarifa.

Kwa mujibu wa mamlaka hayo, tarehe 1 Mei, 1964 Rais wa Jamhuri ya Muungano kwa kushauriana na kukubaliana na Rais wa Zanzibar alitoa Amri mbili zilizoweka utaratibu wa kikatiba na kisheria wa kusimamia kipindi cha mpito. Amri hizo ni Amri ya Masharti ya Kipindi cha Mpito ya Mwaka 1964 na Amri ya Katiba ya Muda ya Mwaka 1964. Amri ya Masharti ya Kipindi cha Mpito ilitamka kwamba tangu siku ya Muungano kila kilichokuwa cha Tanganyika kitageuka kuwa cha Jamhuri ya Muungano.

Aidha, kwa kupitia Amri ya Katiba ya Muda, Katiba ya Jamhuri ya Tanganyika iligeuzwa kuwa Katiba ya Jamhuri ya Muungano baada ya kuifanyia marekebisho katika baadhi ya ibara ili ikidhi mabadiliko yaliyotokana na Muungano. Vilevile, jina la Jamhuri ya Muungano wa Tanganyika na Zanzibar lilibadilishwa na kuwa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania<sup>20</sup> kupitia sheria ya Bunge iitwayo Sheria ya Kubadili Jina la Jamhuri ya Muungano wa Tanganyika na Zanzibar ya mwaka 1964 na

<sup>20</sup> Jina la Tanzania ambalo taifa linajivunia kuwa tunu muhimu; lilibuniwa kupitia shindano la kubuni jina hilo. Watu 16 walijitokeza katika shindano hilo ambapo mwanafunzi Mohammed Iqbar Dar mwenye asili ya Kiasia wa shule ya sekondari ya Aga Khan (Forest Hill) aliibuka mshindi. Mwanafunzi huyo aliyekuwa na miaka 18, alizaliwa mkoa wa Tanga mwaka 1944. Aidha, alikabidhiwa zawadi ya dola za Marekani 200 na Mheshimiwa Sheikh Idriss Abdulwakil, Waziri wa Habari na Utalii wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar tarehe 20 Novemba, 1964.

jina hilo lilianza kutumika rasmi tarehe 28 Oktoba, 1964. Kifungu cha 2 (1) cha Sheria hiyo kinaeleza.

Kwa tafsiri isiyo rasmi kifungu hicho kinamaanisha:

Pamoja na maelekezo ya Kifungu cha 4 cha Sheria za Muungano, inatamkwa kwamba Jamhuri ya Tanganyika na Jamhuri ya Watu wa Zanzibar zitalazimika kuanzia sasa kujulikana kama Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, na sheria zilizopo za Tanganyika na Zanzibar zitasomeka katika msingi huo.

Ibara ya 34 (1) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977 inatamka kwamba, kutakuwa na Serikali ya Jamhuri ya Muungano ambayo itakuwa na Mamlaka juu ya Mambo yote ya Muungano katika Jamhuri ya Muungano, na pia juu ya mambo mengine yote yahasuyo Tanzania Bara. Aidha, Ibara ya 102 (1) inatamka kwamba, kutakuwa na Serikali ya Zanzibar itakayojulikana kama “Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar” ambayo itakuwa na mamlaka katika Zanzibar juu ya mambo yote yasiyo Mambo ya Muungano kwa mujibu wa masharti ya Katiba hii.

Kwa mujibu wa Hati ya Makubaliano ya Muungano ambayo pia imekuwa msingi mkuu wa Katiba ya Jamhuri ya Muungano ya mwaka 1977, ni dhahiri kwamba muundo wa Muungano huu ni wa shirikisho lenye Serikali mbili ambazo ni Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kwa kuzingatia mahitaji na hali halisi ya nchi husika. Muundo wa Muungano ukikwepa kuzingatia mahitaji na hali halisi ya nchi husika, matokeo yake hayawi mazuri kama ilivyokuwa kwa Shirikisho la Senegambia lililokuwa na mazingira sawa na ya Tanganyika na Zanzibar ambalo limejadiliwa kwenye Sura ya Kwanza ya kitabu hiki.

## **Uchaguzi wa Mfumo wa Serikali (Moja, Mbili au Tatu)**

Kwa upande mwingine mtu anaweza kujiuliza ni kwa nini mfumo wa serikali mbili ulichaguliwa na Watanzania na siyo mfumo wa serikali moja au tatu? Mwalimu Nyerere anaelezea katika kitabu chake *Freedom and Unity* (1967):

... Kwa upande wa Tanzania, ingekuwa vigumu sana kuchagua muundo wa serikali moja mwaka 1964, hasa kutokana na ukubwa wa Tanganyika.  
... Zanzibar ni ndogo kijiografia na kwa idadi ya watu...<sup>21</sup>

<sup>21</sup> Nyerere, J.K., *Freedom and Unity*, OUP, Dar es Salaam, 1967.

Uamuzi wa kuchagua mfumo wa serikali mbili badala ya moja au tatu kwa mujibu wa Mwalimu, ulifanyika kwa umakini kwa kuzingatia hali halisi ya nchi zetu na kuhakikisha kwamba pande zote mbili zinakuwa na uwakilishi sawa katika Muungano. Hivyo, Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977, Ibara ya 4(2) inasema kuwa “vyombo vyenye mamlaka ya utendaji vitakuwa ni Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar” ambapo Mfumo huu unaendelea hadi leo.

Kumekuwa na hoja nyingi za wasomi wakihoji uamuzi wa Tanzania wa kuwa na serikali mbili zenye majukumu matatu. Hoja yao kubwa ni kwamba shirikisho la nchi mbili lazima liwe na majukumu matatu yenye serikali tatu kama ilivyo ughaibuni. Lakini ughaibuni hukohuko kuna ubunifu mkubwa unaofanywa katika miundo ya muungano kukidhi mahitaji na hali halisi ya washiriki, mfano mzuri sana ni wa Shirikisho la Bremen (ndani ya Shirikisho la Ujerumani), ambalo washirika wake wawili *City of Bremen* na *Port of Bremen* wana serikali mbili tu na mabunge mawili tu kupunguza gharama na mzigo wa kubeba gharama za mamlaka ya tatu upande wa mshirika mdogo.

Ni katika muktadha huohuo kama wa Bremen, muundo wa shirikisho la Tanganyika na Zanzibar umebeba ubunifu unaoendana na uhalisia wa nchi husika ambao umewezesha Muungano wa nchi hizi mbili kudumu na kushamiri kwa zaidi ya nusu karne na kuwa mfano pekee uliobaki barani Afrika wa Umajumui wa Afrika. Suala si idadi ya serikali, bali mgawanyo wa madaraka kati ya nchi husika na shirikisho na mipaka ya mamlaka kikatiba/kisheria kati yao.

## Ukusanyaji wa Maoni ya Wananchi

Kutokana na maoni ya baadhi ya wananchi kuendelea kuhoji muundo huu wa serikali mbili, Serikali ilitoa Waraka Na. 1 wa mwaka 1998 ambao ulikuwa na mapendekezo tisa ambapo wananchi walitakiwa kutoa maoni yao. Serikali ilitoa fursa kwa wananchi kutoa maoni yao kuhusu muundo wa Muungano kupitia Tume ya Jaji Kisanga ya mwaka 1999. Katika mapendekezo hayo, pendekezo la kwanza lilihusu muundo wa Serikali unaofaa. Kulikuwa na aina tatu za muundo zilizotolewa ambazo ni:

1. Mfumo wa Serikali tatu: Serikali ya Tanganyika, Serikali ya Zanzibar na Serikali ya Muungano au,
2. Mfumo wa Serikali moja: Serikali ya Muungano wa Tanzania au,

3. Mfumo wa Serikali mbili: Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar.

Kazi ya kukusanya maoni ya wananchi ilihusisha mikoa yote 25 ambapo mikoa 20 ilikuwa Tanzania Bara na mikoa mitano ilikuwa Tanzania Zanzibar. Wananchi wapatao 600,000 walishiriki katika zoezi hili kwa njia tofauti kama ilivyopangwa na Tume.

Kwa ujumla, maoni ya wananchi kuhusu muundo wa Serikali yalikuwa: Serikali moja asilimia 6.54, Serikali mbili asilimia 88.87 na Serikali tatu asilimia 4.32.

Tume ilitekeleza majukumu yake na kuwasilisha mapendekezo yake Serikalini. Baada ya Serikali kupitia mapendekezo hayo iliamua kuwa mfumo wa sasa wa Serikali mbili yaani Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar uendelee kutumika kwa kuwa uliungwa mkono na wananchi wengi.<sup>22</sup>

## Muungano Shirikisho au Jumuishi?

Ubunifu wa kikatiba wa Tanzania wa kuhakikisha Muungano unaleta umoja, amani na ustawi katika Taifa na kuendelea kuwa kichocheo cha Umajumui wa Kiafrika na hatimaye Muungano wa Bara la Afrika, umesababisha wanazuoni na wasomi mbalimbali kupishana juu ya aina ya Muungano huu wa Tanzania. Kwa mfano, Ghai na De Smith wao wanauona Muungano wa Tanganyika na Zanzibar kuwa na sura ya shirikisho au nusu-shirikisho mtawalia<sup>23</sup>. Srivastava, Shivji, Kabudi na Mwakyembe wanaona kuwa Muungano huu ni shirikisho, lakini kila mmoja ana mtazamo tofauti katika ufafanuzi wake.

Wanakubaliana kuwa Muungano wa Tanzania umeunda mamlaka tatu na serikali mbili. Mamlaka hizo ni Tanganyika (Tanzania Bara), Zanzibar na Jamhuri ya Muungano wa Tanzania wakati serikali ni ile ya Zanzibar yenye mamlaka yasiyo ya Muungano yanayoihusu Zanzibar na Serikali ya Muungano yenye mamlaka juu ya masuala yote yahasuyo Muungano na masuala yasiyo ya Muungano yaihusuyo Tanzania Bara kama ilivyobainishwa katika Ibara ya 33, Ibara ndogo ya Kwanza na Ibara ya 102 Ibara ndogo ya Kwanza na ya Pili za Katiba ya Jamhuri ya

<sup>22</sup> Taarifa ya Tume ya Jaji Kisanga, 1999.

<sup>23</sup> Ghai, Y.P. "Constitutions and the Political Order in East Africa" 21 Int'l Comp.L, 1972, kur. 303,422; De Smith, S.A. *Constitutional and Administrative Law* (4<sup>th</sup> edn), Penguin Books, 1981 kur. 25-26.



Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977. Baadhi yao wanakiri kuwa ni shirikisho maalum, la kipekee, *sui generis*.<sup>24</sup>

Maalim naye anauona Muungano wa Tanganyika na Zanzibar kuwa na sura ya kipekee tofauti na aina nyingine za muungano duniani na kuishia kukubaliana na wengine kuwa muundo wa muungano unaweza ukachukua sura za miundo mbalimbali na kuleta muundo wa aina yake na ya kipekee kama ilivyo kwa Muundo wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.<sup>25</sup>

## MAMBO YA MUUNGANO

Hati ya Makubaliano ya Muungano, Ibara ya (iv) inalipa Bunge na Serikali ya Jamhuri ya Muungano (SMT) mamlaka juu ya mambo 11 ya Muungano yafuatayo:

1. Katiba ya Tanzania na Serikali ya Jamhuri ya Muungano;
2. Mambo ya Nje;
3. Ulinzi;
4. Polisi;
5. Mamlaka juu ya mambo yanayohusika na hali ya hatari;
6. Uraia;
7. Uhamiaji;
8. Biashara ya Nje na Kukopa;
9. Utumishi wa Umma katika Jamhuri ya Muungano;
10. Kodi ya mapato, kodi ya mashirika, ushuru wa forodha na bidhaa; na
11. Bandari, usafiri wa anga, posta na simu.

Ibara hiyo pia inalipa Bunge na Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, mamlaka kwa mambo yote yaliyoorodheshwa kuwa ya Muungano na kwa mambo yote yasiyo ya Muungano yanayoihusu Tanganyika na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar (SMZ) yenye mamlaka kwa mambo yasiyo ya Muungano yanayoihusu Zanzibar. Pia, Mkataba unaeleza kuwa kutakuwa na Baraza la Wawakilishi Zanzibar na Bunge la Jamhuri ya Muungano yenye mamlaka kama zilivyo Serikali.

<sup>24</sup> Srivastava, B.P., *The Constitution of the United Republic of Tanzania of 1977: Some Salient Features-Some Riddles*, Dar es Salaam, Dar es Salaam University Press; Shivji, I.G. , *The Legal Foundation of the Tanzania's Union and Zanzibar Constitutions*, DUP, 1990; Kabudi, P.J., *International Law Examination of the Union of Tanganyika and Zanzibar*, 1986; Mwakyembe, H.G.), *Tanzania's Eighth Constitutional Amendment and Its Implication on Constitutionalism, Democracy, and the Union Question*, 1995, Hamburg, uk. 186.

<sup>25</sup> Maalim, J.M., *The United Republic of Tanzania in the East African Community: Legal Challenges in Integrating Zanzibar*, Dar es Salaam University Press, Dar es Salaam, 2014.

Ibara ya (iii) imeelekeza kutumika kwa Katiba ya Tanganyika iliyorekebisha kuwa Katiba ya Jamhuri ya Muungano katika kipindi cha mpito ili kuanzisha Bunge na Mamlaka ya Utendaji kwa ajili ya Zanzibar kwa mujibu wa Sheria za Zanzibar. Vyombo hivyo vitakuwa na Mamlaka Kamili ndani ya Zanzibar kwa mambo yasiyokuwa ya Muungano.

Ibara ya (vi) (a) ya Hati ya Makubaliano ya Muungano inamtaja Mwalimu Julius K. Nyerere kuwa Rais wa Kwanza wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Ibara ya (vi) (b) inamtaja Sheikh Abeid Amani Karume kuwa Makamu wa Kwanza wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

## **Kuongezeka kwa Mambo ya Muungano**

Orodha ya Mambo ya Muungano ya mwaka 1964 imeongezewa mambo mengine 11 na kuifanya Orodha hiyo iwe na jumla ya Mambo ya Muungano 22. Yaliyoongezeka ni haya yafuatayo:

1. Mambo yote yanayohusika na sarafu na fedha kwa ajili ya malipo yoyote halali (pamoja na noti); mabenki (pamoja na mabenki ya kuweka akiba) na shughuli zote za mabenki; fedha za kigeni na usimamizi juu ya mambo yanayohusika na fedha za kigeni;
2. Leseni za Viwanda na Takwimu;
3. Elimu ya Juu;
4. Maliasili ya Mafuta, pamoja na mafuta yasiyochujwa ya motokaa na mafuta ya aina ya petroli na aina nyinginezo za mafuta au bidhaa, na Gesi asilia;
5. Baraza la Taifa la Mitihani la Tanzania na mambo yote yanayohusika na kazi za Baraza hilo;
6. Usafiri na usafirishaji wa anga;
7. Utafiti;
8. Utabiri wa Hali ya Hewa;
9. Takwimu;
10. Mahakama ya Rufani ya Jamhuri ya Muungano; na
11. Uandikishaji wa Vyama vya Siasa na mambo mengine yanayohusiana navyo.

## **Sababu za Kuongezeka kwa Mambo ya Muungano**

Ongozeko hili la Mambo ya Muungano mapya 11 lilitokana na mabadiliko yaliyokuwa yanaendelea kufanyika katika Jumuiya ya Afrika Mashariki na mahitaji ya ndani ya wananchi. Orodha hiyo imekuwa ikifanyiwa

mabadiliko kwa mujibu wa Katiba na Sheria na kwa kushirikisha pande zote mbili za Muungano.

Jambo la kwanza kuongezwa, yaani la 12 lilikuwa ni “sarafu, mabenki na fedha za kigeni”. Hili lilifanyika tarehe 10 Juni, 1965 kufuatia kuvunjika kwa Bodi ya Sarafu ya Afrika Mashariki mwaka 1964. Kwa ajili hiyo, kila nchi mwanachama wa Jumuiya ililazimika kuwa na sarafu yake na mipango yake ya kusimamia mambo yake ya kibenki na fedha. Serikali zetu mbili zilikubaliana kuwa masuala hayo yashughulikiwe na Serikali ya Muungano na muswada husika wa Bunge uliidhinishwa kuwa Sheria na Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano, Mhe. Abeid Amani Karume tarehe 10 Juni, 1965 wakati huo akikaimu Urais wa Jamhuri ya Muungano.

Tarehe 11 Agosti, 1967 yaliongezwa mambo ya Leseni za Viwanda na Takwimu (Jambo la 13) na Elimu ya Juu (Jambo la 14). Tarehe 22 Julai, 1968 suala la “rasilimali ya mafuta, petroli na gesi asilia” liliongezwa kwenye Orodha ya Mambo ya Muungano na kuwa jambo la 15 kufuatia makubaliano ya pande zote mbili kuipa Serikali ya Muungano jukumu la kuagiza mafuta ya petroli na gesi asilia kwa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Kufuatia kuvunjika kwa Jumuiya ya Afrika Mashariki mwaka 1977 na kutungwa kwa Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya Mwaka 1977 mambo ya Muungano yaliyoongezeka ni: Baraza la Mitihani la Taifa (jambo la 16); Usafiri na usafirishaji wa anga (jambo la 17); Utafiti (jambo la 18); Utabiri wa Hali ya Hewa (jambo la 19); na Takwimu (jambo la 20).

Jambo la 21 kuongezeka ni Mahakama ya Rufani ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania iliyoanzishwa mwaka 1979 kufuatia kuvunjika kwa Mahakama ya Rufani ya iliyokuwa Jumuiya ya Afrika Mashariki mwaka 1978.

Vilevile, kufuatia mapendekezo yaliyotolewa na Tume ya Nyalali ya kuanzisha nchini mfumo wa vyama vingi vya siasa, likaongezeka suala la 22 la Muungano kuhusu “Uandikishaji wa Vyama vya Siasa na mambo mengine yanayohusiana navyo”.

Suala la ongezeko la Mambo ya Muungano limezalisha mjadala mkubwa ambao sehemu kubwa unachochea na upinzani wa makusudi au uelewa mdogo kwamba ongezeko lilifanyika kibabe au kinyemela bila ya Zanzibar kuhusishwa au bila ya wadau kuhusishwa

wakiwamo wananchi.<sup>26</sup> La hasha, suala hili ni la kikatiba, hivyo, uendeshaji wake unatawaliwa na Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977.

Ibara ya 4(3) ya Katiba inasema:

Kwa ajili ya utekelezaji bora wa shughuli za umma katika Jamhuri ya Muungano, na kwa ajili ya mgawanyo wa madaraka juu ya shughuli hizo baina ya vyombo vilivyotajwa katika ibara hii, kutakuwa na Mambo ya Muungano kama yalivyoorodheshwa katika Nyongeza ya Kwanza iliyoko mwishoni mwa Katiba na pia kutakuwa na mambo yasiyo ya Muungano, ambayo ni mambo mengine yote yasiyo Mambo ya Muungano.

Mambo haya yamekuwa yakiongezeka kwa sababu za msingi zilizoelezwa hapo juu, nyingi (zaidi ya asilimia 80) zikitokana na kuvunjika kwa Jumuiya ya Afrika ya Mashariki na huduma zake za pamoja, ambazo Tanzania ilibidi izibebe. Aidha, kila ongezeko lilijadiliwa na kupata baraka za Serikali zote mbili na kupitia mchakato mahususi wa kikatiba kupitisha mabadiliko husika.

Ibara ya 98(1) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania inaruhusu Bunge kutunga sheria kwa ajili ya kubadilisha masharti yoyote ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania lakini kwa utaratibu maalum ufuatao ulioainishwa na Katiba:

Mabadiliko yoyote katika mambo yanayotajwa kwenye Orodha ya Pili ya Nyongeza ya Pili ya Katiba, yaani **Kuwepo kwa Jamhuri ya Muungano, Kuwepo kwa Ofisi ya Rais wa Jamhuri ya Muungano, Kuwepo kwa Bunge la Jamhuri ya Muungano, Madaraka ya Serikali ya Zanzibar, Mahakama Kuu ya Zanzibar, Orodha ya Mambo ya Muungano na Idadi ya Wabunge kutoka Zanzibar**, sharti yaungwe mkono na theluthi mbili ya Wabunge wote kutoka Tanzania Bara na theluthi mbili ya Wabunge wote kutoka Tanzania Zanzibar (Ibara ya 98(1)(b)).

Mabadiliko yoyote katika sheria zinazotajwa kwenye ORODHA YA KWANZA YA NYONGEZA YA PILI ya Katiba, yaani **Sheria ya Uhamiaji ya mwaka 1995 (Sura ya 54); Sheria ya Uraia ya mwaka 1995 (Sura ya 357); Ibara ya 3, 18, 23, 26 na 27 ya Sheria ya kuthibitisha Tanganyika kuwa Jamhuri, ya mwaka 1962, Toleo la 1965 (Sura ya 500); Sheria ya Utumishi katika Idara ya Mahakama ya mwaka 1962,**

<sup>26</sup> Ubwa, M.A., The Union between Tanganyika and Zanzibar; Legality of Additional Matters outside the Articles of Union, (2005) <https://www.scribd.com/document/45109599>; Mihangwa, J., Tuna Muungano wa Tanganyika na Zanzibar tu, siyo Tanzania, (2014) <https://www.mzalendo.net/makala>

(Sura ya 237), Toleo la mwaka 2007; Sheria ya Utumishi Serikalini ya mwaka 1962, (Sheria Na. 8 ya 2002); Sheria ya kuthibitisha Mapatano ya Muungano wa Tanganyika na Zanzibar ya mwaka 1964 (Sura ya 557), Toleo la 1965, sharti yaungwe mkono na theluthi mbili ya Wabunge wote. (Ibara ya 98(1)(a)).

Ni masharti hayo magumu ya kubadili vipengele mbalimbali vya Katiba kuhusu masuala ya Muungano yanayoifanya Katiba ya Jamhuri ya Muungano isijumuishwe kwenye kundi la katiba tefutefu (*flexible constitutions*) bali kakamizi (*rigid*) kwa nia njema ya kulinda maslahi mapana ya Taifa. Katika muktadha huo, kumekuwa na ongezeko la Mambo 11 tu ya Muungano katika miaka 58 toka mwaka 1964, licha ya ongezeko kubwa la Mambo ya Muungano kuchangiwa na changamoto katika mtangamano wa Afrika Mashariki.

## Uhai wa Muungano

Uhai wa Muungano wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania unatokana na utaratibu uliowekwa wa Serikali za pande zote mbili za Muungano wa kutatua changamoto za Muungano kupitia mfumo rasmi wa Vikao vya Kamati ya Pamoja ya SMT na SMZ ya Kushughulikia Masuala ya Muungano. Mfumo huo wa vikao umeboresha utaratibu na kuongeza kasi ya utatuzi wa hoja za Muungano.

Aidha, Kamati ina utaratibu wa uendeshaji wa vikao unaoshirikisha viongozi na wataalamu kutoka SMT na SMZ. Vikao hivyo hufanyika katika ngazi tatu ambazo ni Makatibu Wakuu wa SMT na SMZ, Mawaziri wa SMT na SMZ na kikao cha Kamati ya Pamoja ya SMT na SMZ, ambacho Mwenyekiti wake ni Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Pamoja na kuwapo na Kamati ya Pamoja ya Kushughulikia masuala ya Muungano, kumekuwa na ushirikiano baina ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kwa masuala yasiyo ya Muungano. Serikali zote mbili zimeweka utaratibu wa vikao vya kisekta vya ushirikiano kwa Wizara, Idara na Taasisi zisizo za Muungano.

Lengo la kufanya vikao hivyo ni kuimarisha ushirikiano wa pande mbili za Muungano kwa manufaa ya Watanzania. Vikao hivyo vinajadili masuala ya kisekta ikiwamo kubadilishana ujuzi, utaalumu na uzoefu kupitia mafunzo, masuala ya sera na ushiriki katika masuala ya kimataifa ili kuleta ufanisi na uwiano wa maendeleo kwa pande zote mbili za Muungano. Vikao hivyo vya ushirikiano hufanyika walau mara mbili kwa mwaka katika ngazi tatu: Mawaziri, Makatibu Wakuu na Wataalamu.



## SURA YA NNE

# UTEKELEZAJI WA MAMBO YA MUUNGANO

## KATIBA YA TANZANIA NA SERIKALI YA JAMHURI YA MUUNGANO

### Katiba ya Jamhuri ya Muungano

Jamhuri ya Muungano wa Tanzania inaongozwa na Katiba mbili: Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977 inayohusika na mambo yote ya Muungano na yasiyo ya Muungano yanayoihusu Tanzania Bara, na Katiba ya Zanzibar ya mwaka 1984 ambayo inahusika na mambo yote yasiyo ya Muungano yanayoihusu Tanzania Zanzibar. Aidha, mambo yote ya Muungano yamewekwa bayana katika Nyongeza ya Kwanza ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977 ambayo katika maelezo yote yanayofuatia itatajwa kwa kifupi kama Katiba ya Jamhuri ya Muungano.

Tangu kutungwa kwa Katiba ya Jamhuri ya Muungano, kumefanyika mabadiliko 14. Kimsingi, lengo la mabadiliko hayo lilikuwa ni kuiboresha na kuifanya iendane na mabadiliko mengine yanayotokea ndani na duniani ili kukidhi matakwa na mahitaji ya muda mrefu ya wananchi kwa ujumla. Utekelezaji wa Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania umekuwa na mafanikio katika maeneo yafuatayo.

### Bunge

Muungano wa Tanganyika na Zanzibar uliwezesha kuanzishwa kwa Bunge la pamoja liitwalo Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ambalo limedumu tangu kuasisiwa kwa Muungano mwaka 1964

likitekeleza majukumu yake ya msingi ya kuwakilisha matakwa ya wananchi ya pande zote mbili kwa kutunga Sheria za nchi, kusimamia utendaji wa Serikali na kuchambua, kujadili na kupitisha Bajeti ya Serikali ya Muungano ya kila mwaka kwa amani, uelewano na weledi.

Katika kutekeleza majukumu yake, Bunge la Jamhuri ya Muungano limeweza kutunga Sheria na kupitisha maazimio mbalimbali ambayo yanatumika pande zote za Muungano. Sheria na maazimio yanayopitishwa na Bunge la Jamhuri ya Muungano hufikishwa Baraza la Wawakilishi la Zanzibar kwa taarifa na hatua nyingine za kibunge, hivyo, kuendelea kuimarika kwa uelewano na mshikamano katika utekelezaji wa masuala ya Muungano.

Hadi kufikia Machi, 2022, Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania lilikuwa na wabunge 393 kutoka pande zote mbili za Muungano ambapo wanawake walikuwa 145 sawa na asilimia 36 na wanaume 248 sawa na asilimia 64. Idadi hiyo ya wabunge wanawake ni sawa na ongezeko la asilimia 4,733 ikilinganishwa na wabunge watatu waliokuwepo katika Bunge la mwaka 1964. Vilevile, kuimarika kwa demokrasia katika uongozi wa mhimili wa Bunge kumwezesha Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kuongozwa na Maspika wawili wanawake, yaani katika Bunge la 10 Anne Semamba Makinda na Bunge la 12 Dkt. Tulia Ackson.

## Utawala Bora

Misingi mikuu ya utawala bora ni pamoja na utawala wa sheria, haki za binadamu, mabadiliko ya uongozi, demokrasia ya vyama vingi, uwazi, uwajibikaji na maridhiano. Tangu kuasisiwa kwa Muungano, Tanzania imekuwa ikizingatia misingi yote ya utawala bora. Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ina mihimili mitatu ya dola, ambayo ni Serikali, Bunge na Mahakama ambapo katika miaka zaidi ya 50 ya Muungano, uhuru wa mihimili hiyo umekuwa ukiimarika hatua kwa hatua kimajukumu, kiutendaji na kiweledi. Pia, imekuwa ikiboresha ushirikiano kati yake bila kuingiliana kwenye majukumu ya msingi. Aidha, uanzishwaji wa Mahakama ya Rufani ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania mwaka 1979 umeongeza wigo wa upatikanaji haki kwa wananchi.

Tanzania ya leo ni tofauti na Tanzania ya kipindi cha ukoloni Bara na Zanzibar ambacho kilitawaliwa na uvunjaji wa haki za binadamu, ikiwamo haki ya kuishi. Watu weusi waliteswa mithili ya wanyama kwa kutumikishwa mashambani, majumbani na sehemu nyingine bila ujira; watu walinyongwa kwa makosa ya kubambikizwa tu kwani mtu mweusi hakuwa na haki ya kujitetea mbele ya Mzungu au Mwarabu.



Katiba ya Jamhuri ya Muungano na Katiba ya Zanzibar zimeorodhesha haki zote za binadamu zilizomo kwenye Azimio la Kimataifa juu ya Haki za Binadamu la mwaka 1948 na kuweka utaratibu wa kikatiba wa kudai haki mahakamani pale ambapo haki za mtu zinapovunjwa au kukiukwa. Kuanzishwa kwa Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora Tanzania chini ya Sheria ya Haki za Binadamu na Utawala Bora Na. 7 ya mwaka 2001 ni ushahidi usiopingika wa kuimarika kwa haki za binadamu na utawala bora nchini. Tume inafanya kazi Tanzania Bara na Tanzania Zanzibar.

Tanzania vilevile imekuwa na mabadiliko ya uongozi kidemokrasia ambapo kila baada ya miaka mitano hufanyika uchaguzi wa viongozi wa kitaifa na wa serikali za mitaa. Kuwapo kwa Sheria ya Vyama vya Siasa nchini (Sheria Na. 5 ya Mwaka 1992) ilirekebisha ili kuruhusu kuandikishwa kwa vyama vingi vya siasa, na hivyo, kuimarisha demokrasia kwa pande zote mbili za Muungano. Mfumo wa vyama vingi umeongeza hamasa kwa wananchi kushiriki masuala ya siasa na kuchagua viongozi wanaowataka. Aidha, mfumo huo umeongeza wigo wa wananchi kuikosoa Serikali kupitia wawakilishi wao Bungeni.

Kupitia Uchaguzi Mkuu wa Kwanza wa Vyama Vingi uliofanyika mwaka 1995, kwa mara ya kwanza katika historia ya Tanzania, Bunge lilipata Wabunge kutoka vyama tofauti vya siasa ambavyo ni Chama Cha Mapinduzi (CCM) wabunge 186 wa kuchaguliwa na wabunge 28 wa viti maalum, *National Convention for Construction and Reform-Mageuzi* (NCCR-Mageuzi) wabunge wa kuchaguliwa 16 na wa viti maalum watatu, *Civic United Front (CUF)* wabunge wa kuchaguliwa 24 na wa viti maalum wanne, Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA) wabunge wa kuchaguliwa watatu na mbunge wa viti maalum mmoja na *United Democratic Party (UDP)* wabunge wa kuchaguliwa watatu na mbunge wa viti maalum mmoja.

Hali hiyo ilibadili kwa kiasi kikubwa taswira ya Bunge la Tanzania na kuijengea heshima Tanzania kwa kuwa na uchaguzi unaofanyika kwa uhuru, haki na amani. Taifa limeshuhudia Awamu Sita za Uongozi wa Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Awamu Nane za Uongozi wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar, zote zikifanyika kwa haki, amani na utulivu.

Sura ya Nne ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania inatambua kuwapo kwa Katiba ya Zanzibar na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar na mamlaka yake ya uongozi wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar na Madaraka yake; Uchaguzi wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar; Baraza la Mapinduzi Zanzibar na Kazi zake na Baraza la

Wawakilishi na madaraka ya kutunga sheria za Zanzibar.<sup>1</sup> Kutokana na matakwa ya Katiba hiyo kumeiwezesha Zanzibar kuwa na Katiba yake na kuanzisha vyombo vya kiutawala ikiwamo Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar, Mahakama Kuu ya Zanzibar na Baraza la Wawakilishi.

Vilevile, kuwapo kwa Tume ya Taifa ya Uchaguzi ambayo ilianzishwa mwaka 1993 chini ya Ibara ya 74(1) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya Mwaka 1977 na Tume ya Uchaguzi ya Zanzibar iliyoundwa kwa mujibu wa Kifungu cha 119 (1) cha Katiba ya Zanzibar ya Mwaka 1984 umewezesha kuimarika kwa demokrasia. Aidha, Tume za Uchaguzi kwa pande zote mbili za Muungano zimekuwa zikitekeleza majukumu yake kwa uhuru bila kuingiliwa wala kupendelea upande wowote. Tume hizi zimekuwa zikisimamia chaguzi zilizohusisha vyama vingi katika ngazi ya Rais, Wabunge, Wawakilishi na Madiwani kuanzia mwaka 1995.

Kuimarika kwa uhuru wa kutoa na kupata habari ni eneo lingine linalodhihirisha kukua kwa utawala bora nchini. Uhuru huo umewezesha kuongezeka kwa vyombo vya habari vikiwamo magazeti, majarida, redio na runinga Tanzania Bara na Tanzania Zanzibar.

## **MAMBO YA NJE**

Wakati wa utawala wa kikoloni, Tanganyika haikuwa na uhusiano na nchi nyingine zaidi ya zile ambazo zimeitawala, hali hii ilikuwa hivyo kwa Zanzibar pia ambayo ilikuwa katika makucha ya utawala wa wachache wa Waarabu kutoka Oman. Hivyo basi, kabla ya Muungano, Zanzibar ilikuwa na mahusiano na nchi chache za Misri, Oman na Uingereza. Kwa upande wa Tanganyika, kabla ya Uhuru nayo ilikuwa na mahusiano na nchi chache hasa Uingereza na Ujerumani.

Mara baada ya kupata uhuru na mwaka mmoja baadaye, Tanganyika ilianzisha uhusiano wa kidiplomasia na baadhi ya nchi kama vile Uingereza, Ujerumani, Japan na Denmark. Tanganyika pia, ilifungua ubalozi wake wa kudumu katika Umoja wa Mataifa, New York, Marekani. Wakati huo Wizara ya Mambo ya Nje ilijulikana kama Idara ya Mambo ya Nje na Ulinzi ndani ya Ofisi ya Waziri Mkuu. Masuala ya Mambo ya Nje yaliendelea kuwa chini ya Idara mpaka mwaka 1963 yalipoundiwa Wizara mahususi ya Mambo ya Nje na Ulinzi. Baada ya Muungano, Wizara ilibeba jina la Wizara ya Mambo ya Nje huku masuala ya ulinzi yakihamishiwa katika Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa.

Baadaye wizara hiyo ilibadilishwa na kuwa Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa kabla ya kuitwa Wizara ya Mambo

<sup>1</sup> Ibara ya 102 – 107 ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, 1977

ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki mwaka 2016 kutokana na kuunganishwa kwa Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa na Wizara ya Ushirikiano wa Afrika Mashariki.

Ikumbukwe mara tu baada ya Mapinduzi ya 1964, nchi 18 zikiwamo za Kiarabu (Misri na Algeria) na nchi kubwa zilizokuwa karibu sana na Sultani (Uingereza na Marekani) ziliyatambua Mapinduzi Matukufu ya Zanzibar, na hivyo, kuifanya Zanzibar ianzishe uhusiano wa kibalozi na nchi 10 kwa kuanzia na kutuma mwakilishi wake Umoja wa Mataifa.<sup>2</sup>

Katika kufikia malengo ya mambo ya nje, hadi Machi 2022 Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ina vituo vya uwakilishi katika nchi 44 duniani na konseli kuu sita. Kati ya balozi hizo 44, tisa zimefunguliwa kipindi cha mwaka 2016 hadi 2022 katika nchi za Qatar, Uturuki, Sudan, Cuba, Israel, Algeria, Jamhuri ya Korea, Namibia na Austria. Konseli Kuu sita zipo katika miji ya Mombasa, Dubai, Jedda, Lubumbashi, Guangzhou na Shanghai. Aidha, Jamhuri ya Muungano wa Tanzania imezipokea balozi 62 za nchi mbalimbali, taasisi na mashirika ya kimataifa 30.

Tanzania imekuwa na mchango mkubwa sana katika medani ya kimataifa kuanzia katika jumuiya za kikanda mpaka Umoja wa Mataifa. Heshima ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kimataifa ni kubwa kutokana na mchango wake katika mapambano ya ukombozi wa nchi za Afrika, kudumisha ulinzi na usalama, mapambano dhidi ya rushwa, biashara haramu na dawa za kulevya.



*Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Samia Suluhu  
Hassan akihutubia Baraza Kuu la Umoja wa Mataifa tarehe  
23 Septemba, 2021*

<sup>2</sup> Chanzo: ASP, The Afro-Shirazi Revolution 1964-1974, Printpak Tanzania Ltd, Dar es Salaam, 1974, uk. 11.

## Mchango wa Tanzania katika Ukombozi

Tanzania imekuwa mstari wa mbele kutetea masuala yahasuyo haki za binadamu duniani, kuunga mkono juhudi za ujenzi wa demokrasia na misingi yake sambamba na utawala bora pamoja na kuhamasisha Umajumui wa Afrika.

Tanzania ni miongoni mwa nchi tano zilizokuwa Mstari wa Mbele wa Mapambano katika kuhakikisha kuwa nchi za Afrika zinapata uhuru wake kutoka katika makucha ya wakoloni na ilikuwa tayari hata kuchelewesha uhuru wake ili nchi nyingine za Afrika zijinasue kutoka kwenye mikono ya wakoloni.



*Viongozi wa nchi tano zilizokuwa mstari wa mbele wa mapambano katika kuhakikisha nchi za Afrika zinapata uhuru (Kutoka kushoto: Julius K. Nyerere wa Tanzania, Samora Machel wa Msumbiji, Quett Masire wa Botswana, Jose Eduardo Dos Santos wa Angola na Kenneth Kaunda wa Zambia) mwaka 1980*

Katika kufanikisha hilo Tanzania ilishirikiana na Angola, Botswana, Msumbiji na Zambia ili kufikia azma ya pamoja ya kulikomboa Bara la Afrika na hasa nchi za Kusini mwa Afrika sambamba na kupinga ubaguzi uliokuwa ukifanywa na Makaburu katika nchi ya Afrika Kusini. Nchi hizi pia zilipambana kusaidia kuuondoa utawala wa wachache katika nchi za Afrika Kusini, Namibia na Rhodesia ya Kusini ambayo kwa sasa inatambulika kama Zimbabwe.

Kipekee, Tanzania ilitoa maeneo mbalimbali yaliyotumika kwa mafunzo ya medani na mbinu za kivita. Maafisa na askari wa Jeshi la Wananchi wa Tanzania (JWTZ) walitumika kutoa mafunzo katika vyyuo na makambi mbalimbali nchini. Vyyuo na Makambi hayo yalikuwa

katika mikoa ya Dar es Salaam, Lindi, Mtwara, Ruvuma, Mbeya, Iringa, Dodoma, Tabora, Tanga, Morogoro, Kagera, Arusha, Mwanza, Singida na Pwani.<sup>3</sup>

Vilevile, Tanzania ilipeleka askari wake kwenda kusaidia majeshi ya ukombozi ya Msumbiji (FRELIMO) kupitia kambi ya kijeshi ya *Farm 17* iliyopo Nachingwea mkoani Lindi iliyokuwa ikitumiwa na jeshi hilo la Msumbiji. Askari wengi wa Tanzania walifariki kishujaa katika harakati za kuhakikisha Msumbiji inajikomboa kutoka kwenye utawala dhalimu wa Wareno.

Kati ya mwaka 1973 hadi 1975 Wareno kwa kushirikiana na makaburu wa Afrika Kusini walishambulia mara kwa mara maeneo ya Mtwara na Lindi kwa ndege za kivita na kuuu, kujeruhi watu wengi na kuharibu mali na miundombinu mbalimbali. Aidha, Wareno walimwaga sumu iliyoharibu na kuteketeza mashamba ya mkonge mkoani Mtwara wakiamini kuwa kufanya vile kungeyumbisha uchumi wa Tanzania ambao kipindi hicho ulitegemea sana mazao ya pamba na katani. Hayo yote yalifanyika baada ya kuona kuwa Tanzania imekuwa ngome kubwa ya wapiganaji wa FRELIMO.

Kuteketezwa kwa mashamba ya mkonge kuliathiri uchumi wa nchi lakini haikuwavunja moyo Watanzania. Badala yake Tanzania ikaongeza nguvu kuisaidia FRELIMO si katika vita tu bali katika kujenga upya utawala wa kiraia ambao ungekidhi matakwa ya watu wa Msumbiji.

Hivyo basi, baada ya Msumbiji kupata uhuru mwaka 1975 Serikali za Tanzania na Msumbiji zilitiliana saini ya makubaliano ya kuanzishwa kwa chuo kilichoitwa Chuo cha Elimu ya Juu kwa Wapigania Ukombozi wa Nchi za Kusini mwa Afrika ambacho kilianzishwa rasmi Dar es Salaam tarehe 13 Januari, 1978. Viongozi walioshiriki kutia saini makubaliano hayo walikuwa Mawaziri wa Mambo ya Nje wa Tanzania, Ndugu Benjamin William Mkapu na mwenzake Ndugu Joaquim Alberto Chissano wa Msumbiji.

Chuo hicho kilitoa mafunzo si kwa askari wa Msumbiji tu bali nchi nyingine kama vile Angola, Zimbabwe, Namibia na Afrika Kusini ambapo mafunzo ya utawala na uongozi wa kimkakati yalitolewa ili kuzijenga upya nchi hizo baada ya kuwa huru. Chuo hicho kwa sasa kinajulikana kama Chuo cha Diplomasia.

Baada ya nchi zilizokuwa Mstari wa Mbele kupata uhuru, Tanzania iliendelea kushirikiana nazo na kuanzisha Jukwaa la Uratibu wa Maendeleo Kusini mwa Afrika (SADCC) mwaka 1980 ili kukabiliana na changamoto zilizotokana na utawala wa kikoloni na ubaguzi wa

<sup>3</sup> Programu ya Urithi wa Ukombozi wa Bara la Afrika.

rangi. Mnamo mwaka 1992 Jukwaa hilo lilibadilishwa na kuwa Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika (SADC) ili liweze kukabiliana na changamoto mpya za kiusalama zikiwamo umaskini, rushwa na matatizo yatokanayo na chaguzi.

## Tanzania na Upatanishi wa Nchi

Kutokana na kutambua umuhimu wa usalama katika maendeleo, Tanzania imeshiriki katika usuluhishi, utatuzi na usimamizi wa migogoro katika nchi za Lesotho, Kisiwa cha Madagascar, Visiwa vya Comoro, Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo (DRC) na Msumbiji.

Aidha, katika Jumuiya ya Afrika Mashariki, Tanzania imeshiriki katika upatanishi wa pande hasimu nchini Burundi kuanzia mwaka 1999 hadi 2015. Kwa nyakati tofauti upatanishi huo ulisimamiwa na Mwalimu Julius Kambarage Nyerere na Mheshimiwa Benjamin William Mkapa.

Vilevile, kati ya mwaka 2008 na 2013 Tanzania ilishiriki katika upatanishi wa pande hasimu nchini Kenya kufuatia mzozo wa kisiasa uliotokana na kutokubaliana juu ya matokeo ya Uchaguzi Mkuu wa mwaka 2007. Kwa nyakati tofauti Marais Wastaafu, Benjamin William Mkapa na Jakaya Mrisho Kikwete, walihusika kupatanisha pande hasimu nchini Kenya.

Msaada na ushawishi wa Tanzania haukuishia kwa nchi za Afrika tu bali ulivuka mipaka mpaka barani Asia. Kwa mfano, China ni miongoni mwa nchi zilizonufaika na msaada wa Tanzania katika medani za kimataifa. Ikumbukwe kwamba nchi ya China ilikuwa katika mzozo baina ya chama cha *Koumintang* (KMT) kilichokuwa kikiongozwa na dikteta Jenerali Chiang Kai-Shek dhidi ya Chama cha Kikomunisti cha China kwa miongo kadhaa. Mzozo huo ulidumu kuanzia mwaka 1922 mpaka mwaka 1949 ambapo serikali iliyokuwa ikiongozwa na dikteta Kai-Shek iliondolewa madarakani kufuatia mapinduzi yaliyoongozwa na Jemedari Mao Tse-Tung.

Licha ya kufanikiwa kuirejesha China chini ya utawala wa wananchi, serikali ya Kai-Shek iliyokuwa ikiungwa mkono na Marekani iliendelea kulazimisha kutambulika kuwa ni serikali halali katika Umoja wa Mataifa. Hali hiyo ilisababisha Jamhuri ya Watu wa China chini ya uongozi wa Mao-Tsetung kukosa nafasi ya uwakilishi katika Umoja wa Mataifa kwa miaka 22 kuanzia mwaka 1949 hadi 1971.

Ni wakati huo ambapo Tanzania kupitia mwakilishi wake wa kudumu katika Umoja wa Mataifa, Dkt. Salim Ahmed Salim, aliyekuwa akiongoza kundi la nchi za Afrika ilipambana vilivyo kuzishawishi nchi za Afrika,

Asia na Latini Amerika ili kuhakikisha China inapata uwakilishi halali katika umoja huo. Hatimaye, tarehe 25 Oktoba, 1971 kura zilipigwa na China kufanikiwa kupata uwakilishi halali kupitia mwakilishi wa chama cha CPC kwa kura 76 dhidi ya kura 35 za Marekani na washirika wake huku nchi 17 zikikaa kimya wakati nchi 3 hazikupiga kura kabisa.

Uwakilishi wa Kai-Shek ulifukuzwa katika umoja huo na kutotambulika kama uwakilishi halali licha ya kukimbilia Taiwan. Mafanikio hayo ya China yalitokana na juhudi za dhiti na za kujitoka kwa moyo kwa serikali ya Tanzania. Yote haya ni matunda ya Muungano wa Tanzania yaliyowezesha Rais Mstaafu wa Marekani Bill Clinton alipokuwa Arusha mwaka 2000 kushuhudia upatanishi wa Burundi uliosimamiwa na Baba wa Taifa, Mwalimu Julius Nyerere na baadaye Baba wa Taifa la Afrika Kusini Nelson Mandela, kuiita Arusha kuwa ni “Geneva ya Afrika”.

## ULINZI NA USALAMA

Kipindi cha utawala wa Wajerumani (1884-1918) katika eneo lililojulikana kama *Deutsch Ostafrika* au Ujerumani Afrika Mashariki, jeshi la kikoloni lilijumuisha maafisa wa Kijerumani na askari wazawa kutoka maeneo yaliyokuwa chini ya utawala wao, yaani Tanganyika, Rwanda, Burundi na Kionga *Triangle* (au Kionga *Dreieck* kwa Kijerumani) ambayo kwa sasa ni sehemu ya Msumbiji.

Jeshi hilo lililoundwa mahususi kulinda maslahi ya Ujerumani Afrika Mashariki kufuatia makubaliano ya Berlin ya nchi za kibeberu mwaka 1884-1885, lilijulikana kama *Schutztruppe* (au Kikosi cha Ulinzi).

Kufuatia kushindwa kwa Ujerumani katika Vita Kuu ya Pili ya Dunia, Afrika Mashariki ya Ujerumani iligawanywa kati ya nchi za Ubelgiji iliyopewa Rwanda na Burundi; Ureno ikachukua Kionga *Triangle* kama sehemu ya Msumbiji, na Uingereza iliyokabidhiwa Tanganyika kama mamlaka ya udhamini. Jeshi nalo likabadilika kuwa la Mwingereza lililojulikana kama *King's African Rifles (KAR)* ambalo kwa tafsiri isiyo rasmi ya Kiswahili linaweza kuitwa ‘Jeshi la Mfalme katika Afrika.’ Jeshi hilo lilizingatia misingi ileile ya uanzishwaji wa *Schutztruppe*.

Kama ilivyokuwa kwa *Schutztruppe*, Jeshi la *KAR* nalo lilifanya kazi ya kulinda maslahi ya Uingereza ndani ya Tanganyika kwa kuwatumia askari kutoka jamii mbalimbali za Tanganyika wakiongozwa na maafisa wachache wa Kiingereza. Baada ya Tanganyika kupata uhuru kutoka kwa Waingereza tarehe 9 Desemba, 1961, Serikali mpya ya kizalendo ililibadilisha jina jeshi hilo na kuliita *Tanganyika Rifles (TR)*

ama *Tanganyika Military Force (TMF)* ambalo lilikabidhiwa bendera iliyokuwa ikitumiwa na *KAR*.

Hata hivyo, licha ya kubadilishiwa jina, jeshi hilo liliendelea kuendeshwa kwa misingi na taratibu zilezile zilizoachwa na *KAR* kutokana na kuendelea kuendeshwa na maafisa na askari wa Kiingereza<sup>4</sup>. Mahitaji ya kuwa na jeshi jipya lenye maadili, malengo na maono mapya yanayoendana na azma ya taifa jipya likajitokeza kwa nguvu baada ya askari wa jeshi hilo kuasi tarehe 20 Januari, 1964 wakipinga, pamoja na mambo mengine, ujira kidogo na jeshi kuendelea kuongozwa na maafisa wa Kizungu.

Uasi huo ulidhibitiwa siku tano baadaye, yaani tarehe 25 Januari, 1964 ambapo Rais na Amiri Jeshi Mkuu, Mwalimu Julius Kambarage Nyerere, aliamua kulivunja rasmi jeshi hilo na kuunda jeshi jipya akiwataka vijana wa TANU (*TANU Youth League*) wajitokeze kwa wingi kuunda jeshi jipya la kizalendo. Kwa upande wa Zanzibar vijana 324 wa ASP Youth League waliunganishwa na vijana wa TANU ili kuunda Jeshi la Wananchi wa Tanzania (JWTZ).

## Jeshi la Ulinzi la Wananchi wa Tanzania (JWTZ)

Mafunzo kwa ajili ya jeshi jipya yalianza tarehe 3 Machi, 1964 na kumalizika rasmi tarehe 1 Septemba, 1964 ambapo Kapteni Mirisho Sarakikya aliteuliwa kuwa Mkuu wa Majeshi na kupandishwa cheo kuwa Brigedia Jenerali huku Luteni Elisha Kavana akiteuliwa kuwa Naibu Mkuu wa Majeshi na kupandishwa cheo kuwa Meja.

Mara baada ya kuanzishwa kwa Jeshi la Ulinzi la Wananchi wa Tanzania (JWTZ), changamoto mbalimbali zikajitokeza zikiwamo za ukosefu wa zana stahili za kijeshi kutokana na ukweli kwamba jeshi la kikoloni liliacha vitu vidogovidogo ambavyo havikuwa na umuhimu mkubwa kwa matumizi na utendaji kazi wa jeshi.

Kutokana na hali hiyo na kwa kuzingatia umuhimu wa jeshi katika kulinda na kutetea maslahi ya nchi, Serikali ilifanya juhudi za makusudi na za dhati kuhakikisha kuwa JWTZ linakuwa jeshi lenye kanuni mahususi, wataalamu, nyenzo na vifaa mbalimbali vya kisasa vinavyokidhi mahitaji ya jeshi hilo.

Matokeo ya uwekezaji huo kwa JWTZ yalithibitika mnamo tarehe 25 Novemba, 1978 baada ya JWTZ kuyaondoa majeshi ya Nduli Idd Amin

<sup>4</sup> Taarifa ya Mheshimiwa Dkt. Stergomena Lawrence Tax (MB) Waziri wa Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa kwa Vyombo vya Habari Kuhusu Mafanikio ya Miaka 60 ya Uhuru wa Tanzania Bara, Tarehe 29 Novemba, 2021 Dodoma.



wa Uganda katika eneo lote la Tanzania kufuatia majeshi hayo ya Amin kuvamia eneo la Mutukula hadi Mto Kagera mnamo mwezi Oktoba, 1978 na kudai ni sehemu ya Uganda.

Katika kudhihirisha umahiri wake kwenye uwanja wa medani, JWTZ kwa kushirikiana na Jeshi la Ukombozi la Uganda yaliingia nchini Uganda na kuuteka mji mkuu Kampala mnamo tarehe 25 Aprili, 1979 hali iliyomlazimisha Iddi Amin kukimbilia ughaibuni alikomalizia maisha yake.

## Mchango wa JWTZ kwa Dunia

JWTZ halijajiweka nyuma katika kushiriki kwenye operesheni mbalimbali za ulinzi za amani ndani na nje ya Bara la Afrika. Pamoja na operesheni hizo, JWTZ halijasita pale inapobidi kutuma maafisa na askari wake kama waangalizi wa Amani na wadhamini katika misheni kadhaa.

JWTZ limeshiriki katika misheni ya Umoja wa Mataifa na Umoja wa Afrika ya Dafur tangu 2008; limeshiriki kulinda amani Lebanon chini ya mwamvuli wa Umoja wa Mataifa; limeshiriki katika ulinzi wa amani Liberia kwa kuombwa na ECOWAS na Umoja wa Afrika; limeshiriki kulinda amani DRC chini ya mwamvuli wa Umoja wa Mataifa na shughuli nyingine nyingi za kulinda amani za Umoja wa Mataifa na Umoja wa Afrika.



*Amiri Jeshi Mkuu wa Majeshi ya Ulinzi na Usalama nchini na Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Samia Suluhu Hassan, akiwa katika picha ya pamoja na Waziri wa Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa, Dkt. Stergomena Tax na Viongozi na Makamanda wa JWTZ mara baada ya kufungua Mkutano Mkuu wa Tano wa Makamanda wa Jeshi la Wananchi wa Tanzania (JWTZ), tarehe 15 Novemba, 2021.*

## POLISI

Utawala wa Kijerumani haukuanzisha Jeshi rasmi la Polisi badala yake ulikuwa ukiwatumia watawala wa vijiji (maakida na majumbe) katika kutekeleza majukumu ya kipolisi. Hali hiyo ilibadilika baada ya Utawala wa Waingereza kupitisha Sheria ya Jeshi la Polisi na Magereza ya mwaka 1919. Kupitia sheria hiyo, tarehe 25 Agosti, 1919 Serikali ya Kiingereza ilianzisha rasmi Jeshi la Polisi kupitia tangazo la Gazeti la Serikali Na. 1. Vol. I Na. 21-2583 ambapo maafisa 31 kutoka Afrika Kusini waliwasili Tanganyika kuanzisha jeshi hilo.

Mwaka 1921, Wakaguzi wa Polisi kutoka Ulaya walianzisha shule ya mafunzo maalum ya upolisi mkoani Morogoro. Mafunzo waliyopatiwa askari hao, yalilenga zaidi mbinu za kumkandamiza Mwafrika, kuwaaminisha kuwa kila walichosema wakoloni ndicho sahihi. Pamoja na askari weusi kufuzu mafunzo, bado walibaki na vyeo vya chini vya kipolisi kwa kuwa vyeo vya juu vyote walipewa askari Wazungu.

Kituo cha kwanza rasmi cha polisi nchini kilifunguliwa Lupa Tingatinga, Mbeya mwaka 1925. Hadi kufikia mwaka 1930, Jeshi la Polisi lilikuwa na Wazungu 78 kwenye nafasi za juu, Waasia 67 kwenye vyeo vya kati na Waafrika 1,719 kwenye nafasi za chini. Mbali na kushika nafasi za chini katika Jeshi la Polisi, Waafrika pia walibaguliwa kwa taratibu za kiutawala, makazi na stahili. Vijana wa Kitanganyika wakiongozwa na baadhi ya askari waliotoka kwenye Vita ya Kwanza na ya Pili ya Dunia, wakaanza kupinga ubaguzi na ukandamizaji ndani ya jeshi hilo. Uhuru ulipokaribia baadhi ya askari wa Kiafrika wakaanza kupandishwa vyeo, hivyo, mwaka 1960 kulikuwa na Waafrika 28 wenye vyeo vya kati jeshini. Muda mfupi baada ya Tanganyika kupata uhuru tarehe 9 Desemba, 1961, Jeshi la Polisi lilibadili mwenendo na mwelekeo wake kutoka kuwatumikia wakoloni na kuanza kuwatumikia wananchi kwa mujibu wa sera za Serikali mpya ya Tanganyika.

Mwaka 1962 Elangwa Shaidi aliteuliwa kuwa Mwafrika wa kwanza kushika nafasi ya juu kabisa katika Jeshi la Polisi ya Kamishna wa Polisi akichukua nafasi ya Kamishna wa Polisi wa Kiingereza CP M.S. Wilson. Mwaka huo huo (1962), maafisa 10 wa Kiafrika waliteuliwa kuchukua nafasi za Wakuu wa Polisi wa Mikoa.

Kwa upande wa Zanzibar, Jeshi la Polisi liliundwa mwaka 1873 kwa ajili ya kusimamia Sheria za kudhibiti biashara ya utumwa. Jeshi hili lilijumuisha askari wa Kiingereza na wa Sultani wa Zanzibar. Hadi

mwaka 1877, jeshi hilo lilikuwa na askari 1,300 wakiwamo Waafrika 300<sup>5</sup>.

Jeshi hilo la Polisi lilianzishwa rasmi kisheria mwaka 1906 na kutambulika kwa jina la Jeshi la Polisi la Zanzibar likiongozwa na maafisa wa Kizungu, Kiarabu na Kihindi. Vijana wa Kiafrika walikuwa wachache sana katika jeshi hilo na walishiriki kwenye ulinzi ambapo kazi kubwa kwa wakati huo ilikuwa kuulinda utawala wa Sultani chini ya Himaya ya Uingereza.

Mnamo mwaka 1907 wakati Zanzibar ikiendelea kuwa chini ya ulinzi wa Waingereza, Sultani alilivunja Jeshi la Polisi baada ya askari wake kugoma kutokana na mishahara midogo na mazingira duni ya kazi na kuunda Jeshi la Polisi lililojumuisha askari wa akiba alioletewa kutoka Tanganyika.

Baada ya Mapinduzi ya Zanzibar, kazi ya kwanza ya Jeshi la Polisi ilikuwa ni kubadilisha uongozi kwa kuteuliwa viongozi walioaminika miongoni mwa wafuasi wa Chama cha ASP na askari polisi kutoka Tanzania Bara kuwahudumia wananchi wa Zanzibar. Mikoa mitatu ya kipolisi iliundwa ili kuleta ufanisi. Mikoa hiyo ni mkoa wa Mjini, mkoa wa Shamba na mkoa wa Pemba.

Baada ya Muungano tarehe 26 Aprili, 1964, Sheria za Jeshi la Polisi la Zanzibar zilifutwa na iliyokuwa Sheria ya Polisi ya Tanganyika ilianza kutumika Tanzania Bara na Tanzania Zanzibar. Kupitia utaratibu huo, Jeshi la Polisi lilianzisha nafasi ya Inspekta Jenerali wa Polisi na Elangwa Shaidi alipandishwa cheo na kuwa Inspekta Jenerali wa Polisi nchini Tanzania ambaye alisaidiwa na Makamishna watatu wa Polisi ambao ni: Edington Kisasi<sup>6</sup>, Kamishna wa Polisi Zanzibar; Hamza Azizi, Kamishna wa Polisi Bara, na Eliphace Elieza Akena, Kamishna wa Polisi CID.

Katika miaka 58 ya Muungano, Jeshi la Polisi la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania limejengeka kuwa taasisi imara ya Muungano inayolinda usalama wa raia na mali zao bila ubaguzi licha ya ukubwa wa nchi (kilomita za mraba 945,087), ukanda mrefu wa pwani wa kilomita 1,424 na nchi kupakana na nchi 8: Kenya, Uganda, Rwanda, Burundi, Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo (DRC), Zambia, Malawi na Msumbiji.

Mafanikio makubwa ya Jeshi la Polisi la Muungano ambayo majeshi yote ya polisi ya kikoloni yalishindwa kufikia hata kwa asilimia moja, ni kulinda utawala wa sheria ambapo kila mtu, tofauti na awali, yuko

---

<sup>5</sup> Taarifa ya Miaka 50 ya Mapinduzi Matukufu ya Zanzibar kuanzia mwaka 1964 hadi mwaka 2014.

<sup>6</sup> Ikumbukwe kuwa Edington Kisasi alikuwa mmoja wa Wajumbe 30 wa Baraza la Mapinduzi la Kwanza mwaka 1964.

sawa mbele ya sheria. Mafanikio mengine ni pamoja na Jeshi kujijengea uwezo na kuimarisha utendaji, maslahi na upatikanaji wa makazi bora ya askari na uwepo wa ushirikiano na majeshi ya polisi ya nchi jirani na nchi nyingine na kujiunga katika Mashirikisho ya Wakuu wa Polisi ya Kikanda na Kimataifa.

## URAIA

Kabla ya Muungano, utambulisho wa raia wa Tanzania na wasio raia ulikuwa unafanyika kwa kutumia Hati za Kusafiria, Hati za Vizazi na Vifo na Serikali za Mitaa (nyumba kumi-kumi). Suala la uraia liliongozwa na Sheria tofauti yaani Sura 452 na 512 kwa Tanzania Bara na Sura 39 kwa Tanzania Zanzibar kama zilivyorekebishwa na “Decree” Na. 5 ya mwaka 1964.

Aidha, kulikuwa na Sheria ya Mzanzibari iliyojulikana kama “*The Zanzibar Act (No. 5) of 1985*” iliyoainisha ni nani Mzanzibari, na hivyo, kuleta utatanishi ulioifanya Tanzania ionekane ina raia wa namna mbili yaani Watanzania na Wanzanzibari. Vilevile, suala la kuwapo kwa taratibu tofauti katika kushughulikia maombi ya uraia kati ya Tanzania Bara na Tanzania Zanzibar nalo lilikuwa ni kikwazo katika kushughulikia masuala ya uraia.

Taarifa ya Kamati ya Shellukindo ya tarehe 27 Septemba 1994 ilipendekeza kuwapo kwa Sheria moja ya uraia wa Tanzania ambayo itatumika katika Jamhuri yote ya Muungano wa Tanzania kama ilivyopendekezwa katika Waraka wa Baraza la Mawaziri Na. 49 wa mwaka 1989 kuhusu Sheria ya Uraia.

Kufuatia mapendekezo hayo, Sheria zilizokuwa zinasimamia masuala ya uraia ziliunganishwa na kuwa Sheria ya Uraia Na. 6 ya mwaka 1995. Aidha, tarehe 30 Julai, 2008, Serikali iliunda Mamlaka ya Vitambulisho vya Taifa kwa Hati Maalum ya Rais kupitia Tangazo la Serikali Na.122. Majukumu ya Mamlaka hiyo ni kuhakiki uraia wa watu waishio nchini na kusajili taarifa zao, kuwapatia vitambulisho na kutengeneza Daftari la Kudumu lenye taarifa za utambuzi wa watu ambazo pia zitatumwa na wadau wengine pamoja na kujenga Mfumo wa Utambuzi na Usajili wa watu Kitaifa.

## UHAMIAJI

Masuala ya udhibiti wa wahamiaji yalianzishwa Tanganyika mwaka 1924, chini ya Sheria ya Uhamiaji Sura Namba 37 ili kusimamia masuala ya uhamiaji nchini. Sheria hiyo ilianza kutumika tarehe 1 Februari,

1925. Kuanzia mwaka 1924 hadi mwaka 1948, shughuli za udhibiti wa wahamiaji na utoaji wa pasipoti zilifanywa na kitengo maalum ndani ya Idara ya Polisi. Idara ya Uhamiaji ilianzishwa rasmi tarehe 13 Julai, 1949 na mwezi Oktoba, 1949 ilibadilishwa jina na kuitwa Idara ya Uhamiaji na Pasipoti.

Baada ya Tanganyika kupata uhuru tarehe 09 Desemba, 1961 Idara iliendelea kuitwa Idara ya Uhamiaji na Pasipoti ikiwa na majukumu ya utoaji wa vibali vya kuingia nchini (viza) kwa wageni walioomba kuingia Tanganyika kwa shughuli mbalimbali, kufanya misako, doria pamoja na shughuli nyingine za upelelezi kuhusiana na masuala ya uhamiaji.

Kwa upande wa Zanzibar, masuala yote ya uhamiaji yalikuwa yanashughulikiwa na Jeshi la Polisi ambalo lilikuwa na kitengo maalum cha kushughulikia masuala hayo. Kuanzishwa kwa kitengo hicho kulitokana na Zanzibar kuwa kivutio kikubwa kwa watu kutoka sehemu mbalimbali hasa Bara Hindi, Bara Arabu na Visiwa vya Ngazija ambao walifika Zanzibar kufanya biashara au shughuli nyingine.

Kazi za kitengo zililenga kulinda maslahi ya wakoloni ambapo watumishi wa Idara katika ngazi za juu walikuwa Waingereza na Wahindi; Waafrika wao walishika nafasi za chini. Kwa ujumla, kitengo kilishughulika na Hati za Ukazi, Uraia na Pasipoti.

Baada ya Muungano, majukumu ya Idara ya Uhamiaji yalipanuka. Kwa upande wa Tanzania Bara, utendaji kazi wa Idara ya Uhamiaji uliendelea kusimamiwa na Sheria ya Uraia Na. 3 ya Mwaka 1961 na Sheria ya Uraia ya Mwaka 1962. Kwa upande wa Zanzibar, masuala ya uraia yalisimamiwa na Sheria ya Uraia ya Zanzibar ya mwaka 1952.

Sheria zote hizo zilifutwa baada ya kutungwa kwa Sheria ya Uraia Tanzania, Sura Namba 357. Masuala ya udhibiti wa wahamiaji yaliendelea kusimamiwa na Sheria ya Uhamiaji iliyofutwa na Sheria ya Uhamiaji, Sura Namba 54 ambayo pia ilifutwa na Sheria ya Uhamiaji, Sura Namba 43. Majukumu ya Idara ya Uhamiaji yalisimamiwa na Tamko la Kanuni na Udhibiti wa Uhamiaji la mwaka 1923 huko Zanzibar.

Mwaka 1995, Sheria zilizokuwa zinasimamia majukumu ya uhamiaji, Tanzania Bara na Tanzania Zanzibar zilifutwa na kutungwa Sheria ya Uhamiaji Na. 7 ya mwaka 1995 na Kanuni zake za Mwaka 1997. Aidha, Sheria zilizokuwa zinasimamia masuala ya uraia ziliunganishwa na kuwa Sheria ya Uraia Namba 6 ya Mwaka 1995 na Kanuni zake za Mwaka 1997. Katika kuboresha huduma za pasipoti, Serikali ilitunga Sheria ya Kusimamia Utoaji wa Pasipoti na Hati za Kusafiria Sura Namba 42 na Kanuni zake za Mwaka 2004.

Idara ya Uhamiaji imeendelea kuboresha utekelezaji wa majukumu yake ya msingi ya kudhibiti uingiaji na utokaji wa watu nchini; kusimamia ukazi wa wageni nchini kwa mujibu wa sheria; kutoa pasi za kusafiria na hati nyingine za safari kwa raia wenye sifa; na kuratibu maombi ya uraia wa Tanzania kwa wageni wanaoishi nchini. Maboresho hayo yamejumuisha matumizi ya teknolojia ya kisasa katika uchukuaji, utunzaji wa kumbukumbu za wageni wanaoingia na kutoka nchini, utoaji wa viza kwa wageni wanaoomba kuingia nchini na uchapishaji wa pasipoti.

Kuimarishwa kwa utoaji wa pasipoti na hati za kusafiria kuliwezesha kupatikana kwa mafanikio makubwa katika kipindi cha mwaka 2010 hadi 2020 yakiwamo kuanzishwa kwa mfumo wa kielektroniki wa usajili wa hati za kusafiria. Vilevile, Idara ya Uhamiaji ina Ofisi Tanzania Bara na Tanzania Zanzibar kwa lengo la kufikisha huduma karibu na wananchi.

## **MIKOPO NA BIASHARA YA NJE**

### **Mikopo**

Mwaka 1965, Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Serikali ya Mapinduzi Zanzibar zilikubaliana kujumuisha suala la mikopo kuwa katika Orodha ya Mambo ya Muungano. Wizara ya Fedha ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ilipewa dhamana ya kusimamia na kuratibu mikopo hiyo. Mnamo mwaka 1966, Benki Kuu ya Tanzania ilianzishwa ikiwa na malengo mbalimbali likiwamo la kupunguza vizingiti vya ukopaji. Mwaka 1974, Serikali ya Jamhuri Muungano ilianza kutekeleza Sheria ya Mikopo, Dhamana na Misaada *Sura Namba 134*.

Mwaka 2004, Sheria ya Mikopo, Dhamana na Misaada, Sura Namba 134 ilifanyiwa marekebisho. Sheria hiyo, pamoja na mambo mengine, inamtaka Waziri wa Fedha kupata ushauri wa Kamati za Usimamizi wa Madeni kabla ya kukopa. Sheria pia iliainisha mgawanyo wa majukumu ya kitaasisi katika usimamizi wa madeni ya Serikali. Aidha, sheria hiyo ilibainisha na kuweka ukomo wa mikopo yenye masharti nafuu isiwe chini ya asilimia 35. Vilevile, zilitungwa sheria mpya zikiwamo za Huduma za Kibenki na Taasisi za Kifedha, Masoko na Mitaji na Benki Kuu. Sheria hizi zilitungwa ili kuleta ufanisi katika ukopaji wa ndani.

Misaada ya Kibajeti hugawanywa ambapo Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania hupata asilimia 95.5 na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar (SMZ) asilimia 4.5. Kwa misaada ya kibajeti ya kisékta, Kifungu cha 15 (1) cha Sheria ya Mikopo, Dhamana na Misaada Sura

Namba 134, kinatoa mamlaka kwa SMZ kupokea misaada hiyo bila kutafuta idhini ya Waziri wa Fedha na Mipango wa SMT.

## Biashara ya Nje

Kabla ya Muungano, shughuli za biashara ya nje zilikuwa zikiendeshwa na taasisi tofauti katika pande zote mbili za Muungano. Kwa upande wa Zanzibar, uagizaji wa bidhaa kutoka nje ulisimamiwa na sekta binafsi iliyoongozwa na wafanyabiashara wa Kihindi.

Kwa upande wa Tanzania Bara, uuzaji wa mazao na uagizaji bidhaa nje ya nchi ulisimamiwa na *General Agricultural Products Export Company - GAPEX*. Aidha, Halmashauri ya Biashara ya Ndani - *Board of Internal Trade - BIT*, ilikuwa na jukumu la kusimamia biashara ya ndani, hususan uagizaji, ukusanyaji na usambazaji wa bidhaa.

Kwa upande wa Zanzibar biashara ya nje ilisimamiwa na Shirika la Biashara za Nje (BIZANJE). Vilevile, BIZANJE lilikuwa na jukumu la kusimamia shughuli za uuzaji wa mazao na bidhaa za Zanzibar nje ya nchi kwa kushirikiana na Shirika la Taifa la Biashara Zanzibar ambalo lilihusika zaidi na usambazaji wa bidhaa zilizoagizwa nje na zile zilizozalishwa ndani ya nchi na kuzisambaza kwa walaji. Mashirika haya yalianzishwa kisheria mwaka 1966 na kuanza kufanya kazi rasmi mwaka 1968.

Katika kuimarisha biashara ya nje kwa pande zote mbili za Muungano, Halmashauri ya Biashara ya Nje ilianzishwa kwa Sheria ya Bodi ya Biashara ya Nje Namba 5 ya Mwaka 1978. Majukumu ya BET yalikuwa ni pamoja na kuratibu, kusimamia ukuzaji wa biashara ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania nje ya nchi na kuhamasisha biashara ya nje kupitia maandalizi na ushiriki katika maonesho ya kimataifa ndani na nje ya nchi.

Hata hivyo, mwaka 2009, chini ya Sheria Na. 9 ya mwaka 2009, ilianzishwa Mamlaka ya Maendeleo ya Biashara Tanzania (*The Tanzania Trade Development Authority - TANTRADE*) ambayo lengo lake ni pamoja na: kuimarisha usimamizi wa biashara ya ndani na kuhamasisha biashara ya nje kupitia maonesho ya biashara ndani na nje ya nchi; uzalishaji kwa kuzingatia wingi na ubora wa bidhaa na huduma; usindikaji kwa kuongeza thamani kwenye mnyororo wa thamani; kufanya tafiti za masoko na bidhaa kwa maendeleo ya viwanda vidogo, vya kati na vikubwa; na kuwajengea wajasiriamali uwezo ili watambue fursa zilizoko kwenye masoko ya kanda na nchi nyingine.

Katika kuimarisha Muungano, hususan katika masuala ya biashara ya nje na ndani, TANTRADE imefungua ofisi Zanzibar ili kuhudumia

wananchi wa pande zote mbili za Muungano kwa karibu. Hatua hiyo ni muhimu katika kuunganisha nguvu ya kuitangaza Tanzania na fursa zake za uwekezaji, utalii na biashara kwa ujumla zinazofanywa katika Vituo vya Biashara vilivyoanzishwa.

## UTUMISHI WA UMMU

Kabla ya Uhuru wa Tanganyika na Mapinduzi Matukufu ya Zanzibar, utumishi wa umma ulisimamiwa na wakoloni na idadi ndogo sana ya Watanganyika na Wazanzibari. Aidha, Wachache waliobahatika kuajiriwa walitumika kulinda maslahi ya wakoloni.

Tanganyika ilipopata uhuru mwaka 1961, ilirithi utumishi wa umma ambao jukumu lake kubwa lilikuwa ni kuihudumia Serikali ya kikoloni na kulinda maslahi yake. Katika kipindi hicho, Tanganyika ilikuwa inakabiliwa na upungufu wa watumishi wazawa wenye sifa na taaluma mbalimbali za kuwawezesha kutekeleza majukumu ya taasisi mpya zilizoanzishwa. Pia, hawakuwapo watumishi wazawa wa kujaza nafasi zilizoachwa wazi na maafisa wa kikoloni ambao walilazimika kuacha kazi baada ya uhuru.

Aidha, Tanganyika ilikuwa na watumishi wa umma 17,565 mwaka 1961 kwa nchi nzima yenye ukubwa wa kilomita za mraba 945,087 na jumla ya watu 10,346,695 ambao idadi kubwa ya watu hao (asilimia 85) walikuwa hawajui kusoma na kuandika. Hivyo, ajenda kubwa ya Serikali ya uhuru ya Tanganyika ilikuwa ni kujenga Utumishi wa Umma utakaoshughulikia changamoto hizo ili wananchi waone mabadiliko na maana ya uhuru wao.

Kwa upande wa Zanzibar, kabla ya Mapinduzi ya mwaka 1964, Mfumo wa Utumishi wa Umma ulikuwa ukitumikia maslahi ya wakoloni kwa wakati huo, hakukuwa na mfumo uliozingatia mahitaji ya kitaasisi na sifa za kitaaluma ambao ungeweza kutoa fursa sawa za ajira huku Utumishi wa Umma ukijengwa na Ofisi nane na Idara nne ambazo ni Ofisi ya Waziri Mkuu; Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali; Ofisi ya Wizara ya Elimu; Ofisi ya Wizara ya Elimu na Ustawi wa Jamii, Ofisi ya Wizara ya Siha, Ofisi ya Wizara ya Mawasiliano na Ardhi; Ofisi ya Mkuu wa Watumishi, Ofisi ya Hazina; Ofisi ya Idara ya Mkaguzi wa Hesabu; Idara ya Mahakama; Baraza la Kutunga Sheria na Tume ya Utumishi. Ofisi na Idara hizo zilikuwa na Watumishi 340, wakati ambapo idadi ya Wananchi ilikadiriwa kuwa ni watu 300,000 kwa mujibu wa Sensa ya Mwaka 1963.

Utaratibu wa utoaji wa ajira kwa kipindi hicho uliozingatia misingi ya kizalendo ya kujitolea katika ujenzi wa taifa kupitia kambi za vijana



au kufanya kazi za kujitolea kwa muda maalum. Baada ya hapo vijana walipata fursa ya kuingia katika ajira. Jukumu la utoaji wa vibali vya ajira lilisimamiwa na Ofisi ya Baraza la Mapinduzi.

## **Utumishi wa Umma katika Jamhuri ya Muungano**

Masuala ya ajira katika Jamhuri ya Muungano wa Tanzania yanasimamiwa na Sheria ya Utumishi wa Umma Na. 8 ya Mwaka 2002 na Kanuni zake za Mwaka 2003 ambazo zimeweka utaratibu wa wazi wa ajira katika utumishi wa umma. Sheria hiyo inatoa fursa sawa za ajira kwa Wananchi wote wa Tanzania ambao wanaomba ajira wenye sifa na vigezo kama elimu, uzoefu na sifa husika.

Kuhusu nafasi za watumishi wa kawaida kwenye Taasisi za Muungano, utaratibu wa muda wa mgao wa ajira uliokubalika kutumika ni asilimia 79 kwa Tanzania Bara na asilimia 21 kwa Tanzania Zanzibar. Utaratibu huu unatekelezwa kwa mujibu wa Waraka wa Serikali (SMT) wa tarehe 10 Mei, 2013. Aidha, pande mbili zimekubaliana kuwa na mfumo shirikishi katika mchakato mzima wa ajira katika Taasisi za Muungano.

## **KODI YA MAPATO, USHURU WA FORODHA NA BIDHAA**

Usimamizi wa Kodi ya Mapato kwa Tanganyika na Zanzibar kabla ya Muungano, ulikuwa chini ya Bodi ya Mapato ya Afrika Mashariki. Wakati huo nchi za Afrika Mashariki zilikuwa zinajumuisha nchi za Kenya, Uganda, Tanganyika na Zanzibar. Baada ya Muungano wa Tanganyika na Zanzibar, Bodi ya Mapato ya Afrika Mashariki ilijumuisha nchi za Kenya, Uganda na Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Baada ya kuanzishwa Jumuiya ya Afrika Mashariki mwaka 1967, Kodi ya Mapato, Ushuru wa Forodha na Bidhaa viliwekwa chini ya Jumuiya ya Afrika Mashariki.

Kufuatia kuvunjika kwa Jumuiya ya Afrika Mashariki mwaka 1977, majukumu ya usimamizi wa kodi yaliwekwa chini ya Serikali. SMT ilianzisha Idara ya Mapato ya Ndani na Mauzo, na Idara ya Ushuru wa Forodha na Ushuru wa Bidhaa. Mwaka 1995, Serikali ya Jamhuri ya Muungano ilianzisha Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA).

Mamlaka hiyo ilipewa majukumu ya kutathmini, kukusanya na kusimamia mapato yote ya Serikali Kuu; kuishauri Serikali katika mambo yote yanayohusiana na Sera za Kodi na uhamasishaji wa ulipaji wa kodi kwa hiari; na kutoa takwimu za kibiashara na machapisho.

Vilevile, TRA ilipewa jukumu la kuboresha huduma kwa walipa kodi na kusimamia ipasavyo Sheria zote zinazohusu Mapato ya Serikali Kuu.

TRA inasimamia Kodi ya Mapato na Ushuru wa Forodha ambayo ni mapato ya Muungano kwa Tanzania Bara na Tanzania Zanzibar. TRA pia inashugulikia kodi zisizo za Muungano kwa Tanzania Bara. Kwa upande wa Zanzibar, Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar ilianzisha Bodi ya Mapato Zanzibar (ZRB) chini ya Sheria Na. 7 ya mwaka 1996 na Bodi hiyo ilianza kazi rasmi mwaka 1998. Majukumu ya ZRB ni kusimamia nakukusanya kodi za ndani zisizo za Muungano kwa upande wa Tanzania Zanzibar.

## **BANDARI**

Uendeshaji wa bandari nchini unaongozwa na sheria mbili: Sheria ya Bandari, Na. 17 ya Mwaka 2004 kwa upande wa Tanzania Bara na Sheria ya Bandari ya Zanzibar Na. 1 ya Mwaka 1997. Sheria hizi mbili zinaanzisha Mamlaka ya Bandari Tanzania na Shirika la Bandari Zanzibar mtawalia.

Sheria ya Bandari ya Tanzania ilitanguliwa na Sheria ya Mamlaka ya Bandari Tanzania ya Mwaka 1977 ambayo ilitungwa kufuatia kuvunjika kwa Jumuiya ya Afrika Mashariki na Shirika lake lililokuwa linasimamia shughuli zote za bandari Afrika Mashariki.

Pamoja na kuwa kila upande unatumia sheria yake, pande hizo mbili zinashirikiana katika kubadilishana taarifa zinazohusiana na masuala ya usafiri majini kupitia *Control Tower* ya Mamlaka na kubadilishana uzoefu kati ya Bodi ya Wakurugenzi na Menejimenti ya Shirika la Bandari Zanzibar na Mamlaka ya Bandari Tanzania. Mamlaka hizo huweka viwango vya ubora wa vyombo vya majini kwa kushirikiana na Mamlaka ya Udhhibiti wa Usafiri Majini Zanzibar na Shirika la Uwakala wa Meli Tanzania (TASAC).

Aidha, Taasisi hizo hushirikiana kwa kuweka kanuni na taratibu za ukaguzi, utoaji wa leseni za meli, manahodha na mabaharia, na ukataji tiketi katika bandari za pande zote za Muungano. Hali kadhalika, Mamlaka ya Bandari Tanzania inaendesha Chuo cha Bandari kilichopo Tandika, Dar es Salaam, kinachopokea pia wanafunzi kutoka Zanzibar.

## **POSTA NA SIMU**

Kabla ya Muungano, huduma za Posta kwa upande wa Tanganyika zilisimamiwa chini ya Sheria iliyoanzisha Shirika la Posta na Simu la Afrika Mashariki. Taasisi hiyo ilikuwa na mamlaka pekee ya kusimamia

na kutoa huduma za posta katika nchi za Kenya, Uganda na Tanganyika. Kwa upande mwingine, Zanzibar ilijiunga na Umoja wa Posta Duniani mwaka 1895.

Pamoja na kuwa mwanachama wa Umoja wa Posta Duniani, Zanzibar haikuwa chini ya Shirika la Posta na Simu la Afrika Mashariki. Baada ya Muungano wa Tanganyika na Zanzibar na hatimaye kuanzishwa kwa Jumuiya ya Afrika Mashariki mwaka 1967, huduma za posta Zanzibar ziliunganishwa katika Jumuiya hiyo kupitia Serikali ya Muungano.

Baada ya kuanzishwa kwa Jumuiya ya Afrika Mashariki mwaka 1967, ofisi nyingi zilianzishwa na nyingine kupanuliwa kwa lengo la kuhakikisha kuwa ofisi hizo zinakuwa posta kamili zinazotoa huduma ikiwa ni pamoja na Wakala wa Benki ya Posta. Kutokana na mpango huo, Makao Makuu ya Posta pamoja na Posta Kuu zilijengwa Dar es Salaam. Kwa upande wa Zanzibar, Posta Kuu ya Kijangwani na Posta za Chakechake, Wete, Mkoani na Mkokotoni zilijengwa.

Shirika jipya la Posta na Simu liliundwa kwa Sheria ya Shirika la Posta na Simu Tanzania Sura Namba 305 kutokana na kuvunjika kwa Jumuiya ya Afrika Mashariki mwaka 1977.

Mwaka 1993, Shirika la Posta na Simu Tanzania lilirekebishwa na kuunda taasisi tatu zilizojitegemea, yaani Kampuni ya Simu Tanzania (TTCL), Shirika la Posta Tanzania na Benki ya Posta Tanzania. Mabadiliko hayo yalilenga kuboresha huduma katika Sekta ya Mawasiliano ili sekta hiyo ichangie vyema zaidi katika maendeleo ya taifa.

Sheria ya Shirika la Posta Tanzania, Sura Namba 303, ililipa Shirika la Posta majukumu ya kuwa mhimili mkuu wa utoaji wa huduma za posta katika Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kuratibu na kusimamia mawasiliano yote ya posta nchini. Shirika pia lilipewa jukumu la kuhakikisha kuwa huduma za msingi za mawasiliano ya posta hasa za barua na vifurushi zinawafikia watu wengi zaidi mijini na vijijini. Majukumu hayo yalikusishwa pia kuweka mipango endelevu ya kuwezesha huduma za posta kuchangia maendeleo ya nchi kiuchumi na kijamii.

Serikali imepanua na kuimarisha mtandao wa ofisi za kutoa huduma za Posta na Simu Tanzania Bara na Zanzibar hadi ngazi za wilaya. Vilevile, Shirika la Posta Tanzania limeunganishwa katika mtandao wa kielektroniki wa kimataifa ambao unawezesha ufuatiliaji wa nyaraka na vipeto, Rejista na Vifurushi vya Kimataifa vinavyopitia mtandao wa posta.

Aidha, utekelezaji wa Mfumo Mpya wa Anwani za Makazi na Misimbo ya Posta umeanza kwa miji ya Dar es Salaam, Zanzibar,

Arusha na Dodoma na unalenga kila mwananchi kuwa na anwani kamili inayotambulisha makazi yake ili kutoa huduma mtambuka.

## Ubinafsishaji wa TTCL

Kutokana na kuongezeka kwa ushindani wa ndani na uendeshaji usio na tija, mwaka 2001 Serikali iliamua kubinafsisha sehemu za hisa za TTCL. Kampuni binafsi ya mawasiliano *Celtel International* ilichukua asilimia 35 ya hisa ndani ya TTCL. Hisa zilizobaki (asilimia 65) ziliendelea kumilikiwa na Serikali.

Mwaka 2005 Kampuni ya *Celtel* ilijitoa kwenye Menejimenti ya pamoja na Serikali ya Tanzania na hivyo pande hizo mbili zikatenganisha masuala ya kifedha, kisheria na kiutendaji. Mwaka 2007 Serikali iliipa kampuni ya Canada (*SashTel International*) mkataba wa miaka mitatu wa kuendesha TTCL. *SashTel* ilianza kuiendesha TTCL kuanzia Julai, 2007. Hata hivyo, mkataba kati ya Serikali na *Sashtel* ulivunjika rasmi mwezi Julai, 2009 kufuatia uendeshaji usioridhisha.

Mwaka 2010 BHART AIRTEL iliingia mkataba wa kununua uendeshaji wa simu za mkononi katika nchi 15 za Afrika na hivyo kuwekeza thamani ya asilimia 35 ya hisa zote ndani ya kampuni ya Zain. Mwezi Februari, 2016 BHART AIRTEL walikubali kuziua hisa zao (asilimia 35) kwa Serikali, hivyo, kuanzia tarehe 23, Juni, 2016 TTCL ikawa mikononi mwa Serikali kwa asilimia 100.

TTCL kwa sasa ndiyo kampuni kubwa Tanzania inayotoa huduma za mawasiliano katika teknolojia ya simu za mezani na kwa simu zisizokuwa na waya; ina mtandao wa simu wa waya ulioenea sehemu kubwa ya Tanzania na inatoa huduma kwa taasisi nyingi muhimu katika uchumi na maendeleo ya jamii ikiwamo Serikali, benki, vyuo, shule na ofisi za kibalozi. Kampuni ya Simu Tanzania ndiyo inayosimamia ujenzi na uendeshaji wa Mkongo wa Taifa wa Mawasiliano.

## USAFIRI NA USAFIRISHAJI WA ANGA

Kabla ya Muungano, utoaji wa huduma za usafiri na usafirishaji kwa njia ya anga uliendeshwa na Shirika la Ndege la Afrika Mashariki lililoundwa tarehe 1 Januari, 1946 chini ya utawala wa Uingereza. Shirika hilo lilikuwa sehemu ya shirika hodhi la Uingereza la utoaji huduma kwa njia ya anga nje ya Uingereza ambalo lilitoa huduma katika makoloni ya Kenya, Uganda na Tanganyika na sehemu nyingine duniani. Baada ya Tanganyika kupata uhuru mwaka 1961, huduma za usafiri na usafirishaji

kwa njia ya anga ziliendelea kuwa chini ya Shirika la Ndege la Afrika Mashariki ambalo lilirithiwa kutoka kwa wakoloni wa Uingereza.

Baada ya Muungano wa Tanganyika na Zanzibar ambao ulishuhudia kuanzishwa kwa Jumuiya ya Afrika Mashariki mwaka 1967, shughuli za usafirishaji wa anga ziliwekwa chini ya Shirika la Ndege la Jumuiya hiyo. Pamoja na shughuli nyingine, shirika hilo lilijishughulisha na usimamizi na uendeshaji wa kiufundi katika masuala ya usafiri wa anga. Hata hivyo, shughuli za utoaji wa huduma za matengenezo, uangalizi wa viwanja na zimamoto zilikuwa chini ya Serikali za nchi wanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki. Hadi kufikia mwaka 1970 huduma za usafiri na usafirishaji wa anga zilifika Uingereza, Pakistani, India, Aden na Rhodesia.

Kufuatia kuvunjika kwa Jumuiya hiyo mwaka 1977, masuala ya usafiri wa anga yalifanywa kuwa ya Muungano na hivyo kuanzishwa Kurugenzi ya Usafiri wa Anga kwa Sheria ya Usafiri wa Anga Sura Namba 80. Vilevile, Shirika la Ndege la Tanzania lilianzishwa ili kutoa huduma ya usafiri wa anga badala ya Shirika la Ndege la Afrika Mashariki ambalo shughuli zake zilikoma baada ya kuvunjika kwa Jumuiya hiyo.

Shirika la Ndege Tanzania lilianza kutoa huduma za usafiri wa anga kwa kutumia ndege tatu, moja aina ya *DC-9* na mbili aina ya *Foker Friendships F27*. Baadaye Serikali ilinunua ndege nyingine aina ya *Boeing B737-200 Combi* (mbili), *Foker Friendships* (mbili), na *Twin Otters* (nne). Kutokana na kudorora kwa uendeshaji wa Shirika hilo ikiwa ni pamoja na kuiingizia Serikali hasara, mwaka 2002, Shirika hilo lilibinafsishwa na kuundwa Kampuni ya Ndege Tanzania (*Air Tanzania Company Ltd (ATCL)*). Hadi kufikia mwaka 2002, *ATCL* ilikuwa na ndege moja aina ya *B737-200* na nyingine ya kukodi ya *B737-300*.

Nia ya Serikali kubinafsisha Shirika la Ndege ilikuwa ni kulifanya shirika hilo kuwa imara na kutoa huduma bora za ndani na nje ya nchi. Hata hivyo, baada ubinafsishaji na uundwaji mpya wa Kampuni ya Ndege Tanzania, bado kampuni hiyo ilishindwa kukua, hivyo, kujiendesha kwa hasara. Hali hii ilileta mzigo wa madeni kwa *ATCL* na Serikali iliamua kuvunja ubia kati ya *ATCL* na Shirika la Ndege la Afrika Kusini mwaka 2006, kwa kununua hisa asilimia 49 zilizokuwa zinamilikiwa na *SAA*. Wakati ubia huu unavunjika, *ATCL* ilikuwa na ndege moja tu aina *Dash Q 300*.

Mwaka 2016, Serikali ilifufua shirika la ndege kwa kununua ndege mpya na kuboresha menejimenti na muundo wa kampuni hiyo. Hadi kufikia mwaka 2021 jumla ya ndege 12 za kisasa zilinunuliwa na zinatoa huduma ndani na nje ya nchi. Ndege hizo ni *Bombardier Dash8 Q400*

tano, *Airbus 220 – 300* nne, *Boeing 787 – 8 Dreamliner* mbili na *Dash8 Q300* moja.



*Ndege aina ya Boeing 787-8 Dreamliner inayomilikiwa na Shirika la Ndege la Tanzania (ATCL)*

Vilevile, hatua mbalimbali zimechukuliwa kuimarisha sekta ya usafiri wa anga, ikiwa ni pamoja na kuuboresha uwanja wa ndege wa Zanzibar, kufungua Ofisi Ndogo ya Msaidizi wa Mamlaka ya Usafiri wa Anga Zanzibar na kuruhusu mashirika ya watu binafsi kuendesha biashara ya usafiri na usafirishaji. Aidha, suala la usimamizi, udhibiti na Sera ya Usafiri na Usafirishaji wa Anga vimeendelea kusimamiwa na kuratibiwa vizuri katika sura ya Muungano. Serikali pia inaendelea kuimarisha usafiri wa anga ambapo Viwanja vya Ndege vyenye lengo la kurahisisha huduma za usafiri na usafirishaji vimeendelea kujengwa na kukarabatiwa katika mikoa mbalimbali nchini.

## **MAMBO YOTE YANAYOHUSIKA NA SARAFU, FEDHA, MABENKI NA FEDHA ZA KIGENI**

Historia ya shughuli za kibenki nchini Tanzania imegawanyika katika sehemu kuu tatu. Sehemu ya kwanza ni enzi za ukoloni na kabla ya Azimio la Arusha mwaka 1967, sehemu ya pili ni baada ya Azimio la Arusha hadi 1991 wakati Sheria ya Benki na Taasisi za Fedha ilipotungwa, na sehemu ya tatu ni baada ya 1991.

## Enzi za Utawala wa Ujerumani (1880 hadi 1919)

Kabla ya mwaka 1919, mfumo wa fedha wa Tanganyika ulikuwa chini ya utawala wa Ujerumani, na Zanzibar ulikuwa chini ya utawala wa Waarabu. Tanganyika ilitumia Rupia ya Kijerumani ambayo ilitengenezwa kwa fedha pamoja na sarafu nyingine iliyoitwa *Heller* ambayo ilikuwa ni moja ya mia ya Rupia kwa ajili ya ubadilishanaji wa bidhaa na huduma.

Kwa upande wa Zanzibar ilitumika Rupia za madini ya fedha (*silver rupees*) na Riali. Fedha halali kwa wakati huo ilitolewa na USultani wa Zanzibar kuanzia mwaka 1882. Amri ya kuanzisha pesa hizi ilitolewa na Sultani Barghash ibn Said ibn Sultan. Rupia ya India na *Dolar ya Maria Theresia* zilitumika pamoja na Riali katika biashara Zanzibar. Kutokana na mwingiliano mkubwa na nchi za Afrika Mashariki, Zanzibar ikaamua kujiunga na Bodi ya Sarafu ya Afrika Mashariki mwaka 1936.

Mnamo mwaka 1905, Wajerumani walianzisha Benki ya Biashara (*Deutsch-Ostafrikanische Bank*) jijini Dar es Salaam. Benki hiyo ilikuwa na kiwanda cha kutengeneza pesa ya Kijerumani katika mkoa wa Tabora ambapo kiwanda hiki kiliwajibika kutengeneza pesa za kutosha kwa mahitaji ya fedha ya wakati huo. Enzi za utawala wa Wajerumani, ni benki mbili tu zilizokuwa zimeandikishwa: Benki ya *Deutsche Ostafrikanische* na *Handelsbank fur Ostafrika*.

## Enzi za Utawala wa Waingereza, 1919 - 1961

Baada ya Vita Kuu ya Kwanza ya Dunia, Tanganyika iliwekwa chini ya uangalizi wa Uingereza na mfumo wake wa sarafu ukaunganishwa na ule wa Kenya na Uganda ambazo zilikuwa chini ukoloni wa Waingereza. Rasilimali zote za mabanki ya Kijerumani zilipigwa mnada ili kuruhusu Benki za Uingereza kufungua ofisi zao. Fedha aina ya '*Specie*' na '*Pice*' ikaanzishwa kwa ajili ya kutumika Bara. Mwaka 1905 sarafu ya Rupia ya India ilifanywa kuwa sarafu rasmi ya nchi za Afrika Mashariki hadi ilipoanzishwa Bodi ya Sarafu ya Afrika Mashariki.

Baada ya Vita Kuu ya Pili ya Dunia, benki tatu: *National* na *Grindlays Bank*, *Standard Bank* na *Barclays Bank D.C.O* zilianzishwa na Waingereza ili kuchukua nafasi ya benki zilizokuwapo wakati wa utawala wa Wajerumani. Mwanzoni mwa miaka ya 1950, benki nyingine kutoka India zilifungua matawi Tanganyika, hizi zilikuwa: Benki ya India na

Benki ya Baroda, ambazo zilizofungua matawi Dar es Salaam, Moshi na Mwanza. Pia, taasisi ya Anglo-French inayojulikana kama Benki ya Ottoman, iliendesha shughuli zake Dar es salaam, Kigoma na Moshi. Hadi kufikia mwaka 1967, sekta ya benki ilikuwa na benki tisa nchini.

## **Kuanzishwa kwa Bodi ya Sarafu ya Afrika Mashariki**

Bodi ya Sarafu ya Afrika Mashariki ilianzishwa ili kusimamia masuala ya fedha kwa nchi zilizokuwa chini ya utawala wa Uingereza kuanzia mwaka 1919 hadi mwaka 1965. Bodi hii ilianzishwa mara tu baada ya Vita Kuu ya Kwanza ya Dunia, yaani Waingereza walipoanza kuitawala Tanganyika. Wajibu wa Bodi hii ulikuwa ni kuchapisha noti, kutengeneza sarafu, kusimamia usambazaji wa fedha katika Afrika Mashariki, kuhakikisha kuna kiwango cha fedha kinachohitajika katika mzunguko ili kukidhi mahitaji.

Bodi hii ilianza na nchi za Tanganyika, Kenya na Uganda ambapo Zanzibar ilijiunga mwaka 1936. Bodi ilikuwa na madaraka ya kutoa noti na sarafu kulingana na michoro iliyopitishwa na Waziri wa Mambo ya Nje wa Uingereza. Waziri huyo aliweka kiwango cha kubadilisha fedha kati ya sarafu ya Bodi ya Sarafu ya Afrika Mashariki na paundi ya Uingereza. Kazi kubwa ya Bodi ilikuwa ni kuhakikisha kwamba thamani ya shilingi katika nchi za Afrika Mashariki inakuwa sawa na shilingi ya Uingereza; hili liliwezekana kwa sababu dhamana za paundi ya Uingereza zilitumika kuipa uzito sarafu ya Afrika Mashariki muda wote wa uhai wake.

Ilipofika mwaka 1923, shilingi iliimarika na kuwa sarafu rasmi kwa nchi za Kenya, Uganda na Tanganyika. Bodi ya Sarafu ya Afrika Mashariki ilihitimisha kazi zake mwaka 1966 wakati nchi za Afrika Mashariki za Tanzania, Kenya na Uganda kila moja ilipoamua kuanzisha Benki Kuu yake.

## **Benki Kuu ya Tanzania (BoT)**

Bunge la Jamhuri ya Muungano lilipitisha Sheria ya Benki Kuu Na. 12 ya mwaka 1965 na kuwezesha Benki Kuu ya Tanzania kuanza kazi rasmi tarehe 14 Juni 1966. Sheria hiyo ilifanyiwa marekebisho na kuwezesha kutungwa kwa Sheria ya Benki Kuu ya Tanzania ya mwaka 1978 na Sheria ya Benki Kuu ya Tanzania ya mwaka 1995. Benki Kuu ya Tanzania imekuwa ikiendesha shughuli zake katika matawi sita ya Dodoma (Makao Makuu), Dar es Salaam, Mwanza, Arusha, Mbeya, Mtwara na Tawi la Zanzibar.





*Jengo la Benki Kuu ya Tanzania lililopo Barabara ya Mirambo, Dar es Salaam*

## **Baada ya Azimio la Arusha, 1967-1991**

Kufuatia Azimio la Arusha mwaka 1967, benki zote za biashara binafsi zilitaifishwa na kubakiwa na benki 6 ambazo zilimilikiwa na Serikali. Benki hizo ni Benki ya Taifa ya Biashara, Benki ya watu wa Zanzibar, Benki ya Posta, Benki ya Nyumba Tanzania, Benki ya Uwekezaji Tanzania na Benki ya Maendeleo Vijijini. Benki hizi zilianzishwa ili kutoa huduma kwa wananchi pamoja na kutoa mikopo kwa mashirika yaliyokuwa yakimilikiwa na Serikali. Mwaka 1991 Sheria ya Benki na Taasisi za Fedha, ilitungwa, ambayo iliruhusu uanzishwaji wa benki binafsi za biashara.

## **Baada ya 1991**

Kutungwa kwa Sheria ya Benki na Taasisi za Fedha mwaka 1991, kulitoa mamlaka kwa Benki Kuu ya Tanzania (BoT) kutoa leseni, kudhibiti na kusimamia benki na taasisi za fedha. Mwaka 1992, Sheria ya Fedha za Kigeni ya mwaka 1992 ilitungwa na iliipa Benki Kuu mamlaka ya kutoa leseni na kudhibiti maduka ya kubadilisha fedha za kigeni. Kwa kuifanya sekta ya fedha kuwa huria, benki binafsi (ndani na nje) zilianzisha biashara nchini, zikitoa huduma za kifedha katika soko huria. Benki binafsi za awali kuanzishwa ni pamoja na: *Meridian Biao Tanzania Ltd*

(1992), *Standard Chartered Bank Tanzania Ltd* (1993) *Eurafrikan Bank Tanzania* (1994) na *Citibank Tanzania Ltd* (1995).

## LESENI ZA VIWANDA NA TAKWIMU

Kihistoria, utoaji wa leseni za viwanda ni jukumu linalotokana na utekelezaji wa Sheria ya Usajili na Utoaji wa Leseni za Viwanda iliyoanza kutumika rasmi mwaka 1967. Hii ni baada ya jukumu hilo kuorodheshwa kama Jambo la 13 la Muungano kufuatia kuanzishwa kwa iliyokuwa Jumuiya ya Afrika Mashariki.

Jukumu la leseni za viwanda linasimamiwa na Wakala wa Usajili wa Biashara na Utoaji Leseni (BRELA). BRELA Ilianzishwa mwaka 1999 chini ya Sheria ya Wakala wa Serikali, Sura Namba 245. Mrajisi wa Viwanda na Bodi ya utoaji wa Leseni za Viwanda wanashirikiana na Naibu Msajili wa Viwanda Zanzibar. Aidha, BRELA imeendelea kutoa ushirikiano wa karibu kwa Serikali ya Mapinduzi Zanzibar kila inapohitajika. Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar ina wajumbe wawili katika Bodi ya Leseni za Viwanda.

Kwa mujibu wa Sheria hiyo, viwanda vyote vinavyotakiwa kuanzishwa vyenye mtaji unaozidi shilingi milioni 100, vinapaswa kuidhinishwa na Bodi ya Usajili na Utoaji wa Leseni za Viwanda (inayoundwa na wajumbe kutoka pande zote za Muungano) baada ya kukidhi vigezo. Kwa upande wa viwanda vidogo vyenye mtaji chini ya shilingi milioni 100, Sheria hiyo inampa mamlaka Msajili ya kusajili na kutoa leseni bila ya kupitia Bodi.

## ELIMU

Wakoloni wote bila ya kuwatofautisha, waliingia Afrika kwa nguvu au kwa hila wakiwa na lengo kuu la kuvuna bure rasilimali za bara hili. Katika kutekeleza malengo yao ya kikoloni, nguvu kubwa ilitumika kujidhatiti kimadaraka na kuvuruga kabisa utamaduni au mfumo mzima wa maisha wa jamii za Kiafrika kwa kutumia elimu, dini, nguvu ya dola na hata ushawishi wa lawalawa. Hakika, Afrika ilipoteza rasilimali nyingi, ubunifu na kujiamini kutokana na hila hizo.

Kwa kuwa azma kuu ya wakoloni ilikuwa kuchota rasilimali nyingi iwezekanavyo kutoka kwa watawaliwa, ikiwamo rasilimali watu na mali asili mbalimbali, kazi ya kwanza waliyoifanya ilikuwa kuvuruga utamaduni wa watawaliwa, wapoteze utambulisho wao na wasijithamini wala kujiamini tena kama binadamu miongoni mwa binadamu. Ni katika muktadha huo, Mwalimu Nyerere alisema mara tu baada ya

uhuru wa Tanganyika kuwa “Taifa lisilo na utamaduni wake ni sawa na Taifa mfu”. Elimu na dini vilitumika sana kuua utamaduni wa Mwafrika kwa viwango vinavyotofautiana.

Pili, pamoja na kwamba jambo la Muungano hapa ni Elimu ya Juu, elimu ya juu haiwezi kutoa mchango chanya katika jamii bila kupokea watoto wa kutosha na walioandaliwa vizuri ngazi ya elimu ya msingi na sekondari. Hivyo, jambo hili Namba 15 la Muungano halitekelezeki bila pande zote mbili za Muungano kujizatiti ngazi ya elimu ya msingi na sekondari.

Ifahamike kuwa, kabla ya kuja kwa wageni katika mwambao wa Tanganyika na Zanzibar, kila kabila upande wa Bara au jamii ya Zanzibar ya Wahadimu, Watumbatu na makabila mengine yaliyokuja baadaye, lilikuwa na mfumo wake wa elimu ya kijadi iliyojumuisha maarifa, stadi, maadili, utamaduni, mbinu na taratibu nzuri za kufanya kazi na kujilinda kutokana na mabaa ya njaa, magonjwa na maadui wa usalama wa jamii na wa mali zao.

Elimu hiyo ilirithishwa kutoka kizazi kimoja hadi kingine na mambo ya kujifunza yaligawanyika kirika na kutolewa na watu wazima nyumbani, kazini na katika nyanja nyingine za maisha. Nidhamu, amani na utulivu katika jamii zote hizo, vilidumishwa na dini zao za kimila au imani zao za jadi na kusimamiwa na watu wa marika mbalimbali. Mfumo huu wa maisha ulibadilika mara baada ya wakoloni kuingia nchini.<sup>8</sup>

## Elimu Kipindi cha Ukoloni

Wageni wa kwanza kuingia pwani ya Afrika Mashariki walitokea Mashariki ya Kati na Asia, wakifuatiwa na Wareno, Wajerumani na baadaye Waingereza. Kila mmoja alikuja na dini yake na mfumo wake wa elimu kukidhi malengo na mahitaji yao. Sera zao zilikuwa zilezile: “wagawe uwatawale” na “wabague, watambue nafasi zao”.

Watoto walizoezwa ubaguzi wangali wadogo kwa kutenganishiwa shule: za Wazungu, Waarabu, Wahindi na mataifa mengine na shule za Waafrika zilitofautiana sana kwa wingi, malengo, mitaala, sifa na taaluma za walimu, lugha ya kufundishia, na ubora wa vifaa na majengo ya shule na nyumba za walimu.

<sup>7</sup> Soma utangulizi katika Ndagala, D. D, Utamaduni na Maendeleo Nchini Tanzania, Dar es Salaam, 2018.

<sup>8</sup> Maudhui ya Hotuba ya Miaka 45 ya Muungano ya Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete, Rais wa Awamu ya Nne wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Mwaka 1890 skuli kwa watoto wa Kihindi ilianzishwa Zanzibar na mwaka 1907 watoto, wajukuu na jamaa za Sultani nao wakapata shule yao maalum. Aidha, mwaka 1920 skuli kwa ajili ya watoto wa Kiafrika ikaanzishwa ili baadaye baadhi yao waweze kuendelezwa na kutumika serikalini.

Kati ya mwaka 1890 na 1963 Waafrika walioendelezwa au kupata elimu ya juu zaidi walikuwa 36 katika kipindi hicho cha miaka 73. Kwa hesabu za haraka, ina maana ya kwamba serikali ya Sultani ilimpeleka elimu ya juu kijana mmoja tu wa Kiafrika kila miaka miwili.

Kwa mfano, mwaka 1958 vijana 126 kutoka Zanzibar walikuwa wanasomeshwa katika vyuo mbalimbali nchini Uingereza. Kati ya hao, mmoja tu alikuwa kijana wa Kiafrika<sup>9</sup> pamoja na kwamba katika kipindi hicho Waafrika walikuwa asilimia 85 ya wakazi wa Zanzibar. Kwa kifupi hali ya elimu Zanzibar kipindi chote cha ukoloni wa Mwarabu na Mwingereza, ilikuwa duni sana hasa kwa Waafrika waliokuwa wengi visiwani.

## Tanzania Bara

Wakati Tanzania Bara inapata uhuru wa ndani tarehe 9 Desemba mwaka 1961, kulikuwa na shule za msingi 3,000 zilizojengwa katika kipindi cha ukoloni wa Mjerumani na Mwingereza cha miaka 78, zikiwa na wanafunzi 486,000.

Katika kipindi cha miaka 57 tu ya Muungano (1964 – 2021), Tanzania Bara ilikuwa na jumla ya shule za msingi 18,152 (Serikali shule 16,406 na binafsi shule 1,746) kutoka shule 3,000 zilizokuwa na jumla ya wanafunzi 10,460,785 kutoka 486,000.

Kwa upande wa elimu ya sekondari, Tanzania Bara ilirithi kutoka kwa wakoloni shule za sekondari 63 (zikiwamo seminari 9) zilizokuwa na wanafunzi 13,897. Katika kipindi cha miaka 57 (1964 – 2021), Tanzania Bara ilijivunia jumla ya shule za sekondari 5,143 (Serikali shule 3,863 na binafsi shule 1,280) kutoka shule 63 tu zilizokuwa na wanafunzi 2,338,457 kutoka wanafunzi 13,897.

Takwimu hazidanganyi, zinajieleza zenyewe kuwa ukoloni ulichelewesha sana maendeleo ya elimu ya msingi na sekondari Tanzania Bara. Haikuwa kwa bahati mbaya bali kwa makusudi ya wakoloni kuwa na jeshi kubwa la watawaliwa mbumbumbu, wasiohoji, wasiojiamini na walio tayari muda wote kuburuzwa kwa matakwa ya wakoloni. Ndiyo

<sup>9</sup> Bakari, M.A., *The Democratisation Process in Zanzibar: A Retarded Transition*, Institute of African Affairs, Hamburg, 2001, uk. 93 na Hettiger, M., *kama hapo juu*, uk. 10.

maana Mwalimu Nyerere alitangaza vita mara baada ya uhuru dhidi ya ujinga, maradhi na umaskini.

Mbali na kampeni hiyo dhidi ya ujinga, Muungano ulichochea zaidi ari ya kupanua na kuimarisha elimu ya msingi na sekondari kwa kasi ili kufanikisha azma ya Muungano ya kuzalisha wataalamu wetu wenyewe kwa wingi kupitia elimu ya juu.

Ndiyo sababu mara baada ya uhuru wa Tanganyika na Muungano wa Tanganyika na Zanzibar, hatua kadhaa zilichukuliwa kuondoa vikwazo vya maendeleo ya kasi ya elimu nchini. Mwalimu Nyerere alianza kwa kupiga marufuku mwaka 1962 utoaji wa elimu kwa msingi wa ubaguzi wa rangi, ukabila na udini. Elimu bila malipo baada ya uhuru ikawakomboha kutoka kwenye ujinga maelfu ya watoto wa wakulima na wafanyakazi na kubadilisha kabisa sura ya elimu nchini.

Aidha, mwaka 1967 Serikali ilitangaza Azimio la Arusha lililolenga kuiweka nchi kwenye mfumo wa “Siasa ya Ujamaa na Kujitegemea”. Azimio likazalisha Elimu ya Kujitegemea iliyobadilisha mfumo mzima wa utoaji elimu, dhana na fikra za elimu ya kikoloni na kuwaepusha vijana na utegemezi.

Kufuatia kutangazwa kwa Azimio la Arusha na pia kutungwa kwa Sheria ya Elimu ya Mwaka 1969, Serikali ilitaifisha shule zote zilizokuwa zikimilikiwa na watu binafsi na mashirika ya kidini kuzuia mgawanyiko wa watoto wa taifa jipya. Wakati huo huo Serikali ilifanya ugatuzi wa masuala ya elimu hasa ya msingi na sekondari,<sup>10</sup> kwa lengo la kupeleka rasilimali fedha na uendeshaji wa masuala ya elimu karibu na wananchi. Huu ndio ulikuwa msingi wa upanuzi wa kasi wa elimu ya msingi na sekondari ulioelezwa kwa takwimu hapo juu.

## Zanzibar

Mara baada ya Mapinduzi ya tarehe 12 Januari, 1964 na Muungano wa Tanganyika na Zanzibar wa tarehe 26 Aprili, 1964, Rais wa Zanzibar Sheikh Abeid A. Karume alichukua hatua zifuatazo kusahihisha makosa katika elimu ya kikoloni. Tarehe 1 Julai, 1964 ubaguzi wote katika elimu na huduma zote za kijamii ulipigwa marufuku:

1. Kwa kuanzia, skuli 11 kati ya skuli 20 za binafsi zikataifishwa kuondoa kabisa viashiria vyovyote vile vya ubaguzi;
2. Tarehe 23 Septemba, 1964 tangazo la elimu bure kwa wote likatolewa kutoa fursa kwa wasio na uwezo kifedha kupata elimu;

<sup>10</sup> Placidius Ndibalema, “Expansion of Secondary Schools in Tanzania: Policy Practices, trends and Implications to Quality Education”, Seminar Paper, <https://www.grin.com/document/191864>

3. Ajira kwa watoto wadogo wanaotakiwa kwenda skuli, zikapigwa marufuku na kuokoa maelfu ya watoto wa Kiafrika waliokuwa wanatumikishwa majumbani na mashambani badala ya kwenda skuli kwa kisingizio cha ukosefu wa nafasi za masomo; na
4. Ujenzi wa skuli mpya za msingi ukaanza ili kupokea watoto wengi zaidi wa Kiafrika waliokuwa wamekosa fursa za kwenda skuli kutokana na sera za kibaguzi za kikoloni. Kufikia mwishoni mwa mwaka 1964, skuli 13 mpya zilijengwa.

Ilikuwa lazima hatua zote hizo zichukuliwe mapema ili kutoa fursa kwa maelfu ya watoto wa Kiafrika waliowekwa pembeni na mfumo wa kikoloni wa Serikali ya Sultani. Picha kamili ya mchango wa serikali ya kikoloni ya Sultani wa Zanzibar katika sekta ya elimu kwa miaka takriban 200 iliyokuwa madarakani, ukilinganisha na mchango wa Serikali ya Mapinduzi Zanzibar chini ya Muungano kwa miaka 57 tu, ni kama ifuatayo:

Serikali ya kikoloni katika miaka yake yote 200 madarakani ilikuwa na **skuli 1 (moja) tu ya maandalizi iliyokuwa na watoto 60**, wakati Serikali ya Mapinduzi Zanzibar katika kipindi cha miaka 57 tu ya Muungano ina **skuli za maandalizi 774 zenye watoto 91,074** (ongezeko la skuli 773 kutoka skuli 1 na watoto 91,014 kutoka watoto 60);

Serikali ya kikoloni ilikuwa na **skuli 62 za msingi zilizokuwa na wanafunzi 24,334**, wakati Serikali ya Mapinduzi Zanzibar ina **skuli 545 za msingi zenye wanafunzi 331,425** (ongezeko la skuli 483 kutoka skuli 62 na wanafunzi 329,091 kutoka wanafunzi 24,334); na

Serikali ya kikoloni ilikuwa na **skuli 5 (tano) za sekondari zilizokuwa na wanafunzi 1,038**, wakati Serikali ya Mapinduzi Zanzibar chini ya Muungano ina **skuli za sekondari 302 zenye wanafunzi 129,829** (ongezeko la skuli 297 kutoka skuli 5 za sekondari na wanafunzi 128,791 kutoka wanafunzi 1,038).<sup>11</sup>

Picha tunayoipata hapa ni ya ongezeko kubwa sana la shule ngazi mbalimbali za elimu na ongezeko kubwa sana la wanafunzi, wengi wakiwa Waafrika walionyimwa nafasi ya kusoma kutokana na mfumo wa ubaguzi wa utawala wa kikoloni wa Waarabu wakisaidiwa na Waingereza. Kasi kubwa ya mabadiliko katika kipindi kifupi cha miaka 57 tu baada ya Mapinduzi na chini ya Muungano ni ushahidi, pasi na shaka, kuwa utawala wa Kiarabu wa karibu miaka 200 uliirudisha nyuma sana Zanzibar kielimu na kwa ujumla kimaendeleo.

<sup>11</sup> Taarifa ya Utekelezaji Kipindi cha Januari - Desemba 2021, Ofisi ya Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Waliumizwa zaidi na mfumo huo wa kibaguzi na wa kikoloni walikuwa Waafrika ambao kipindi Mapinduzi yanafanyika, walikuwa asilimia 85 ya watu wote wa Zanzibar, lakini walikuwa na nafasi ndogo kuliko watu wote (chini ya asilimia 12) kufikiwa na huduma mbalimbali za kijamii ikiwamo elimu. Ikabidi hatua kadhaa zichukuliwe mara tu baada ya Mapinduzi kurekebisha hali hiyo kwa kutoa upendeleo maalum kwa watoto wa Kiafrika ambapo kufikia mwaka 1966 idadi ya vijana wa Kiafrika walioingia sekondari ikapanda hadi 1,111 sawa na asilimia 66.1 ya watoto wote.<sup>12</sup>

Mabadiliko haya chanya katika elimu yaliondoa ubaguzi wa rangi, udini na utafa katika utoaji wa elimu Zanzibar baada ya Mapinduzi Matukufu ya mwaka 1964, ingawa baadhi ya watafiti hasa kutoka nchi za Magharibi wanadai kuwa mabadiliko hayo yalileta ubaguzi mpya wa rangi visiwani, wa Waafrika kuwanyanyasa na kuwabagua Waarabu, Wahindi na wageni wengine katika utoaji wa elimu.<sup>13</sup>

Hakuna anayekataa kwamba mara baada ya Mapinduzi Matukufu ya Zanzibar, Serikali ya Mapinduzi Zanzibar na Serikali ya Muungano zilielekeza nguvu nyingi sana kufutilia mbali (kijamii, kiuchumi na kisiasa) alama na mabaki yote ya utumwa, utwana na ujakazi Zanzibar. Msukumo huo wa kusahihisha makosa ya nyuma unaotambulika kama *affirmative action* au *positive discrimination* (kwa Kiswahili ubaguzi chanya), haukuasisiwa na wanamapinduzi wa Zanzibar bali ni utaratibu wa miaka mingi unaokubalika duniani na kuendana na ulinzi wa haki za binadamu.

## ELIMU YA JUU

Tarehe 25 Oktoba, 1961, miezi miwili tu kabla ya Uhuru wa ndani wa Tanzania Bara, Chuo Kishiriki cha Chuo Kikuu cha London, Uingereza kilianzishwa Dar es Salaam na kuitwa Chuo Kikuu cha Dar es Salaam kikiwa na wanafunzi wa mwanzo 14 kwenye jengo la TANU, Jengo la SUKITA, mtaa wa Lumumba. Mwaka 1963 chuo hiki kilijiunga na vyuo vikuu vishiriki vyanza vya Makerere (Uganda) na Nairobi (Kenya) kuunda Chuo Kikuu cha Afrika Mashariki.

Ni Kutokana na umuhimu kwa nchi zetu kuwa na wataalamu wazalendo katika fani mbalimbali, pande zote mbili za Muungano ziliiona haja ya suala la Elimu ya Juu kuliingiza kwenye Orodha ya Mambo ya Muungano mwaka 1967 kama ilivyoielezwa katika Sura

<sup>12</sup> Hettiger, M., *The Racialization of Politics in Revolutionary Zanzibar*, pdf, p.35.

<sup>13</sup> *kama hapa juu*, uk. 36.

ya Tatu ya kitabu hiki. Mwaka 1970 Chuo Kikuu cha Dar es Salaam kilipandishwa hadhi na kuwa Chuo Kikuu kamili kufuatia kugawanywa kwa Chuo Kikuu cha Afrika Mashariki katika Vyuo Vikuu vitatu vya Kenya, Uganda na Tanzania.

Vyuo vikuu na vya elimu ya juu viliongezeka kwa kasi Tanzania Bara, baadhi ya vyuo hivyo ni: Chuo Kikuu Kishiriki cha Kilimo cha Sokoine kilichoanzishwa mwaka 1984 ambapo kabla ya hapo kilikuwa Chuo Kikuu Kishiriki cha Chuo Kikuu cha Dar es Salaam tangu mwaka 1970; Chuo cha Maendeleo ya Uongozi (IDM) kilichoanzishwa mwaka 1972 ambacho mwaka 2001 kilipandishwa hadhi kuwa Chuo Kikuu Mzumbe; na Chuo Kikuu cha Dodoma kilichoanzishwa mwaka 2007.

Hadi kufikia mwaka 2021, Tanzania Bara ilikuwa na jumla ya Vyuo Vikuu na Vyuo Vikuu Vishiriki 50 kati ya hivyo 15 vya umma na 35 binafsi, vyenye jumla ya wanafunzi 465,571. Kati ya idadi hiyo, wanafunzi wa vyuo vikuu ni 206,305 (wanaume 117,638 na wanawake 88,667). Idadi ya wanafunzi katika vyuo vya elimu ya juu ni 259,266 (wanaume 146,986 na wanawake 112,280).

Kwa upande wa Zanzibar, kabla ya Mapinduzi na Muungano hakukuwa na chuo hata kimoja. Lakini baada ya Mapinduzi Matukufu, Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar iliimarisha utoaji wa elimu ya juu ambapo hadi mwaka 2021, Zanzibar ilikuwa na vyuo vikuu na vyuo vya elimu ya juu vinavyotoa elimu ya juu. Kwa mfano, vyuo vifuatavyo vya elimu ya juu vinatoa huduma zake Zanzibar: Chuo Kikuu cha Taifa cha Zanzibar (SUZA) – (1999), Chuo Kikuu cha Abdulrahman Al-Sumait (1998), Chuo Kikuu cha Zanzibar (ZU) – (1998), Taasisi ya Teknolojia ya Karume (Karume Institute of Science and Technology – KIST - 2009) na Chuo cha Utawala wa Umma (2007). Haya ni mabadiliko makubwa katika sekta ya elimu Zanzibar na katika kipindi kifupi cha Muungano ukilinganisha na kipindi cha ukoloni.

## **Maboresho ya Elimu ya Juu**

Mwaka 2005 Serikali ilianzisha Tume ya Vyuo Vikuu ili kusimamia ubora wa elimu ya juu nchini. Tume ina wajibu wa kuhakikisha kuwa kila chuo kinazingatia viwango stahili vya mazingira ya kufundishia, majengo, mitaala, walimu na taratibu za mitihani. Aidha, Tume inaratibu udahili wa wanafunzi katika Vyuo Vikuu na Taasisi za Elimu ya Juu nchini na nje ya nchi na kutoa ithibati kwa shahada, stahada na vyeti kutoka taasisi mbalimbali za elimu ya juu ulimwenguni.

Tangu kuanzishwa kwa Tume hii, udahili wa wanafunzi wanaojiunga na Vyuo vya elimu ya juu kutoka pande zote za Muungano hufanyika



kwa kuzingatia vigezo muhimu vinavyowawezesha kusoma vyuo wanavyopata nafasi katika Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Kwa kipindi kirefu, baada ya uhuru wa Tanganyika na Mapinduzi ya Zanzibar, elimu kwa ngazi zote ilikuwa inagharimiwa na Serikali. Kufuatia mageuzi ya kiuchumi yaliyofanyika nchini miaka ya 1990 ambayo yalibadilisha mfumo wa uchumi wa nchi kutoka uchumi hodhi kuwa uchumi wa soko, Serikali ilianzisha utaratibu wa uchangiaji wa elimu ya juu kwa awamu 3 ili kupunguza gharama za uendeshaji za Serikali.

Awamu ya kwanza ilianza kutekelezwa kuanzia Julai 1992 ambapo wanafunzi walianza kugharimia nauli, ada ya maombi, ada ya usajili, fedha ya tahadhari, ada ya Serikali ya Wanafunzi, matibabu, gharama za vitambulisho na ada ya mitihani.

Awamu ya pili ilitekelezwa kuanzia Julai 1994 ambapo, pamoja na gharama zilizohamishiwa kwa wanafunzi na wazazi wao katika awamu ya kwanza, wanafunzi walianza pia kugharimia mahitaji ya chakula na malazi. Kwa kuwa gharama hizo zilionekana kuwa kubwa, Serikali ilianzisha utaratibu wa utoaji mikopo kwa wanafunzi kwa ajili ya gharama za chakula na malazi.

Kupitia utaratibu wa kuchangia gharama za elimu ya juu, wanafunzi wengi zaidi walijiunga na vyuo, jambo ambalo liliongeza mzigo wa kugharimia elimu. Katika kukabilina na changamoto hiyo, Awamu ya tatu ya uchangiaji wa gharama za elimu ya juu ilianza ambapo wanafunzi wanachangia gharama za ada ya mafunzo, utafiti, mahitaji maalum ya vitivo na mafunzo kwa vitendo.

Katika awamu hii, Serikali ilianzisha Bodi ya Mikopo ya Elimu ya Juu kwa mujibu wa Sheria Na. 9 ya mwaka 2004 ambayo ilirekebishwa kwa Sheria Na. 9 ya mwaka 2007. Malengo ya kuanzishwa kwa Bodi hiyo ni kutoa mikopo kwa wanafunzi na wahitaji waliodahiliwa katika masomo ya shahada au stashahada ya juu katika taasisi za elimu ya juu zinazotambuliwa na Serikali nchini na nje ya nchi. Vilevile, imepewa jukumu la kukusanya mikopo inayotolewa kwa wahitimu walionufaika na mikopo husika kuanzia mwaka 1994 ili itumike kuwanufaisha waombaji wengine wanaohitaji.

Katika kutekeleza majukumu yake kwa ukamilifu, Bodi hiyo inafanya kazi pande zote mbili za Muungano na imefungua Ofisi ya Kanda Zanzibar ambayo inatoa huduma kwa wanafunzi wanaosoma katika vyuo vya elimu ya juu Zanzibar.



*Jengo la Kompyuta la Chuo Kikuu cha Taifa Zanzibar (SUZA)*



*Jengo la Utawala la Chuo Kikuu cha Dodoma (UDOM)*

## **BARAZA LA MITIHANI LA TAIFA**

Usumamizi wa mitihani ya elimu ya sekondari unafanywa na Serikali kupitia Baraza la Mitihani la Taifa ambalo ni chombo cha Muungano. Baraza la Mitihani la Taifa lilianzishwa kwa Sheria ya Baraza la Mitihani la Taifa, Sura Namba 107, kufuatia kujitoa kwa Tanzania Zanzibar katika Bodi ya Mitihani ya Afrika Mashariki mwaka 1970 na Tanzania Bara mwaka 1971.

Kufuatia uamuzi wa kujitoa katika Bodi hiyo, Serikali hizo mbili ziliendelea kushirikiana katika masuala ya mitihani hadi mwaka 1977 ilipoamuliwa kuwa suala hilo liwe miongoni mwa Mambo ya Muungano.

Baraza la Mitihani la Taifa, limefanikiwa kuendesha mitihani ya kumaliza elimu ya msingi, kidato cha nne na kidato cha sita, walimu ngazi ya cheti, stahahada na mitihani ya maarifa kwa ufanisi na limeweza kutunuku vyeti kwa watahiniwa wote waliofaulu mitihani hiyo.

Aidha, Baraza hilo limefanikiwa kuweka mfumo wa kusimamia mitihani na utoaji vyeti kwa kuimarisha miundombinu husika ikiwamo Kituo cha Kusahihisha Mitihani Mbezi - Dar es Salaam, na mfumo wa kompyuta wa usahihishaji mitihani unaotumia karatasi maalum.

## **UTAFITI**

Mwaka 1977, masuala ya utafiti yaliingizwa katika orodha ya Mambo ya Muungano. Hii ni kutokana na azma ya Serikali ya kutaka kuendeleza ubunifu, sayansi na teknolojia na kuratibu shughuli za utafiti zinazofanywa na taasisi mbalimbali Tanzania Bara na Tanzania Zanzibar. Katika kutekeleza azma hiyo, mwaka 1986 Serikali ilianzisha

Tume ya Taifa ya Sayansi na Teknolojia, kwa Sheria ya Tume ya Taifa ya Sayansi na Teknolojia, Sura Namba 226.

Tume hiyo ina ofisi zake Dar es Salaam na Zanzibar ambazo zinasimamia, kuendeleza na kuratibu tafiti za kisayansi kwa kukusanya, kutunza, na kusambaza taarifa za sayansi na teknolojia na kuwezesha maendeleo na uhaulishaji wa teknolojia.

Tume ya Sayansi na Teknolojia, inashirikiana na takriban taasisi 68 zinazofanya tafiti katika Sekta za Kilimo, Mifugo na Uvuvi, Maliasili, Afya, Uchumi, Elimu ya Juu, Sayansi ya Jamii, Nishati na Viwanda. Tume pia imewaendeleza watafiti zaidi ya 500 kitaaluma katika ngazi za shahada ya umahiri na uzamivu.

Serikali pia imeanzisha taasisi nyingine za sayansi na teknolojia kwa lengo la kuendeleza wananchi katika fani za uhandisi na ufundi na hivyo kuchangia katika maendeleo ya Tanzania. Miongoni mwa taasisi hizo ni Chuo Kikuu cha Sayansi na Teknolojia Mbeya na Chuo Kikuu cha Sayansi na Teknolojia Nelson Mandela, Arusha.

Kupitia tafiti katika maeneo mbalimbali ya kipaumbele kwenye Sekta ya Kilimo, Serikali imegundua mambo kadhaa ikiwamo chanjo inayostahimili joto kwa ajili ya udhibiti wa magonjwa makubwa ya kupumua kwa kuku. Pia, tafiti zimeleta mafanikio katika kudhibiti inzi wanaoharibu matunda kwa kutumia njia ya kibaiolojia na njia ya kemikali na hivyo kupunguza uharibifu wa matunda kwa asilimia 90 na kuongeza mapato ya wakulima. Maeneo mengine ni pamoja na utafiti katika miradi inayolenga kuendeleza kilimo cha viazi vitamu, mihogo na mwani. Miradi hiyo inalenga kupata mbegu bora na kuimarisha afya ya walaji na kuinua kipato kwa mkulima.

Eneo lingine la utafiti linalotekelezwa kimuungano, ni usimamizi na matumizi salama ya nguvu za atomiki na usalama wa mionzi nchini. Kutokana na maendeleo makubwa ya matumizi ya teknolojia duniani, mwaka 2003 Serikali ilianzisha Tume ya Nguvu za Atomiki Tanzania kama chombo cha Muungano kwa Sheria ya Tume ya Nguvu za Atomiki Sura Namba 188. Lengo ni kusimamia, kudhibiti, kutafiti na kuendeleza matumizi salama ya vyanzo vya mionzi kwa manufaa ya jamii ya Tanzania.

Serikali, kupitia Tume hiyo, imesimamia vyema na kuendeleza matumizi salama ya nguvu za atomiki katika sekta za afya, kilimo, viwanda, madini na nishati (gesi asilia). Katika sekta ya afya, Tume inadhibiti upimaji kwa kutumia mionzi na utoaji wa vibali kwa vyakula vyote vinavyoingia nchini baada ya ukaguzi wa mionzi katika vyakula hivyo.

## UTABIRI WA HALI YA HEWA

Kabla ya Muungano huduma za utabiri wa hali ya hewa zilitolewa chini ya vyombo vya huduma ya pamoja vya serikali ya kikoloni ya Mwingereza ambapo mwaka 1963 jukumu hilo liliamishwa taasisi ya *East African Common Services Organisation (EACSO)*. Mwaka 1964, taasisi hiyo ilibadilishwa na kuwa *East African Meteorological Department (EAMD)* na ilikuwa na jukumu la kuhudumia nchi za Afrika Mashariki ikijumuisha Kenya, Uganda, Tanganyika na Zanzibar katika masuala ya hali ya hewa.

Baada ya kuvunjika kwa Jumuiya ya Afrika Mashariki mwaka 1977, huduma za utabiri wa hali ya hewa ziliongezwa katika Orodha ya Mambo ya Muungano. Huduma hizo ziliwekwa chini ya Idara Kuu ya Hali ya Hewa iliyoanzishwa kwa Sheria ya Hali ya Hewa, Sura Namba 157.

Mwaka 1999 Mamlaka ya Hali ya Hewa Tanzania ilianzishwa. Kwa sasa masuala ya hali ya hewa yanasimamiwa na Mamlaka ya Hali ya Hewa Tanzania (*Tanzania Meteorological Authority - TMA*) iliyoanzishwa kwa mujibu wa Sheria ya Mamlaka ya Hali ya Hewa Tanzania Na. 2 ya mwaka 2019. Taasisi hii imeanzishwa na kupewa wajibu wa kutoa huduma za hali ya hewa, kuratibu na kudhibiti shughuli za hali ya hewa katika Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Huduma za hali ya hewa ni muhimu kwa ustawi wa sekta mbalimbali za kiuchumi na kijamii, zikiwamo uratibu wa maafa, uvuvi, usafiri wa majini, usambazaji wa taarifa za hali ya hewa kupitia vyombo vya habari, usalama na usafiri wa anga. Kwa upande wa Zanzibar Mamlaka inatekeleza majukumu yake kupitia Ofisi ya TMA iliyopo Zanzibar. Vituo vya mwanzo vya hali ya hewa kuanzishwa nchini vilikuwa *Kazeh Hill* huko Tabora mwaka 1929 na Chukwani, Zanzibar mwaka 1930.

Ufanisi wa huduma za utabiri wa hali ya hewa na ushauri stahiki unaotolewa kwa wananchi umesaidia kutoa tahadhari kwa wananchi juu ya mvua kubwa, upepo mkali na ukubwa wa mawimbi baharini na kwenye maziwa kwa wanaotumia vyombo vya usafiri na shughuli nyingine za kila siku Tanzania Bara na Tanzania Zanzibar.

## TAKWIMU

Kabla ya Uhuru wa Tanganyika na Mapinduzi ya Zanzibar, huduma za ukusanyaji, uchambuzi, usambazaji na uhifadhi wa takwimu zilikuwa zikitolewa na kila nchi kulingana na sheria na taratibu zilizowekwa na nchi husika. Mara baada ya Uhuru wa Tanganyika mwaka 1961, Idara

ya Takwimu ilianzishwa chini ya Sheria ya Takwimu, Sura Namba 443 ikiwa na jukumu la kufanya sensa ya watu; kukusanya, kuhifadhi, kuchambua na kuchapisha takwimu zinazohusiana na uchumi, jamii na utamaduni; na kuratibu mfumo wa takwimu za kiuchumi na kijamii.

Mwaka 1967, baada ya kuundwa kwa Jumuiya ya Afrika Mashariki masuala ya takwimu kwa Tanganyika na Zanzibar, yalikuwa chini ya Jumuiya ya Afrika Mashariki, na mwaka huohuo Sensa ya Kwanza ya Watu na Makazi ilifanyika. Matokeo ya Sensa hiyo yalionesha kwamba Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ilikuwa na watu 12,313,469 ambapo kati ya hao Tanzania Bara ilikuwa na watu 11,958,654 na Tanzania Zanzibar ilikuwa na watu 354,815.

Baada ya kuvunjika kwa Jumuiya ya Afrika Mashariki mwaka 1977, suala la takwimu ambalo ni miongoni mwa mambo yaliyokuwa yakishughulikiwa katika ngazi ya Jumuiya liliingizwa katika Orodha ya Mambo ya Muungano.

Katika kuboresha ukusanyaji na uchambuzi wa takwimu nchini, Serikali ilianzisha Ofisi ya Taifa ya Takwimu kuwa Wakala wa Serikali, na mwaka 2002 ilitunga Sheria mpya ya takwimu na kuipa majukumu ya kuendesha Sensa ya Watu na Makazi katika Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Aidha, Wakala ilipewa jukumu la kuratibu shughuli zote za kitakwimu nchini; kuwa kitovu cha utunzaji wa takwimu zote rasmi nchini; na kuwa kitovu cha rejea kwa mashirika ya kimataifa na kampuni za kigeni zinazohitaji taarifa za kitakwimu kuhusu Tanzania. Ofisi ya Taifa ya Takwimu inashirikiana na Ofisi ya Mtakwimu Mkuu wa Serikali Zanzibar katika Sensa ya Watu na Makazi, Sensa ya Kilimo, na Marekebisho ya Takwimu za Pato la Taifa, Utafiti wa Nguvukazi, Utafiti wa Viashiria vya UKIMWI na Malaria na Utafiti wa masuala ya Idadi ya Watu na Afya.

Kuanzia mwaka 1964, Serikali imefanya Sensa ya Watu na tafiti mbalimbali na kutoa viashiria vya kiuchumi na kijamii vilivyoweza kuandaliwa mipango mbalimbali ya maendeleo ya kitaifa. Katika kipindi cha miaka 57 ya Muungano, Sensa ya Watu na Makazi ilifanyika mwaka 1967, 1978, 1988, 2002 na 2012. Kwa mujibu wa takwimu za Sensa ya Watu na Makazi ya mwaka 2012, Tanzania ilikuwa na watu 44,928,923, ambapo kati yao watu 40,640,425 (sawa na asilimia 90.6) ni wenye umri wa mwaka sifuri hadi hamsini (50) waliozaliwa baada ya Muungano.

Kwa upande wa Tanzania Bara, takwimu zinaonesha kuwa kulikuwa na idadi ya watu 43,625,354, kati ya hao watu 39,456,065 (sawa na asilimia 90.5) wamezaliwa baada ya Muungano na kwa Tanzania

Zanzibar kati ya watu 1,303,569, watu 1,184,360 (sawa na asilimia 90.9) wamezaliwa baada ya Muungano.

## **MAHAKAMA YA RUFANI**

Mahakama ya Rufani ya Tanzania ilianzishwa mwaka 1979 kwa mujibu wa Ibara 117 (1) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977 baada ya kuvunjika kwa Mahakama ya Rufani ya Afrika Mashariki. Mahakama hiyo ina mamlaka ya juu zaidi ya kuamua mashauri yanayokatiwa rufaa kutoka Mahakama Kuu za Tanzania Bara na Tanzania Zanzibar isipokuwa kwa mashauri ya kikatiba yanayohusu tafsiri ya Katiba ya Zanzibar na Mahakama ya Kadhi. Hadi kufikia mwaka 2021 Mahakama ya Rufani ilikuwa na Majaji 25. Aidha, Mahakama ya Rufani ina vituo saba kwa Tanzania nzima ambavyo ni: Dar es Salaam (Makao Makuu), Mwanza, Dodoma, Arusha, Zanzibar, Mbeya na Tanga.

## **UANDIKISHAJI WA VYAMA VYA SIASA**

Kufuatia uamuzi wa Serikali wa kuruhusu demokrasia ya vyama vingi vya siasa nchini mwaka 1992 na kutungwa kwa Sheria ya Vyama vya Siasa, Sura Namba 258, suala la uandikishaji wa vyama vya siasa liliorodheshwa miongoni mwa Mambo ya Muungano.

Mara baada ya mfumo wa vyama vingi kuanzishwa, Ofisi ya Msajili wa Vyama vya Siasa ilianzishwa rasmi kwa mujibu wa Sheria ya Vyama vya Siasa ambayo ilianza kutumika tarehe 1 Julai, 1992. Mfumo wa vyama vingi vya siasa, umeimarisha demokrasia, uhuru wa kutoa maoni kwa mujibu wa katiba na uwazi katika uendeshaji wa shughuli za umma ikiwa ni pamoja na masuala ya Muungano.

## SURA YA TANO

# HOJA ZA MUUNGANO NA UTATUZI WAKE

### HOJA ZA MUUNGANO

Hoja za Muungano ni masuala yanayojitokeza katika Sekta/Taasisi za Muungano au zisizo za Muungano za Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania (SMT) au Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar (SMZ) ambayo yanaweza kuathiri utekelezaji wa mambo ya muungano au yasiyo ya muungano. Serikali za pande mbili za Muungano zimeweka utaratibu wa wazi na huru wa vikao vya pamoja kwa ajili ya kujadili hoja hizo na kuzitafutia ufumbuzi. Vikao hivyo hufanyika kupitia Kamati ya Pamoja ya SMT na SMT ya Kushughulikia Masuala ya Muungano. Kabla ya utaratibu wa vikao vya Kamati ya Pamoja, Serikali ilikuwa ikiunda Tume na Kamati mbalimbali kwa ajili ya kufanya uchunguzi wa hoja zilizokuwa zinaibuliwa kwa lengo la kushauri hatua stahiki zinazopaswa kuchukuliwa.

### KAMATI NA TUME ZILIZOUNDWA

Juhudi mbalimbali zimekuwa zikichukuliwa na Serikali zote mbili ambazo ni pamoja na kuundwa kwa Tume na Kamati kwa ajili ya kushughulikia hoja za Muungano. Miongoni mwa Tume na Kamati hizo ni pamoja na: Tume ya Dkt. Salmin Amour 1984; Tume ya Jaji Nyalali 1990; Tume ya Edwin Mtei 1991; Kamati ya Shellukindo 1992; Tume ya Jaji Kisanga 1999; na Kamati ya Pamoja ya SMT na SMZ ya Kushughulikia Masuala ya Muungano mwaka 2005. Uundwaji wa Tume na Kamati hizo unadhihirisha utashi na utayari uliopo wa kushughulikia hoja mbalimbali zilizopo na kuzipatia ufumbuzi kwa njia ya maafikiano na maridhiano.

## Tume ya Jaji Kisanga 1999

Baada ya muda mrefu wa kufuatilia mijadala ya wananchi kuhusu Katiba, Serikali iliamua kuwashirikisha wananchi wengi zaidi katika mijadala ya Katiba, na hivyo, kuunda Tume iliyoongozwa na Jaji Kisanga mwaka 1999. Majukumu ya Tume hiyo ilikuwa ni kupata maoni ya wananchi kuhusu Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977. Moja ya mapendekezo yalihusu muundo wa Serikali unaofaa.

Kazi ya kukusanya maoni ya wananchi ilihusisha mikoa yote 25 ya Tanzania Bara na Tanzania Zanzibar. Wananchi wapatao 600,000 walishiriki katika zoezi hili kwa njia tofauti kama ilivyopangwa na Tume.

Baada ya zoezi hilo, maoni ya wananchi kuhusu Muundo wa Serikali kwa pande zote mbili za Muungano yaliunga mkono muundo wa Serikali mbili kwa wastani wa asilimia 88.87. Maoni haya yalionesha dhahiri kuwa Muungano unaungwa mkono na kwamba, wananchi wengi walipendelea mfumo wa Serikali mbili.

## Kamati ya Shellukindo 1992

Kamati ya Shellukindo ya mwaka 1992 iliundwa kwa lengo la kuchunguza kwa kina mambo yanayoleta vikwazo katika Shughuli za Muungano. Kamati hiyo ilikuwa na wajumbe 11 kutoka pande zote za Muungano chini ya Uenyekiti wa Mheshimiwa William Shellukindo.

Taarifa hiyo iliyojulikana kama ‘Taarifa ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Kuhusu Kuondoa Vikwazo vya Muungano’ iliwasilishwa katika Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania tarehe 19 Agosti, 1994. Bunge lilijadili na kupitisha taarifa hiyo na kuelekeza kwamba, SMZ na SMT zitekeleze maoni na mapendekezo yaliyomo kwenye taarifa hiyo.

Mwaka 1995 Serikali zote mbili zilianza kuyafanyia kazi maoni na mapendekezo ya Kamati na hatua zilizochukuliwa ni pamoja na: kufanya marekebisho ya 11 na 12 ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977; kuweka bayana Masuala ya Muungano katika nyongeza ya kwanza ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977; kuanzisha Sekretarieti ya Masuala ya Muungano iliyowekwa chini ya Ofisi ya Makamu wa Rais mwaka 1998 na kupewa hadhi ya kuwa Idara kamili mwaka 2005.

Hatua nyingine zilizochukuliwa ni kutunga: Sheria ya Uraia Na. 6 ya mwaka 1995; Sheria ya Usalama wa Taifa Na. 15 ya mwaka 1996; Sheria ya Uhamiaji Na 7 ya 1995; Sheria ya Benki Kuu ya Tanzania, Na. 1 ya



1995, kuweka utaratibu wa mgao wa faida ya Benki Kuu kwa asilimia 95.5 kwa SMT na asilimia 4.5 kwa SMZ; Sheria ya Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) Na. 11 ya 1995; kuweka utaratibu wa mgawanyo wa misaada kutoka nje kwa asilimia 95.5 kwa SMT na asilimia 4.5 kwa SMZ; Sheria ya Tume ya pamoja ya fedha, Na. 15 ya 1996 na kuanzishwa kwa Tume ya Pamoja ya Fedha mwaka 2003. Aidha, hatua nyingine zilizochukuliwa ni kuondoa mamlaka ya Mahakama ya Rufaa kusikiliza mashauri yanayohusu Mahakama ya Kadhi.

## **KAMATI YA PAMOJA YA SMT NA SMZ YA KUSHUGHULIKIA MASUALA YA MUUNGANO**

Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kushirikiana na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kupitia Kamati ya Pamoja ya SMT na SMZ ya Kushughulikia Masuala ya Muungano iliyoundwa mwaka 2005 na kuanza vikao mwaka 2006, imekuwa ikifanya vikao vinavyojumuisha wajumbe kutoka pande zote mbili za Muungano. Vikao hivyo hufanyika katika ngazi za Wataalamu, Makatibu Wakuu, Mawaziri na Kamati ya Pamoja ya SMT na SMZ chini ya Uenyekiti wa Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa lengo la kuhakikisha hoja zote zinatafutiwa ufumbuzi wa kudumu.



*Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Dkt. Philip Isdor Mpango akizungumza na Viongozi mbalimbali walioshiriki wakati wa Utiaji saina wa hati za makubaliano ya kuondoa hoja 11 za Muungano zilizopatiwa ufumbuzi. Hafla iliyofanyika katika Ukumbi wa Taasisi ya Utalii SUZA, Maruhubi, Zanzibar Agosti 24, 2021.*

Tangu kuanzishwa kwa Kamati ya Pamoja ya Kushughulikia Masuala ya Muungano mwaka 2006, hoja 25 ziliibuliwa ambapo hadi kufikia mwaka 2021 hoja 18 zilijadiliwa, kupatiwa ufumbuzi na kuondolewa kwenye orodha ya hoja za Muungano:

### **Utekelezaji wa Sheria ya Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora**

Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977, imeweka masuala ya haki za binadamu na utawala bora kuwa ya kikatiba. Kwa kuwa Katiba na mikataba ya kimataifa husimamiwa na kutekelezwa na Serikali ya Jamhuri ya Muungano, hoja ya msingi iliyojitokeza ni kuwa Sheria ya Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora, Sura Namba 391 inayosimamiwa na Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora ilikuwa haitekelezwi Zanzibar. Hivyo, Sheria hiyo ilirekebishwa mwezi Oktoba, 2006 ili kuiwezesha Tume kufanya kazi pande zote mbili za Muungano.

### **Utekelezaji wa Sheria ya Usafirishaji Majini (Merchant Shipping Act) na Uwezo wa Zanzibar Kujiunga na Shirika la Bahari Duniani (International Maritime Organisation - IMO)**

Masuala yote yanayohusu uchukuzi na usalama majini katika mikataba yote ya kimataifa inayoihusu Jamhuri ya Muungano wa Tanzania yanatekelezwa kupitia Sheria ya Usafiri Majini (*The Merchant Shipping Act*), Sura Namba 165. Zanzibar iliomba kujiunga na Shirika la Kimataifa la Usafiri Baharini (*International Maritime Organization - IMO*) ili kufaidika na fursa zilizopo. Kwa mujibu wa Sheria ya *Merchant Shipping Act* na taratibu za *IMO*, uanachama hutolewa kwa mataifa na husimamiwa na sheria moja.

Kutokana na hali hiyo mwanachama wa *IMO* ni Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Hata hivyo, baada ya mashauriano kati ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Shirika la Kimataifa la Usafiri Baharini (*International Maritime Organization - IMO*), ilikubalika kuwa Zanzibar iwe na Mamlaka yake ya Usafiri Majini (*Zanzibar Maritime Authority*) chini ya Sheria ya Usafiri Baharini (*The Maritime Transport Act*) iliyoanza kutumika mwaka 2006. Kupitia Sheria hiyo, Zanzibar inatekeleza baadhi ya majukumu kulingana na mikataba ya kimataifa chini ya usimamizi wa Serikali ya Muungano wa Tanzania.

### **Ushiriki wa Zanzibar katika Jumuiya ya Afrika Mashariki**

Kulikuwa na hoja kuhusu nafasi ya SMZ kuwasilisha miradi ya maendeleo ya kiuchumi kwa ajili ya kujumuishwa katika Miradi ya

Kikanda inayotekelezwa katika Jumuiya ya Afrika Mashariki. Katika kuhakikisha kuwa Zanzibar inashiriki kikamilifu na kutumia fursa zilizopo katika Jumuiya ya Afrika Mashariki, Zanzibar iliwasilisha miradi ya maendeleo ya kiuchumi kwa ajili ya kujumuishwa katika Miradi ya Kikanda inayotekelezwa katika Jumuiya ya Afrika Mashariki.

Miradi iliyowasilishwa kwa Sekretarieti ya Jumuiya kwa ajili ya kutafutiwa fedha kwa Wadau wa Maendeleo na Wawekezaji ni Ujenzi wa Uwanja wa Ndege wa Pemba; Mradi wa Ujenzi wa Bandari ya Maruhubi na Mradi wa Ujenzi wa Chelezo (*Dry Dock Construction*) na Kivuko (*Roll on Roll off - RORO*) kati ya bandari ya Zanzibar, Dar es Salaam, Pemba, Tanga na Mombasa.

### **Ushiriki wa SMZ katika Masuala mbalimbali ya Kimataifa na Kikanda**

Kulikuwa na hoja kwamba, Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki haiipi nafasi ya kutosha Zanzibar ya kuwa na ushirikiano wa kiuchumi unaohitajika na Taasisi za Kimataifa. SMT na SMZ ziliandaa Mwongozo wa Ushirikishwaji wa SMZ Kwenye Masuala ya Kimataifa na Kikanda ambao umezingatia maeneo ya ziara za viongozi wa kitaifa; mikutano ya kimataifa; nafasi za masomo ya elimu ya juu nje ya nchi na utafutaji wa fedha za misaada au mikopo ya kutekeleza miradi mbalimbali kutoka nje ya nchi. Mwongozo huu ulipitishwa na kuridhiwa na Kamati ya Pamoja ya SMT na SMZ ya Kushughulikia Masuala ya Muungano tarehe 9 Februari, 2019.

### **Utafutaji na Uchimbaji wa Mafuta na Gesi Asilia**

Kulikuwa na hoja ya namna ya kugawana mapato ya rasilimali ya mafuta na gesi asilia itakapopatikana. SMT na SMZ zilijadili na kuamua kutumia Kampuni ya ushauri elekezi *Aberdeen University Petroleum and Economic Consultants (AUPEC)* ya Uingereza kutoa ushauri wa kitaalamu kuhusu mgawanyo wa mapato ya rasilimali ya mafuta na gesi asilia kwa nchi zilizoungana. Kampuni ya AUPEC ilikamilisha kazi hiyo na mapendekezo kuwasilishwa SMT na SMZ.

Baada ya majadiliano baina ya Viongozi wa SMT na SMZ, pande zote mbili zimekubaliana kuliondoa suala la utafiti na uchimbaji wa mafuta na gesi asilia katika orodha ya Mambo ya Muungano. Hivyo, Sheria ya Mafuta Na. 21 ya Mwaka 2015 ilitungwa na kuipa Zanzibar Mamlaka ya kuanzisha chombo/vyombo vya kusimamia masuala ya mafuta na gesi asilia kwa kutumia Sheria ya Zanzibar na Zanzibar ilitunga Sheria yake ya Mafuta na Gesi Asilia ya mwaka 2016.

## Utaratibu wa Vikao vya Kamati ya Pamoja ya SMT na SMZ ya Kushughulikia Masuala ya Muungano

Kulikuwa na hoja kuhusu kutokuwapo kwa Utaratibu wa Vikao vya Kamati ya Pamoja ya SMT na SMZ ya Kushughulikia Masuala ya Muungano. Hoja hii ilipatiwa ufumbuzi kwa kuridhiwa kwa Utaratibu wa Vikao vya Kamati ya Pamoja ya SMT na SMZ ya Kushughulikia Masuala ya Muungano katika kikao cha Kamati ya Pamoja kilichofanyika tarehe 9 Februari, 2019.

## Uingizaji wa Maziwa kutoka Zanzibar katika Soko la Tanzania Bara

Kulikuwa na changamoto ya kuzuiwa kwa maziwa ya AZAM kuingia katika soko la Tanzania Bara kutokana na Sheria ya Magonjwa ya Wanyama Sura ya 156 na Kanuni zake. Suala hili limepatiwa ufumbuzi baada ya kanuni kufanyiwa marekebisho, ikiwa ni pamoja na kupunguziwa tozo kutoka shilingi 2000 hadi shilingi 250 kwa lita ya maziwa yanayotengenezwa kutokana na unga wa maziwa unaoagizwa nje ya nchi. Aidha, tarehe 25 Februari, 2019 Wizara ya Mifugo na Uvuvi (Mifugo) ya SMT iliingia Mkataba wa Makubaliano ya uingizaji wa maziwa ya AZAM katika soko la Tanzania Bara.

## Gharama za Kushusha Mizigo (Landing Fees) Bandari ya Dar es Salaam kwa Mizigo inayotoka Zanzibar

Kulikuwa na hoja kwamba, gharama za kushusha mizigo katika Bandari ya Dar es Salaam (*Landing Fees*) kwa mizigo inayotoka Zanzibar ni kubwa ikilinganishwa na mizigo inayotoka nje ya nchi yaani shilingi 4,000 CBM/tani moja kwa mizigo ya nje ya nchi inayoingia Tanzania Bara na shilingi 11,000 CBM/tani moja kwa mizigo ya Zanzibar inayoingia Tanzania Bara.

Kwa mujibu wa *Tariff Book of Port Dues and Charges*<sup>1</sup> ya Aprili, 2013 iliyopitishwa na Mamlaka ya Udhhibiti na Usafiri wa Nchi Kavu na Majini (*SUMATRA*) viwango vinavyotozwa kwa mizigo inayotoka Zanzibar ni vya chini ikilinganishwa na viwango vinavyotozwa kwa mizigo inayotoka nchi nyingine kuingia Tanzania Bara au mizigo inayotoka nchi nyingine kupitia Bandari ya Dar es Salaam kwenda nchi nyingine (*Transit Cargo*).

<sup>1</sup> Kitabu cha Tozo na Ushuru wa Bandari.

Viwango vinavyotozwa ni kama ifuatavyo: - *Shore handling*<sup>2</sup> ni dola za Marekani 7 kwa mizigo inayotoka nje ya nchi wakati kwa mizigo kutoka Zanzibar ni dola za Marekani 2; *Wharfage* ni asilimia 1.6 ya thamani ya mzigo kwa mizigo kutoka nje wakati kwa mizigo kutoka Zanzibar ni dola za Marekani 2 CBM/tani moja; na *Stevedoring* ni dola za Marekani 6 kama mzigo unachukuliwa eneo la kushushia na dola za Marekani 7 kama mzigo unachukuliwa eneo la yadi wakati kwa mizigo kutoka Zanzibar ni dola za Marekani 2 CBM<sup>3</sup>/tani moja.

### **Usimamizi wa Ukokotoaji na Ukusanyaji wa Kodi kwenye Huduma za Simu Unaofanywa na Mamlaka ya Mapato Zanzibar (Zanzibar Revenue Board - ZRB)**

Kulikuwa na hoja kwamba baada ya kuzimwa mfumo uliokuwa unatumika kukokotoa kodi kwenye huduma za simu (*Electronic Revenue Collection System - e-RCS*) ambao ulikuwa unatumika kukusanya na kugawana kodi baina ya pande mbili za Muungano, ZRB iliendelea kutumia mfumo huo kukusanya kodi jambo lililoleta malalamiko kutoka kwa Kampuni za Simu.

Mfumo wa ukokotoaji na ukusanyaji wa kodi kwenye huduma za simu ulipatiwa ufumbuzi baada ya Timu ya Wataalamu kutoka Wizara ya Fedha na Mipango SMT na SMZ kuufanyia maboresho na kuanza kufanya kazi rasmi mwezi Januari, 2020.

### **Mkataba wa Mkopo wa Fedha za Ujenzi wa Barabara ya Chake Chake hadi Wete – Pemba**

Hoja hii ilihusu kuchelewa kusainiwa kwa Mkataba wa Mkopo wa Ujenzi wa Barabara ya Chake Chake hadi Wete – Pemba kutokana na mkataba huo kuwa na kipengele ambacho kiliitaka SMT kuweka baadhi ya Mali zake kama dhamana ya mkopo. Baada ya mazungumzo baina ya Serikali na mkopeshaji, mapendekezo ya Serikali ya kuondoa kipengele hicho yalikutubaliwa na mkopeshaji, na hivyo, Serikali ilisaini mkataba huo tarehe 19 Aprili, 2020.

### **Mkataba wa Mkopo wa Fedha za Mradi wa Ukarabati wa Hospitali ya Mnazi Mmoja**

Hoja iliyokuwapo ni kuchelewa kusainiwa kwa Mkataba wa Mkopo wa Fedha za Mradi wa Ukarabati wa Hospitali ya Mnazi Mmoja kutokana

<sup>2</sup> Mchakato wa kupokea, kuhifadhi na kusafirisha mizigo inayotoka na/au kwenda nje ya nchi.

<sup>3</sup> Kipimo cha mizigo (Cargo) kwa mita za ujazo (Cubic Metre)

na mkataba huo kuwa na kipengele kilichoitaka Serikali kuweka baadhi ya Mali zake kama dhamana ya mkopo. Mazungumzo yalifanyika na kipengele kuondolewa kwenye mkataba, na hivyo, Serikali ilisaini mkataba huo tarehe 19 Aprili, 2020.

### **Uteuzi wa Makamu Mwenyekiti wa Tanzania Revenue Appeals Tribunal (TRAT) kutoka Zanzibar**

Hoja ilikuwa SMZ kuchelewa kuteua Makamu Mwenyekiti wa Baraza la Rufaa za Kodi. Hoja hiyo ilipatiwa ufumbuzi baada ya SMZ kuteua Makamu Mwenyekiti wa TRAT tarehe 24 Aprili, 2019.

### **Uteuzi wa Mjumbe wa Bodi ya Bima ya Amana (Deposit Insurance Board - DIB) kutoka Zanzibar**

Hoja ilikuwa SMZ kuchelewa kuwasilisha jina kwa ajili ya uteuzi wa mjumbe wa Bodi ya Bima ya Amana. Hoja ilipatiwa ufumbuzi baada ya SMZ kuwasilisha jina la mjumbe wa Bodi ya Bima ya Amana tarehe 22 Machi, 2019.

### **Uvuvi katika Ukanda wa Uchumi wa Bahari Kuu**

Sheria ya Mamlaka ya Uvuvi katika Ukanda wa Uchumi wa Bahari Kuu ilikuwa haitekelezwi Zanzibar kutokana na kutozihusisha taasisi za SMZ zinazoshughulikia masuala ya Uvuvi katika Bahari Kuu. Hivyo, Sheria hiyo ilifanyiwa marekebisho mwezi Februari, 2007 kupitia Sheria Na. 4 ya Mwaka 2007 na kuzitambua taasisi zinazohusika na matumizi ya Bahari Kuu kwa upande wa Zanzibar na kuzijumuisha katika Kamati ya Utendaji ya Mamlaka ya Uvuvi wa Bahari Kuu.

Marekebisho hayo yameiwezesha Mamlaka kuanza kazi zake rasmi mwaka 2010. Sambamba na marekebisho ya sheria, hatua nyingine muhimu zilizochukuliwa ni pamoja na kufunguliwa kwa akaunti ya amana kwa ajili ya kuweka mapato yatokanayo na shughuli za Uvuvi wa Bahari Kuu, kufikiwa kwa makubaliano ya kugawana mapato kuwa, asilimia 50 ni kwa ajili ya uendeshaji wa Mamlaka ya Uvuvi na asilimia 50 itagawanywa kwa asilimia 30 Tanzania Bara na asilimia 20 Zanzibar.

Pamoja na marekebisho yaliyofanywa kupitia Sheria Na. 4 ya Mwaka 2007, Sheria hiyo haikuorodheshwa na Baraza la Wawakilishi. Hivyo, Sheria ya Kusimamia na Kuendeleza Uvuvi wa Bahari Kuu Na. 5 ya Mwaka 2020 ilitungwa na Bunge la Kumi na Moja (11) la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na kusainiwa na Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Sheria hiyo iliorodheshwa na Baraza la Wawakilishi tarehe 23 Februari, 2021.

Kuorodheshwa kwa Sheria hiyo na Baraza la Wawakilishi kumeifanya Mamlaka ya Kusimamia Uvuvi wa Bahari Kuu kutambulika rasmi Zanzibar na kuongeza ufanisi. Mamlaka hiyo ina majukumu ya kutoa leseni za uvuvi katika Bahari Kuu, kudhibiti viwango vya uvuvi, kusimamia rasilimali ya uvuvi na hifadhi ya mazingira ya bahari na uendelezaji wa rasilimali za uvuvi katika Bahari Kuu.

### **Ajira kwa Watumishi wa Zanzibar katika Taasisi za Muungano**

Kulikuwa na hoja ya kupungua kwa kiwango cha ushindani katika soko la ajira kwa Wazanzibari kunatokana na tofauti ya mitaala ya elimu ya msingi na sekondari kati ya Tanzania Bara na Tanzania Zanzibar. Kamati ya Kukuza Mitaala iliyoundwa ikiwa na wajumbe kutoka pande mbili za Muungano ililinganisha mihutasari ya ngazi zote za elimu (Msingi hadi Vyuo) ya Tanzania Bara na Tanzania Zanzibar na kubaini kuwa tatizo siyo tofauti ya mitaala bali ni nafasi ya Wazanzibari katika Taasisi za Muungano.

Hatua mbalimbali zilichukuliwa ili kutatua changamoto, zikiwamo kuhamasisha Wazanzibari kuomba ajira zinazotangazwa na Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania au taasisi za Muungano; matangazo ya ajira kutangazwa kupitia vyombo vya habari vya Tanzania Bara na Tanzania Zanzibar; taasisi za Muungano kufungua Ofisi Zanzibar ikiwa ni pamoja na Sekretarieti ya Ajira katika Utumishi wa Umma na usaili kufanyika Zanzibar pia.

Utaratibu wa muda wa mgao wa ajira uliokubalika kutumika kuhusu nafasi za Watumishi wa kawaida kwenye taasisi za Muungano (isipokuwa kwa Vyombo vya Ulinzi na Usalama) ni asilimia 79 kwa Tanzania Bara na asilimia 21 kwa Tanzania Zanzibar. Aidha, SMT na SMZ zimekubaliana kuwa na mfumo shirikishi katika mchakato mzima wa ajira katika taasisi za Muungano.

### **Mgawanyo wa Mapato yatokanayo na Misamaha ya Mikopo ya Fedha kutoka IMF; Misaada ya Kibajeti (General Budget Support – GBS); na Uwezo wa Zanzibar kukopa Ndani na Nje ya Nchi**

Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania imekuwa ikipata misaada mbalimbali kutoka kwa Washirika wa Maendeleo kwa ajili ya kutekeleza programu za maendeleo. Hata hivyo, mgawanyo wa mapato hayo kwa pande zote mbili za Muungano ulihitaji kufanyiwa maboresho. Majadiliano yalifanyika na Serikali zote ziliridhia kuwa

Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar iendelee kupata mgao wa asilimia 4.5 ya misaada na mikopo ya kibajeti.

Pamoja na makubaliano hayo, hoja ya uwezo wa Zanzibar kukopa ndani na nje ya nchi ilipatiwa ufumbuzi ambapo sasa ina uwezo wa kukopa ndani ya nchi bila ya kikwazo. Kwa mikopo ya nje, SMZ inakopa kupitia udhamini wa Serikali ya Muungano ambapo SMT huhamisha mkopo unaoombwa kutoka nje kwenda SMZ. Serikali zote mbili zinashirikiana katika maandalizi ya bajeti, ikiwamo mapendekezo ya upatikanaji wa misaada na mikopo ya kibajeti kutoka nje.

Aidha, kulikuwa na makubaliano ya awali na IMF kuhusu matumizi ya fedha za MDRI (*Multilateral Debt Relief Initiative*) zitokanazo na misamaha ya mikopo ya IMF kwamba, Zanzibar itatumia fedha hizo kununua vifaa vya kutengenezea barabara, kilimo n.k. Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar ilihitaji kununua magari kwa ajili ya matumizi yake kupitia fedha za MDRI suala ambalo halikuwapo katika makubaliano ya awali baina ya Tanzania na IMF.

Wizara ya Fedha na Mipango SMT ilifanya majadiliano na IMF kuhusu Zanzibar kujumuisha ununuzi wa magari kati ya vitu vinavyoweza kupatikana kutoka katika msamaha huo. Hatimaye, SMZ ilipata fedha za misamaha hiyo na kununua magari kwa ajili ya matumizi ya Serikali.

Vilevile, utaratibu wa kupokea fedha za misaada ya kibajeti ya kissekta kutoka kwa Washirika wa Maendeleo kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo umeelekezwa kwenye Kifungu cha 15 (1) cha Sheria ya Mikopo, Dhamana na Misaada Sura 134, ambapo SMZ ina jukumu la kupokea misaada hiyo bila kutafuta idhini ya Waziri wa Fedha na Mipango wa SMT.

## **Mkataba wa Mkopo wa Fedha za Ujenzi wa Bandari ya Mpigaduri**

Kulikuwa na hoja ya kuchelewa kukamilishwa kwa Mkataba wa Mkopo kwa ajili ya Ujenzi wa Bandari ya Mpigaduri. Serikali iliunda timu ya wataalamu ili kupitia upya Andiko la Mradi wa Ujenzi wa Bandari ya Mpigaduri. Pamoja na mambo mengine, timu hiyo ilibaini kuwa andiko la mradi liliandaliwa na kampuni ambayo ni mkandarasi tarajiwa wa mradi kwa mujibu wa hati ya makubaliano (MoU) ya mwaka 2012 baina ya kampuni hiyo na SMZ. Suala hili lingeweza kusababisha mgongano wa kimaslahi. Hivyo, timu ilishauri andiko la mradi liandaliwe na mtaalamu elekezi huru ili kuepusha mgongano wa kimaslahi. Baada ya ushauri huo, SMZ ilisitisha makubaliano na kampuni hiyo na kutafuta mtaalamu elekezi huru wa kuandaa andiko jipya.



## Mapato Yanayokusanywa na Idara ya Uhamiaji kwa Upande wa Zanzibar


Mapato yanayokusanywa na Idara ya Uhamiaji Zanzibar yanapaswa kuwekwa kwenye Mfuko Mkuu wa Serikali kwa mujibu wa Sheria ya Bajeti Na. 11 ya Mwaka 2015 na kutumika katika kugharimia shughuli za Muungano kulingana na bajeti zilizotengwa. Hivyo, kulikuwa na hoja kwamba, mapato yanayokusanywa na Idara ya Uhamiaji upande wa Zanzibar kubakizwa Zanzibar ni kinyume na Sheria ya Bajeti Na. 11 ya Mwaka 2015.

Wizara ya Fedha na Mipango ya SMT ilipendekeza kutekelezwa kwa utaratibu wa kuruhusu mapato yanayotokana na tozo za visa kutumika pale yalipokusanywa kama ilivyo kwenye mapato mengine ya Muungano. Mapendekezo haya yalipitishwa na Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania mwezi Juni, 2021.



# VIAMBATISHO

## 1. HATI YA MUUNGANO WA TANGANYIKA NA ZANZIBAR



ARTICLES OF UNION

between

THE REPUBLIC OF TANGANYIKA AND THE PEOPLES' REPUBLIC OF ZANZIBAR

ARTICLES OF UNION  
between  
THE REPUBLIC OF TANGANYIKA AND THE PEOPLES' REPUBLIC OF ZANZIBAR

WHEREAS the Governments of the Republic of Tanganyika and of the Peoples' Republic of Zanzibar, being mindful of the long association of the peoples of these lands and of their ties of kinship and amity, and being desirous of furthering that association and strengthening these ties and of furthering the unity of African peoples, have met and considered the union of the Republic of Tanganyika with the Peoples' Republic of Zanzibar:

AND WHEREAS the Governments of the Republic of Tanganyika and of the Peoples' Republic of Zanzibar are desirous that the two Republics shall be united in one Sovereign Republic in accordance with the Articles hereinafter contained:-

It is therefore AGREED between the Governments of the Republic of Tanganyika and of the Peoples' Republic of Zanzibar as follows:-

- (i) The Republic of Tanganyika and the Peoples' Republic of Zanzibar shall be united in one Sovereign Republic.
- (ii) During the period from the commencement of the union until the Constituent Assembly provided for in Article (vii) shall have met and adopted a Constitution for the united Republic [hereinafter referred to as the interim period] the united Republic shall be governed in accordance with the provisions of Articles (iii) to (vi).
- (iii) During the interim period the Constitution of the united Republic shall be the Constitution of Tanganyika so modified as to provide for -
  - (a) a separate legislature and executive in and for Zanzibar as from time to time constituted in accordance with the existing law of Zanzibar and having exclusive authority within Zanzibar for matters other than those reserved to the Parliament and Executive of the united Republic;
  - (b) the offices of two Vice-Presidents one of whom (being a person normally resident in Zanzibar) shall be the head of the aforesaid executive in and for Zanzibar and shall be the principal assistant of the President of the United Republic in the discharge of his executive functions in relation to Zanzibar;
  - (c) the representation of Zanzibar in the Parliament of the united Republic;
  - (d) such other matters as may be expedient or desirable to give effect to the united Republic and to these Articles.

- 2 -

(iv) There shall be reserved to the Parliament and Executive of the united Republic the following matters -

- (a) The Constitution and Government of the united Republic
- (b) External Affairs
- (c) Defence
- (d) Police
- (e) Emergency Powers
- (f) Citizenship
- (g) Immigration
- (h) External Trade and Borrowing
- (i) The Public Service of the united Republic
- (j) Income Tax, Corporation Tax, Customs and Excise
- (k) Harbours, Civil Aviation, Posts and Telegraphs.

And the said Parliament and Executive shall have exclusive authority in such matters throughout and for the purposes of the united Republic and in addition exclusive authority in respect of all other matters in and for Tanganyika.

(v) The existing laws of Tanganyika and of Zanzibar shall remain in force in their respective territories subject -

- (a) to any provision made hereafter by a competent legislature;
- (b) to such provision as may be made by order of the President of the united Republic for the extension to Zanzibar of any law relating to any of the matters set out in Article (iv), and the revocation of any corresponding law of Zanzibar;
- (c) to such amendments as may be expedient or desirable to give effect to the union and to these Articles.

(vi) (a) The first President of the united Republic shall be MWALIMU JULIUS K. NYERERE and he shall carry on the Government of the united Republic in accordance with the provisions of these Articles and with the assistance of the Vice-Presidents aforesaid and of such other ministers and officers as he may appoint from Tanganyika and Zanzibar and their respective public services.

(b) The first Vice-President from Zanzibar to be appointed in accordance with the modifications provided for in Article (iii) shall be SHEIKH ABKID KAMUNE.

(vii) The President of the united Republic in agreement with the Vice-President who is head of the Executive in Zanzibar shall -

- (a) Appoint a Commission to make proposals for a Constitution for the united Republic.

/ (b)

- 3 -

(b) Summon a Constituent Assembly composed of Representatives from Tanganyika and from Zanzibar in such numbers as they may determine to meet within one year of the commencement of the union for the purpose of considering the proposals of the Commission aforesaid and to adopt a Constitution for the united Republic.

(viii) These Articles shall be subject to the enactment of laws by the Parliament of Tanganyika and by the Revolutionary Council of the Peoples' Republic of Zanzibar in conjunction with the Cabinet of Ministers thereof, ratifying the same and providing for the Government of the united Republic and of Zanzibar in accordance therewith.

IN WITNESS WHEREOF Julius K. Nyerere, the President of the Republic of Tanganyika, and Abeid Karume, the President of the Peoples' Republic of Zanzibar, have signed these Articles, in duplicate, at Zanzibar, on this  
 22<sup>nd</sup>. day of APRIL, 1964.

Julius K. Nyerere

for the Republic of Tanganyika

Abeid Karume

for the Peoples' Republic of Zanzibar

## 2. MTAZAMO WA MAKUNDI MBALIMBALI KUHUSU MUUNGANO

### Wasomi na Wanazuoni

Kumekuwa na mitazamo tofauti kutoka kwa wasomi na wanazuoni mbalimbali waliopata kuandika au kuzungumza kuhusu Muungano wa Tanganyika na Zanzibar kuhusu uhalali, muundo, faida pamoja na changamoto zake.

**Amrit Wilson** ambaye ni msomi wa kimagharibi alidhani kuwa Muungano wa Tanganyika na Zanzibar ulikuwa zao la Vita Baridi. Ifahamike wazi kwamba katika kipindi cha Vita Baridi, pande mbili zilizokinzana yaani Magharibi (Ubepari) na Mashariki (Ujamaa/Ukomunisti) zilitumia mbinu ya misaada ya aina mbalimbali ili kuzishawishi nchi nyingine kuhamia upande mmoja au mwingine. Hivyo, Muungano wa Tanganyika na Zanzibar ulipotokea ni watu wachache tu wa nje waliouona muungano huo kuwa ni matokeo ya karne kadhaa za mwingiliano mkubwa na ushirikiano kati ya bara na visiwani. Watu wengi walibebwa na hisia za Vita Baridi ambazo, kama Sura kadhaa za kitabu hiki zinavyoonesha, hazikuwa msingi mahsusi.

Msomi wa kitanzania aishiye Marekani **Godfrey Mwakikagile** aliona kuwa Muungano wa Tanzania ulifikiwa haraka, bila maandalizi ya kutosha na hivyo mustakabali wake kutia mashaka<sup>1</sup>. Ni dhahiri Mwakikagile alifikia tamati hiyo kwa kushindwa kuzingatia kabisa muingiliano na ushirikiano wa miaka mingi kati ya pande hizo mbili za Muungano.

Naye **Issa Shivji**, mbali na kuuona Muungano wa Tanzania kuwa kipekee, anaamini kuwa ulikosa maandalizi ya kutosha<sup>2</sup>. Shivji, kama Mwakikagile, anawaona Mwalimu Nyerere na Sheikh Karume peke yao wakisaini Hati ya Makubaliano ya Muungano bila kuangalia nyuma yao kuona dhamira ya wananchi wa nchi hizo mbili.

Mwanazuoni mwingine wa kitanzania, **Aley Soud Nassor**<sup>3</sup> anaona Muungano wa Tanzania ukidumu kutokana na waasisi wa Taifa la Tanzania kujitoa mhanga kuhakikisha malengo ya umajumui wa Afrika

<sup>1</sup> Mwakikagile, G., *The Union of Tanganyika and Zanzibar: Product of the Cold War?* New Africa Press, Dar es Salaam, 2016.

<sup>2</sup> Shivji, I.G., *Pan-Africanism or Pragmatism? Lessons of Tanganyika-Zanzibar Union*, Mkuki na Nyota Publishers, Dar es Salaam, 2008.

<sup>3</sup> Kongamano la Maadhimisho ya Miaka 60 ya Uhuru wa Tanganyika na miaka 59 ya Jamhuri ya Tanganyika, lililofanyika katika ukumbi wa Chuo Kikuu cha Taifa Zanzibar (SUZA), Zanzibar tarehe 6 Desemba, 2021.



yanafikiwa. Kwa maoni yake, jitihada za aina hiyo zilishindikana maeneo mengine kwa kukosa uongozi madhubuti uliojitoa kufikia azma hiyo. Anatoa mfano wa Rais Abeid Amani Karume kukubali kuwa Makamu wa Rais ili Tanganyika na Zanzibar ziungane.

**Abdul Sheriff** anabainisha kuwa Muungano wa Tanganyika na Zanzibar ni zao la mahusiano ya kiuchumi ya muda mrefu. “Watu kutoka Tanganyika walikuwa wakija Visiwani [Zanzibar] kwa wingi [hasa katika karne ya 19] kwa ajili ya kutafuta ajira katika msimu wa kuchuma Karafuu”. Pia kabla ya mikarafuu kukua, kulikuwa na biashara ya utumwa, pembe za ndovu, vipusa, madini, bidhaa za nguo, vifaa mbalimbali shughuli zilziwahusisha watu wa bara na visiwani kwa wingi.

Maoni ya mwanazuoni wa Tanzania **Haroub Othman** ni kuwa kwa Tanganyika na Zanzibar kuungana, nchi hizi mbili “zimefanikiwa mahali ambapo nchi nne za Afrika Mashariki kwa pamoja zimeshindwa” na kwamba pamoja na matatizo mengi, Muungano “umeleta mshikamano na Amani katika ukanda (wa Afrika Mashariki).<sup>4</sup>

**Harrison Mwakyembe** anadai kuwa muundo wa Muungano wa Tanzania wa serikali mbili kusimamia majukumu matatu, pamoja na kwamba si mgeni duniani, hutumika sehemu chache sana duniani zenye mazingira yanayofanana na yale ya Tanzania ya washirika katika Muungano kupishana sana kwa ukubwa wa nchi, ukubwa wa rasilimali na idadi ya watu.<sup>5</sup> Katika mazingira kama hayo muundo wa Serikali tatu haubebeki bila marekebisho kadhaa ya msingi kama yaliyofanyika Tanzania.

## Viongozi wa Dini

**Sheikh Soraga Fadhil Suleiman Soraga** anasema “Ni jambo la kujivunia kwamba Muungano wetu umekuwa imara zaidi. Tunafahamu kuwa kulikuwa na nchi ambazo zilijaribu kuungana lakini zikaishia njiani, kwa mfano Senegal na Gambia ziliungana na kuishia njiani. Kwa hiyo, Muungano wetu ni wa kihistoria kwa Afrika na Ulimwengu mzima. Tunajivunia kutanuka kwa demokrasia na kuimarika kwa umoja wetu pamoja na mwingiliano wa kijamii.

Naye **Mwadhama Polycarp Pengo** alishatamka kuwa Muungano wa Tanzania haukuwa jambo la bahati nasibu bali neema na mpango

<sup>4</sup> Othman, H., *Tanzania: The Withering Away of the Union*, Chr. Michelsen Institute, Bergen, 1973, uk. 45&67.

<sup>5</sup> Mwakyembe, H.G., *Tanzania's Eighth Constitutional Amendment & Its Implications on Constitutionalism, Democracy and the Union Question*, LIT Verlag, Hamburg, uk.186

wa Mwenyezi Mungu. Ni neema na mpango huo huo wa Mwenyezi Mungu ulioifanya Zanzibar na Tanganyika kuungana baada ya uhuru kuwa kitu kimoja. Hivyo, kwa mujibu wa Kardinali Pengo, suala la Muungano linapaswa kuchukuliwa kwa uzito wa pekee kwa kutambua kuwa wamepewa jukumu na Mwenyezi Mungu kuulinda na kuuomba Muungano.<sup>6</sup>

## Wanasiasa

Rais Mstaafu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, **Dk. Jakaya Mrisho Kikwete** alitamka mwezi Aprili mwaka 2014 kuwa “Muungano wa Tanzania umejengeka katika misingi ya historia ya uhusiano wa damu, harakati za pamoja na ushirikiano wa vyama vya ukombozi vya Tanganyika na Zanzibar katika kupigania uhuru”.<sup>7</sup>

Rais Mstaafu wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, **Dkt. Ali Mohamed Shein** alitamka vile vile mwezi Aprili, 2014 kuwa “kuna kila sababu ya kuwakumbuka na kuwaenzi waasisi wa Taifa letu ... Marehemu Mwalimu Julius Kambarage Nyerere na Marehemu Sheikh Abeid Amani Karume. Ni ukweli usiofichika kwamba, Muungano wetu ambao msingi wake ni historia ya karne nyingi ya ushirikiano wa watu wa pande mbili na hatimaye kurasimishwa na waasisi wetu hao mwaka 1964, umezidi kuimarika na kuenziwa”.

Spika Mstaafu wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, **Pius Msekwa** anasema yafuatayo: (i) mafanikio makubwa kuliko yote ya Muungano wa Tanzania ni kuwa bado upo, haujavunjika; (ii) majaribio yote ya Muungano barani Afrika baada ya uhuru kama vile Muungano wa Misri na Syria, Gambia na Senegal na kadhalika, yote yalishidikana baada ya muda. Hivyo, Muungano wa Tanganyika na Zanzibar unabaki kuwa wa pekee Afrika uliofanikiwa; (iii) hakuna muungano duniani usiokuwa na changamoto, Muungano wa Tanzania unazo vile vile na jambo zuri ni kuwa utaratibu wa vikao vya pamoja umewekwa kuzishughulikia changamoto zozote zile zinapojitokeza<sup>8</sup>.

Pia, **Jaji Joseph Sinde Warioba** Waziri Mkuu Mstaafu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania alisema kuwa, kudumu kwa Muungano wa Tanganyika na Zanzibar kunatokana na dhamira ya dhati ya wananchi wa pande zote mbili kuunga mkono kuanzishwa kwa Muungano huo

<sup>6</sup> Kardinali Pengo, *Muungano si bahati nasibu*, [tec1956.blogspot.com](http://tec1956.blogspot.com), Mei 2, 2016.

<sup>7</sup> Taarifa ya Miaka 50 ya Muungano wa Tanganyika na Zanzibar 1964-2014, Uk viii.

<sup>8</sup> Mahojiano na Mzee Msekwa nyumbani kwake Oysterbay, Dar es Salaam, Machi, 2022.

mwaka 1964 kutokana na ukweli kuwa, uhusiano wa watu wa pande zote mbili ulikuwepo hata kabla ya Muungano kurasimishwa<sup>9</sup>.

## Vijana

**Idrissa Twalha** kutoka Tanzania Bara anasema faida ya Muungano ni namna pande hizi mbili (Bara na Visiwani) zilivyounganika kiuchumi akitolea mfano namna wananchi wanavyopata urahisi wa kufanya biashara. Hata hivyo, anasema anahisi kuna changamoto zinatakiwa kufanyiwa kazi ili kila upande unufaike na Muungano. “Kwa mfano, unaweza ukachukua bidhaa Zanzibar ili uje kuuza Bara kodi yake ni kubwa kuliko kawaida wakati hizi ni nchi ambazo zimeungana,” amesema Twalha.<sup>10</sup>

**Hassan Abdallah** mkazi wa Tanzania Bara anaipongeza Serikali kwa kuwaunganisha Watanzania na kwamba wanatoa taswira nzuri nje ya nchi kwamba wanatoka nchi zilizoungana baada ya uhuru. Kila Mtanzania anaposafiri anaonekana mstaarabu kwa mataifa ya nje. “Muungano wetu unatuunganisha tunakuwa wamoja, hatubaguani,” amesema.

**Ali Suleiman Shaame** wa Micheweni, Pemba amesema “kwanza, katika kusaidia kuongezeka kwa kipato binafsi, wananchi wa pande mbili wanaitumia fursa ya Muungano kujikwamua kimaiisha kwa kuanzisha shughuli mbalimbali za kiuchumi kupitia pande mbili za Muungano bila vikwazo vyovyote. Tuna wafanya biashara wengi tu na wamewekeza pande zote za Muungano na wanaendelea kupata mafanikio. “Pili, wananchi wanaendelea kupata nafasi na fursa za kuongoza taifa la Tanzania ... kupitia pande zote mbili, ambazo kwa kipindi cha nyuma fursa hizi hazikuwepo kama zilivyo hivi sasa. Tatu, Umoja na mshikamano wa Watanzania umeimarika sana kupitia maingiliano ya wananchi wa Tanzania bila kujali kabila wala dini wote wamekuwa wamoja na kufanya kazi zao kwa mashirikiano makubwa pamoja na kudumisha Amani na utulivu”.

**Rashid Mohamed Rashid** wa Kisauni, Zanzibar naye anasema: “Nilipomaliza masomo yangu ya Sekondari katika Skuli ya Sekondari ya Lumumba Mjini Unguja, Zanzibar mwaka 2013 nilitaka kujiunga na Chuo kizuri ambacho kinatoa fani ambayo niliipendelea. Hata hivyo kutokana na uchache wa Vyuo Vikuu Zanzibar na kukosa fani hiyo nilifanikiwa kupata Chuo katika Mkoa wa Tanga Wilayani Lushoto

<sup>9</sup> Mahojiano na Jaji Warioba nyumbani kwake Oysterbay, Dar es Salaam, Februari 2022.

<sup>10</sup> Chanzo: Idhaa ya Kiswahili ya Sauti ya Ujerumani (DW), Mahojiano tarehe 27/04/2021.

kilichojulikana kama ‘*Sebastian Kolowa Memorial University*’ ambapo niliweza kusomea fani ya Shahada ya Uhifadhi wa Mazingira.

“Masomo yangu nikiwa nje ya Zanzibar yalizidi kuwa mepesi baada ya kujiona kuwa sikuwa ugenini bali ni nyumbani, na suala la ada la kukamilisha masomo yangu halikuwa kikwazo kwa kuwa nilikuwa ni mnufaika wa Mkopo kutoka Bodi ya Mikopo ya Tanzania. Kwa hili daima nitajivunia kuasisiwa kwa Muungano.

“Muungano wa Tanganyika na Zanzibar ni tunu na unaendelea kuimarika kila muda. Muungano huu kwa kiasi kikubwa ni moja ya matunda makubwa yaliyoachwa na waasisi wa Mataifa haya yalioungana. Muungano huu umekuwa na faida kubwa kijamii, kiutamaduni, kisiasa na kufaidisha pande zote za muungano huu. Muungano wetu tulikotokea umekuwa ukitajwa kuwa na changamoto mbalimbali lakini kama ilivyo jambo lolote la mashirikiano, hata hivyo viongozi wa pande zote wamekuwa wakishirikiana kutatua changamoto hizo na kwa sasa zimebaki changamoto chache sana ambazo pia nazo zipo katika hatua za kuondolewa”.

Naye Kijana **Abadhar Abdulla**, kutoka Bwejuu, Zanzibar anasema: “Kwa maoni yangu Muungano una umuhimu sana kutokana na matunda tunayojivunia yaliyopo kwa sasa ambapo mwanzo yalikuwa hayakupatikana kielimu. Hapo mwanzo hakukuwa na muingiliano wa kuwawezesha wasomi katika suala zima la kupata mkopo wa elimu ya juu ambao unatoka Bara kufaidika Wazanzibari, ila Muungano ndio umetuzalishia jambo hili.

“Suala zima la ajira ambalo ni changamoto kwa Wazanzibari, Muungano umetusaidia kwa kiasi kikubwa kupata asilimia ya kufanya kazi Tanganyika bila ya kikwazo chochote kwa Wazanzibari ambapo kabla ya uhuru hili halikuwepo.”

**Hasina Yussuf Juma**, Mjumbe wa Baraza la watendaji, Baraza la Vijana Zanzibar: Muungano wa Tanganyika na Zanzibar uendelee kuwepo kwa sababu tuna amani na mshikamano. Kiuchumi pia tumesonga mbele kwa sababu kusingekuwa na muungano basi Zanzibar na Tanganyika tungekuwa na upungufu wa uchumi. Kwa mfano Zanzibar kungekuwa na uhaba wa mbuga za wanyama pia utalii wa milima. Na hata pia Tanganyika wasingekuwa na utalii wa visiwa na uvuvi”.

**Asha Mohammed Abdallah**, kutoka ZAIDAT, anasema: “Nimekuwa nikisoma na kufuatilia taarifa na makala mbalimbali zinazozungumzia Muungano wa Tanganyika na Zanzibar kwa ajili ya kuelimika zaidi na kuelewa mambo mbalimbali kwa miaka mingi. Kwa maoni yangu Muungano huu umekidhi vigezo na upo wazi kwa wananchi wote

kujadili na kutoa maoni juu ya masuala mbalimbali juu ya Muungano huu bila vikwazo vyovyote. Wananchi walio wengi wanafurahi kuwepo kwa Muungano huu kwa sababu ya faida wanazopata za kibiashara, kimatibabu na kimatembezi (uhuru kwenda popote).

**Maliki Rashidi** wa Mtongani, Dar es Salaam anasema wenzake wengi wanaoorodhesha changamoto za Muungano ni Watanzania kutoka Zanzibar ambao hawakushuhudia utawala wa Mwarabu na wala hawasomi vitabu vya historia. “Mengi wanayapata vijiwani ati Sultani kipindi chake alikuwa anagawa tende na haluwa! Mimi natoka Tanga, Babu yangu aliniambia Sultani na watu wake hawakutuona sisi kama binadamu bali mali yao ya kutumia. Serikali ianze kufundisha kwa nguvu zote historia ya ukoloni wa Mwingereza, Mjerumani na Mwarabu bila kupepesa macho ama sivyo manung’uniko ya Muungano yataendelea kutokana na uelewa mdogo tu.”<sup>11</sup>

**Mosses Widmel**, mhitimu wa sheria Chuo Kikuu cha Dar es Salaam anashauri kuwa, elimu ya kina kuhusu historia ya nchi zetu mbili zilizoungana mwaka 1964 haina budi kutolewa mapema iwezekanavyo kuanzia shule za msingi hadi vyuo vikuu kupepusha kuzuka kwa “kizazi cha watumwa wasiojielewa”.

“Wapo wanafunzi wenzetu waliokuja na kampeni ya kuvunja muundo wa Muungano tulionao na tuwe na Muungano wanaouita wa “mkataba”. Tukawauliza huyo ndiyo mnyama gani maana kila muundo wa muungano ni wa mkataba mahsusi. Kumbe wana maana ya Muungano dhaifu sana, confederation! Yaani tuwe kabisa ndoto ya *pan-africanism* tuliyoibeba kwa faida ya Afrika ili kuwafurahisha watawala wa jana? Tuliwaambia wenzetu *no way!*”<sup>12</sup>

Mwanaharakati wa miaka mingi **Julius Nyanda Miselya** alisema Muungano unahitaji kujitoa mhanga ili kupata faida kubwa ya nguvu ya pamoja. “Mzee Karume, mwana-umajumui wa kiafrika wa mstari ya mbele, aliishangaza dunia kwa kuwa tayari kuachia Urais wake na kuwa Makamu ili Tanganyika na Zanzibar ziungane na kupanda mbegu ya kwanza ya uwezekano wa kuwa na Shirikisho la Afrika.

“Nyerere naye akatukazia macho tuache kulilialilia fursa za upendeleo za Zanzibar chini ya Muungano kama vile haki ya kuwa na ardhi bara na visiwani bila kizuizi, haki ambayo Mtanzania bara hana. Haki ya uongozi bara na visiwani ya Wazanzibari ambayo Wabara hawana. Wabara sasa tumeikubali hali hiyo kwa kuwa Muungano wetu umebeba

<sup>11</sup> Mahojiano na Maliki kwenye mnada wa samaki Kunduchi Beach, Jumamosi tarehe 26 Februari, 2022.

<sup>12</sup> Mahojiano na Mosses, Posta jijini Dar es Salaam Jumanne tarehe 8 Machi, 2022.

maana kubwa kwa Afrika na kimataifa ambayo hatuwezi kuipoteza kwa changamoto ndogo ndogo kama hizo”.<sup>13</sup>

## Nukuu za Waasisi wa Muungano wa Tanganyika na Zanzibar

### Mwalimu Julius Kambarage Nyerere

“Watu wazima wamezungumza Muungano kwamba tuuvunje au uendele. Ilikuwa ipo hatari ya kuvunjika na wala haijaisha. Watu wanazungumza Uzanziabari baadhi ni viongozi wetu. Wanajivunia Uzanziabari. Nadhani wengine wanafikiria hata kujitenga”. **13 MACHI, 1995**

“Huwezi kuutukuza Uzanziabari kwa kujiiita sisi Wanzanzibari na wao Watanganyika. Wanzanzibari wakijitenga kutokana na ulevi tu; sisi Wanzanzibari na wao Watanganyika, wakumbuke kwamba Muungano ndio unaowafanya waseme “sisi “Wanzanzibari” “wao Watanganyika”. Nje ya Muungano, hawawezi kusema hivyo: kuna “wao Wapemba” “sisi Waunguja”. **13 MACHI, 1995**

“Watanganyika wakiwakataa Wanzanzibari kwa tendo la dhambi ileile ya “sisi Watanganyika” “wao Wanzanzibari” wakatukuza ‘usisi Tanganyika’ na kwa ajili hiyo wakawafukuza Wanzanzibari, hawatabaki salama. Hapatakuwa na Tanganyika wakishakujitenga tu, Watanganyika hawabaki salama”. **13 MACHI, 1995**

“Hapatakuwa na Tanganyika. Wakishajitenga tu, Wanzanzibari wako kando hivi, mmewafukuza mnajidai wakubwa ninyi: “hawa nani hawa, wao wana Rais sisi hatuna kwa nini? “Watimue” Mnawatimua, mkampata Yelstin wenu akawatimua. Hambaki. Kwani Mtasemaje? Mtakuwa mmeshasema sababu ya kuwafanya ya ‘wale ni wao’ na ‘ninyi ni ninyi’ ‘wao’ vipi Wanzanzibari; halafu mbaki ninyi?” **13 MACHI, 1995**

“Lakini mtaniwia radhi kama nikifanya masahihisho moja au mawili sahihisho lenyewe ni hasa kwa maneno aliyoyasema Bwana Kawawa mwanzo. Nafurahi Bwana Kawawa kasimama katusifu mimi na Bwana Karume kwa sababu ya Muungano na kwa kweli Muungano wetu ni kitu kikubwa na kama kuna watu wameleta ule Muungano wanastahili kusifiwa, kwa nini wasisifiwe? Ni haki ni kitu kikubwa hiki, kwamba nchi

<sup>13</sup> Mahojiano na Miselya, Posta jijini Dar es Salaam Jumanne tarehe 8 Machi, 2022.

mbili zinaweza zikaunganika zikawa nchi moja.” **RTD, 09. DESEMBA, 1964**

“Nchi zilizotengwa na Wakoloni kwa muda mrefu sana zinaweza zikarudishwa zikawa kitu kimoja, ndugu wawili ambao wamejengewa ukuta kama ukuta uliojengwa Ujerumani, ukuta ule unabomoka ndugu wawili wale wanarudi wanakuwa hali moja ni jambo kubwa!!! Jambo kubwa!” **09 DESEMBA, 1964**

“Jambo kubwa sana, matatizo hayo tunaweza kuyagawa katika sehemu mbili: kwanza nchi, matatizo yanayohusu ‘Nchi’. Pili, matatizo yanayohusu Watu, Nafsi. “Nchi namna gani? Leo, nchi moja na nchi nyingine ni sawasawa, wanaita wenyewe kwa kiingereza kila nchi ni *sovereign*, ina madaraka kamili, ina ukamilifu wa madaraka yake, na nchi mbili zikiungana ndio kusema kila moja ya nchi zile inakubali kuyavua yale madaraka yake na uko ugumu nchi nyingi zinapata tabu kuyavua madaraka iliyokuwa nayo yawe kitu kingine. Tanganyika ivue madaraka, Kenya ivue madaraka, Unguja [Zanzibar] ivue madaraka, Uganda ivue madaraka. [Kisha] madaraka yale kipewe kitu kipya kabisa madaraka yale.

“Yapo matatizo kila nchi ina wivu wa madaraka yake kila nchi haipendi kuvua madaraka yale nasema lipo tatizo. Na nchi inapokubali hakuna budi wananchi wapate sifa kuambiwa na kukubali kuvua madaraka yake waliokuwa nayo. Mara nyingi yana maana mara nyingine kilemba cha ukoka, Wananchi wana haki ya kuelewa kuvua madaraka yale na kuyatumbukiza katika kapu kubwa madaraka yale. Nchi yenyewe inaona tabu kuacha madaraka yake.

‘Pili matatizo ya watu, nafsi. Msiyapuuze hayo matatizo yana maana: nchi ni nini? Nchi si barabara na miti na majumba ni watu na watu ni nafsi. Basi yapo matatizo ya nafsi manaake nini. Hii nchi ina *President* (Rais) wake, *Vice President* [Makamu wa Rais] wake na Mawaziri wa kilimo, *Prime Minister* (Waziri Mkuu), vile vile na upande wa pili. Sasa mnazungumza habari ya kuunganisha nchi kuwa moja: huyu *President* atakwenda wapi? Nchi itakapounganika na kuwa moja nani atakuwa *President* au tutakuwa wawili? Hilo si swali dogo ni kubwa ni swali la Nafsi mimi Julius nauliza nchi itakapokuwa moja mimi nitakuwa wapi?

“Hasara! Kama kuna watu ambao kweli wameyapuuzwa maswali hayo (ya mimi nitakuwa nani?) na hawakuuliza hata kidogo ni Karume na Rashid Kawawa maana hatima yao ni nini juu ya Muungano, hawa watu wawili. Mimi nimebaki palepale (Rais, na) wao kila mmoja kateremka. Karume

aliyekuwa *President* sasa kawa ni Makamu wa kwanza kwangu, Rashid aliyekuwa wa pili kwangu sasa ni wa tatu kwangu (yaani Makamu wa Pili wa Rais). Na hakuna (hata) mmoja wao nimesikia anauliza jambo hili hata kidogo, hata! Sikusikia hata kidogo Karume anasema tuwe *Mapresident* wawili hata! Hata sikusikia Rashid anasema mimi sasa nabaki wapi? Hata! Hata mimi nasema katika watu wawili waliosema kwamba inawezekana kuteremka chini kwa manufaa ya Umoja wa Afrika ni hao wawili”. **RTD 09 DESEMBA, 1964**

“Ushirikiano na migogoro ni pande mbili za sarafu moja; vyote vinatokana na uhusiano wa mtu na wenzake. Kadri kundi linavyokuwa kubwa ndivyo kunavyokuwa na uwezekano mkubwa wa kupata maendeleo kupitia ushirikiano, na pia ndivyo kunavyokuwa na uwezekano mkubwa wa kujitokeza migogoro”. **FREEDOM AND UNITY 307, 2012<sup>14</sup>**

Hakuna Mungu atakayeleta Umoja wa Afrika kwa hiari pekee na kusema, “Pale pawe na umoja” **FREEDOM AND UNITY 216, 2012**

“...Mataifa ya Afrika mbalimbali yapo hatarini kuhusishwa na pande tofauti za migogoro ambayo haiwahusu. Kama kungekuwa na maadili ya Umoja wa Afrika halisi usaliti usingewezekana” **FREEDOM AND UNITY: 213, 2012**

“Moja ya jambo gumu tunalopaswa kukabiliana nalo tunapoelekea kupata Umoja wa Afrika ni kwamba umoja huu una maana - kwa upande wa nchi mbalimbali - kukabidhi uhuru na – kwa upande wa kiongozi binafsi - kukabidhi madaraka. Lazima tukabiliane na hali hiyo ipasavyo ukizingatia mpaka sasa hakuna kukabidhi huko.” **FREEDOM AND UNITY: 253, 2012**

“Afrika lazima iende pamoja kama kitu kimoja, vingenevyo haitafika kule inakotaka.” **FREEDOM AND UNITY: 327, 2012**

“Kwa kuwa kila mmoja wetu ni dhaifu sana akijitenga kiasi kwamba tunashindana kupata utajiri; na aina ya uchumi uliungana unamdhooifisha kila mmoja kadri anavyojongea uelekeo tofauti kwa wakati mmoja.” **FREEDOM AND UNITY: 336, 2012**

“Kuzungumzia umoja ni suluhisho la maovu yote, itakuwa ni ajabu kutembea uchi mbele ya mdomo wa simba mwenye njaa.” **FREEDOM AND UNITY: 212, 2012**

<sup>14</sup> Quotable Quotes of Mwalimu Julius K. Nyerere, Christopher C. Liundi, 2012.



“Kwa Afrika Umoja haupaswi kuwa kama ndoto; umoja unaweza kuwa dira inayotuhamasisha. Na suala hilo, linatutegemea sisi.” **FREEDOM AND UNITY: 216, 2012**

“Na mabadiliko hayo yanapaswa kuwa chanya, yanapaswa kuanzishwa na kuratibiwa na Afrika na si tu mwitiko wa masuala yanayoathiri Bara la Afrika” **FREEDOM AND UNITY: 22, 2012**

“Ukweli ni kwamba kila sehemu ya Afrika inahitaji Afrika kwa ujumla, na Afrika kwa ujumla inahitaji kila sehemu ndogo ya Bara la Afrika.” **FREEDOM AND SOCIALISM: 218, 2012**

“Afrika si bara dhaifu ukilinganisha na mabara mengine duniani kama wakati mwingine inavyodhaniwa. Linakuwa bara dhaifu pale mataifa mbalimbali yanaporuhusu kujitenga.” **FREEDOM AND SOCIALISM: 221, 2012**

“Umoja wa Afrika haujapotea. Na kamwe hautapotea wakati kuna watu wanaofahamu umuhimu wake na wapo tayari kuupigania. “**FREEDOM AND SOCIALISM: 294, 2012**

“Muungano kati ya Tanganyika na Zanzibar ni kiashirio kwamba umoja unaweza kupatikana ikiwa kuna nia, licha ya changamoto mbalimbali zilizopo.” **FREEDOM AND DEVELOPMENT: 177, 2012**

## **Sheikh Abeid Amani Karume**

“Wananchi wa Tanzania wakati umefika sisi wenyewe kuwa macho, kuwa macho kwenyewe kwa kulinda uhuru wetu sababu uhuru wetu ndio maisha yetu, ndio neema, ndio kila kitu chetu”. **RTD 17, NOVEMBA 1964 ZANZIBAR**

“Kila dola ulimwenguni lina wajibu wa kulinda uhuru wa dola yake sababu uhuru ndio rasilimali ya wananchi leo wananchi wa Tanzania tukae macho kuhifadhi uhuru wetu tulioutafuta miaka kadha wa kadha ulimwenguni”. **RTD 17, NOVEMBA 1964 ZANZIBAR**

“Serikali ya Tanzania ni Serikali sawasawa na Serikali zingine ulimwenguni, ilivyokuwa ni serikali kamili jambo la kwanza iwe na uwezo wa kulinda amani na salama ya wananchi wake”. **RTD 17, NOVEMBA 1964 ZANZIBAR**

“Misada iliyopo leo ndani ya Serikali ya Tanzania, msaada wa kwanza afundishe njia ya kuleta amani katika nchi ya watu, huyu ndiye mwenye kunisaidia. Jambo la kwanza Serikali ya Tanzania inaendeshwa

na usukani wa wana wa nchi wenyewe, haikubali usukani wa nchi kuendeshwa na wageni”. **RTD 17, NOVEMBA 1964 ZANZIBAR**

“Tanzania ina serikali kamili sawa na Serikali yeyote Ulimwenguni hatuna ugomvi na dola yeyote. Serikali ya Tanzania wapo watu wachache katika nchi yetu wakitumia Sultani, wametumia ngazi yao kwa jina la Sultani, kila wanalolipata Sultani. Hatuna ugomvi na dola yeyote, hatutaki kutawaliwa na mtu. Sasa vibaya eti, tutawaliwe. Serikali ya Tanzania pamoja na wana wa Tanzania, wote Serikali inayotakiwa ya wenyewe watu sio ya mtu. **RTD 17, NOVEMBA 1964 ZANZIBAR**

“Tunamhakikisha President wa Tanzania President Mwalimu Julius Nyerere tamko alilolitamka kwamba serikali yetu iko tayari na imeshakuwa tayari kumsaidia mwafrika yeyote anayegombania [anayepigania] Uhuru katika nchi yake. Tunamhakikishia wafuasi tuko tayari. Tamka tu na tupo tayari saa yeyote, wakati wowote, tamka tu! Eheeeee! **RTD 17, NOVEMBA 1964 ZANZIBAR**

“Tunaona meli, maana ndio kitu ninachokijua, nimetumikia meli kubwa lakini imeundwa vipande vipande vipande. Pande la chuma hili limegongwa na mwenzie na hapa, limekuja lingine ndiyo [limeunganishwa na] imekuwa meli halafu raha. Ndani mna watu wanalala, mna vitanda. Basi watu wanataka Waafrika wenyewe wawe kitu kimoja, Waafrika wa Zanzibar na Waafrika wa Tanganyika ndio hamu yao kubwa kugombania uhuru wa Waafrika, wawe kitu kimoja”. [kwa kuungana] **RTD 17, NOVEMBA 1964 ZANZIBAR**

“Kuwa Afrika yote itaungana, itakuwa chini ya Kiongozi mmoja tu wa kiafrika na hapo ndiyo Waafrika wataona matunda ya Afrika na hapo ndiyo mtapata matunda ya Afrika. Waafrika wote wataungana na kuwa chini ya kiongozi mmoja tu wa kiafrika”. **RTD 17, NOVEMBA 1964 ZANZIBAR**

“Na hapo ndiyo Waafrika watapata matunda ya Kiafrika na hapo ndiyo Waafrika mtaona utamu wa Uhuru wenu. Haya mapingamizi yote haya wasiokuwa Waafrika wamekwisha tambua kuwa iko faida kubwa Waafrika wakiungana wenyewe kwa wenyewe, watapata faida kubwa. Wale wanaopinga sisi Waafrika, tumeshatambua iko faida kubwa. Na kama wataizika sisi tutaifufua, ndiyo kazi yetu”. **RTD 17, NOVEMBA 1964 ZANZIBAR**

“Mimi Karume namwambia President Nyerere wa Tanzania Mwalimu Julius Nyerere kwamba wakati wowote, saa yeyote, muda wowote juu

yake mkononi mwake fikra ya kuunganisha Afrika mimi niko nyuma yake mpaka kufa kwangu. Hakuna haja ya kutokea jambo la kuungana na Waafrika akasema kwamba ningojee nikamshauri Mzee Karume kisiwani, asitumie aendelee tu”. **RTD 17, NOVEMBA 1964 ZANZIBAR**

“Baadhi ya watu wengi wanataka kufahamu Serikali ya Unguja [Zanzibar] na Tanganyika zimechanganyika zimekuwa ni Union [Jamhuri ya Muungano] moja tu. Napenda mfahamu wananchi wote kazi hii si kazi ya Mwalimu Julius Nyerere, kazi hii si kazi ya Abeid Karume, jambo hili la (wananchi) wenyewe Waafrika wenyewe wote” **TAREHE 23 APRILI, 1964**

“Watu wengi wamefanya *announcement* (matangazo) na magazeti kwamba Serikali ya Unguja (Zanzibar) na Tanganyika zitafanya *Union* (Muungano) moja, hii ni kweli lakini tunapenda kuwahakikishieni raia wote wa Serikali ya Jamhuri ya (Watu wa Zanzibar) Unguja kwamba *union* hiyo ni kutafuta maslahi ya wana wa nchi wenyewe, kutafuta maslahi ya maendeleo mapya katika nchi zetu mbili; *union* hiyo haitavunja urafiki wetu na marafiki zetu; *Union* hiyo itaongeza uhusiano mwema baina yetu na marafiki zetu, baina yetu na watu wote wa makabila mbalimbali na madola mbalimbali tuwe kitu kimoja kwa sababu *union* hiyo ndiyo itakayoanza kazi tuli odhamiria ya kuondoa ubaguzi baina ya binadamu..... *union* haitokuwa na dola hii bora na dola hii si bora”, **TAREHE 24 APRILI, 1964**

“Muungano wa Tanganyika na Unguja (Zanzibar) una thamani kubwa kwetu sisi Waafrika”. **TAREHE 26 APRILI, 1967**

“...lakini vijana hatuna budi kukuhakikishieni kwamba hakuna hata mmoja asiyejua kwamba waafrika wako ndani ya mateso kwa haki zao wenyewe, kwa kujua hivyo nadhani vijana ndio mmepata uongozi maalum ambao huo wa mwenge kupita mkizunguuka nao. Huo mwenge una maana namna chungu mzima, hapa mnauona unawaka lakini sisi tutakuambieni kidogo; huu mwenge ni uhai wa Waafrika, huu mwenge unawamulika maadui wote unaowadhili na kuwakandamiza Waafrika katika Afrika yao wenyewe. Huu mwenge unaendelea kuangaza kila mahala kwa kuendelea kutafuta uhuru wa Waafrika ambao mpaka sasa hawajapata kujitawala katika nchi zao. **RUVUMA, MBINGA 10 SEPTEMBER, 1966**

“Viongozi wa Tanzania ndani ya imani yao na ukweli wao hakuna kitu wanachokitaka bila ya Umoja wa Afrika na azma kubwa ianzie mkusanyiko wa Afrika Mashariki wanaouita “*East African Federation*”

sote viongozi wa Afrika ya Mashariki tuwe mkono mmoja, tuwe kitu kimoja, tuwe Serikali moja, tuwe uwezo mmoja, tuwe na nguvu moja. Lakini msione yamepoa, msivunjike nguvu vijana yapo njiani yanakuja, bado wingu moja tu la mvua, ikishapiga mtaona miche yote inachipua". Mapokezi ya mwenge wa uhuru. **RUVUMA, MBINGA 10 SEPTEMBER, 1966**

### **3. AWAMU ZA UONGOZI KATIKA JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

#### **Awamu ya Kwanza ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mwaka 1964 Hadi 1985**

Awamu hii ilikuwa chini ya Rais wa Kwanza wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mwalimu Julius Kambarage Nyerere, Makamu wa kwanza wa Rais alikuwa Sheikh Abeid Amani Karume na Makamu wa Pili wa Rais alikuwa Ndugu Rashid Mfaume Kawawa. Aidha, aliyekuwa Makamu wa Kwanza wa Rais alikuwa pia Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi na Makamu wa Pili wa Rais alikuwa pia Waziri Mkuu wa Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Utaratibu huu uliendelea kwa takribani miaka 21. Wakati Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania alipotoka upande wa Zanzibar, Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano ndiye aliyekuwa Makamu wa Kwanza na Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi alikuwa Makamu wa Pili wa Rais.

Mwaka 1972 Sheikh Abeid Amani Karume aliuawa na wapinga Mapinduzi. Kutokana na kifo hicho, Mheshimiwa Aboud Jumbe Mwinyi alichaguliwa kuchukua nafasi ya Makamu wa Kwanza wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi. Alitumikia nafasi hiyo kuanzia mwaka 1972 - 1984.

Mheshimiwa Edward Moringe Sokoine alikuwa Waziri wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kuanzia mwaka 1977 - 1980 na 1983 - 1984 alipofariki dunia. Mhe. Cleopa David Msuya alikuwa Waziri Mkuu na Makamu wa Pili wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kuanzia mwaka 1980 - 1983. Mheshimiwa Dkt. Salim Ahmed Salim alikuwa Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kuanzia mwaka 1984 - 1985.

Kutokana na hali ya kisiasa ya Zanzibar mwaka 1984, aliyekuwa Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Sheikh Aboud Jumbe alijiuzulu na Ndugu Ali Hassan Mwinyi aliteuliwa kushika wadhifa huo mwaka 1984 - 1985. Mwaka 1985 Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mwalimu Julius K. Nyerere aling'atuka na Ndugu Ali Hassan Mwinyi alichaguliwa kuwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

**VIONGOZI WA AWAMU YA KWANZA YA SERIKALI YA  
JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA KUANZIA MWAKA  
1964 HADI 1985**



*Mwl. Julius Kambarage Nyerere  
Rais wa Jamhuri ya Muungano wa  
Tanzania  
1964 - 1985*



*Sheikh Abeid Amani Karume  
Makamu wa Kwanza wa Rais wa  
Jamhuri ya Muungano wa Tanzania  
na Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti  
wa Baraza la Mapinduzi  
1964 - 1972*



*Ndg. Rashid Mfaume Kawawa  
Makamu wa Pili wa Rais wa Jamhuri  
ya Muungano wa Tanzania  
na Waziri Mkuu  
1964 - 1977*



*Sheikh Aboud Jumbe Mwinyi  
Makamu wa Kwanza wa Rais wa  
Jamhuri ya Muungano wa Tanzania  
na Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti  
wa Baraza la Mapinduzi  
1972 - 1984*

**VIONGOZI WA AWAMU YA KWANZA YA SERIKALI YA  
JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA KUANZIA MWAKA  
1964 HADI 1985**



*Ndg. Edward Moringe Sokoine  
Waziri Mkuu wa Jamhuri ya  
Muungano wa Tanzania  
1977- 1980 na 1983 - 1984*



*Ndg. Ali Hassan Mwinyi  
Makamu wa Kwanza wa Rais wa  
Jamhuri ya Muungano wa Tanzania  
na Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti  
wa Baraza la Mapinduzi  
1984 - 1985.*



*Ndg. Cleopa David Msuya  
Waziri Mkuu na Makamu wa Pili wa  
Rais wa Jamhuri ya Muungano wa  
Tanzania 1980 - 1983*



*Dkt. Salim Ahmed Salim  
Waziri Mkuu wa Jamhuri ya  
Muungano wa Tanzania  
1984- 1985*

## **Awamu ya Pili ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Kuanzia Mwaka 1985 Hadi 1995**

Awamu hii ilikuwa chini ya uongozi wa Ndugu Ali Hassan Mwinyi. Makamu wa Pili wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania alikuwa Sheikh Idris Abdulwakil ambaye alikuwa ni Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi kuanzia mwaka 1985 – 1990.

Mheshimiwa Jaji Joseph Sinde Warioba alikuwa Makamu wa Kwanza wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Waziri Mkuu kuanzia mwaka 1985 – 1990.

Mheshimiwa John Samwel Malecela alikuwa Waziri Mkuu na Makamu wa Kwanza wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kuanzia mwaka 1990 – 1994.

Mheshimiwa Cleopa David Msuya alikuwa Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kuanzia mwaka 1994 -1995.

Mwaka 1992 Serikali zetu ziliona umuhimu wa kuruhusu mfumo wa vyama vingi vya Siasa nchini. Hivyo basi, mwaka 1994 nafasi ya Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ilifanyiwa mabadiliko kufuatia mfumo wa demokrasia ya vyama vingi.

Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977, ilifanyiwa marekebisho kupitia Sheria Namba 34 ya mwaka 1994 ambapo iliweka utaratibu wa kumpata Makamu wa Rais. Makamu wa Rais alipatikana kwa kuchaguliwa katika uchaguzi ule ule pamoja na Rais baada ya kupendekezwa na chama chake wakati ule ule anapopendekezwa mgombea wa kiti cha Rais na walipigiwa kura kwa pamoja. Mgombea kiti cha Rais akichaguliwa basi na Makamu wa Rais atakuwa amechaguliwa.

Katika awamu hii Sheria mbalimbali zilitungwa ambazo ni: Sheria ya Maadili ya Viongozi wa Umma Sheria Namba 13 ya mwaka 1995; Sheria ya Uhamiaji Namba 7 ya mwaka 1995; Sheria ya Mamlaka ya Kodi Namba 11 ya mwaka 1995; Sheria ya Benki Kuu ya Tanzania Namba 1 ya mwaka 1995; na Sheria ya Uraia Namba 6 ya mwaka 1995.



**VIONGOZI WA AWAMU YA PILI YA SERIKALI YA JAMHURI YA  
MUUNGANO WA TANZANIA MWAKA 1985 HADI 1995**



*Ndg. Ali Hassan Mwinyi  
Rais wa Jamhuri ya Muungano wa  
Tanzania  
1985 - 1995*



*Sheikh Idris Abdulwakil  
Makamu wa Pili wa Rais wa Jamhuri  
ya Muungano wa Tanzania na Rais  
wa Zanzibar na Mwenyekiti wa  
Baraza la Mapinduzi  
1985 - 1990*



*Dkt. Salmini Amour  
Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi  
1990 - 2000*

**VIONGOZI WA AWAMU YA PILI YA SERIKALI YA JAMHURI YA  
MUUNGANO WA TANZANIA MWAKA 1985 HADI 1995**



*Mhe. Jaji Joseph Sinde Warioba  
Waziri Mkuu na Makamu wa  
Kwanza wa Rais wa Jamhuri ya  
Muungano wa Tanzania  
1985 - 1990*



*Mhe. John Samwel Malecela  
Waziri Mkuu na Makamu wa  
Kwanza wa Rais wa Jamhuri ya  
Muungano wa Tanzania  
1990 - 1994*



*Ndg. Cleopa David Msuya  
Waziri Mkuu na Makamu wa Pili wa Rais  
wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania  
1994 - 1995*

## **Awamu ya Tatu ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Kuanzia Mwaka 1995 Hadi 2005**

Awamu hii ilikuwa chini ya uongozi wa Mheshimiwa Benjamin William Mkapa. Mheshimiwa Dkt. Omar Ali Juma alikuwa Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kuanzia mwaka 1995 – 2001 alipoaga dunia. Kufuatia kifo cha Mheshimiwa Dkt. Omar Ali Juma, Mheshimiwa Dkt. Ali Mohamed Shein aliteuliwa kushika wadhifa wa Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kuanzia mwaka 2001 – 2005.

Mheshimiwa Fredrick Tulway Sumaye alikuwa Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kuanzia mwaka 1995 – 2005.


Katika awamu hii kuna Sheria mbalimbali ambazo zilitungwa, baadhi ya sheria hizo ni:- Sheria ya Tume ya Pamoja ya Fedha Na 14 ya mwaka 1996; Sheria ya Biashara ya Bima ya Tanzania Namba 18 ya mwaka 1996; na Sheria ya Usalama wa Taifa Namba 15 ya mwaka 1996.

Ofisi ya Makamu wa Rais iliundwa kwa mujibu wa Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya Mwaka 1977 Ibara ya 47, ikisomwa pamoja na Sheria Namba 34 ya Mwaka 1994, Kifungu cha 11. Katika awamu hii, Sekretarieti ya Masuala ya Muungano ilianzishwa chini ya Ofisi ya Makamu wa Rais mwaka 1998 na kupewa hadhi ya kuwa Idara kamili mwaka 2005.

**VIONGOZI WA AWAMU YA TATU YA SERIKALI YA JAMHURI  
YA MUUNGANO WA TANZANIA MWAKA 1995 HADI 2005**



*Mhe. Benjamin William Mkapa  
Rais wa Jamhuri ya Muungano wa  
Tanzania  
1995 - 2005*



*Mhe. Dkt. Omar Ali Juma  
Makamu wa Rais wa Jamhuri ya  
Muungano wa Tanzania  
1995 - 2001*



*Mhe. Dkt. Ali Mohamed Shein  
Makamu wa Rais wa Jamhuri ya  
Muungano wa Tanzania  
2001 - 2005*



*Mhe. Fredrick Tulway Sumaye  
Waziri Mkuu wa Jamhuri ya  
Muungano wa Tanzania  
1995 - 2005*

## **Awamu ya Nne ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Kuanzia Mwaka 2005 Hadi 2015**

Awamu hii iliongozwa na Mheshimiwa Dkt. Jakaya Mrisho Kikwete. Mheshimiwa Dkt. Ali Mohamed Shein alikuwa Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kuanzia mwaka 2005 – 2010 na kuanzia mwaka 2010 - 2020, Mheshimiwa Dkt. Ali Mohamed Shein alichaguliwa kuwa Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi.

Mheshimiwa Dkt. Mohammed Gharib Bilal alikuwa Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kuanzia mwaka 2010 - 2015.

Mheshimiwa Edward Lowassa alikuwa Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kuanzia mwaka 2005 – 2008. Mwezi Februari, 2008 Mheshimiwa Edward Lowassa alijiuzulu wadhifa huo na Mheshimiwa Mizengo Kayanza Pinda aliteuliwa kushika wadhifa wa Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kuanzia mwaka 2008 - 2015.

Mwaka 2006 Kamati ya Pamoja ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania (SMT) na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar (SMZ) iliundwa ili kushughulikia changamoto za Muungano na kuzipatia ufumbuzi chini ya uenyekiti wa Mheshimiwa Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

**VIONGOZI WA AWAMU YA NNE YA SERIKALI YA JAMHURI  
YA MUUNGANO WA TANZANIA KUANZIA MWAKA 2005  
HADI 2015**



*Mhe. Dkt. Jakaya Mrisho Kikwete  
Rais wa Jamhuri ya Muungano wa  
Tanzania  
2005 - 2015*



*Mhe. Dkt. Ali Mohamed Shein  
Makamu wa Rais wa Jamhuri ya  
Muungano wa Tanzania  
2005 - 2010  
Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa  
Baraza la Mapinduzi  
2010 - 2015*



*Mhe. Dkt. Mohamed Gharib Bilal  
Makamu wa Rais wa Jamhuri ya  
Muungano wa Tanzania  
2010 - 2015*

**VIONGOZI WA AWAMU YA NNE YA SERIKALI YA JAMHURI  
YA MUUNGANO WA TANZANIA KUANZIA MWAKA 2005  
HADI 2015**



*Mhe. Dkt. Amani Abeid Karume  
Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa  
Baraza la Mapinduzi  
2000 - 2010*



*Mhe. Edward Ngoyai Lowassa  
Waziri Mkuu wa Jamhuri ya  
Muungano wa Tanzania  
2005 - 2008*



*Mhe. Mizengo Kayanza Peter Pinda  
Waziri Mkuu wa Jamhuri ya  
Muungano wa Tanzania  
2008 - 2015*

## **Awamu ya Tano ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mwaka 2015-2021**

Awamu hii iliongozwa na Mheshimiwa Dkt. John Joseph Pombe Magufuli. Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania alikuwa Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan kuanzia mwaka 2015 – 2021. Mwezi Machi, 2021 Taifa lilimpoteza Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mheshimiwa Dkt. John Joseph Pombe Magufuli na hivyo, Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan aliapishwa kuwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kama inayoelekezwa na Katika ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977 Kifungu cha 37 (5).

Mheshimiwa Kassim Majaliwa Majaliwa alikuwa Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kuanzia mwaka 2015 – 2021.

Katika kipindi hiki, vikao vya Kamati ya Pamoja ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania (SMT) na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar (SMZ) ya Kushughulikia Masuala ya Muungano viliendelea kufanyika na kujadili changamoto za Muungano. Kimsingi Muungano uliendelea kuimarika na hivyo kudumisha amani na utulivu nchini.



**VIONGOZI WA AWAMU YA TANO YA SERIKALI YA JAMHURI  
YA MUUNGANO WA TANZANIA KUANZIA MWAKA 2015  
HADI 2021**



*Dkt. John Pombe Joseph Magufuli  
Rais wa Jamhuri ya Muungano wa  
Tanzania  
2015 - 2021*



*Mhe. Samia Suluhu Hassan  
Makamu wa Rais wa Jamhuri ya  
Muungano wa Tanzania  
2015 - 2021*



*Mhe. Dkt. Ali Mohamed Shein  
Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa  
Baraza la Mapinduzi  
2015 - 2020*



*Mhe. Kassim Majaliwa Majaliwa  
Waziri Mkuu wa Jamhuri ya  
Muungano wa Tanzania  
2015 - 2021*

## **Awamu ya Sita ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Kuanzia Mwaka 2021**

Awamu ya Sita inaongozwa na Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan. Mheshimiwa Philip Isdor Mpango ni Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kuanzia mwaka 2021. Mheshimiwa Kassim Majaliwa Majaliwa ameendelea kuwa Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania katika Awamu hii.

Katika kipindi hiki, Kamati ya Pamoja ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania (SMT) na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar (SMZ) ya Kushughulikia Masuala ya Muungano ilijadili na kufanikiwa kuzipatia ufumbuzi hoja 11 kati ya hoja 18 zilizokuwepo.

Taifa letu limeendelea kuwa na amani na utulivu kwani ni jambo lililo dhahiri kuwa Muungano wetu umekuwa ndio utambulisho wetu ndani na nje ya Tanzania.

**VIONGOZI WA AWAMU YA SITA YA SERIKALI YA JAMHURI  
YA MUUNGANO WA TANZANIA KUANZIA  
MWAKA 2021 HADI SASA**



*Mhe. Samia Suluhu Hassan  
Rais wa Jamhuri ya Muungano  
wa Tanzania  
2021 hadi sasa*



*Mhe. Dkt. Philip Isdor Mpango  
Makamu wa Rais wa Jamhuri ya  
Muungano wa Tanzania  
2021 hadi sasa*



*Mhe. Dkt. Hussein Ali Mwinyi  
Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa  
Baraza la Mapinduzi  
2020 hadi sasa*



*Mhe. Kassim Majaliwa Majaliwa  
Waziri Mkuu wa Jamhuri ya  
Muungano wa Tanzania  
2015 hadi sasa*

#### 4. Kamati iliyoandaa Kitabu cha *Muungano wa Tanganyika na Zanzibar: Chimbuko, Misingi na Maendeleo*

Dkt. Harrison G. Mwakymbembe	Mwenyekiti wa Baraza la Chuo Kikuu cha Sayansi na Afya Muhimbili (MUHAS)	Mwenyekiti
Bi. Mary N. Maganga	Ofisi ya Makamu wa Rais	Mjumbe
Bw. Thabit I. Faina	Afisi ya Makamu wa Pili wa Rais, Zanzibar	Mjumbe
Bw. Abdallah H. Mitawi	Ofisi ya Makamu wa Rais	Mjumbe
Bw. Sigsbert R. Kavishe	Ofisi ya Makamu wa Rais	Mjumbe
Dkt. Abdallah R. Mkumbukwa	Chuo Kikuu cha Taifa cha Zanzibar (SUZA)	Mjumbe
Bw. Khalid B. Hamrani	Afisi ya Makamu wa Pili wa Rais, Zanzibar	Mjumbe
Bw. Abbass A. Mwalimu	Chuo cha Diplomasia, Kurasini	Mjumbe
Bw. Hassan K. Hassan	Idara ya Habari Maelezo, Zanzibar	Mjumbe
Bw. Mbaraka S. Hasuni	Afisi ya Makamu wa Pili wa Rais, Zanzibar	Mjumbe
Bi. Hanifa M. Selengu	Ofisi ya Makamu wa Rais	Mjumbe
Bi. Judith Y. Mhina	Idara ya Habari Maelezo (SMT)	Mjumbe
Bi. Cesilia D. Nkwamu	Ofisi ya Makamu wa Rais	Mjumbe
Bw. Edwin M. Ninde	Ofisi ya Makamu wa Rais	Mjumbe
Bw. Kalokola S. Rwabizi	Ofisi ya Makamu wa Rais	Mjumbe
Bw. Robert T. Hokororo	Ofisi ya Makamu wa Rais	Mjumbe

Bw. Ramadhan M. Ramadhan	Afisi ya Makamu wa Pili wa Rais, Zanzibar	Mjumbe
Bw. James T. Likangaga	Ofisi ya Makamu wa Rais	Mjumbe
Bw. Iddi S. Mohammed	Afisi ya Makamu wa Pili wa Rais, Zanzibar	Mjumbe
Bw. Joseph M. Innocent	Ofisi ya Makamu wa Rais	Sekretarieti
Bi. Judith T. Anaclety	Ofisi ya Makamu wa Rais	Sekretarieti





Muungano wa Tanganyika na Zanzibar umejengeka kutokana na historia ya uhusiano wa udugu wa damu, harakati za pamoja na ushirikiano wa vyama vya ukombozi vya Tanganyika na Zanzibar katika kupigania uhuru. Mahusiano hayo yaliyowezeshwa na kudumishwa na waasisi wa Jamhuri ya Tanganyika na Jamhuri ya Watu wa Zanzibar, Mwalimu Julius Kambarage Nyerere na Sheikh Abeid Amani Karume ndiyo yaliyorasimisha Muungano wa Tanganyika na Zanzibar. Hivyo, tunawashukuru Waasisi hao kwa kutujengea na kuturithisha misingi ya udugu, uzalendo, amani, mshikamano na utulivu ambavyo ni guzo kuu ya Muungano wetu.

- Mheshimiwa **Samia Suluhu Hassan**, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na
- Mheshimiwa **Dkt. Hussein Ali Mwinyi**, Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi

